**2 MEI, 2024**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Kumi na Saba – Tarehe 2 Mei, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* - KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**SPIKA:** Ahsante sana, Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* - KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**SPIKA:** Maswali kwa Waziri Mkuu Waheshimiwa Wabunge.

Sasa nimwite Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya maswali yanayotoka kwa Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo majina hapa ya Wabunge ambao wameonesha nia ya kumuuliza maswali Mheshimiwa Waziri Mkuu, tutaanza na Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Chama cha Demokrasia na Maendeleo.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kumekuwa na madai kwa baadhi ya wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo ilivunjika mwaka 1977. Wastaafu hawa wamekuwa wakihangaika kutoka mikoa mbalimbali kufuatilia haki yao katika Jiji la Dar es Salaam mara kwa mara lakini wamekuwa wakirudi bila mafanikio yoyote.

Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya malipo ya wastaafu hawa ili waweze kupata haki zao kama zipo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tuna Watanzania ambao walifanya kazi kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki na baada ya kuvunjika kwa

Jumuiya ya Afrika Mashariki wapo ambao walikuwa wanadai haki zao za utumishi, ofisi yangu pia Ofisi ya Wizara ya Mambo ya Nje imekuwa ikipokea malalamiko haya na tumekuwa tukiyafanyia kazi kwa kuwaelekeza waende kwa mwajiri wao.

Mheshimiwa Spika, kumbukumbu tulizonazo wapo ambao waliwasilisha madai na nyaraka wameshalipwa, sasa kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge anahitaji kujua hao wanaohangaika ambao bado hawajapewa haki zao na kwa kuwa pia Serikali yetu inasimamia haki ya kila aliyetenda kazi yake, basi kama wapo wawasilishe madai hayo kwa mwajiri wao ili tathmini iweze kufanywa na kama haki ipo watapewa haki zao, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Chama Cha Mapinduzi.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, Mheshimiwa Waziri Mkuu kumekuwa na ongezeko kubwa sana la mvua hapa nchini na hali hii tumeiona hivi karibuni.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kubadilisha maji ya mvua kuwa vyanzo vya maji ili kusudi iweze kuleta manufaa kwa wananchi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Toufiq, Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, upo ukweli kwamba tunayo mabadiliko ya hali ya tabianchi ambayo katika vipindi tofauti tunapata jua. Miaka mitatu, minne iliyopita tumepata jua kali sana na tukapata uzoefu wa ukame, lakini kuanzia mwaka jana mwezi wa tisa na wa kumi tumepata mvua nyingi sana ambazo zinaendelea mpaka sasa. Swali hili tumeshawahi kutoa ufafanuzi tulipokuwa tunazungumzia suala la maafa yanayoendelea nchini, lakini nashukuru Mheshimiwa Mbunge

anataka kujua Serikali ina mpango gani wa kutumia maji haya ya mvua kuwa ni fursa kwa matumizi yetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu kupitia Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Wizara ya Maji tayari zimeweka mpango kazi wa kutumia mabonde tuliyonayo na maji yanayotiririka kwenye mabonde hayo, lakini hizi mvua nyingi ambazo pia zimeanzisha mifereji mingi ambayo maji yanaendelea kutiririka kutumia maji hayo kama fursa ya kutumika na wananchi kupitia Wizara ya Maji, kwa kupata maji ya kunywa, kwa ajili ya kilimo, uvuvi na kwa ajili ya kunyweshea mifugo.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo sasa iko kwenye mpango wa ujenzi wa miradi mbalimbali ya umwagiliaji, kwa hiyo, tutakwenda kuchimba mabwawa ili tutumie maji haya tuyakusanye pamoja, tuweze kutekeleza azma ya Serikali ya kupeleka mfumo wa umwagiliaji kwenye maeneo yote yenye fursa hiyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mifugo nayo inatumia fursa hii na mabwawa haya na ambayo pia inaratibiwa na Wizara yenyewe kutengeneza mazingira mazuri kwa ajili ya wafugaji wetu, kwa ajili ya kunyweshea mifugo. Wizara ya Maji yenyewe pia inatumia fursa hii hii kwa kuanzisha mabwawa yatakayokusanya maji pamoja ili kupeleka maji kwenye miji iliyo karibu na maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Dodoma kwa mfano, Farkwa una mfereji mkubwa sana unatoka Kondoa wa Mto Farkwa ambao pia unatiririsha maji mengi, Serikali imeshatenga fedha na imeshatangaza zabuni kuziba maji yake, tuyakusanye pamoja ili tuweze kuleta maji ya matumizi ya binadamu hapa Jijini Dodoma, maji hayo tutayapeleka pia Wilaya ya Bahi ambapo kuna shughuli kubwa ya kilimo tutatumia kwa umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, tunafanya hivyo kwenye Bonde la Mto Rufiji, tunafanya hivyo kwenye Bonde la Kilombero kule Ifakara, tunafanya hivyo kwenye Bonde la Mto Ruvuma, Wilaya za Nanyamba, Newala. Juzi tulikuwa na kikao kikubwa tu cha kushuhudia kusaini mikataba ya

umwagiliaji na hili tulizungumza na mimi nilitoa maelezo pale ya namna Serikali itakavyotumia fursa hii kwa ajili ya kuwapoozesha wananchi wanaokaa maeneo hayo kunufaika na mvua hizi na maji haya ambayo tunayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninakuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imejipanga vizuri kutumia maji tiririka kwa ajili ya kuwawezesha Watanzania kupata fursa mbalimbali kwenye maeneo haya yanayosimamiwa na Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo pamoja na Wizara ya Maji, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, Serikali inatoa ruzuku ya mbolea lakini mara zote mbolea hii inafungwa katika kifungashio cha kilo 50. Wapo Watanzania ambao maeneo yao ni madogo, wapo Watanzania ambao pia kipato chao ni kidogo na wangetamani kununua mbolea katika uwezo wao wa kipato na kimaeneo.

Je, Serikali iko tayari kutoa mwongozo ili mbolea ianze kufungwa katika vifungashio vya kuanzia labda kilo tano, kumi, ishirini na hadi hamsini? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mbunge wa Mlalo kule Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwa ushauri wake kwa Serikali kwamba tunao wakulima wanaolima kwa viwango tofauti kilimo cha maeneo madogo madogo, heka moja, mbili au nusu heka au bustani na wako wanaolima ukubwa wa kati na mashamba makubwa.

Mheshimiwa Spika, mbolea tuliyonayo sasa ni ile ya kilo 25 na kilo 50 ambayo ni nyingi kwa wale wanaotaka kulima bustani ndogo, na kwa kuwa huu ni ushauri na leo Wizara ya Kilimo inawasilisha bajeti yake hapa, basi Wizara imesikia itachukua kama moja ya michango ya Waheshimiwa Wabunge kwa ushauri kwa Serikali na watakapokuwa wanahitimisha bajeti yao ya Wizara ya Kilimo na hili nalo litakuwa ni moja kati ya ufafanuzi utakaotolewa na Wizara.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunalichukua na tunalifanyia kazi kupitia Wizara ya Kilimo, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Samweli Hhayuma Xaday, Mbunge wa Hanang.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, Mheshimiwa Waziri Mkuu, nchini kwetu tuna baadhi ya mashamba makubwa ambayo yanamilikiwa na Serikali, lakini mengine ni Taasisi za Serikali, tuna mashamba mengine yamebinafsishwa lakini mengine yako kwa wawekezaji, mengi ya mashamba hayo utakuta hayatumiki ipasavyo na tija haionekani, katika maeneo hayo kuna wakulima ambao hawana mashamba.

Je, Serikali ina kauli gani ili hayo mashamba yaweze kutumika kwa tija, wakati huo huo tukiangalia maslahi ya wawekezaji pia tukiangalia hitaji la ajira kwa vijana wetu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hhayuma, Mbunge wa Hanang, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ninakiri kwamba tunao wawekezaji tulishawapa mashamba makubwa, miongoni mwao hawakutekeleza kuyatumia tena kuyatumia kwa malengo yaliyokusudiwa. Mheshimiwa Mbunge anakumbuka nilifanya ziara kwenye Wilaya yake ya Hanang na tulitembelea eneo linaitwa Bassotu ambako pia wanalima mashamba makubwa ya mpunga. Wawekezaji wa aina ile

pale Bassotu walilenga kuzalisha mpunga mwingi na maeneo mengine ngano.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na malalamiko ya wananchi tulipotembelea kwenye eneo lile wakisema kuwa mashamba yamebaki wazi na wawekezaji hawajaendeleza.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali kwa mashamba yote makubwa ambayo leo hii hayatumiki kwanza tunafanya tathmini ya mashamba yote makubwa nchini ambayo wawekezaji tuliwapa kwa malengo maalumu na kwa mikataba, tunapitia mikataba ile, tunapitia malengo ya mikataba ile na utekelezaji wa mikataba ile.

Mheshimiwa Spika, ninakiri kwamba baadhi ya wawekezaji wengine wameshindwa kuyatumia maeneo haya na wananchi wanatamani kwenda kuyatumia, Serikali tunazo sheria ambazo pia zinaongoza mikataba tuliyoiweka ya mtu yeyote ambaye tulimpa kwa ajili ya uwekezaji na ameshindwa kutekeleza, kupitia majadiliano yetu tunampa nafasi ya kujadiliana na Serikali kama mwekezaji na kama ambavyo umesema bila kuathiri uwekezaji, tunampa nafasi, kama ameshindwa kabisa mashamba hayo yote tunayarudisha na kuyatangaza upya kwa wawekezaji ambao wana nia ya kuwekeza.

Mheshimiwa Spika, pale ambapo hatupati wawekezaji pia kuna wananchi wanahitaji tunapeleka kwenye mamlaka za eneo hilo kwa maana ya halmashauri na vijiji waweze kutumia pia mashamba haya kama fursa ya kuendeleza kilimo chao. Najua pia kuna mashamba ambayo wawekezaji wamewekeza hawajayatumia, lakini amekwama na taratibu tu za kupata labda mikopo, vifaa na bado ana miaka mitatu, minne hajalima, huyu tunazungumza naye ili atoe fursa kwa wananchi walioko jirani kutumia angalau kwa muda kwa mazao yasiyo ya kudumu ili wananchi nao waweze kunufaika.

Mheshimiwa Spika, natambua Halmashauri ya Hanang ilikaa pamoja na yenyewe ikapata mgao wake na wananchi wanaotamani eneo lile nao pia wanataka wapate fursa ya kulima, majadiliano bado yanaendelea na Wizara ya Kilimo inaendelea

kuratibu na kusimamia eneo lile. Hii sasa ni pamoja na maeneo mengine yote makubwa na hatua hizi za Serikali za kuchukua mashamba ambayo yameshindikana kwenye uwekezaji ambao tumekubaliana.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wenye maeneo makubwa kama hayo, tutaendelea na utaratibu wetu wa kufuata sheria, lakini na mikataba tuliyoiweka ili tuweze kuyarejesha mashamba haya tuweze kuwagawia wananchi ambao wanaweza kuyatumia vizuri pia kumpa mwekezaji anayeweza kutekeleza masharti ambayo tumemwekea kwenye mashamba hayo.

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo majibu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, mnamo tarahe 28 Aprili, 2024 ukiwa kwenye mbio za watoto wenye usonji ulitangaza kwamba Daraja la Tanzanite litafungwa kuanzia saa 12.00 asubuhi mpaka saa 3.00 asubuhi kwa ajili ya kupisha mazoezi kwa wananchi wetu.

Je, Serikali ina mkakati gani wa dhati kwa mikoa mingine yote nchini kuhakikisha zoezi hili linaenda sambamba na tamko lako la Jijini Dar es Saalam ili kukabiliana dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza kwa Watanzania?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kunti Majala, Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli tarehe 28 Aprili, 2024 siku ya Jumamosi tulikuwa na mbio za marathoni Jijini Dar es Salaam zinazolenga kuchangia fedha kwa watoto wenye tatizo la usonji

lililodhaminiwa na mama mwenye mtoto mwenye tatizo hilo la usonji. Uzoefu wetu na kwa mujibu wa taarifa za Wizara ya Afya ambazo pia Waziri wa Afya Mheshimiwa Ummy Mwalimu tulikuwa naye alipokuwa anatoa taarifa alionesha kwamba Taifa letu kwa sasa Watanzania wengi wanakabiliwa na magonjwa yasiyoambukiza yanayotokana na mtindo wa kuishi pia kutoshughulisha miili yetu na tatizo hili limekuwa kubwa nchini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ushauri wa wataalamu mbalimbali tumeanza kushuhudia watu au makundi yakianzisha mifumo ya kufanya mazoezi ya pamoja, lakini pia mtu mmoja mmoja na wanafamilia tunakutana nao wakifanya mazoezi ya viungo. Kwa sasa Jiji la Dar es Salaam linaongoza kuwa na vikundi vingi sana kila wilaya vya mazoezi. Tuna vikundi Temeke vya *jogging*, tuna vikundi Ilala, tuna vikundi Kinondoni, Ubungo na Kigamboni na nimeanza kuona pia hata Waheshimiwa Wabunge wakiunga mkono vikundi hivi kwa kuvinunulia sare na kuvihamasisha kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ipo motisha inaanza kuja, upo umuhimu na upo uelewa unaanza kuja, Watanzania wanajua umuhimu wa kufanya mazoezi. Sasa ni jukumu letu Serikali kuweka utaratibu mzuri wa kuwawezesha Watanzania kwenye maeneo yao kufanya mazoezi na kuushughulisha mwili ili kuepukana na magonjwa yasiyoambukiza.

Nashukuru pia hata Mheshimiwa Spika wewe, umeanzisha marathoni kwa Waheshimiwa Wabunge, kila mwezi Juni tunakuwa na siku moja nzuri, lakini pale ambapo inakupendeza na wewe pia una mshindano yako kule Mbeya na wiki ijayo tutakuwa Mbeya kwa ajili ya marathoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni mfumo mzuri ambao pia Wizara ya Afya imekuwa ikisisitiza kwa ajili ya afya ya Watanzania. Kwa kuwa Jiji la Dar es Salaam lina makundi mengi na tunaona wanazagaa barabarani, tumeona ipo dalili tunaweza tukapata tatizo la wale wafanya mazoezi kupata ajali na msongamano wa magari wa Jiji la Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeona ni muhimu tuanze na Jiji la Dar es Salaam kupanga siku moja ya kufanya mazoezi kwa angalau kwa saa tatu kuanzia saa 12.00 asubuhi mpaka saa 3.00 asubuhi ili Watanzania wote, wanafamilia, mtu mmoja mmoja au makundi, yakutane kwenye njia ile ya ufukwe wa bahari kutoka *Coco beach* kupitia Daraja letu pendwa la Tanzanite, kufika Aga Khan na ile barabara ya kwenda *Ocean Road* pale *junction*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara hii iliyoko kwenye fukwe, itumike kama eneo la mazoezi kwa siku ya Jumamosi kuanzia saa 12.00 mpaka saa 3.00 asubuhi ili kila mmoja kwa umbali anaoutaka yeye mwenyewe, kwa aina ya mazoezi anayoyataka yeye mwenyewe, awe huru na kusiwe na mwingiliano na magari. Kwa kuwa siku za Jumamosi asubuhi kunakuwa hakuna msongamano wa magari, bado wana nafasi wale wachache watakao kuwa wana shughuli kupita na kutumia barabara nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunaanza kuzindua mazoezi hayo Jumamosi ya keshokutwa na mimi nitakuwepo pale, Waziri wa Afya atakuwepo pale. Tutakapokuwa tunaanza zoezi hili, tutahakikisha hatukwazi wale wote wanaotaka kusafiri kwenda katikati ya Jiji kwa sababu tuna barabara nyingi tu ambazo zinafika katikati ya Jiji kwa wakati huo na ziko huru. Pia tunatoa mianya ya kila Mtanzania kuanza mazoezi kwa siku hizo na kila Jumamosi kwake iwe ni siku nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeamua barabara hii kwa sababu tuna fursa ya kutunza magari, yeyote anayetoka mbali, anatoka Ubungo, anatoka Temeke, anatoka Kigamboni, anaweza kuja na gari yake, akafika viwanja vya gymkhana, aka-*park* gari, akaingia barabarani kufanya mazoezi, akimaliza anachukua gari, anarudi. Pale Agha Khan kuna eneo la ufukwe, tunaweza kuweka magari, mtu anaweka gari lake, anaingia barabarani anafanya mazoezi kwa uhuru wake na kwa umbali anaoutaka yeye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia huku Oysterbay kuna eneo la farasi ambalo ni la wazi, nalo pia litatumika kwa kuegesha magari.

Wanaingia barabarani, wanafanya mazoezi kwa umbali wanaoutaka wao. Pia palepale *Coco beach* nako kuna eneo pale ambalo asubuhi hakuna biashara zaidi ya maandalizi, nako panafaa kutunza magari na watu kuwaruhusu kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa kuwa tunaanza zoezi hili, aina ya vyombo vya usafiri vitakavyotumika kwenye njia hizi ambavyo vinaweza kuruhusiwa, labda *ambulance* imebeba mgonjwa wa dharura, inaweza kupita kwa sababu yenyewe ina alama au gari la zimamoto kama kuna dharura tutaruhusu, lakini pia kama gari ya *TANESCO* kumetokea tatizo lolote lile na wanataka kwenda kutatua, haya yanaruhusiwa pamoja na baiskeli ambayo inatumika kwa ajili ya mazoezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vyombo hivyo ndivyo vinavyoruhusiwa kwenye eneo hilo na naliagiza Jeshi la Polisi kusimamia eneo hili ili kuona kuwa hakuna mwingiliano wa watu na magari ya abiria. Waheshimiwa Wabunge, wote naamini mmesafiri kwenye nchi za wenzetu, tumeona nchi nyingi wanafunga maeneo kwa ajili ya kutoa fursa za jamii yake kufanya mazoezi. Wakati mwingine hata burudani tu siku ya Jumapili kuanzia saa 4.00 asubuhi mpaka 12.00 jioni barabara inafungwa kuruhusu watu kufanya shughuli zao za kijamii na sisi tunaanza na Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nini wito kwa mikoa mingine? Natoa wito kwa Wakuu wa Mikoa kuanza zoezi kama hili kwenye maeneo yao. Wafanye tathmini ya maeneo mazuri kufanya mazoezi, lakini siyo lazima kufunga barabara, inategemea na mazingira ya maeneo hayo. Unaweza kuandaa uwanja wakakutana hapo na wakafanya mazoezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo hili litawezesha pia Watanzania kuwa na afya njema na siku hiyo ya Jumamosi, Mheshimiwa Waziri wa Afya atatoa taarifa yake, msisitizo wake na hamasa yake ili Watanzania wote tushiriki katika mazoezi ya viungo kwa ajili ya kuepukana na magonjwa yasiyoambukiza.

Mheshimiwa Spika, haya ndiyo maelezo ya swali hilo, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Hao ndiyo Waheshimiwa Wabunge waliokuwa wameonesha nia ya kukuuliza maswali. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, kulikuwa na swali hapa linalohusu wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki ya wakati huo halafu ikavunjika.

Sasa hili swali huwa linakuja, linarejea, linakuja, linarejea, mimi ninafikiri upande wa Serikali ukaangalie kwenye nyaraka zake, je, wapo wanaodai? Kwa sababu nyaraka za waajiriwa wa kipindi hicho zipo, watazamwe, wote walishalipwa? *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama wapo wanaodai, walipwe kwa sababu haya maswali yanaendelea kurejea na wengine huenda walifariki na haki zao zipo na wengine huenda wapo, wanajipa moyo kwamba kuna wanachodai kumbe hakuna. Bora mtazame ili mje mseme hakuna anayewadai ili Mheshimiwa Mbunge anavyofuatwa na hao wastaafu, aseme kwamba Serikali imesema kwamba hakuna anayedai au Serikali kipindi hiki mjipe muda kwamba mnatazama hizo. Mje mliseme liishe kwa sababu hii Jumuiya ilikufa siku nyingi, hii ni mpya tuliyonayo sasa. Sasa hao watu ni wazee sana kuendelea kuanza kudai haya madai. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Maswali ya Kawaida.

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, Mbunge wa Viti Maalum.

Subiri Mheshimiwa, nilikuwa namwangalia Mheshimiwa Waziri wa Nchi hapa wa Utumishi, ananionesha kwamba ni mimi ndiyo najibu. Kwa hiyo, ngoja nikuite vizuri.

Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 217

**Idadi ya Wafanyakazi wa Ndani Nchini**

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI** aliuliza: -

Je, kuna wafanyakazi wangapi wanaofanya kazi za ndani nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Utafiti wa Watu wenye Uwezo wa Kufanya Kazi Nchini wa mwaka 2020/2021 *(Integrated Labour Force Survey –2020/2021)* unaonesha kuwa kuna jumla ya wafanyakazi 216,429 wanaofanya kazi za ndani ambapo kati ya hao, wanaume ni 64,776 na wanawake ni 151,653.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maryam Mwinyi, swali la nyongeza.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali na idadi ya utafiti ambao umefanywa mwaka 2021. Ili kulinda haki za wafanyakazi majumbani; je, Serikali ina mkakati gani wa kuridhia Mkataba wa *C189* ili kuondoa changamoto za wafanyakazi hao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa tayari *VETA* ina mtaala wa wafanyakazi majumbani; je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha elimu hiyo inawafikia wafanyakazi hao? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, kuhusu hatua za Serikali kurasimisha kama inaweza kuwa lugha nzuri ya Kibunge, ule Mkataba Na. 189 wa Haki za Wafanyakazi wa Nyumbani, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako kuwa hatua za kimsingi zimekwishakamilika ikiwemo hatua za mwanzo kabisa kama Bunge lako lilivyoelekeza za kutoa elimu kwa waajiri, wafanyakazi wa ndani na kile Chama cha Waajiri.

Mheshimiwa Spika, pia maelekezo yako ya kwamba elimu itolewe kwanza ili baada ya elimu kutolewa, basi mkataba huo uletwe Bungeni kwa ajili ya hatua zinazofuatia. Nataka kuliambia Bunge lako, hata jana Mheshimiwa Makamu wa Rais wakati anahutubia wafanyakazi katika kilele cha Siku ya Wafanyakazi Duniani, alieleza juu ya hatua sasa zimekwishakamilika na Serikali iko

katika hatua za mwisho za kuleta mkataba huo Bungeni ili tuweze kuupitisha.

Mheshimiwa Spika, juu ya Chuo cha *VETA*, mkakati gani Serikali inao kuhakikisha kwamba elimu hiyo inafika. Nataka kulihakikishia Bunge lako, lakini pia kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba *VETA* katika utaratibu wake wa mitaala yake na matangazo yanayoendelea kupitia vyanzo mbalimbali, mitandaoni na kwenye *social media* tutaendelea kuuhabarisha umma juu ya uwepo wa programu hizi ili wananchi wale wanaotaka kujiunga, watumishi wetu wa ndani wanaotaka kujiunga, waweze kujiunga katika utaratibu huu ili waweze kupata elimu kama ambavyo inatakiwa kupatikana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, wafanyakazi wengi wa nyumbani wanapitia changamoto mbalimbali hasa unyanyasaji na kukosa haki zao; je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba wafanyakazi hawa wanalindwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka mikakati mingi, mojawapo ikiwepo ni ufunguzi wa ma-*desk* yanayojadili au yanayopokea taarifa za watu wote ambao wanapata manyanyaso katika sehemu za kazi. Katika kufanya hili, Serikali imeendelea kupokea taarifa mbalimbali na baadhi ya watu ambao wanawanyanyasa watumishi wa ndani wamefikishwa mpaka kwenye vyombo vya sheria ikiwemo mahakamani na baadhi ya kesi zinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na kuwaambia Watanzania kwamba wale wote ambao wanahisi kunyanyaswa katika maeneo yao ya kazi hasa hii kada ya watumishi

wa ndani, basi watoe taarifa katika maeneo husika ili Serikali iweze kuchukua hatua stahiki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa waajiri wa wafanyakazi wa ndani wako wengi na wanatofautiana kimapato; je, nini kima cha chini cha mshahara kwa wafanyakazi wa ndani? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, narejea maelezo ya jana ya Mheshimiwa Makamu wa Rais alipokuwa anahutubia watumishi au wafanyakazi katika kilele cha Siku ya Wafanyakazi Duniani, alieleza na ninaomba ni-*quote* mbele yako. Mheshimiwa Makamu wa Rais alieleza, kwanza hatua za Serikali zinazofanyika ku-*rectify* huu mkataba ambao sasa hivi ndiyo tumeueleza katika swali la msingi lililoulizwa na Mheshimiwa Maryam Mwinyi.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine Mheshimiwa Makamu wa Rais alieleza juu ya Serikali kuendelea kutambua juu ya haki za msingi ambazo wafanyakazi wa ndani wanazo. Katika kuhakikisha kwamba jambo hilo linasimamiwa vizuri, ametoa maelekezo kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu inayosimamia Kazi na Ajira kwamba jambo linalohusu wafanyakazi wote ikiwemo wafanyakazi wa ndani, lazima liwe ni jambo la msingi la kuangaliwa na wafanyakazi hao lazima wapewe haki zao zinazostahili.

Mheshimiwa Spika, juu ya kima cha chini, Serikali haijatoa bado kima cha chini cha wafanyakazi hawa wa ndani. Ni makubaliano yao wenyewe kwa sababu tasnia hii ya wafanyakazi wa ndani ndiyo sasa tunakwenda kuirasimisha ili iweze kumpa utu huyu mfanyakazi wa

ndani anayefanya kazi za kumsaidia mwenye nyumba wake, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa sababu ameuliza swali mahususi na nadhani huwa kuna mkeka ule mnatengeneza kwamba wafanyakazi kwenye kada hii, ngazi hii, ngazi hii, nadhani na watumishi wa nyumbani kuna mahali ambapo wanaingia. Kwa hiyo kwa sababu ameuliza swali mahususi kwamba ni kiasi gani wanapaswa kulipwa, ni muhimu apewe majibu ili wale wafanyakazi wa ndani wanaolipwa tofauti na hiyo, wajue haki zao. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama vile alivyosema waende mahali wakaseme, basi wakaseme mimi huwa nalipwa pungufu ya hii. Kwenye ule mkeka nadhani na wao wapo mahali ambapo wanaweza kuingia kama watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba, sasa aulize swali lake.

Na. 218

**Kukamilisha Ujenzi wa Bwalo Shule ya Sekondari Nanyamba**

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha ahadi yake ya ujenzi wa bwalo katika Shule ya Sekondari Nanyamba ili iwe kidato cha tano na sita?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Zainab Athman Katimba, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, mwaka 2018/2019 Halmashauri ya Mji wa Nanyamba ilitenga shilingi milioni 60 kwa ajili ya ujenzi wa bwalo katika Shule ya Sekondari Nanyamba na mwaka 2021/2022 ilitenga shilingi milioni 40. Ujenzi wa bwalo hilo umefikia hatua ya umaliziaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali itatenga fedha za ukamilishaji wa bwalo hilo na ujenzi wa miundombinu mingine kadiri ya upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kuipandisha hadhi Shule ya Sekondari Nanyamba kuwa kidato cha tano na sita utafanywa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri kwa kuomba kibali Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia baada ya miundombinu hitajika kukamilika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa Serikali iliahidi kutoa fedha za ukamilishaji wa ujenzi huu wakati wa ziara ya Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI; je, ni lini Serikali itatoa fedha hizo?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kwa kuwa shule hii ina miundombinu yote ambayo inafaa kuanza kusajili wanafunzi wa kidato cha tano isipokuwa mabweni tu; je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kutoa fedha kwa haraka ili shule hii sasa ianze kusajili watoto au wanafunzi wa kidato cha tano? Nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Serikali kufanya ziara kupitia Mheshimiwa Naibu Waziri kuja kuona miundombinu ile na kuahidi kuleta fedha, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari Serikali imepokea maombi hayo na tayari inayafanyia kazi. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwa kadri ya upatikanaji wa fedha, bwalo hilo litaweza kujengwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali la pili la Mheshimiwa Mbunge, namhakikishia kwamba Serikali inafahamu umuhimu wa kuwa na bwalo hilo na miundombinu mingine muhimu inayohitajika kwa ajili ya shule hiyo kusajiliwa kuwa kidato cha tano na sita. Kwa hiyo, Serikali itaendelea kufanya jitihada za dhahiri kabisa kuhakikisha fedha zinapatikana kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu hiyo hitajika ili shule hiyo iweze kupandishwa hadhi kuwa kidato cha tano na cha sita. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mliosimama nimewaona. Moja kwa moja kwenye swali, ukisema swali refu nakukata, namwita anayefuata na usikasirike kwa sababu mmesimama wengi.

Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, swali la nyongeza.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itajenga bweni kwenye Shule ya Sekondari Kimnyaki ili kuondolea watoto wa kike athari ya hatari ambao ni wengi kwenye shule hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa kuwa na mabweni katika

shule zetu na Serikali kupitia miradi tofauti tofauti, imekuwa ikitoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya mabweni. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, Serikali itaendelea kuwashirikisha wananchi kupitia halmashauri, kuweza kujenga hosteli, lakini pia Serikali kupitia miradi yake itaendelea kujenga mabweni hayo ili iweze kuwasaidia wanafunzi waweze kupata mabweni.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, swali la nyongeza.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, ni lini Serikali itajenga bwalo na uzio katika Shule ya Sekondari ya Kizwite, Mkoani Rukwa, Sumbawanga Mjini? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na mabwalo, lakini pia na uzio. Serikali kupitia halmashauri itaendelea kutenga fedha kupitia mapato ya ndani kwa ajili ya kuhakikisha miundombinu hii muhimu inajengwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, Serikali iliahidi kujenga bwalo na kuanzisha kidato cha tano na cha sita katika Shule ya Sekondari ya Saashisha; je, ni lini Serikali itaanza kazi hii?

**SPIKA:** Sasa hayo maelezo ya mwanzo ulitoa ya nini? Uliza swali moja kwa moja.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itajenga bwalo katika Shule ya Sekondari ya Saashisha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kwa kadiri ya

upatikanaji wa fedha nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itajenga bwalo katika shule hii ya Saashisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa, Mbunge wa Handeni Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 219

**Ujenzi wa Miundombinu ya Shule za Sekondari Handeni**

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga bwalo la chakula, majengo ya utawala na mabweni ya wanafunzi katika Shule za Sekondari Misima na Handeni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa uwepo wa miundombinu mbalimbali ikiwemo majengo ya utawala, bwalo na mabweni katika shule za sekondari. Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali kupitia Mradi wa *EP4R* imetoa shilingi milioni 130 za kujenga bweni moja katika Shule ya Sekondari Handeni ambalo lipo kwenye hatua ya umaliziaji.

Mheshimiwa Spika, aidha, mwaka 2023/2024 Serikali kwa kushirikana na Kampuni ya Barrick Tanzania imetoa shilingi milioni 432 kwa ajili ya kujenga mabweni mawili, madarasa sita na matundu kumi ya vyoo katika Shule ya Sekondari Misima.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwenye bajeti kwa ajili ya kuendelea kujenga miundombinu ya bwalo na mingine katika shule za sekondari nchini zikiwemo Shule za Sekondari Misima na Handeni.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kwagilwa Reuben, swali la nyongeza.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, kwa kuwa shule hizi mbili zote zina maabara moja moja na zina michepuo ya sayansi na hivyo wanafunzi wanalazimika kufanya kwenye maabara moja masomo yote matatu; je, ni lini Serikali itatuletea fedha kwa ajili ya kujenga maabara za *chemistry, physics* na *biology* kwenye shule hizi mbili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa shule hizi zina kidato cha tano na cha sita ambao wanaishi katika mabweni, lakini hawana mabwalo na wala shule zenyewe hazina majengo ya ofisi za utawala; je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kutupatia fedha kwa ajili ya kujenga mabwalo na ofisi za utawala kwenye shule hizi mbili? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali ya Mheshimiwa Mbunge yote mawili kwa pamoja; nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kutafuta fedha kupitia miradi yake, bajeti ya maendeleo ya mapato ya ndani ya Halmashauri pamoja na Serikali Kuu ili kujenda miundombinu hii muhimu, miundombinu ya jengo la utawala, mabwalo pamoja na maabara kama alivyoomba Mheshimiwa Mbunge kwa kadiri ya upatikanaji wa fedha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sharti la maswali mafupi linawahusu na wenye maswali ya msingi. Mheshimiwa Vita Kawawa, swali la nyongeza.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana; je, ni lini Serikali au Serikali inaweza kuanza kutuwekea bajeti kwa ajili ya kujenga mabweni na mabwalo katika shule zetu za sekondari katika Wilaya ya Namtumbo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua sana umuhimu wa miundombinu ya mabweni katika shule zetu za sekondari. Serikali imekuwa ikifanya jitihada kubwa sana kupitia miradi yake mbalimbali ili kuhakikisha kwamba inajenga mabweni hayo. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa kadiri ya upatikanaji wa fedha Serikali itaendelea kuhakikisha miundombinu hiyo muhimu katika elimu inapatikana na inajengwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itajenga mabweni katika Shule za Sekondari Labay na Dinamu katika Jimbo la Mbulu Vijijini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kupitia Bajeti ya Serikali Kuu, mapato ya ndani ya halmashauri na miradi iliyopo katika sekta ya elimu, Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba miundombinu hii muhimu inajengwa kwa kadiri ya upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, swali la nyongeza.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mpango mkakati gani wa kutuletea fedha za kujenga bweni la watoto wa kike kwenye Kata ya Tumbi, Manispaa ya Tabora?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kuwa Serikali inatambua

umuhimu mkubwa wa kuwa na mabweni katika shule zetu hizi na itaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa bweni katika shule aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itatuletea fedha za kujenga mabweni katika shule za sekondari zote katika Jimbo la Tunduru Kaskazini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kwa kadiri ya upatikanaji wa fedha na kwa kuzingatia vipaumbele Serikali inamhakikishia Mheshimiwa Mbunge italeta fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabweni katika shule alizozitaja katika jimbo lake.

**SPIKA:** Mheshimiwa Charles Kajege, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itajenga mabweni katika shule za sekondari zilizoko katika Jimbo la Mwibara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali inatambua umuhimu mkubwa wa ujenzi wa mabweni katika shule zetu za sekondari, hivyo itaendelea kuhakikisha kwamba inatafuta fedha kupitia miradi, mapato ya ndani ya halmashauri pamoja na Serikali Kuu kwa ajili ya kuhakikisha kwamba inajenga miundombinu hii munimu katika sekta ya elimu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, swali la nyongeza.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itamalizia ujenzi wa mabweni na mabwalo katika Jimbo la Iringa Mjini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu mkubwa wa miundombinu hii katika shule zetu, kwa maana ya mabwalo na mabweni Serikali itaendelea kutafuta fedha na kuhakikisha kwamba inajenga miundombinu hii muhimu kama alivyoomba Mheshimiwa Mbunge.

**SPIKA:** Mheshimiwa Timotheo Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, je, ni kwa nini Serikali haioni umuhimu wa kukamilisha mabwalo kwenye Shule za Bungu na Mnyuzi ambayo yalishaanza lakini hayajakamilika kwa sababu ya upungufu wa fedha? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa kwa kadiri ya upatikanaji wa fedha Serikali inakusudia kuja kujenga mabwalo haya katika shule yake.

**SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, Mbunge wa Morogoro Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 220

**Ujenzi wa Shule Maalum ya Sekondari ya Wasichana Dutumi**

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Shule Maalum ya Sekondari ya Wasichana Dutumi, Kata ya Bwakira, Morogoro Vijijini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita kupitia Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari *(SEQUIP)* inajenga shule 26 za bweni za wasichana za kitaifa katika mikoa yote nchini.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa shule hizi unafanyika katika mikoa yote nchini kwa awamu mbili, ambapo awamu ya kwanza ilihusisha mikoa kumi na awamu ya pili mikoa 16. Bajeti ya ujenzi wa shule hizi ni shilingi bilioni 4.1 ambayo inatolewa kwa awamu mbili ikiwemo awamu ya kwanza shilingi bilioni tatu na awamu ya pili bilioni 1.1.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeshatuma fedha katika mikoa yote nchini kwa ajili ya ujenzi wa shule za bweni za wasichana za mikoa ikiwemo shule ya Mkoa wa Morogoro inayojengwa katika Kata ya Bwakira, Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro.

Mheshimiwa Spika, shilingi bilioni tatu imekwishatumwa kwa ajili ya ujenzi wa shule hii na ujenzi upo katika hatua ya umaliziaji. Serikali inatarajia kutuma shilingi bilioni 1.1 kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha 2023/2024 ili kukamilisha miundombinu yote inayohitajika katika shule ya wasichana ya mkoa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Kalogeris.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya utawala katika Jimbo la Morogoro Kusini upande wa kata yana uhitaji wa zaidi ya sekondari

mbili na sehemu nyingine tatu ili kuwapunguzia watoto kutembea umbali mrefu kufuata elimu.

(a) Je, Serikali ina mpango gani katika kujenga shule nyingine za sekondari kwenye Kata ya Mvuha na Kata ya Bwakira Chini ili kuweza kuwanusuru watoto wetu kutembea umbali mrefu?

(b) Je, Serikali ina mpango gani katika kujenga nyumba za walimu pamoja na mabweni kwenye kata ambazo ziko pembezoni na ni milimani, mfano Kata za Kibogwa, Bwakira Juu, Singisa pamoja na Kibungo Juu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kwenye swali la kwanza la Mheshimiwa Mbunge naomba kumhakikishia kwamba kata alizozitaja tayari zipo katika awamu ya tatu ya mpango wa Serikali wa kujenga shule za sendondari katika kata. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba kabla ya mwaka huu wa fedha kwisha kwa maana ya 2023/2024 fedha zitakuwa zimeletwa kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi wa shule hizo alizozitaja Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la pili, Mheshimiwa Mbunge anauliza kuhusiana na ujenzi wa mabweni na nyumba za walimu, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari kwenye miradi ya elimu fedha zinatengwa na zinatoka kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu hii muhimu. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kutafuta fedha kuhakikisha inajenga miundombinu hii muhimu kama alivyoomba. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mbunge wa Busega, sasa aulize swali lake.

Na. 221

**Ujenzi wa Daraja Kata ya Lutubiga – Busega**

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga daraja linalounganisha Kijiji cha Lutubiga na Mwasamba – Busega?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kujenga daraja linalounganisha Kijiji cha Lutubiga na Mwasamba Busega. Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali kupitia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini *(TARURA)* imetenga shilingi milioni 360 katika bajeti yake kwa ajili ya ujenzi wa daraja hilo na kufungua barabara mpya kilometa 4.2 kwa kiwango cha changarawe ili kuunganisha Kijiji cha Lutubiga na Mwasamba.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TARURA* itaendelea kuhudumia miundombinu ya Halmashauri ya Wilaya ya Busega kulingana na upatikanaji wa fedha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, swali la nyongeza.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, wanafunzi wanaokwenda kusoma Mwasamba wanaotoka Lutubiga sasa wameshindwa kwenda kusoma Mwasamba kwa sababu ya daraja hili na imebidi tuwaombee kwenda kusoma shule ya mbali kidogo:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kuhakikisha kwamba sasa tunawaokoa wanafunzi ili kutengeneza sehemu hii waweze kwenda kusoma?

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kutengeneza barabara na madaraja yaliyoharibiwa na mvua katika Jimbo la Busega?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Mbunge yote mawili kwa pamoja na kwanza namhakikishia kuwa Serikali inatambua kwamba kutokana na changamoto tulizokuwanazo za mvua nyingi, miundombinu mingi ya barabara hizi imeharibika na Serikali inachukua hatua mbalimbali ikiwemo ya kuongeza bajeti. Kwa hiyo, bajeti ya *TARURA* imeongezeka na Mheshimiwa Rais ameongeza bajeti kutoka shilingi bilioni 275 na sasa bajeti ni shilingi bilioni 710. Pia fedha za bajeti ya dharura imeongezeka kutoka shilingi bilioni 21 na sasa ni shilingi bilioni 131. Hii yote inafanyika kama jitihada ya makusudi ya kuhakikisha kuwa kunapotokea mazingira ya dharura kama aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge Serikali inaweza kufika na kufanya ukarabati na kuhakikisha kwamba kunakuwa na mawasiliano katika barabara hizi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa jitihada hizi za Mheshimiwa Rais za kutenga bajeti, Serikali imepokea maombi yako na itayafanyia kazi kuhakikisha kwamba barabara hizi zinafikiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Njalu Silanga, swali la nyongeza.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Daraja la Mto Gamaloha Kata ya Nkuyu na Mwaswale litajengwa kama ilivyoahadiwa na Mheshimiwa Rais?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, ahadi za viongozi wakuu ikiwemo ahadi za Mheshimiwa Rais ni kipaumbele katika mipango ya Serikali. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa amekumbushia, tutaendelea kufuatilia kuhakikisha kwamba ahadi hii ya ujenzi wa daraja alilolitaja inatekelezwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe, Mbunge wa Kibiti sasa aulize swali lake.

Na. 222

**Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme Ruakule – Kibiti**

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa kituo cha kupoza umeme katika Kijiji cha Lungunga, Kata ya Ruakule – Kibiti?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, mradi wa ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Ruakule kilichopo katika Kijiji cha Lungunga, Kata ya Ruakule, Wilaya ya Kibiti Mkoa wa Pwani kinatarajiwa kujengwa wakati wa utekelezaji wa Mradi wa Gridi Imara Awamu ya Pili. Aidha, kwa sasa Serikali ipo kwenye hatua ya utekelezaji wa mradi kwa awamu ya kwanza ambapo miradi 27 inatekelezwa. Awamu ya pili ya Mradi wa Gridi Imara inatarajiwa kutekelezwa mwaka wa fedha 2026/2027.

**SPIKA:** Mheshimiwa Twaha Mpembenwe, swali la nyongeza.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza, lakini naomba kuweka rekodi vizuri kwenye *Hansard,* kile ni Kijiji cha Lungungu na ni Kata ya Ruaruke.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Serikali yaliyo mazuri na yenye matumaini nina maswali mawili ya nyongeza. Kumekuwa na katikakatika ya mara kwa mara kwa umeme katika Jimbo la Kibiti; je, Serikali ina mkakati gani wa kuwezesha kutatua tatizo hilo?

Mheshimiwa Spika, lakini la pili kumekuwa na upungufu *(low voltage)* katika Jimbo la Kibiti. Umeme unasafiri kutoka Mbagala unakuja Mkuranga ambapo kuna matumizi makubwa sana ya viwanda; je, Serikali ina mkakati gani wa kuwezesha kutatua tatizo hilo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwenye swali la kwanza kuhusiana na kukatika kwa umeme niwape pole wananchi wa Kibiti kutokana na changamoto hii. Hivi karibuni tumekuwa tuna mvua kubwa sana hali ambayo imesababisha changamoto kwenye miundombinu ya umeme hususani nguzo kulala na kuanguka na hivyo kusababisha waya kukatika.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa timu zetu ziko *site* kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunarekebisha miundombinu na kuondoa changamoto hii. Hata hivyo, suluhisho la muda mrefu ni kuweka nguzo za zege. Tayari tumekwishaagiza nguzo za zege 64,315 na Kibiti watanufaika.

Mheshimiwa Spika, na swali la pili linalohusiana na *low voltage,* tayari tumeanza utekelezaji wa mradi wa njia ya umeme kutoka Chalinze – Kinyerezi – Mkuranga pamoja na Vituo vya Kupooza Umeme vya Chalinze, Kinyerezi na Mkuranga kwa ajili ya kuboresha *voltage* kwa ukanda huo wakati tunasubiria utekelezaji wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Kibiti. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa

Mbunge kuwa mradi huu ukikamilika utaboresha umeme kutoka Mbagala – Mkuranga hadi Kibiti. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maluum, Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 223

**Kuleta Muswada wa Sheria ya Taaluma ya Ustawi wa Jamiii**

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA** aliuliza:-

Je, lini Serikali italeta Muswada wa Sheria ya Taaluma ya Ustawi wa Jamii ili kusimamia na kulinda taaluma hii na kuwepo watoa huduma wenye leseni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Mwanaidi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Wizara imepokea na kupitia maoni yaliyotolewa na wadau wa huduma za ustawi wa jamii. Aidha, hadi sasa Wizara imefanikiwa kuandaa Andiko Dhana ya Waraka uliowasilishwa Baraza la Mawaziri ikiwa ni hatua ya maandalizi ya sheria hiyo. Hivyo hatua hii ikikamilika muswada huo wa sheria inayopendekezwa utawasilishwa katika Bunge lako Tukufu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema andiko limepelekwa kwenye Baraza la

Mawaziri; je, ni lini watafanya haraka ili muswada huu uweze kufika Bungeni kwa kuwa ni kwa muda mrefu wadau wameomba, ni zaidi ya miongo miwili? Hilo ni swali la kwanza.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kada hii ya ustawi wa jamii ni kada inayofanya kazi muhimu sana katika jamii ya Watanzania ikiwemo kusaidia waathirika wa unyanyasaji wa kijinsia na mambo mengine mengi ambayo yanaathiri Taifa letu; je, ni lini mtaongeza idadi ya wafanyakazi kwa kuwa ni kada ambayo ina wafanyakazi wachache, chini ya 80%; ajira mpya zitakapokuja wao mtawaajiri wangapi ili kuweza kusaidia kadhia hii? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la kwanza, ni kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi, mara baada ya mchakato wa matayarisho ya sheria hii uliopendekezwa kukamilika basi muswada huu utawasilishwa katika Bunge hili Tukufu na kujadiliwa.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili Wizara tayari imeshaomba kibali kwa ajili ya maafisa hao wa ustawi wa jamii. Tutakapopata kibali hicho tutaajiri maafisa hao na kuwapeleka sehemu zote husika zinazohitaji maafisa hao kwani tunafahamu kwamba maafisa hawa ni muhimu katika jamii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, swali la nyongeza.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, ajira zinavyotolewa nchini mara nyingi wanaajiri maafisa maendeleo ya jamii. Mimi napenda kujua Serikali inataka kuifuta kada ya ustawi wa jamii au hizi kazi zao zote zinaendelea kwa pamoja? Kama ni ndivyo basi kada moja ifutwe iendelee na kada moja kati ya hizo yaani kada ya maendeleo ya jamii na kada ya ustawi wa jamii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, kada ya ustawi wa jamii ni muhimu sana kwa kuwa inafanya kazi zake kwa ajili ya kuhudumia jamii na kada ya maendeleo ya jamii inafanya kazi kwa ajili ya kuwaelimisha wananchi ili kuhakikisha kwamba wanafanya vyema katika maendeleo ambayo wanayapata katika jamii zetu. Kwa hiyo, kada zote ni muhimu na sisi kama Wizara tumeandaa na tumekwishaomba kibali cha kuajiri Maafisa Maendeleo ya Jamii na Maafisa Ustawi wa Jamii ili kuhakikisha wanafanya kazi zao kwa wakati, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Haya, ahsante sana. Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi, sasa aulize swali lake.

Na. 224

**Mfuko wa Kuimarisha Bei ya Mazao Nchini**

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanzisha Mfuko wa Kuimarisha Bei za Mazao ili kusaidia wakulima wa pamba na mazao mengine bei zinaposhuka?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa kilimo imeanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo kupitia Tangazo la Serikali Na. 22 la tarehe 20 Januari, 2023 (Sehemu ya Kanuni za Sheria ya Fedha ya mwaka 2022) baada ya kuidhinishwa na Waziri wa Fedha na Mipango kwa ajili ya kuchapwa kwenye Gazeti la Serikali. Mfuko huo umelenga kuchochea ukuaji wa maendeleo ya sekta ya mazao

ya kilimo, kufidia bei za mazao inaposhuka, kutoa ruzuku ya pembejeo za kilimo (mbolea, mbegu bora, viuatilifu), kuchochea uwekezaji katika shughuli za utafiti wa kilimo na kuwajengea uwezo wakulima, wasindikaji, maafisa ugani na watafiti wa kilimo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, swali la nyongeza.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na nina swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mfuko huu sasa umeanzishwa, ni lini sasa Serikali itaanza kufidia bei za mazao ya wakulima zinapoanguka?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Mashimba kwa kuendelea kulifuatilia jambo hili. Nikuhakikishie kuwa mfuko tayari umeshaanzishwa mwaka wa fedha 2022/2023 na jukumu ambalo tunalifanya sasa hivi Serikali ni kuandaa vyanzo vya mapato vitakavyowezesha huu mfuko uweze kufanya kazi muda wote. Panapotokea tatizo au changamoto yoyote ya kushuka kwa bei, Serikali imekuwa iki-*interfere* kama ambavyo tulifanya katika mwaka wa fedha 2019/2020 katika zao la pamba ambapo Serikali ilitoa zaidi ya shilingi bilioni 100.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, ningependa kufahamu Serikali imejipangaje kutafuta soko la uhakika la zao la mahindi kwa mwaka huu kwa sababu wamevuna kwa wingi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ni kwamba katika jambo ambalo tuwaondoe hofu wakulima ni kwamba Serikali sasa hivi tunaweza tukasema tuna faida moja kubwa. Nchi jirani kwa mfano nchi ya Zambia, Malawi zote zimeshaomba kufanya biashara ya soko la mahindi na Tanzania. Kwa hiyo, maana yake mazao ambayo yanazalishwa na wananchi tuna uhakika wa soko na tutaendelea kufanya hivyo kwa kupanua wigo zaidi katika nchi nyingine.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Santiel Eric Kirumba, sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 225

**Changamoto ya Ajira kwenye Miradi ya Kimkakati - Shinyanga**

**MHE. SANTIEL E. KIRUMBA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua changamoto ya ajira kwenye miradi ya kimkakati ya *SGR* na *ECOP* kwa Mkoa wa Shinyanga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa David Kihenzile, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, mikataba ya ujenzi wa reli ya *SGR* imezingatia uwepo wa kipengele cha uwiano wa ajira ya wazawa na wageni. Aidha, mradi wa reli wa *SGR* ni mradi wa Watanzania wote ambapo pamoja na kuifungua nchi kiuchumi, umeendelea kutoa ajira kwa Watanzania wenye sifa kwa kuzingatia mahitaji ya mradi. Hadi kufikia Machi, 2024 mradi wa *SGR* umetoa jumla ya ajira zaidi ya

30,176 za moja kwa moja kwa Watanzania na ajira zaidi ya 150,880 zisizo za moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwezi wa Februari na Machi, 2024 wafanyakazi wazawa ambao walikuwa wameajiriwa kwenye mradi wa *SGR* kipande cha tano (Mwanza – Isaka) walikuwa 6,826, kati ya hao wafanyakazi 2,070 wanatoka katika Mkoa wa Mwanza, 1,387 wanatoka Mkoa wa Shinyanga, 365 wanatoka katika Mkoa wa Tabora, 376 kutoka Mkoa wa Simiyu na 2,628 kutoka mikoa mingine ya Tanzania kwa pamoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Santiel Eric Kirumba, swali la nyongeza.

**MHE. SANTIEL E. KIRUMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali, kwa jinsi inavyoonesha kwa takwimu za Mheshimiwa Naibu Waziri…

*(Hapa Mbunge alipita katikati ya Mzungumzaji na Spika)*

**SPIKA:** Mheshimiwa rejea kwenye kiti chako, anayeuliza swali yupo nyuma yako. Uliyehama kiti rejea kwenye kiti chako anayeuliza swali yupo nyuma yako.

Mheshimiwa Santiel, swali la nyongeza.

**MHE. SANTIEL E. KIRUMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali, Mheshimiwa Naibu Waziri umeelezea kwamba kwa kipindi cha kuanzia Februari hadi Machi, 2024 kwa Mkoa wa Shinyanga ni watu 356 wameweza kupata ajira katika reli hii ya *SGR,* lakini ajira hizi zimekuwa zikitolewa kimtandao, nini kauli ya Serikali kuhakikisha ajira hizi zinafika kwenye ngazi ya chini ili watu wengi waweze kupata fursa hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Serikali imewekeza pesa nyingi sana katika *MGR* na *SGR* hasa Serikali hii ya Awamu ya Sita, ni lini utekelezaji huu utakamilika ili kuweza kutatua changamoto ya ajira,

kwa sababu Watanzania wengi wana kiu hasa Mkoa wetu wa Shinyanga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza tuseme tunapokea changamoto na ushauri, kwa sababu Mheshimiwa Mbunge anaelezea changamoto kubwa ambayo wanaipata wananchi katika kupokea matangazo kwa mfumo wa mtandao, hivyo tunaielekeza Mamlaka ya Reli *(TRC)* kuhakikisha kwamba inaboresha kwa kusimamia wakandarasi walio chini yake mfumo wa matangazo ili Watanzania wengi waweze kufahamu na hatimaye kunufaika na ajira zinazotolewa kwenye miradi yetu hii ya kisekta.

Mheshimiwa Spika, pili, Mheshimiwa Mbunge anataka kufahamu mpango na lini tutakamilisha ujenzi wa reli katika Taifa letu. Mpaka tunapozungumza hapa, Taifa letu limeweka rekodi ya kipekee ya ujenzi wa reli *(MGR* na *SGR)* katika hatua tofauti. Kipande cha kwanza cha kutoka Dar es Salaam kinachokwenda mpaka Morogoro – Makutupora – Isaka, kilometa 219 wakandarasi karibu maeneo yote wapo *site*.

Mheshimiwa Spika, juzi wewe mwenyewe ni shahidi na Mheshimiwa Mbunge tumeshaanza majaribio kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro na kutoka Morogoro mpaka Makutupora, ni maelekezo ambayo Mheshimiwa Rais aliyatoa kwamba Wizara ya Uchukuzi ihakikishe *SGR* inaanza kufanya kazi ifikapo mwezi Julai. Maelekezo hayo tayari yanafanyiwa kazi na utekelezaji unakamilika.

Mheshimiwa Spika, pia ukiacha hiyo, awamu ya pili tumeshaanza ujenzi na mkandarasi yupo *site* kutoka Tabora mpaka Kigoma kilometa 506 na tupo kwenye hatua za mwisho za manunuzi kutoka Uvinza mpaka Gitega ambako kuna machimbo ya Nickel.

Mheshimiwa Spika, kama haitoshi Serikali inao pia mpango wa kujenga wa *SGR* kutoka Mtwara mpaka Bambabay na Liganga na

Mchuchuma. Pia tupo kwenye hatua mbalimbali za ujenzi za kutafuta wakandarasi pamoja na uthamini wa kutoka Kaliua…

**SPIKA:** Haya ahsante sana, ameelewa tayari. Mheshimiwa Selemani Zedi swali la nyongeza.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, miradi ya *SGR* ina changamoto sana ya ajira hasa kwa wazawa ambao wako maeneo ya miradi ukilinganishwa na miradi ya bomba la mafuta; je, Shirika la Reli liko tayari kwenda kujifunza kwa wenzao wa *TPDC* ambao wanasimamia miradi ya bomba la mafuta na wana-*manage* vizuri suala la ajira kwa wazawa wa maeneo ya miradi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, tuko tayari.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako. Mheshimiwa Olelekaita, swali la nyongeza.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, bomba la mafuta linapita Kiteto karibu kilometa 117, hatuoni sana wananchi wa Kiteto wakiajiriwa pamoja na kwamba mnasema wazawa wapo. Ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha maeneo yanayopitiwa na miradi hii inakuwa na *quarter* ya kuajiri wale wanaotoka pale?

**SPIKA:** Sasa ameuliza mahususi kuhusu huko, nadhani unaniangalia kuashiria kwamba unayo majibu. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Zedi ametoka kupongeza mfumo mzuri huko, kwa hiyo, nafikiri hata yeye atapata fursa ya kukaa na Mheshimiwa Zedi ili pengine aone wenzake wakoje, lakini hata hivyo lije kama swali la msingi nitalifanyia kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, Mbunge wa Iramba Mashariki, sasa aulize swali lake.

Haya, sasa Wabunge wawili mmesimama, Mheshimiwa Ighondo Ramadhani kwa niaba.

Na.226

**Kudhibiti Tembo Waharibifu Mwangeza - Iramba**

**MHE. ABEID R. IGHONDO K.n.y. MHE. FRANCIS I. MTINGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaweka Kituo Kidogo cha Askari Wanyamapori Kata ya Mwangeza ili kudhibiti tembo wanaofanya uharibifu kila mara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dunstan Kitandula, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuchukua hatua za haraka katika kukabiliana na changamoto ya wanyama wakali na waharibifu kwenye maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Kata ya Mwangeza, Wilayani Mkalama. Mathalani, katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 doria takribani 27 zimefanyika kudhibiti matukio saba ya tembo na kiboko yaliyoripotiwa. Sambamba na jitihada hizo, Serikali kupitia *TAWA* imewapatia mafunzo maalum Askari Wanyamapori wa Vijiji wanne ambao wanafanya kazi ya kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu kwa kushirikiana na Askari Wahifadhi wa *TAWA* na Afisa Wanyamapori wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kujenga vituo vya askari kadiri rasilimali watu na fedha itakavyopatikana. Hivyo, nimuombe

Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi waendelee kutoa ushirikiano katika kukabiliana na changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu ikiwemo kutoa taarifa mapema ili kupunguza athari za wanyamapori wakali na waharibifu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ighondo Ramadhani, swali la nyongeza.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, sasa Serikali iko tayari kutoa fidia kwa madhara ambayo wamepata wananchi kutokana na uvamizi huu wa wanyamapori? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, katika Jimbo la Singida Kaskazini tunao Msitu wa Mgori ambao hivi sasa upo chini ya *TFS*. Wananchi wamekuwa wakiomba kuachiwa eneo la ukanda wa matumizi kwa ajili ya matumizi ya kijamii, je, Serikali sasa inasemaje kuhusu kuwapa wananchi eneo hilo la ukanda wa matumizi ili waweze kutumia kwa shughuli zao za kijamii? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri jibu swali la nyongeza la kwanza. Swali la nyongeza la pili litajibiwa kama swali la msingi maana halina uhusiano na swali la msingi. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutoa fidia kwa wananchi pale ambapo tunapata madai kutoka kwenye halmashauri zetu. Baada ya kufanya uthamini Serikali imekuwa ikiendelea kutoa fidia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, Serikali ina mkakati gani madhubuti wa kudhibiti wimbi kubwa la tembo ambalo linavamia makazi ya wananchi na kusababisha madhara mbalimbali kama vile kulemaza wananchi, mazao na vitu vingine tofauti na ujenzi wa vituo vya wanyamapori ambavyo mmeviweka? *(Makofi)*

**SPIKA:** Umeshaeleweka. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, maeneo mengi ambayo yamekuwa na changamoto ya uvamizi wa tembo ni maeneo ambayo wananchi wamekwenda kuvamia kwenye maeneo karibu na hifadhi, kumekuwa na shughuli nyingi za kibinadamu kwenye maeneo hayo. Vilevile yapo maeneo ambayo tembo wanatoka kwenye hifadhi zetu kwenda nje ya hifadhi kufatuta maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kupambana na changamoto hii, Serikali inao mkakati wa muda mfupi na muda mrefu wa kuondoa shoroba zetu ili shughuli za kibinadamu zisifanyike kwenye maeneo hayo. Vilevile kwa yale maeneo ambayo tembo wanatoka kwenye hifadhi kwenda nje kutafuta maji, tumekuwa na utaratibu wa kujenga mabwawa ndani ya hifadhi hizo ili kuepusha tembo kutoka nje ya hifadhi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali.

Waheshimiwa Wabunge mnaozungumza tusikilizane kwanza, nitaanza na tangazo la wageni kisha tutaendelea na matangazo mengine na ratiba iliyo mbele yetu.

Kwanza tutaanza na wageni walioko Jukwaa la Spika; wa kwanza kabisa ni wageni wa Mheshimiwa Hussein Bashe ambaye ni Waziri wa Kilimo na tutaanza na Ndugu Gerald.

Waheshimiwa Wabunge tusikilizane, Ndugu Gerald Mweli, *ndc* - Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, ahsante sana. *(Makofi)*

Wapo pia Dkt. Hussein Omar - Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Florens Turuka - Katibu wa Baraza la Kumshauri Rais Mambo ya Kilimo na

Chakula, Bwana Andrew Massawe - Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Baraza la Kumshauri Rais Mambo ya Kilimo na Chakula. *(Makofi)*

Yupo pia Mheshimiwa Balozi Mahmoud Thabit Kombo ambaye ni Balozi wa Tanzania nchini Italia na mwakilishi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sikilizeni kwanza utambulisho wake, ni Balozi Tanzania nchini Italia na Mwakilishi wa Kudumu wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa *(FAO),* Mpango wa Chakula Duniani *(WFP)* na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo *(IFAD),* karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia Ndugu Amos Makala, Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Mary Chatanda, Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania, ahsante sana. *(Makofi)*

Tunaye pia Ndugu Ally Hapi, Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wazazi Chama Cha Mapinduzi, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Mohamed Ali Kawaida, Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi, ahsante sana. *(Makofi)*

Sasa hawa waandishi wa leo wamechanganya itifaki hapa, kwa hiyo wageni mvumilie kidogo, wote mtatajwa lakini muamini kwamba mmetajwa kwa nafasi zenu siyo kwa maana ya namna mlivyotajwa hapa mbele.

Yupo Ndugu Fadhili Maganya, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Chama Cha Mapinduzi Tanzania, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye Ndugu Rehema Sombi - Makamu Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Pia yupo Ndugu Jokate Urban Mwegelo - Katibu Mkuu, Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi, ahsante sana. *(Makofi)*

Tunaye Ndugu Musa Mwakitinya - Naibu Katibu Mkuu, Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi, Bara. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Paul Israel - Mwakilishi wa Naibu Katibu Mkuu Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi, Zanzibar, ahsante sana. *(Makofi)*

Natafuta nimalize viongozi wa Chama Cha Mapinduzi halafu nianze wengine.

Haya mwingine wa Chama Cha Mapinduzi ni Dkt. Frank Hawesi - Katibu wa *NEC,* Uchumi na Fedha wa Chama Cha Mapinduzi, haya ahsanteni sana. *(Makofi)*

Yupo Askofu Benson Bagonza, Askofu Dayosisi ya Karagwe – KKKT, haya ahsanteni sana. *(Makofi)*

Tunaye Ndugu Ludovick Lyimo, Katibu Mkuu Dayosisi ya Dodoma – KKKT, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Sheikh Mustafa Rajab Shaabani, Sheikh Mkuu wa Dodoma, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo *Fr*. Chesco Peter Msaga ambaye ni Naibu Katibu Mkuu *TEC,* karibu sana. *(Makofi)*

Pia tunao Ndugu Peter Oldhom - Mwakilishi wa *EU,* Ndugu Frank Nyabundege - Mtendaji Mkuu wa *TADB* na Ndugu Abdul Majid Nsekela - Mtendaji Mkuu *CRDB*, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Theobald Sabi - Mtendaji Mkuu wa *NBC,* Ndugu Filbert Mponzi - *Chief Retail Banking NMB,* Ndugu Christopher Mwalugenge - Mkuu wa Kitengo cha Kilimo Wateja Wakubwa *NMB,* Ndugu Fredrick Nshekanabo - Afisa Mkuu wa Fedha *CRDB Bank* na

Ndugu Fulgence Bube - Mkurugenzi wa *Mtibwa Sugar,* karibu sana. *(Makofi)*

Mgeni mwingine ni Dkt. Mwatima Juma ambaye ni Mjumbe wa Baraza la Kumshauri Mheshimiwa Rais katika Masuala ya Kilimo na Chakula, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa ni wageni wengine tulionao hapa Bungeni, tutaanza na wageni wenu kisha wageni waliokuja kwa ajili ya mafunzo.

Kwanza ni wageni 65 wa Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda ambaye ni Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia na hawa ni viongozi wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Wilaya ya Rombo, Mkoa wa Kilimanjaro, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 30 wa Mheshimiwa David Ernest Silinde ambaye ni Naibu Waziri wa Kilimo na hawa ni viongozi wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Jimbo la Tunduma, Mkoa wa Songwe, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Exaud Kigahe ambaye ni Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara na huyu ni Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM kutoka Iringa. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Rashid Shangazi ambao ni Waheshimiwa Madiwani kutoka Lushoto, Mkoani Tanga. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi ambaye ni kaka yake anatoka Kibondo. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Abubakari Asenga ambaye ni Mhandisi Mshauri wa Barabara ya Kidatu – Ifakara, kutoka Kilombero, Mkoa wa

Morogoro na yupo pia mgeni wa Mheshimiwa Festo Sanga ambaye ni mdau wa kilimo kutoka Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Cecil Mwambe ambao ni viongozi wa Chama Kikuu cha Wakulima Mtwara *(MAMCU)*. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa ambao ni rafiki zake kutoka Kampuni ya Mbegu *ASA*. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Asia Halamga ambao ni rafiki zake kutoka Babati. *(Makofi)*

Wageni nane wa Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara ambao ni watumishi wa Taasisi ya Watu Wenye Ulemavu *(Foundation for Disabilities Hope)* ya Dodoma. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Venant Daud, mkulima wa tumbaku kutoka Jimbo la Igunga, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 18 wa Mheshimiwa Fatma Toufiq, hawa ni Wachungaji wa Kanisa Anglikana na wenza wao. *(Makofi)*

Tunao wageni 27 wa Mheshimiwa Jesca Msambatavangu ambao ni viongozi na wachezaji wa Klabu ya *Ceasiaa Queens Fc.* Sasa hapa wameishia neno kutoka, sijui kama wanatoka Iringa ama wapi, lakini wanakaribishwa sana wageni wa Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 17 wa Mheshimiwa Amina Daud Hassan ambao ni wanafunzi wa Shahada ya Awali ya Sanaa katika Tafsiri na Ukalimani kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na hawa ni wanafunzi 70 na watumishi wawili kutoka Chuo cha Uhasibu Dar es Salaam. Sijui wamekaa upande gani? Aah, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao viongozi nane kutoka Umoja wa Kampuni Binafsi za Ulinzi *(MUKUTA)*, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndiyo wageni tulionao asubuhi hii na wengine watatangazwa kadiri watakavyokuwa wanapata nafasi ya kuingia hapa ndani na sasa tunaendelea na ratiba yetu.

Kabla hatujaendelea, juzi wakati nikiachia Kiti kwa Mwenyekiti, nilieleza juu ya mambo mawili ambayo tungeyafanyia kazi leo na tutaanza na hayo kabla ya kusikiliza hoja ya Mheshimiwa Waziri. Kwanza ni kuhusu mikopo ya kausha damu, halafu itakuja hoja ya tembo. *(Makofi)*

Sasa mikopo ya kausha damu kwa sababu Serikali mlikuwepo Bungeni ni zamu yenu kuwasikiliza ili halafu tujue Bunge liseme nini kuhusu jambo hilo. Kwa hiyo, natoa nafasi kwa Mheshimiwa Waziri, dakika tano, juu mikopo ambayo inawakausha damu wananchi. Mheshimiwa Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

Sasa ili isiwe hoja yako, ibaki kuwa ni hoja ya Mbunge, semea pale pale kwa sababu Mheshimiwa Felista Njau ndiye aliyeleta hoja.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kusema kuhusu hoja iliyojitokeza. Kwa mujibu wa Sheria za Fedha zinazosimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania hakuna kampuni yoyote ya simu ambayo imepewa leseni ya kutoa mikopo kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, ili taasisi au mtu binafsi aweze kutoa mikopo kwa wananchi anapaswa kuwa na leseni kutoka Benki Kuu ya Tanzania na kukidhi matakwa ya Sheria ya Fedha ya Benki Kuu *(The Banking and Financial Institutions Act)* ya mwaka 2006 na Sheria za Huduma za Fedha *(Microfinance Act)* ya mwaka 2018.

Mheshimiwa Spika, kampuni za simu zinatoa huduma za fedha kwa kutumia leseni ambazo zimepewa za kutoa huduma za mifumo ya malipo kulingana na matakwa ya sheria pamoja na kanuni zake.

Kampuni hizo kama ambavyo tunafahamu ziko sita ambazo ni M-Pesa, Honora, Tigo Pesa, *Airtel Money*, Viettel ya HaloPesa, T-Pesa ya *TTCL* pamoja na AzamPesa.

Mheshimiwa Spika, mikopo inayotolewa kwa wananchi kupitia simu za kiganjani hutolewa kwa ushirikiano kati ya taasisi zilizopewa leseni ya kutoa mikopo pamoja na kampuni ya simu ambayo inafanya jukumu hilo. Hadi kufikia Machi, 2024 kampuni za simu ambazo mifumo yake ya malipo hutumika katika kutoa mikopo kwa kushirikiana na benki pamoja na taasisi za fedha ni kama ambavyo nimetoka kuzigusia, ipo M-Pesa, *VICOBA,* pamoja na *Tanzania Commercial Bank* ambazo wana mtiririko wa aina ya mikopo ambayo wanaitoa ikiwemo *M-Pawa Savings*, Songesha, Wakala Wezesha, Wakala Songesha, *Mgodi Saving*, *Make a Loan*, Halali Pesa, pamoja na *Insurance Premier Financing* ambapo hizi ziko kwenye benki ikiwemo *NCBA, Microfinance Mwanga Hakika, Diamond Trust Access Bank, Amana Bank, NMB, CRDB, Azania, BOA* pamoja na *Jumo Financing*.

Mheshimiwa Spika, mikopo yote hutolewa na watoa huduma ndogo ndogo za fedha kupitia benki ambapo huwafikia wananchi wote wenye uhitaji na wenye kutumia huduma za kifedha kupitia simu za mkononi kwa njia ya mifumo ya malipo ya kampuni za simu ambazo wateja wao wapo nchi nzima. Hii inawasaidia wananchi kupata mikopo wanoyohitaji kwa kuwa haihitaji kuwa na akaunti ya benki wala dhamana ya mikopo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kumlinda Mtumiaji wa Huduma za Fedha za mwaka 2019, watoa huduma wote wa fedha wanaosimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania wanatakiwa kutoa elimu ya fedha kwa wateja wao juu ya huduma wanazotoa ikiwemo elimu ya mikopo. Aidha, kanuni hizo zinawataka kutoa mikopo baada ya mkopaji kuridhia masharti ya mikopo husika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Benki Kuu kuwahimiza watoa huduma za fedha kutoa elimu kwa wateja wao, Benki Kuu ya Tanzania katika nyakati tofauti imekuwa ikitoa elimu kwa wananchi

juu ya huduma za fedha na kuwataka kutojihusisha na huduma za kifedha kutoka kwa watoa huduma wasio na leseni kutoka Benki Kuu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mikopo inayotolewa na benki na taasisi za fedha kupitia mifumo ya kampuni za simu ni kama ilivyoainishwa awali. Pamoja na mikopo hiyo kutoa unafuu na kupata umaarufu wa kuitwa kausha damu, lakini hutolewa na taasisi ambazo hazina leseni ya Benki Kuu ya Tanzania. Hili jambo la kausha damu limejengwa kwenye mahusiano tu ya mtu na mtu, kila kijiji kina mtu mmoja maarufu anakuwa mkopeshaji, lakini anakuwa hayupo kwenye utaratibu rasmi wala hana leseni.

Mheshimiwa Spika, aidha, Benki Kuu ya Tanzania imechukua hatua mbalimbali za kuzuia mikopo hii ikiwa ni pamoja na kuzitaka kampuni za simu kuhakikisha mifumo yao haitumiki katika shughuli zozote zinazohusisha mikopo hiyo. Pia ziendelee kutoa elimu kwa wananchi ili waepukane na kuchukua mikopo hiyo kutoka kwenye taasisi ambazo hazijasajiliwa na watu ambao hawana leseni ya kutoa mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, vilevile Benki Kuu inaendelea kufuatilia ili kuweza kuchukua hatua stahiki kwa wale wahusika ambao wanafanya shughuli hizo na kukiuka taratibu zilizowekwa. Hata hivyo, kati ya sababu zinazochangia gharama za mikopo ya kidigiti kuwa kubwa ni pamoja na mikopo hiyo kutolewa papo kwa hapo na bila takwa la dhamana. Hivyo, sehemu ya gharama hizo inaakisi hatari ya kutokulipika kwa aina hiyo ya mikopo.

Mheshimiwa Spika, hakuna kampuni ya simu inayotoa mikopo moja kwa moja, bali ni benki na taasisi za fedha zenye leseni kutoka Benki Kuu ndizo ambazo hutoa mikopo hiyo kupitia mifumo ya kampuni za simu kwa makubaliano maalum baina yao. Hata hivyo Benki Kuu inafuatilia kwa karibu mwenendo wa utoaji wa mikopo ya kidigiti iliyoidhinishwa na pindi itakapobainika kuwa kuna ukiukwaji wa matakwa ya leseni ya utoaji wa mikopo hiyo, hatua stahiki zitachukuliwa, hii ikiwa ni pamoja na kuwafutia leseni. Tayari Benki Kuu

imeshafuta baadhi ya leseni za watoa huduma ndogo ndogo za kifedha baada ya kubainika kwamba wanakiuka taratibu na masharti waliyokuwa wamepewa.

Mheshimiwa Spika, natoa rai kwa Benki Kuu ya Tanzania kuimarisha usimamizi wa sekta ya fedha hususan watoa huduma ndogo ndogo za fedha na watoa huduma za mifumo ya malipo. Lengo ni kuhakikisha kuwa wanazingatia matakwa ya Sheria ya Benki Kuu na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 na Sheria ya Mifumo ya Malipo ya mwaka 2015 pamoja na Sheria ya Huduma za Fedha ya mwaka 2015. Aidha, nawasihi wananchi wapate huduma za fedha kutoka kwa watoa huduma rasmi zinazosimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania ili kuepuka huduma za fedha kutoka kwa watoa huduma wasio rasmi na ambao wanatoa masharti magumu ikiwemo riba kubwa almaarufu kausha damu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii si kwa fedha tu, wengine wanakopeshana anapewa kilo tano za mbegu ya vitunguu, baada ya miezi miwili anatakiwa kulipa magunia matano; yote haya ni kausha damu ambayo wananchi wanatakiwa waepuke kuchukua mikopo ya aina hiyo ili kuweza kuepukana na adha hii ambayo inajitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, hoja hii ilianzia kwenye swali ambalo liliulizwa na Mheshimiwa Felista Njau, kisha yakaulizwa maswali ya nyongeza. Nadhani mmojawapo wa waulizaji alikuwa Mheshimiwa Shally Raymond, ndiye aliyesababisha hii hoja.

Sasa kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri ni kwamba kampuni za simu hazitoi mikopo moja kwa moja, kama nimeelewa sawasawa, ni benki ndizo zinatoa kupitia simu. Nimeelewa sawasawa Mheshimiwa Waziri?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ni kwamba kampuni za simu hazina leseni za kutoa mikopo. Kwa hiyo, kitendo hicho wanachofanya cha kutoa mikopo, wanafanya kwa *partnership* na benki yenye leseni ya kutoa mikopo.

**SPIKA:** Ngoja, Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane kidogo kwa sababu tunataka kutoa ushauri kwa Serikali. Kama kampuni za simu hazina leseni za kutoa mikopo na wananchi hawaendi benki wanapata mikopo kupitia simu, maana yake mkataba upo kati ya benki na kampuni ya simu ambayo haina leseni. Sasa huu mkataba *BOT* inaukubalije? Kwamba wewe katoe mkopo wakati hauna leseni ili niirejeshe hii huku kwa Mheshimiwa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba niishie kwenye hiki kipengele cha kwanza, mwenzangu anayesimamia mitandao amalizie kwenye upande huo wa teknolojia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, sisi tunachokifanya ni kwa sababu benki zetu hazijaenea nchi nzima, kwa hiyo, tunawarahisishia wananchi kwa kuruhusu benki kufanyakazi na mitandao ya simu ili kumrahisishia mwananchi aweze kufikiwa kule kwenye kijiji. Sasa kuhusu makubaliano hayo na mauziano ya teknolojia, kwa ridhaa yako, Waziri anayesimamia sekta aendeleze ufafanuzi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tusikilizane. Mheshimiwa Nape Nnauye.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, kazi ya TEHAMA ni kuwezesha shughuli nyingine zifanyike kwa namna ambayo bila TEHAMA ingekuwa ni ngumu kufanya kazi hizo na ndiyo maana kwa mfano, kupitia TEHAMA tunaweza kununua bidhaa mtandaoni. Mfanyabiashara wa bidhaa fulani anatumia *platform* hii kufikisha fedha na wakati huo huo kufanya mawasiliano ile bidhaa ifike mahali ambapo inatakiwa kufika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *platforms* hizi hazichukui leseni ya biashara, kwa hiyo, hata hapa kinachofanyika ni hicho kwamba mitandao ya simu haichukui leseni ya kutoa mikopo isipokuwa kwa kuwa ni wawezeshaji wa utoaji wa huduma wanaenda kwa mtoa huduma, wanaingia mkataba na mtoa huduma, kwa sababu hii *platform* yao inatumiwa na mpokea huduma, kwa hiyo, wao wanakuwa katikati. Ni kama barabara kwamba biashara inatoka huku inakwenda huku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kampuni ya simu haiwezi kuchukua leseni na pia haiwezi kufanya kazi ya kutoa mkopo na ndiyo maana Benki Kuu inampa leseni mwenye huduma za fedha na inampa masharti ya kufanya hivyo. Sisi kazi yetu ni kuwezesha tu. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa nimekuona unataka kutoa Taarifa. Ngoja tuweke taarifa za msingi kwanza, tuwe tumeelewana halafu nitatoa nafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Nape kwenye hiyo mikataba wanakubaliana riba? Riba ile ni ya benki ama ni ya kampuni ya simu? *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, makampuni ya simu hayawezi kufanya biashara ya mkopo, anaye-*deal* na riba siyo kampuni ya simu, anaye-*deal* na riba ni yule mwenye leseni ya kutoa mkopo, yeye ndiyo amepewa masharti na Benki Kuu aendaje, afuateje masharti. Kwa hiyo, huyu hapa ni mwezeshaji wa biashara tu.

**SPIKA:** Haya umeeleweka.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Nirejee, ngoja ngoja. Nirejee kwako Mheshimiwa Waziri wa Fedha, *BOT* ina mwongozo wowote kuhusu riba au benki inaamua kuanzia asilimia sifuri ya mkopo mpaka 100%, yaani kwamba

umekopa shilingi 100,000 na utalipa shilingi 100,000. Kuna sharti lolote kutoka *BOT* au hakuna, kwa hiyo, benki inaweza ikasema 80%, 90% au 100%, kuna mwongozo wowote au hakuna? *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, masuala yote yanayohusiana na riba kuna sheria ambazo zinalinda walaji, lakini soko linaamua masuala ya riba. Kwa hiyo, kwa mujibu wa sheria za kimataifa riba katika nchi ambazo zinafuata mfumo wa soko, Benki Kuu haipangi riba kwamba kuanzia kesho riba za benki itakuwa asilimia tano, hatufanyi hivyo. Taasisi za kifedha zinazosimamia benki kuu zote yanayofuata mifumo hiyo, soko linaamua masuala ya riba.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa nchi yetu tuna utaratibu wa kuwalinda walaji ambapo hapo ndiyo maeneo ambayo tunatolea miongozo ya kuweka utawala katika masuala ya riba ili kuweza kuwalinda walaji. Kwa hiyo, hata hivi sasa leseni zinapotolewa kuanzia kwenye uandikishaji wa hizi *microfinance* kuna miongozo ambayo wanasainishana mtu huyu anapoomba leseni pamoja na msimamizi kuhusu namna ya kuwalinda walaji. Kwa hiyo, kuna sheria inayolinda walaji.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Ngoja Mheshimiwa mtaalamu wa benki nimekuona utapata tu nafasi.

Mheshimiwa Waziri, je, nitakuwa sahihi nikisema hivi, nchi hii hatuna mikopo ya kausha damu kwa sababu hata Benki Kuu inajua soko linajiendesha lenyewe. Nitakuwa nipo sahihi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kisheria hatuna mikopo ya kausha damu. Kausha damu ni mimi naenda kuchukua fedha kwa Mheshimiwa Nape halafu nakaushiwa damu kwa kufuatana na makubaliano niliyokubaliana na Mheshimiwa Nape. Hii hata Mwenyekiti wa Kitongoji anakuwa hajui... *(Kicheko)*

**SPIKA:** Sawa, sasa swali langu lilikuwa kwamba...

**WAZIRI WA FEDHA:** ... ni mimi nimeenda kwa Mheshimiwa Ndejembi nimepewa riba ambayo ni inanikausha damu...

**SPIKA:** Ngoja, swali langu lilikuwa kwamba mimi kama Mwenyekiti wa Kitongoji, ninazo fedha zangu na naamua kukopesha kwa 100%, sikosei popote kwa sababu si hakuna sheria ninayokosea wala mwongozo wowote kama ambavyo benki... *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ngoja, ni kama ambavyo benki pia inaruhusiwa kuanzia sifuri mpaka 100 kwa hiyo, hiyo ipo sawa, nimeelewa sawa sawa?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ukifanya hivyo unakosea kwa sababu mikopo yoyote..., tusikilizane.

Mheshimiwa Spika, ukifanya hivyo unakosea kwa sababu mikopo inatawaliwa na sheria, utakuwa hauna leseni ya kufanya hivyo. Hamna leseni iliyotolewa kutoa mikopo ya kausha damu. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Nimeelewa, kwa hiyo mwenye leseni kama benki, kama simu ama yeyote asilimia yoyote anayotaka inaruhusiwa, isipokuwa huyu ambaye hana leseni ndiyo haruhusiwi, nimeelewa vizuri? Hoja ni leseni.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, hata mwenye leseni siyo asilimia yoyote, lazima azingatie mwongozo, lakini wale wanaofanya kausha damu yale ni makubaliano ya kirafiki ambayo hayapo *governed* na utaratibu ambalo ni kosa kisheria.

**SPIKA:** Kabla sijawaruhusu Wabunge, Mheshimiwa Waziri sasa hapo umenichanganya kidogo, kwa sababu kama hakuna mwongozo maana yake hata benki zinaruhusiwa kutoza riba yoyote kwa sababu si ni soko lipo wazi? Kwa sababu yenyewe yana leseni. Kwa hiyo riba ni yoyote? *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ingekuwa hivyo kungekuwepo na *fluctuation* kubwa sana ya riba kwenye benki, lakini sasa hivi ukiangalia kwenye benki kuna *range* ambayo benki zinatumia na zinaenda kufuatana na mwongozo. Ingekuwa hivyo hata benki kungekuwepo na kausha damu.

Mheshimiwa Spika, kilio hiki kikubwa kinatokana... kwa wafanyakazi mfano wamewekewa wigo wa kukopa, wamewekewa asikope zaidi ya robo tatu ya mshahara wake. Atakapomaliza ule wigo ambao anatakiwa akope kwenye taasisi rasmi ambazo zitamuuliza kwamba wewe mshahara wako umeshazidi robo tatu, anaondoka anaenda kwa rafiki ambaye hajasajiliwa ambaye hatamuuliza ile robo tatu, ambalo hilo linakuwa la kimahusiano...

**SPIKA:** Haya.

**WAZIRI WA FEDHA:** ...lakini utaratibu wa sheria za kifedha una mwongozo ambao hautoi fursa tu ya mtu kujifanyia kiholela, uhuru na soko haina maana ya uholela. Kwa hiyo, kuna sheria zinazolinda walaji/watumiaji kwa maana hiyo wa huduma za kifedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, mimi nafikiri kuna jambo moja ambalo tunalazimika kufahamu kwamba mkopo una muda na *rate per annual*, mkopo lazima uwe na muda, lakini sasa hii wanayofanya *M-Pawa* na kadhalika ni tozo tu, yaani kwamba ni tozo wanafanya kumuokoa mteja wao ambaye amekwenda kufanya muamala akawa hana fedha ya kutosha wakati ule na anayestahili kwenda pengine benki kuongezea salio lake kwenye M-Pesa. Kwa hiyo, inasaidia sana, lakini niseme kwamba hutaona mtu aliyesema kwamba M-Pawa unachukua kwa muda wa wiki moja *at a rate of three percent or four percent, no,* ni tozo wanakubaliana, wanakubaliana na mabenki kwamba wata-*share* hiyo tozo wana-*share* kati ya benki na yule mtoa huduma ya TEHAMA.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi naamini kwamba siyo, huwezi kusema..., halafu hizi za *microfinance institution* na tunajua kwamba kuna sheria tulipitisha hapa na kuna kanuni Benki Kuu imetoa, kama kukiwa na taasisi ya kutoa huduma za fedha kwenye *level* hii ya *micro* lazima unatuma Benki Kuu ile *lending policy* yako kwamba sera yangu na mkakati wangu wa kukopesha utakuwa ni hivi na riba itakuwa ni kati ya asilimia sifuri mpaka tuseme tano kwa mwezi au kwa miezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ukipeleka Benki Kuu wanai-*vet,* wanakupa kibali kwamba *okay, go ahead* na ndiyo wanakupa kibali na leseni yako inakuwa *valid*.

Kwa hiyo, nataka kusema kwamba kuna mwongozo na miongozo hiyo ipo *valid* na inabadilika mara kwa mara kwa sababu pia riba zile zinabadilika mara kwa mara, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sina uhakika kama tutaweza kufikia kuishauri Serikali ya kufanya nini. Mheshimiwa Dkt. Kikoyo.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, wakati Mheshimiwa Waziri anaongelea haya masuala, tatizo tulilonalo katika nchi hii hatuna sheria inayowalinda watumiaji na ndiyo tatizo linapoanzia.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wakati anaelezea pale nikawa najiuliza, hivi katika mkanganyiko huu mtumiaji akipata madhara yoyote anakwenda kumshitaki nani? Anakwenda kuishitaki kampuni ya simu au anakwenda kuishitaki benki? Kama tunavyofahamu sheria za mikataba, huyu mtumiaji ataishia kupata hasara na madhara makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani mimi niishauri Serikali walete sheria, tutunge sheria mahususi ya kuwalinda watumiaji hasa kwenye sekta ya afya na sekta ya fedha maana kuna mkanganyiko mkubwa sana. Hata kwenye baadhi ya maduka makubwa hapa Dodoma, unakwenda kwenye duka wanakwambia hatuna chenji, chenji ile

anakupa pipi. Sasa kuna tatizo kubwa sana kwenye uchumi wetu. Hapa Dodoma maduka makubwa, badala ya kukupa chenji yako anakupa pipi... *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Spika, naomba...

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Inatokea wapi Taarifa?

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, hapa kwa Kingu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kingu.

**TAARIFA**

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa Taarifa.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mchangiaji kaka yangu kuwa tuna *Fair Competition Act* ambayo inamlinda mlaji na tuna Baraza la *Consumer Protection* chini ya Sheria *Fair Competition Act*. *Unless otherwise* anachokishauri Mheshimiwa Mbunge labda tuongeze *scope* itakayoangalia walaji katika sekta za *finance,* lakini kwa upande wa sekta za afya na sekta zingine zote na mimi ni mtaalamu ambaye nimepita pale nimefanya katika taasisi ile. Kwa hiyo ninaelewa vizuri juu... *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa ya mwisho.

**SPIKA:** Haya naona Taarifa inataka kutoka juu ya Taarifa.

Waheshimiwa Wabunge, tunayo hoja, tuna hoja mbele yetu hapa wachangiaji dakika moja, nenda moja kwa moja kwenye hoja tuliyonayo hapa mezani. Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, dakika moja.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, mimi ninafikiri kwamba Mawaziri hawajafahamu adha inayowapata Watanzania hususani wanawake. Kwenye kampuni za simu, kwa mfano sijui kama ni sahihi kuitaja kampuni ina kitu kinaitwa Tigo Nivushe inakupa *percent* unakopa shilingi milioni moja unalipa kwa asilimia. Kwa hiyo, swali linakuja ile asilimia inachuka kampuni ya simu au huyo mtu ambaye ameingia ubia na hiyo kampuni ya simu? Lakini hii kausha damu ni kitu halisi na kipo, mtu anatoa leo mwanamke anayekopa labda shilingi 100,000 ndani ya siku mbili anatakiwa alipe shilingi 150,000 na mwisho wa siku anachukuliwa makabati, *tv* na vitu kama hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ninaomba lazima Mheshimiwa Waziri alichukue hili, naona kama hajajiandaa, alichukue hili akakae na watu wake walifanyie kazi waje na jibu sahihi hapa kwa sababu kausha damu ni kitu halisi na kipo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana, ahsante sana. Mheshimiwa Zaytun Swai.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kampuni zote za simu zina idara mbili, Idara ya *Telecom* ambayo ina-*deal* na mambo ya simu na *technology,* lakini kuna idara ya *mobile money business* ambayo lazima ipate leseni kutoka Benki Kuu ya Tanzania. Hizi riba ambazo tunaziongelea hapa zipo *regulated* na *BOT*. Kwa hiyo, bado nashauri Wizara ya Fedha kupitia Benki Kuu ya Tanzania iweze kuangalia riba hizi, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nakaribia mwisho wa hoja hii. Mheshimiwa Yahaya Massare.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, hoja ya mtoa hoja ni masuala yaliyopo mtaani ambayo watu wanakopeshwa hela kidogo riba inakuwa kubwa na kwa muda mfupi. Hili ndilo ambalo Serikali inatakiwa ilione na ione namna ya kufanyia kazi na wale watu hawana leseni aidha ya *BOT* au ya taasisi yoyote ya fedha na hao ndiyo wanaosababisha hii kausha damu kwa sababu haipo katika mfumo rasmi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba Mheshimiwa Waziri aone namna ya kulibeba hili na kulifanyia kazi kama kwa haraka imeshindikana au Bunge lako Tukufu lione na liazimie kuifanya hii mikopo kule mtaani ambapo ndiko kwenye shida...

**SPIKA:** Haya, ahsante sana.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** ...iweze kuchukuliwa na Serikali na kufanyiwa *regulation*. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Shally Raymond atafuatiwa na Mheshimiwa Felista Njau, tunafunga hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, ahsante, mikopo hii ina mvuto sana kwenye simu na ni rahisi sana kwa yeyote ku-*access*, zipo zinaitwa nyingine *Kisasi Microfinance*, *Zango Trading,* kuna *Mkopo Faster, Credit Land* na kadhalika lakini zina-*charge* 80% *(eighty percent)*. Ukikopa leo shilingi 40,000 baada ya siku saba unatakiwa unaanze kulipa, unapochelewa wanaanza sasa kusambaza jina lako kwa ndugu, jamaa na marafiki au yeyote ambaye yupo kwenye *list* yako. Ndiyo hapo tunaona kwamba hao wenye simu wanashirikiana, wamejuaje watu wenye simu yangu au wenye simu ya huyo. Matusi, kejeli watu wetu wanaathirika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Felista Njau.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, ahsante na nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, tukiwa tunaongelea mikopo ya kausha damu ambayo imeathiri mikoa mingi, niende moja kwa moja mikopo hii taasisi nyingine zina ofisi na zina leseni, kwa mfano mikopo iliyoandikwa oya, kausha damu, kichefuchefu, *new answer* wana ofisi na wana-*charge* 60% mpaka 80%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mikopo hii unarejesha kila siku ndiyo sharti la kwanza. Unarejesha shilingi 22,000 kwa siku mpaka ikifika tarehe 30 siku moja ukivusha, hujapeleka wanakuja na gari wanabeba kitanda, godoro na kila kitu.

Mheshimiwa Spika, nataka nijue *limit* ya hii mikopo ya *microfinance* kwamba riba yao mwisho ni ngapi? Maana yake mwongozo wa Benki Kuu upo, lakini haufuatwi, wananchi wanaathirika, Wizara ya Fedha haijatoa majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nipate pia *limit* ya riba ya mabenki, kwa sababu hapa ameongea Mheshimiwa Waziri kwa mikanganyiko ya benki. *Microfinance* riba mwisho ni kiasi gani? Watu wanatozwa riba mpaka 100%. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante...

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, athari ni kubwa kwenye mikopo ya kausha damu siyo suala la blah blah...

**SPIKA:** Haya ahsante sana...

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, siyo suala la blah blah, watu wanakufa. Siku hizi wananiita balozi wa kausha damu, watu wanakufa, wananitumia picha na namna watu wanavyojiua. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, siyo mkopo wa mtu mmoja mmoja kama alivyosema Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Haya ahsante.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, ni mkopo kwenye taasisi zenye usajili, naitaka Serikali isikimbie kivuli, nendeni mkafanye utafiti, nendeni mfuatilie.

**SPIKA:** Mheshimiwa Felista.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, Benki Kuu ni mtoto wenu, nendeni mkafuatilie.

**SPIKA:** Mheshimiwa Felista.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, mkafuatilie wananchi wanaathirika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, umeeleweka, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Nape, nilikuona umesimama.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, na mimi pia.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ...

**SPIKA:** Dakika moja.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, sawa, la kwanza hili jambo lilipoanza mtandaoni siyo kwamba Serikali tulifumba macho, Wizara yangu iliwaagiza *TCRA* ambao ndiyo wasimamizi wa sekta hii wakaita kampuni za simu na kuwataka wakapitie wale wanaofanya nao kazi kuhakikisha wana leseni halali za *BOT* na hiyo ndiyo ambayo italimaliza hili jambo, kama kuna yeyote anafanya shughuli hii na mtu ambaye hana leseni.

Mheshimiwa Spika, matokeo yake yaliyokuja kwetu...

**SPIKA:** Mheshimiwa Nape, hapo unazungumzia kampuni za simu, siyo?

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, *exactly*.

**SPIKA:** Waziri wa Fedha ameshasema kwamba kampuni za simu hakuna hata moja yenye leseni ya kutoa mikopo.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, hawana leseni, lakini kwa sababu wamekaa katikati ya wenye leseni na wananchi ndiyo maana nimesimama kutoa ufafanuzi kwamba hili linalozungumzwa hapa...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** ...lina pande zote na mpaka wananchi wenyewe...

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** ... kwa sababu...

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Waheshimiwa....

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane. Mheshimiwa Nape, malizia.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, hoja yangu ni kwamba upande wa Serikali

tumechukua hatua na tunaendelea kuelimisha watu, lakini ipo hoja ya msingi upande wa wananchi ambao wanakwenda kuchukua hizi huduma. Kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Fedha, wengi wao wakienda kwenye taasisi ambazo ni *legit* kwa kuwa wameshafikia ukomo wa kukopa hawaendi huko matokeo yake wanakwenda kufanya utaratibu na watu pembeni ambao kwa mujibu wa sheria ni makosa. Kwa hiyo, nao wanaingia kwenye makosa.

**SPIKA:** Haya ahsante.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa nadhani pamoja na sisi Serikali kuchukua hatua na kulifanyia kazi hili jambo kwa kina, sisi na Wizara ya Fedha ni vizuri tutoe wito pia kwa wananchi wasiparamie mikopo ambayo kwa kweli haina kichwa wala miguu, ni rahisi kuipata, lakini ina gharama...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nape, Waheshimiwa Wabunge tusikilizane kidogo.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Tusikilizane nataka kufunga hoja.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Tusikilizane Waheshimiwa, tusikilizane.

Mheshimiwa Nape tunapata changamoto ama ngoja amalize Mheshimiwa Waziri kwanza ufafanuzi. Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, niende kwenye hoja ambayo Mheshimiwa Felista aliitoa. Kwa mujibu wa Kanuni ya kuwalinda walaji, *microfinance* zote wigo wao wa juu kwa mwezi hawatakiwi kuzidi 3.5% hata kwenye leseni zao hivyo ndivyo ilivyo. Sasa kinachotokea, masuala ya kimkopo yapo hivyo na Mheshimiwa Dkt. Kimei amesema hapa.

Mheshimiwa Spika, kuna mkopo unaochukua kwa mwezi, kuna mkopo unaochukua kwa miezi sita, kuna mkopo unaochukua kwa miezi 12, kuna mkopo unaochukua kwa miezi 18, hii yote ukifanya *pro rata* zake ina viwango vinakuwa tofauti. Kwa maana hiyo, hapa ni kwenye upande mmoja tunaoongelea kwenye mfumo ulio rasmi.

Mheshimiwa Spika, hili jambo tunaloongelea hapa lina *combination* zote na ndiyo maana tunashindwa kuelewana, kuna mambo ambayo ni rasmi kwenye taasisi zilizosajiliwa rasmi na kuna mambo ambayo siyo rasmi, ni mtu yeye mwenyewe anaenda kwa rafiki yake, kuna mtu mmoja tu ana mtaji wake wa siri, siri, lakini anajulikana kwamba ukiwa na shida ukienda anakukopesha na wanafanya makubaliano ambayo yapo nje ya utaratibu wa Kiserikali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, haya mambo, kwa sababu shida ina kawaida ya kusukuma kama chatu na mnyama, mnyama anakuwa anajua kabisa pale pana chatu, lakini anakuwa anasukumwa anavutwa na mvuto mpaka anaenda anamezwa. Sasa na shida ndivyo zinavyowasukuma wananchi wetu kwamba anakuwa na shida, anajua ile riba ilivyo anakuja kutambua baada ya kuwa ameshaingia kwenye matatizo. Kwa hiyo, mimi rai yangu kwa wananchi, kwanza Serikali tumelichukua hili jambo na tunaendelea kulifanyia kazi kwa kina zaidi. *(Makofi)*

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Haya malizia Mheshimiwa.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, tumelichukua hili jambo kama Serikali, tunaenda kulifanyia kazi kwa kina zaidi ili tuweze kuboresha zaidi, tutafanya semina ya wawakilishi wa wananchi na taasisi zote za kifedha ili tukubaliane kuhusu jambo hili ili Waheshimiwa Wabunge waziambie taasisi zangu zote ni namna gani wanataka sheria zile zisimamie vizuri maslahi ya wananchi wanaowawakilisha.

Mheshimiwa Spika, tutafanya semina hiyo katika Bunge hili linaloendelea, tutaleta taasisi zote za kifedha zije zifanye semina siku nzima, hata wiki nzima ili tupeane majukumu haya na tuweze kutengeneza jambo ambalo litalinda walaji.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, hoja hii kama nilivyokwishasema ilijitokeza wiki iliyopita, tukatoa nafasi ili Serikali ilete ufafanuzi na Serikali imetoa ufafanuzi wa hali halisi.

Kwanza, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na kisha tumepata ufafanuzi kutoka Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na Serikali katika upande wao nao wamekiri kwamba si maeneo yote ambayo taasisi zetu za kifedha zimefika na kwa hiyo, wananchi wanajikuta wanahudumiwa na wale watu ambao wapo karibu hapo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hii hoja ya mikopo yenye riba kubwa sana, si hoja tu kwa maelezo yaliyotoka hapa, si hoja tu ya wale wanaotoa mikopo kwa urafiki, kwa kujuana ama kwa kijijini yupo mtu mmoja, taasisi za kifedha pia zinadai riba kubwa hata zenye leseni.

Sasa kwa sababu zile leseni zinavyotolewa zinatolewa na upande wa Serikali, hili ndilo jambo linatakiwa kwenda kutazamwa, kwa nini? Kwa sababu hata yule mwingine kama hii taasisi ambayo imesajiliwa inaweza kusema riba mpaka 80%, yule wa kijijini si na yeye atafanya hivyo kwa sababu hata huyu mwingine ndicho anachofanya? Hata yeye wa simu kama wanafanya hivyo na yeye ndicho atakachofanya, kwa sababu ulichofanya ni kwamba hujaenda kwa mwenye simu umeenda kwa huyo ambaye anayo mkononi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mwanzo mimi nilikuwa nimeelewa ni wale wanaweka tu matangazo mahali, vibao wamebandika na siyo hawa ambao wana leseni, lakini kwa maelezo yaliyotoka kwa Waheshimiwa Wabunge hata wenye leseni bado wanatoa mikopo ya aina hii. Sasa wale mnao uwezo wa kuwafuatilia, hilo kwa sababu mnao uwezo wa kuwafuatilia tusiwasukumie wananchi kwamba wananchi wenyewe wanakimbia, wananchi wenyewe wanakwenda, wananchi wanakwenda kwa sababu hawana namna nyingine na kwa sababu sote tunakubali kwamba taasisi zetu za kifedha hazijafika huko, Mheshimiwa Waziri umehitimisha hapa vizuri na ndiyo maana nafikiri umesikia makofi mengi hapa. Serikali lichukueni jambo hili kwa uzito unaostahili, kwa sababu wananchi wanapata taabu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo basi, sasa Bunge kwenye hoja hii kwa namna mijadala ilivyokuwa imeniwia ngumu kidogo kusema Bunge linaazimia nini kwenye hoja hii, kwa sababu inaonekana ni pana kuliko ilivyofikiriwa mwanzo kwamba pengine ni kundi fulani na hivi na hivi, lakini inaonekana hata taasisi zenyewe za kifedha pia zinatoa hiyo mikopo ambayo ina riba kubwa ambazo zinashindwa kubebeka. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ninafikiri Mheshimiwa Waziri, kwa kile ulichohitimisha hapo upande wa Serikali lichukueni hili mlifanyie kazi na muone namna ya kutoa mwongozo, kwa nini? Mkisema tu ni soko ndiyo maana niliuliza hapa, hata tukisema 100% hilo soko je, ni sawa? Hapa mwishoni umesema kwa hizi zilizosajiliwa mwisho asilimia 3.5. Fanyeni

tathmini hizi riba mliziweka lini? Kwa sababu pia maisha yamebadilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri hapo ameeleza watu kama wanaweza kupata mikopo kwa simu, sasa maana yake wanaweza kutafutwa. Kwa nini? Simu si zimesajiliwa. Je, bado kule kuogopa ni kukubwa kiasi hicho? Kwamba mtu anayekopa shilingi 1,000 inabidi alipe 1,000 kwa sababu unaogopa hatalipa.

Kwa hiyo, mazingira yamebadilika na ninyi pia mfanye hii kazi kwa maana ya kutazama mabadiliko yaliyopo na kama, hee! Ninatafuta neno la Kiswahili la *risks* hapo, ni kubwa kiasi hicho ama zimepungua na ninyi punguzeni upande wa riba kwa wananchi wasipate taabu hizi wanazozipata sasa hivi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, tunashukuru kwa hilo la kwamba mnalichukua, sasa nina uhakika wananchi watakuwa wanawaza sasa wamelichukua mpaka lini? Itakuwa ni hoja ameichukua mpaka lini? Sasa kwa sababu tumekubaliana hapa, kwamba ni jambo pana kidogo, kwa hiyo, siyo hoja ambayo tunaweza kumwambia Waziri kesho, ama wiki ijayo, wanahitaji muda ili watathmini hali ilivyo na waweze kuona ni mwongozo gani watautoa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ni ngumu kidogo kusema muda gani, lakini ninaamini kwa sababu bado tupo hapa kwenye hiki kipindi, watumie muda mrefu kuwasikiliza Waheshimiwa Wabunge maadamu tupo hapa na baadaye wakawasikilize wananchi huko, kwa sababu kwa kweli athari ni kubwa sana. Halafu pengine tutasikia kama watakuwa wamepiga hatua yoyote kwenye Bunge la mwezi wa tisa, watatuambia kama wamepiga hatua yoyote, lakini kwa maana ya majibu, nadhani itachukua muda kwa sababu lazima wafanye utafiti.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, tutawasikia Bunge lijalo la mwezi wa Septemba mtakuwa mmefikia hatua gani na kutazama hii mikopo ili wananchi wetu wasipate athari kubwa, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hoja nyingine ilikuwa inahusu tembo kuvamia makazi ya watu. Sasa tutaenda kwenye hoja hiyo Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Angellah Kairuki. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi.

Mheshimiwa Spika, tarehe 30 Aprili, 2024 uliweza kutoa maelekezo kufuatia hoja ya aliyoitoa Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo, kwamba Wizara ya Maliasili tuweze kuja na taarifa ya hatua gani tumeweza kuchukua na hasa katika suala zima la utatuzi wa changamoto za wanyamapori wakali na waharibifu, ambao katika hoja yake alieleze namna ambavyo wamezagaa katika Wilaya ya Mbarali na alitaja Vijiji vya Igunda, Ikanutwa, Igava na Iluwalanje na katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kutatua changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu ikiwemo Wilaya ya Mbarali, Wizara ya Maliasili na Utalii tumeendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kutekeleza mikakati yetu mikuu mitatu ukiwemo mkakati wa utatuzi wa migogoro baina ya binadamu na wanyamapori ni mkakati wa miaka mitano, mkakati wa kusimamia na kuhifadhi tembo nchini ni mkakati wa miaka 10, pamoja na mpango wetu kazi wa kuongoa shoroba za wanyamapori nchini shoroba 61.

Mheshimiwa Spika, katika hatua hizo tumeendelea kufanya doria kwa ajili ya kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu wakiwemo tembo katika maeneo mbalimbali. Vilevile tumejenga vituo 154 nchi nzima ambavyo vinajumuisha ofisi za Kanda ili kuimarisha shughuli za uhifadhi ikiwemo doria za udhibiti wa wanyamapori wakali na waharibifu hasa tembo katika maeneo yenye changamoto hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya takribani 16 tumeweza kwa mwaka 2022/2023 kujenga vituo 16, lakini kwa mwaka 2023/2024

tumeweza pia katika vijiji mbalimbali na katika Wilaya 15 nako pia kuweza kujenga vituo vya askari wa wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, tumeendelea pia kutoa mafunzo ya mbinu rafiki kwa ajili ya kujikinga na tembo na tumetoa mafunzo haya kwa wakufunzi takribani 1,626 katika Wilaya 28, kufuatia Wilaya ya 44 ambazo zina changamoto kubwa ya wanyamapori wakali na waharibifu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mbarali, tumeendelea kutoa elimu kwa jamii vilevile nako tumeweza kutoa mafunzo ya mbinu rafiki kwa wakufunzi takribani 41, katika vijiji vya Igunda, Iluwalanje, Ikanutwa, Vikae pamoja na Igava lakini pia na maeneo mengine mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa kushirikiana na wadau wetu wa uhifadhi, tumeendela kujenga uwezo wa jamii hasa kushiriki katika uhifadhi ikiwemo na udhibiti wa wanyamapori wakali na waharibifu. Vilevile tumeweza kutoa mafunzo kwa Askari Wanyamapori wa Vijiji takribani 882, tumeweza kuwapa mafunzo ya kujikinga na wanyamapori wakali na waharibifu na lengo letu la kutoa mafunzo haya ni pamoja na kuongeza nguvu na ufanisi katika udhibiti wa matukio ya wanyamapori. Mafunzo haya ni endelevu na tutaendelea kuyatoa Mbarali na kwingineko. Vilevile tutaendelea kuwashirikisha Askari Wanyamapori wa Vijiji katika kufanya doria za kudhibiti wanyamapori hawa katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, vilevile kama Wizara kupitia taasisi zetu za *TAWIRI* pamoja na *TANAPA,* tunaendelea kutoa mafunzo ya ukakamavu, mbinu za kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu kwa askari wetu wa wanyamapori na kwa upande wa Mbarali tumeweza kutoa mafunzo haya kwa vijiji 23 ikiwemo vijiji vile alivyovitaja wakati wa hoja yake na hasa katika vijiji vya kata yetu hii ya Igava.

Mheshimiwa Spika, tunaendelea pia kufuatilia mienendo ya wanyamapori wakali na waharibifu wakiwemo tembo na tunatumia

teknolojia mbalimbali kwa kuwafunga mikanda maalumu ya *GPS collar*. Mpaka sasa katika mifumo mitatu muhimu ya ikolojia tumeweza kufunga mikanda 157 katika mifumo mitano ambayo ni Mfumo wa Ikolojia wa Tarangire - Manyara, Serengeti, Selous - Mikumi, *Lake Natron* - Longido pamoja na Mfumo wa Ikolojia wa Selous-Nyasa.

Mheshimiwa Spika, lengo la kufunga mikanda hii maalumu ni kutuwezesha kuweza kuona mahali tembo walipo na kutuwezesha kuwadhibiti mapema kabla hawajasababisha madhara. Tumebaini mifumo ya ikolojia takribani nane ambayo tunahitaji mikanda takribani 200 na kwa gharama ya shilingi bilioni 3.2, maana yake mkanda mmoja tu kuufunga wa *collar* hiyo, *GPS collar* ya *table* si chini ya shilingi milioni 16.

Mheshimiwa Spika, tumeendelea pia kutangaza namba zetu maalumu za simu kwa ajili ya kutoa taarifa ili wananchi waweze kutoa taarifa zao na kuweza kupata msaada kwa haraka. Tumetoa namba 14, moja ya Wizara, lakini 13 kwa ajili ya ofisi zetu za Kanda. Vilevile tumeendelea na *operation* mbalimbali za kutumia helikopta kwa ajili ya kuweza kuwafukuza tembo ambao wamekuwa wakizagaa kutoka katika hifadhi kwenda katika maeneo mbalimbali ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, tumeshafanya zoezi hili kwa Wilaya ya Nachingwea na Liwale, tumefanya pia kwa Wilaya ya Same, tumefanya pia kwa Wilaya ya Bunda na Mvomero hivi karibuni mwezi Aprili ambako tumeweza kufunga mikanda kwa tembo kiongozi na tayari tumepata mafanikio ambapo tembo zaidi ya 91 tayari wameshaweza kurudishwa hifadhini. Kwa hapa kwa upande wa Wilaya ya Mbarali, tumeshandaa zoezi…

**SPIKA:** Dakika moja malizia Mheshimiwa.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, tumeandaa zoezi kwa upande wa Mbarali tarehe 8 na 9 Mei, tunaenda kufunga mikanda kwa ajili ya tembo watatu na tutakuwa huko kwa ajili ya kuweza kufukuzana na tembo hao ili tuweze kuwafuatilia vizuri

mienendo yao wakati na baada ya zoezi letu hili la kuwaondoa katika makazi.

Mheshimiwa Spika, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea kuongeza vitendea kazi, vilevile tumepanga kunununa helikopta tatu, maana yake hata hii yenyewe tunayoenda kufanya mazoezi haya ni helikopta ambayo tunapata kupitia kwa mdau. Zoezi tu ukichukulia mfano la Wilaya ya Mvomero limetugharimu si chini ya shilingi milioni 70 kuweza kufanya. Vilevile hata ukifunga mikanda hiyo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Angellah, muda wako kengele imeshagonga. Malizia sekunde 30.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru na niendelee kutoa pole kwa wananchi wote ambao wamepata kadhia hii na changamoto, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote kama Wizara tunaendelea kuchukua hatua mbalimbali kuchimba mabwawa kuhakikisha kwamba tembo hawa hawatoki ndani ya hifadhi wakati wa ukame kwenda nje katika maeneo ya wananchi na mazao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile inapotokea madhara tunaendelea kuhakikisha tunalipa vifuta jasho, jambo ambalo hatulifurahii sana, vilevile kuendelea kutumia teknolojia kwa ajili ya kuweza kuwabaini na kuweza kuwarudisha.

**SPIKA:** Haya ahsante.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi hii, nikuhakikishie kwamba tutaendelea kuchukua hatua.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya. Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, ninawaona mmesimama, tuketi.

Waheshimiwa Wabunge, hoja hii mtakumbuka ilikuwa imeletwa na Mheshimiwa Bahati Ndingo, Mbunge wa Mbarali, akilitaka Bunge liweze kuiona hoja kama ni hoja ya dharura ama vipi, lakini nikatoa nafasi ili upande wa Serikali waweze kutoa maelezo, halafu nipime kama ni hoja ya dharura ama inaweza kushughulikiwa katika utaratibu wa kawaida.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimewaona mliosimama ninafikiri mmesimama pengine kutokana na maelezo yaliyotoka, lakini kwa utaratibu wa kawaida nilikuwa nitaka nisikie ili nijiridhishe kama ni hoja ya dharura ama inaweza kushughulikiwa katika utaratibu wa kawaida, kwa sababu hii ni tofauti na hoja hii iliyopita. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa ninawaona mmesimama wengi na kwa muda wetu ulivyo siwezi kuwaruhusu wote kuzungumza, labda Waheshimiwa Wabunge wawili wanaotoka maeneo ambayo yanaathiriwa na kuingiliwa na tembo. Haya kwa sababu nimesema wawili atazungumza Mheshimiwa Tadayo, Mheshimiwa Aida Khenani umeuliza swali leo, kwa hiyo keti atazungumza Mheshimiwa Cecilia Paresso.

Mheshimiwa Tadayo halafu Mheshimiwa Paresso na Mheshimiwa Bahati Ndingo atamalizia. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kupata nafasi hii kuzungumzia hoja hii.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote niishukuru Serikali kwa kuwa pale ambapo tunapata madhara kama haya tunapotoa taarifa mara nyingi huwa wanaitikia, wanakuja na wanatusaidia. Kwa hiyo, niishukuru Serikali kupitia Wizara ya Maliasili ya Utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mimi ambaye Jimbo langu la Mwanga linapakana na Hifadhi ya Mkomazi pamoja na *Tsavo National Park* ya

Kenya, tatizo hili ni kubwa kiasi ambacho tunaona kwamba hatua nyingi za Serikali ambazo inazichukua ni zile za dharura ambazo mara nyingi zinachukuliwa wakati madhara yameshatokea. Ni vizuri zaidi na nimejaribu kusikiliza maelezo ya Serikali kwa siku hii ya leo, tukajielekeza zaidi kwenye sababu hasa ya tatizo hili ni nini?

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mwanachi wa kawaida anachokiona ni kwamba tembo wameongezeka, wamekuwa wengi lakini kama miaka miwili iliyopita taarifa zilikuwa zinaonesha *actually* tembo wamepungua. Upande wa Serikali wanasema kwamba wananchi wameingia kwenye ushoroba na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, sasa kama tembo wameongezeka au wamepungua au wananchi wameingia kwenye shoroba kikubwa ni kwamba tembo wanatoka kwenye maeneo yao wanakuja kwenye maeneo ambayo wananchi wakakaa na hilo ndilo ambalo linatakiwa lishughulikiwe.

Mheshimiwa Spika, sasa ipo namna moja ambayo inasemekana labda tukichimba mabwawa na kadhalika, lakini inaoneka sababu zinatofautiana kwa sababu kwangu mimi sasa hivi kwa msimu wa mvua tembo wamepungua, lakini kule Mbarali ambako pia mvua inanyesha, tembo wameongezeka, kwa hiyo, inaonekana ipo sababu nyingine kubwa zaidi ambayo watafiti wanatakiwa watupe majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba pamoja na Wizara kufanya juhudi kwa sasa suala hili ni mtambuka, linapaswa kuihusisha Serikali nzima. Ukiangalia hata kwa wenzetu kama mmesikia Botswana juzi juzi mpaka Rais wao amewaambia Wajerumani kwamba…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Sekunde 30 malizia Mheshimiwa, kengele imeshagonga.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru.

Mheshimiwa Spika, Rais wa Botswana amewaambia niwaletee tembo 20,000 Berlin waone kama wataendelea kutunga sheria za kuuzia *I mean* ku-*export trophy* ambazo hata zimewindwa kwa uhalali. Marekani hali kadhalika Mheshimiwa Mwenyekiti wangu atakumbuka tulipata nafasi ya kuongea na Wabunge wa *Congress,* kuna sheria inatungwa kule ya kuzuia Wamarekani ku-*import* hizi *trophies* ambazo zimeuzwa kihalali.

**SPIKA:** Haya ahsante sana.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Kwa hiyo, ni suala mtambuka, ninaomba Serikali kwa ujumla ilichukulie hatua. Ninashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika hoja hii.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba sote tunakubaliana umuhimu wa sekta ya utalii kwa nchi yetu, hilo ni jambo muhimu sana. Sekta hii ya utalii na vilivyomo katika utalii ikiwemo hawa tembo wakati mwingine na ndiyo uhalisia imekuwa ni kero na changamoto kubwa sana kwa wananchi wetu katika maeneo mengine. Hiyo mikakati ambayo Mheshimiwa Waziri ameieleza hapa ni mikakati ambayo haitoi suluhisho leo au kesho kwa tembo wakiingia katika maeneo yetu. Wananchi wataendelea kupata hiyo adha, mazao, vifo na vitu vingine ambavyo wanakutana navyo hasa sisi ambao tunatoka katika Wilaya ambazo zinapakana na hifadhi katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama haitoshi lazima twende na Serikali lazima ifikirie mikakati ya zaidi ya haya ambayo inayataja hapa. Mfano, unaposema tunaenda labda Serengeti unampeleka mtalii, je, huyu mtalii anahitaji kuona tembo 1,000 au 10,000? Bila shaka mtalii huyu anahitaji kuona tembo mmoja/wawili ama watatu aridhike, sasa kwa nini Serikali isifikirie kuvuna tembo hawa na kuwaweka kwenye

kanda *(zone)* mbalimbali ili tupunguze hizi athari ambazo wananchi wanazipata katika maeneo ambayo hifadhi inazunguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kama haitoshi, tunahitaji Serikali ije na mkakati wa kupanga ardhi ya nchi hii. Unapoongea habari ya shoroba zimevamiwa na kujengwa ni kwa sababu hakuna mipango mikakati ya matumizi ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna mawasiliano na ushirikiano kati ya sekta ambayo inajua hapa ni shoroba na sekta ya ardhi kwa sababu sekta ya ardhi inagawa ardhi, mtu anaenda kujenga kumbe ni shoroba, hakuna hiyo mipango mikakati, ni muhimu sana ikazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho, wananchi wakipata adha hii hiki kinachoitwa fidia, kifuta jasho na kifuta machozi ni hadithi ambayo haitekelezeki. Mwananchi anaharibiwa mazao, anajaziwa fomu, anafanyiwa tathmini anaambiwa atapewa kifuta jasho, miaka na miaka hakuna kifuta jasho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, familia inapoteza mtu kwa kuuawa na tembo, hakuna hicho kifuta machozi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele imeshagonga Mheshimiwa ahsante sana.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, ni kidogo na hakiendani na uhalisia na pia hakitolewi kwa wakati. Hili ni janga, tunahitaji wananchi wetu unapomwambia utalii ni muhimu kwa Taifa a-*feel* huo umuhimu wa Taifa kwa yeye kuishi kwa amani katika mazingira yetu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana, shukrani. Mheshimiwa Jerry Silaa.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, mimi ninaomba kwa dakika chache nichangie

hoja ambayo Mheshimiwa Angellah Kairuki, Waziri wa Maliasili na Utalii, ametoa Taarifa ya Wizara yake.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba sisi Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ni wadau katika mpango wa kuhakikisha kwenye yale maeneo yenye ushoroba ambao unaunganisha hifadhi na hifadhi kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii tunafanya kazi ya kutengeneza mipango ya matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, kazi hii tunayoifanya ni kuhakikisha vijiji vile vinavyopakana na hifadhi vinakuwa na mpango wa matumizi bora ya ardhi. Vilevile kuendelea kusisitiza kwa viongozi wa vijiji na viongozi wa Serikali kwenye wilaya ambazo zina vijiji vinavyopakana na hifadhi kuisimamia ile mipango ya matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, nia hasa ni kuhakikisha wanyama wanavyopita kwenye zile shoroba hawaingiliani na shughuli za kijamii za wananchi na wakati mwingine kulazimika kuingia kwenye maeneo ya wananchi. Nalithibitishia Bunge lako kuwa maeneo yote ambayo tayari Wizara ya Maliasili na Utalii imetushirikisha tumeshafanya mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa vijiji zaidi ya 21.

Mheshimiwa Spika, pia zipo shoroba nyingine ambazo tunaendelea kufanyia kazi na sisi tunaamini kama mipango hii itakamilika na vijiji hivi vikazingatia matumizi bora ya ardhi kwenye vijiji basi inaweza ikapunguza kwa upande wa matumizi ya ardhi mwingiliano baina ya wanyama pori na wananchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Bahati.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, mimi ninashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini ni dhahiri kwamba Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori tuna haja ya kufanya utafiti kwa sababu kila tembo anapopita tunaambiwa ni ushoroba.

Sasa hivi *style* ya tembo ambao wako Mbarali wanatoka hifadhini, wanaenda kuvamia mazao ya wananchi na wanarudi hifadhini. Miaka ya nyuma tulitarajia tembo wakipita kutoka Hifadhi ya Ruaha kwenda Kipengere, lakini kwa sasa hawa tembo ni dhahiri wamenogewa na mazao ya wananchi. Kwa hiyo, ipo haja hii Taasisi ya Tafiti ifanye tafiti na waje na majibu sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali inafanya uwekezaji mkubwa, inajenga vituo kweli, kwa mfano, Mbarali laiti tungevitumia vizuri vituo vyetu kama kile cha Ikoga na kituo chetu kile cha Nyota kingeweza kudhibiti tembo. Leo hata gari la doria hakuna pale, watawezaje kupambana na tembo?

Mheshimiwa Spika, sisi tunawapigia simu tukishaona, wananchi wakishaona tembo wanaanza kutoka hifadhini wanatoa taarifa, lakini hata vifaa kwenye hivi vituo hakuna. Mheshimiwa Waziri, Wizara ya Maliasili imefanya kazi kubwa, ime-*train* vijana wengi kuwapa mafunzo ya kupambana na hawa, sisi Mbarali tulivyowasiliana na Wizara wakasema hawana askari wa kutosha. Tukawaambia tunaomba mtumie hawa vijana mliowapa mafunzo, wameomba shilingi milioni 25, huu mwezi wa tatu hata malipo ya kununua vifaa kwa wale vijana hawapewi, watafanyaje kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni dhahiri janga hili ni kubwa, pamoja na kazi kubwa ambayo Serikali inafanya, lakini ni lazima tuweke mkakati wa dharura. Wananchi wetu wanapoteza maisha, kaka yangu hapa wa Nachingwea watu 16 wamepoteza maisha. Mbarali sisi Ndugu Innocent tumemzika wiki mbili zilizopita amefariki kwa kukanyagwa na tembo. Kwa hiyo, hili jambo ni la dharura, ni lazima Serikali ije na mpango wa kutuhakikishia usalama wa Wana-Mbarali na maeneo mengine. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Spika, samahani, kwa kumalizia, wananchi wa Mbarali kwenye vijiji hivyo nilivyotaja, mazao yao yote kama nilivyokwambia tatizo hili limeanza toka mwezi wa pili,

hakuna kilichofanyika. Mazao yao yote yameliwa, tunaomba Serikali ione haja ya kuwasaidia chakula wananchi hawa, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri kuna hoja hapo ya fedha zilizoombwa kwa sababu askari hawatoshi. Kwa hiyo, wale wameomba walioko kule ili wasaidie kufukuza hao tembo.

Pia nakumbuka na Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka katika taarifa hii Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii zile fedha zilizokuwa zimetafutwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambazo zilikuja kipindi kile cha UVIKO-19 Wizara mbalimbali zilipewa fedha. Wengine vituo vya afya vikajengwa, wengine shule, wengine madarasa, Maliasili walikuwa wanunue magari kama nakumbuka vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, niko sahihi? Washa kisemeo.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, uko sahihi.

**SPIKA:** Ilikuwa wanunue magari?

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, yah.

**SPIKA:** Yameshakuja yale magari au bado?

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, magari yalikuwa yananunuliwa kwa maana ya kila taasisi ndani ya Wizara ilikuwa ina idadi yake ya magari ya kununua. Kwa taarifa tulizonazo kwenye Kamati sehemu kubwa ya magari yale yaliyokuwa yameagizwa yalishafika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kuna hoja ya huko Mbarali ambako tembo wamekula, hakuna gari ya doria na pia fedha haijakwenda.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwa upande wa hoja ya magari nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ipo katika mpango. Vilevile pamoja na Mradi wa UVIKO, tunao pia mradi ambao tumesaini na Taasisi ya *GIZ* wa takribani shilingi bilioni 13 na katika mradi huo vitendea kazi ikiwemo pamoja na magari pia imo.

Mheshimiwa Spika, pili, tutakapokuja kusoma bajeti yetu, tunashukuru tayari tumekuwa kila mwaka tukifanya makusanyo kupitia taasisi zetu za uhifadhi na tunayo asilimia tatu ya makusanyo ya taasisi zetu inapaswa kwenda katika uhifadhi. Bahati nzuri safari hii tumeruhusiwa kwamba hazitaenda kwenye Mfuko Mkuu, tutapata *retention* ya kubaki na fedha hizo kwa ajili ya kuweza kufanya hatua au afua za moja kwa moja. Tunaamini kupitia hatua hiyo kuanzia mwezi Julai basi itatuwezesha kuchukua hatua za haraka ikiwemo vitendea kazi kama magari, vilipuzi, baruti pamoja na vifaa vingine. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge hilo litatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ajira kwa miaka mitatu tumepanga kutoa ajira takribani 1,187 na ndiyo maana kwa sasa kwa sababu hatuwezi tukaajiri watumishi wengi zaidi kwa wakati mmoja tukitambua ukubwa wa maeneo yetu ya uhifadhi, tunaendelea kushirikiana na halmashauri zetu kuwatumia askari wanyamapori wa vijiji kwa kuwapa mafunzo, kuwapa sare, kuwapa vifaa na kuwapa posho kidogo ili waweze kutusaidia katika zoezi hili la doria kwa kushirikiana na askari wetu wa uhifadhi na askari wengine wa mgambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge tutalifuatilia hilo pamoja na fedha nyingine zinazohitajika katika maeneo mbalimbali. Azma yetu ni kuhakikisha kwa kadiri inavyowezekana kuleta ufanisi kwa watendakazi wetu kule chini. Tunajua wao ndiyo wanafanya kazi kubwa sana tukitambua changamoto hii ambayo imeenea katika maeneo mengi.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kama utaniruhusu nijibie zote?

**SPIKA:** Hoja ya nini?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, alitoa hoja ya *TAWIRI* kuendelea na utafiti, nimhakikishie…

**SPIKA:** Hiyo ametoa ushauri, kwa hiyo, ule unapokea tu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, *okay*, napokea ushauri wote uliotolewa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema awali hoja hii ilikuwa imeletwa kama hoja ambayo niitazame kwa mujibu wa kanuni zetu ili tuweze kuona kama Bunge linaona hoja hiyo ijadiliwe kama hoja ya dharura.

Sasa kwa taarifa aliyoitoa Mheshimiwa Waziri kabla hatujaanza michango hapa, ni dhahiri kwamba Serikali inaendelea na utekelezaji wa mambo mbalimbali ili wale tembo wasilete athari kwa wananchi. Ule utekelezaji sasa ndiyo wenye changamoto, lakini kwa maana ya mpango kuwepo na utekelezaji upo unaendelea.

Waheshimiwa Wabunge, changamoto ni kama hizi za kuchelewesha fedha, mkishaambiwa tembo wameingia mkikaa miezi mitatu sasa hao tembo si watakuwa wamemaliza chakula? Kwa hiyo, hata kama haziwezi kupelekwa zote ni dhahiri lazima mnahitaji majibu ya haraka kwenye hoja kama hizi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri sijajua sasa ni kitengo gani huko kwako kinachoshughulika na haya. Ni muhimu kutazama hayo maombi yanayotoka kwenye maeneo hasa ambayo hayana hao wahifadhi wenyewe ili wale ambao mmewapa mafunzo wafanye hiyo kazi na ili weweze kufanya kazi lazima wawezeshwe, kwa sababu

kama hakuna gari la uhifadhi maana yake lazima wakodi gari. Kama wanakodi gari pesa watatoa wapi kama hawakupewa? *(Makofi)*

Kwa hiyo, hayo ni mambo ambayo inabidi mfanye marakebisho kidogo. Majibu yawe yanatoka kwa haraka hasa kwa yale maeneo ambayo ninyi hamna watu wenu moja kwa moja.

Suala la pili lililozungumzwa hapa ni kuhusu hii fedha inayoitwa kifuta jasho. Kama hivi tembo wamekula mazao nadhani ndani ya Serikali mna vitengo vyenu tofauti mtafanya ushirikiano ili wananchi ambao walikuwa wamejitafutia chakula na sasa amekula mnyama ambaye tunamhifadhi, basi tuone namna ya kuwahifadhi hawa binadamu ambao wanapata madhara. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, maneno haya sasa ni kwa maeneo yote ambayo yanapata athari za hawa tembo, si kwamba ni hoja tu ya Mbarali. Kwa hiyo, tusaidie maeneo yote Mheshimiwa Waziri na kama ulivyosema bajeti yako inakuja, mojawapo ya maeneo ambayo yanapaswa kutengewa fedha za kutosha ni hili eneo ambalo linaleta athari kwa wananchi kutoka kwa wanyama tembo (ndovu) na wanyama wengine, maana hapa nimeletewa ujumbe kwamba kuna maeneo ambayo wananchi wanasumbuliwa na tumbili na kwingine wanasumbuliwa na nyani. Je, na wao walete hoja yao hapa? *(Makofi)*

Kwa hiyo, ni maeneo yote ya Waheshimiwa Wabunge ambayo yamepakana na hifadhi, lakini pia yale ambayo na wanyama wa kila aina maadamu wanaleta athari kwa wananchi, hayo myafanyie kazi.

Waheshimiwa Wabunge, nimeletewa pia ujumbe hapa kwamba wapo viongozi wengine ambao hawakupata nafasi ya kutambuliwa wakati tukiwatangaza hapa.

Kwanza ni Ndugu Riziki Kingwande ambaye ni Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Wanawake Tanzania upande wa Bara, karibu sana. *(Makofi)*

Mgeni mwingine ambaye nimeletewa ujumbe kwamba hakutambulishwa ni Mheshimiwa Hawa Ghasia ambaye ni Mjumbe wa Kamati ya Utekelezaji ya Umoja wa Wanawake Tanzania. *(Makofi)*

Ahsante sana, pia huyu ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Masoko Kariakoo. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wageni wa Mheshimiwa Waziri tena na hawa ni Wakuu wa Wilaya ambao Miradi ya Umwagiliaji inatekelezwa katika maeneo yao. Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya karibuni sana Bungeni na ahsanteni sana. *(Makofi)*

Wapo pia Madiwani na Viongozi wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Mkoa wa Tabora na Wilaya ya Nzega na hawa wanaongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Tabora, wote wasimame kwa pamoja. Mkuu wa Mkoa pamoja na viongozi wote wa chama kutoka Mkoa wa Tabora na wale wa Wilaya pia. Haya hapa na Waheshimiwa Madiwani wapo, kwa hiyo, naamini na wao wamesimama. Haya ahsanteni sana na karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo sasa tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimwite sasa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, aje awasilishe hoja yake.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nakushukuru kwa fursa, lakini naomba hotuba yote pamoja na

marekebisho yake iweze kuingia katika *Hansard* za Bunge na Kumbukumbu za Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu baada ya kuzingatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, sasa lijadili na kukubali kupitisha utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kufikia siku ya leo tukiwa na afya njema ili tuweze kujadili bajeti hii ya sekta ya kilimo ambayo inagusa maisha ya wakulima kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kusimamia shughuli za kilimo nchini. Ninamwahidi Mheshimiwa Rais na Watanzania kuwa nitatumia uwezo wangu wote kwa uaminifu na uadilifu mkubwa kuhakikisha kuwa kilimo kinachangia kikamilifu katika kuhakikisha usalama wa chakula na lishe nchini, kulisha wengine kibiashara na kuinua kipato cha wakulima ili kupunguza umasikini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaungana na Wabunge wote kutoa pole kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa msiba mkubwa tulioupata wa kuondokewa na aliyekuwa Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili, Hayati Alhaji Ali Hassan Mwinyi. Ninatoa pole pia kwa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, watoto na ndugu wote wa Hayati Alhaji Ali Hassan Mwinyi na Watanzania wote. Tutaendelea kuuenzi mchango mkubwa wa Rais wetu wa Awamu ya Pili katika ujenzi wa Taifa letu kwa kuongoza mageuzi ya kiuchumi kutoka uchumi hodhi kuwa uchumi

unaoongozwa na misingi ya soko uliowezesha kuimarisha ushirikiano na mashirika ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, ninatoa pole kwa Mheshimiwa Rais, Watanzania wote na familia kwa kuondokewa na aliyekuwa Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa. Tutaendelea kumkumbuka kwa umahiri wake mkubwa katika usimamizi, uwajibikaji, ujasiri, ushupavu na ufanyaji wa maamuzi katika kuleta maendeleo kwa Taifa. Mimi binafsi ninamshukuru kwa dhati kwa kunilea na kunikuza kisiasa na kiuongozi. Mafunzo yake ya msingi yamenijenga kuwa na utii kwa Taifa letu, chama chetu na viongozi wetu wakuu. Aidha, yanatufundisha kuwa kiongozi anapaswa kuwa na maono, kufanya maamuzi, kuyasimamia maamuzi hayo na kuwa na msimamo kwenye mambo ya msingi kwa maendeleo ya Taifa letu. Daima tutaendelea kumkumbuka katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, ninatoa pole kwa familia na wananchi wa Jimbo la Mbarali kwa kuondokewa na aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo Mheshimiwa Francis Leonard Mtega. Vilevile ninatoa pole kwa familia na wananchi wa Jimbo la Kwahani Zanzibar kwa kuondokewa na aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil. Ninaungana na wewe na Wabunge wenzangu na Watanzania kwa ujumla katika kuomboleza misiba hii mikubwa.

Mheshimiwa Spika, ninatoa pole kwa wananchi wa Jimbo la Rufiji na wakulima wa Rufiji, Karatu, Mlimba na Hanang pamoja na maeneo mengine yaliyopatwa na maafa. Wizara ya Kilimo imelichukulia suala hilo kwa uzito mkubwa kwa kutuma timu ya wataalamu kufanya tathmini ya ardhi na mazao yaliyoathiriwa na mafuriko, kuainisha mahitaji ya chakula na pembejeo za kilimo, kutoa elimu kupitia maafisa ugani kuhusu kilimo cha mazao ya muda mfupi na pia kuhakikisha wadau wanafikisha misaada ya chakula na pembejeo.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa kipaumbele katika uendelezaji wa sekta ya kilimo. Hatua hiyo imewezesha kuongeza hamasa ya wadau wa kilimo kuwekeza katika maeneo mbalimbali ya mnyororo wa thamani wa mazao.

Mheshimiwa Spika, aidha, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye pamoja na majukumu yake makubwa aliyonayo, amekuwa mstari wa mbele katika kusisitiza kilimo endelevu kinachozingatia utunzaji wa mazingira, kuimarisha usalama wa chakula na kupambana na umasikini na yeye mwenyewe kufanya shughuli za kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ninapenda kutumia fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa hapa Bungeni wakati wa kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2024/2025. Hotuba hiyo imetoa maelezo na maelekezo kuhusu maendeleo ya sekta ya kilimo hususani katika uendelezaji wa kilimo cha umwagiliaji, maendeleo ya ushirika na upatikanaji wa masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nitumie fursa hii kumpongeza Dkt. Doto Mashaka Biteko, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninaamini kupitia yeye uratibu wa shughuli za kilimo utaendelea kuimarika na kuwezesha kufikiwa kwa malengo yaliyowekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikupongeze wewe binafsi kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa *IPU*. Nimpongeze Naibu Spika Mheshimiwa Zungu pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa uongozi wenu wenye weledi, ujuzi na ustadi mkubwa ambao umewezesha utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya nchi yetu ikiwemo sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, niwapongeze Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Jimbo la Njombe na Mwenyekiti wa

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Kilimo na Mifugo pamoja na Mheshimiwa Joseph Kizito, Mbunge wa Jimbo la Madaba na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kwa kuchaguliwa na Bunge kuwa Wenyeviti wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ninaipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa ushauri, maoni na miongozo mbalimbali ya kuendeleza sekta ya kilimo. Niwahakikishie Kamati kuwa maoni na ushauri wao umezingatiwa katika kipindi chote cha utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2023/2024 na maandalizi ya mpango wa mwaka 2024/2025. Aidha, ninawapongeza Wabunge wote kwa umahiri wenu mkubwa katika kuchangia mijadala inayoendelea katika Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge hili la Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee ninampongeza Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Jimbo la Tunduma kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Kilimo. Ninamshukuru sana kwa ushirikiano anaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile ninampongeza aliyekuwa Naibu Waziri wa Kilimo Ndugu Anthony Peter Mavunde, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Madini. Ninamshukuru sana kwa ushirikiano wake katika kipindi chote alichofanya kazi katika Wizara ya Kilimo na ninamtakia mafanikio mema katika utekelezaji wa majukumu yake mapya, kwani sina mashaka naye katika uzalendo wake na uwezo wake wa kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo - Ndugu Gerald Mweli, Naibu Katibu Mkuu - Ndugu Hussein Mohamed Omar, pamoja na wakurugenzi wote wa Bodi na Wakala zilizo chini ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee ninawashukuru wakulima wote na sekta binafsi kwa mchango wao mkubwa katika

kuhakikisha kuwa nchi inakuwa na usalama wa chakula na kuongeza uuzaji wa mazao nje ya nchi. Pia ninawashukuru taasisi za fedha, wabia wa maendeleo na asasi zisizo za Serikali kwa mchango wao wa kukuza sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, ninatoa shukrani za kipekee kwa wananchi wa Jimbo la Nzega Mjini kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kipindi chote cha kuwawakilisha hapa Bungeni. Aidha, ninawapongeza kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali ambazo zinalenga katika maendeleo ya jimbo letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ninawashukuru sana watumishi wa Halmashauri ya Mji wa Nzega, Mkurugenzi, viongozi na Madiwani kwa ushirikiano wao wanaoendelea kunipatia katika utekelezaji wa majukumu yangu. Ninawaahidi kuendelea kuwatumikia kwa juhudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sekta ya kilimo katika mwaka 2023 imekua kwa 4.2% kutoka 2.7% ya mwaka 2021 na imechangia 26.5% katika Pato la Taifa ikilinganishwa na 26.2% katika mwaka 2022. Vilevile imetoa ajira 65.6%, imechangia 65% ya malighafi za viwanda na kuendelea kuchangia 100% ya upatikanaji wa chakula. Mauzo ya mazao ya kilimo nje ya nchi katika mwaka 2022/2023 yamefikia dola bilioni 2.3 ikilinganishwa na dola bilioni 1.2 mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa mazao ya chakula katika msimu wa mwaka 2022/2023 ulifikia tani milioni 20.4 ikilinganishwa na tani milioni 17.1 katika msimu wa mwaka 2021/2022 sawa na ongezeko la 19%. Katika kipindi hicho uzalishaji wa mazao ya nafaka ulikuwa 11.4% na mazao yasiyo ya nafaka 8.9%. Uzalishaji huu ulitosheleza mahitaji ya chakula ya tani milioni 16 kwa mwaka 2023/2024 na kuwepo kwa ziada ya tani milioni nne na kulifanya Taifa letu kujitosheleza kwa chakula kwa 124% ikilinganishwa na utoshelevu wa 114% kwa msimu wa mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 na mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imeendelea kujenga na kukarabati miundombinu ya umwagiliaji yenye jumla ya hekta 256,185. Kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu hiyo kutaongeza eneo la umwagiliaji kutoka hekta 727,000 mwaka 2020/2021 hadi kufika hekta 983,000 ambazo ni sawa na 81% ya hekta milioni 1.2 ambayo ni maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, hadi kufika Aprili, 2024 vyama vya ushirika 7,522 vilikaguliwa wakati lengo likiwa ni vyama 7,300. Aidha, Tume imeendelea kuratibu uanzishwaji wa Benki ya Ushirika ambapo jumla ya hisa zenye thamani ya bilioni 17.1 zimenunuliwa sawa na 85% ya mtaji hitajika wa shilingi bilioni 20.

Mheshimiwa Spika, ninawasilisha hotuba hii ambapo Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ikiwa imetimiza miaka mitatu. Katika mwaka wa fedha 2023/2024 nilisimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni 970 kwa ajili ya utekelezaji wa vipaumbele vitano ambavyo ilikuwa ni kuongeza uzalishaji na tija, kuongeza ajira zenye staha na ushiriki wa vijana katika sekta ya kilimo, kuimarisha usalama wa chakula, kuimarisha upatikanaji wa masoko, mitaji na mauzo ya nje na kuimarisha maendeleo ya ushirika na jumla ya vipaumbele 27 vilitekelezwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara imetekeleza vipaumbele na mikakati yote kama tulivyowaahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 shilingi bilioni 970 ziliombwa kwa mafungu yote; ambapo shilingi bilioni 767 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 202 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Aprili shilingi bilioni 522.45 sawa na asilimia 53.8 ya fedha zilizoidhinishwa zimetolewa. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 421.7 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi

ya maendeleo na shilingi bilioni 100 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ilikadiria kukusanya mapato ya shilingi bilioni 16.67 kutokana na vyanzo mbalimbali. Hadi Aprili, 2024 shilingi bilioni 6.47 sawa na 38.8% ya makadirio zimekusanywa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafanikio, leo ninasimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha mafanikio ya utekelezaji wa bajeti hiyo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kutokana na kutofautiana kwa takwimu za mazao zinazopatikana katika mifumo mbalimbali ya Serikali na kwa kuwa shughuli za kilimo msingi wake mkubwa ni kukuza uchumi wa nchi na kuondoa umasikini, Wizara imeyagawa mazao ya kilimo katika makundi mapya manne ambayo ni mazao ya chakula (mazao ya nafaka, bustani, mafuta na mazao ya asilia ya kiashara). Ili takwimu hizo ziweze kushabihiana na mifumo ya Serikali ikiwemo mifumo ya Benki Kuu, Mamlaka ya Mapato na Ofisi ya Taifa ya Takwimu huzingatia makundi hayo, hivyo kuongeza ufanisi katika kupanga mipango ya kuendeleza sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu mazao ya chakula yanayojumuisha mazao 12 ambayo yanatengeneza Mfuko wa Mazao ya Chakula *(food basket);* uzalishaji wa mazao hayo katika msimu wa 2022/2023 ulifikia tani milioni 20 ikilinganishwa na tani milioni 17 katika msimu wa mwaka 2021 sawa na ongezeko la 19%. Uzalishaji wa mazao ya bustani umeongezeka kutoka tani milioni 7.9 hadi tani milioni 8.43 katika mwaka 2022/2023 sawa na ongezeko la 6.7% dhidi ya lengo la tani milioni 6.26.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa mazao ya mafuta umefika tani milioni 2.14 ikilinganishwa na tani milioni 1.70 za msimu wa kilimo 2021/2022 sawa na ongezeko la 25%. Aidha, uzalishaji wa mazao ya asilia ya kibiashara umeongezeka kutoka tani milioni 1.12 mwaka

2023/2024 hadi kufika tani milioni 1.26 sawa na ongezeko la 78.5% ya lengo la kuzalisha tani milioni 1.6 na uzalishaji unaendelea.

Mheshimiwa Spika, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa sasa Tanzania ni mzalishaji wa pili wa tumbaku Afrika kutoka katika kundi linaloitwa *others* ambapo uzalishaji umeongezeka kutoka tani 70,690 mwaka 2021/2022 na sasa kuna uzalishaji wa tani 125,592 msimu ujao tunatarajia kufika tani 200,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati wa utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2023/2024 nchi yetu ilikabiliwa tatizo la upungufu wa sukari ambao ulitokana na mambo makubwa mawili; mabadiliko ya tabianchi ambayo mvua za *El-Nino* ziliathiri uzalishaji na tabia za wafanyabiashara kutengeneza uhaba *(artificial scarcity)* kwa kutokuingiza sukari ya kuziba pengo kulingana na vibali vya uagizaji au kwa kuhodhi sukari katika ghala zao ili bei ipande.

Mheshimiwa Spika, hali hiyo ilisababisha kupanda kwa bei ambapo kipindi cha Januari, 2024 wastani wa bei ya jumla kwa wazalishaji wakubwa nchini ilikuwa ni kati ya shilingi 3,800 mpaka 4,000. Aidha, kwa wauzaji wa jumla ilikuwa ni kati ya shilingi 4,500 na 5,000 na bei ya rejareja katika baadhi ya maeneo ilifikia kati ya shilingi 6,000 mpaka 10,000 kwa kilo moja katika maeneo mengi hali ambayo ilikuwa inahatarisha usalama wa nchi na uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na tatizo hilo, Wizara ilichukua hatua zifuatazo: -

(a) Kutangaza bei elekezi ya sukari nchi nzima ambayo ilikuwa ni kati ya shilingi 2,600 mpaka 3,200 kwa rejareja;

(b) Kuratibu uingizwaji wa sukari nchini tani 410,000 kupitia *NFRA* na wazalishaji wa sukari ilitoa ambapo uingizaji wa sukari ulianza mwezi Januari na utaenda kwa awamu hadi mwezi Disemba. Uingizaji wa sukari hiyo utazingatia ugavi, mahitaji na uwezo wa viwanda vya sukari kurudi katika uzalishaji;

(c) Kufanya marekebisho ya Kanuni ya *NFRA* na kuiweka sukari kuwa sehemu ya usalama wa chakula; na

(d) Kuanza marekebisho ya Sheria ya Sukari Na. 6 ya mwaka 2001 kwenye Sheria ya Fedha ya mwaka 2024 ili kuiwezesha *NFRA* kununua sukari na kuihifadhi sukari kwenye Hifadhi ya Chakula cha Taifa, kunusuru hali ya upatikanaji wa sukari inapotokea tatizo la aina yoyote. Hatua hiyo inalenga kuondoa uhodhi kwa baadhi ya wenye viwanda bila kuathiri dhamira ya Serikali ya kulinda viwanda vya ndani.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuvilinda viwanda vya ndani na kuwalinda wakulima wa miwa, lakini ulinzi huo hautakuwa kwa gharama ya kuwatesa Watanzania milioni 61. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu ninaomba niwaambie wamiliki wa viwanda vya sukari nchini kuwa sukari ni chakula cha Watanzania masikini na ni suala la usalama wa nchi. Hivyo, Serikali haitavumilia wala haitaruhusu tena tatizo hilo kujirudia. Ni wajibu wetu kuvilinda viwanda vya ndani, lakini ni wajibu wetu pia kuwalinda Watanzania na usalama wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu ninawaomba wenye viwanda wafanye mabadiliko ya chama chao cha wazalishaji *(Tanzania Sugar Producers Associations)* ili kuhakikisha umoja huo unakuwa na uwakilishi wa wazalishaji wakubwa na wadogo kama ambavyo Serikali imewaelekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa mazao umechangiwa na kuongezeka kwa tija ya mazao kama inavyoonekana kwenye hotuba yangu ukurasa wa 64.

Mheshimiwa Spika, katika kufikia mafanikio hayo Wizara imetekeleza mikakati mingine ifuatayo: -

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la kuimarisha utafiti; jumla ya shilingi bilioni 40.73 zilitengwa kwa ajili ya kutafiti na kuzalisha

mbegu za awali pamoja na kujenga na kukarabati miundombinu ya utafiti. Ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili, 2024 jumla ya mbegu tani 787 za awali zimezalishwa, ujenzi wa Kituo cha Utafiti cha Kahawa cha Mwayaya, Buhigwe, Kigoma umekamilika, ujenzi wa maabara ya kuzalisha miche kwa njia ya chupa ya *TARI* Mlingano umefika 98%, ukarabati wa maabara ya udongo *TARI* Mlingano umefika 80% ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji katika vituo 12 vya utafiti yenye ukubwa wa hekta 874 umefika wastani wa 37%.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uzalishaji na usambazaji wa mbegu, jumla ya shilingi bilioni 43.03 zilitengwa kwa ajili ya uzalishaji na usambazaji wa mbegu na miche bora, kuimarisha miundombinu ya uzalishaji wa mbegu na ununuzi wa dhana za kilimo.

Mheshimiwa Spika, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili, 2024 upatikanaji wa mbegu bora ulifika tani 68,473 sawa na 53.64% ya mahitaji ya mbegu kwa mwaka ambapo uzalishaji wa ndani ulifika tani 49,000 dhidi ya tani 33,000 zilizokuwepo mwaka wa fedha uliopita. Aidha, tani 1,619 za mbegu bora za ngano zimepatikana na tani 1,015 zimesambazwa kwa wakulima katika mpango wa ruzuku; tani 1,974 za mbegu bora za alizeti zimepatikana na tani 725 zimesambazwa kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku na jumla ya miche milioni 29 ya mazao mbalimbali imezalishwa na kusambazwa kwa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji yenye ukubwa wa hekta 805.5 iliyoanza mwaka 2022 na hekta 795 iliyoanza mwaka 2023/2024 ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Shamba la Msimba hekta 200 ujenzi umefika 45% na shamba la Arusha hekta 200 umefika 55%; Shamba la Kilimi hekta 200 ujenzi umekamilika; Bwawa lenye ujazo wa lita milioni 45 katika shamba la mbegu Arusha ujenzi umekamilika; Bwawa lenye ujazo wa lita milioni 45 katika shamba la Msimba umefikia 70% na uwekaji wa miundombinu ya umwagiliaji kwa njia ya matone katika Shamba la Tengeru umekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uwekezaji kwenye huduma ya ugani jumla ya shilingi bilioni 15 zilitengwa kwa ajili ya shughuli za ugani. Naomba kulitaarifu Bunge lako kuwa vishikwambi 4,446 vimenunuliwa ambapo vishikwambi 946 vimesambazwa kwa Maafisa Ugani katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Tanga na usambazaji unaendelea; leseni za kudumu 143 zimenunulia ili kuwezesha *soil scanner* 143 kufanya kazi iliyokusudiwa na huduma ya upimaji wa afya kwa wakulima wadogo imeanza na ni bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia visanduku vya ugani 1,000 vimenunuliwa na kusambazwa kwa Maafisa Ugani 1,000; usanifu wa nyumba za Maafisa Ugani umekamilika na taratibu za ujenzi wa nyumba 50 za kwanza katika halmashauri 46 zimeanza; magari 51 na pikipiki 550 zimenunuliwa kwa ajili ya Maafisa Ugani ngazi za mkoa na halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika eneo la upimaji wa afya ya udongo na kutoa ruzuku ya mbolea, shilingi bilioni 174.3 zilitengwa kwa ajili ya kupima afya ya udongo na kuratibu utoaji wa ruzuku ya mbolea. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa mashamba yenye ukubwa wa hekta 438,000 yakiwemo mashamba ya *BBT* yamepimwa afya ya udongo katika Mikoa ya Tanga, Manyara, Simiyu, Dodoma, Mbeya, Kagera, Kigoma, Njombe, Pwani na Tanga na kati ya mashamba hayo hekta 49,155 zimepimwa afya ya udongo kwa kutumia *soil scanner* zilizosambzwa katika halmashauri.

Mheshimiwa Spika, tani 1,000,005 za mbolea zimepatikana sawa na 123% ya makadirio ya mahitaji ya tani 848,000 kwa mwaka wa fedha huu na tani 471,839 zenye thamani ya shilingi 136,000,000 zimesambazwa kwa wakulima kupitia mpango wa ruzuku. Aidha, mbolea tani 92,134 zenye thamani ya shilingi bilioni 13.7 zimetolewa kama ruzuku kwenye zao la tumbaku.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeiwezesha *TFC* mtaji wa shilingi bilioni 40 na kufanya mtaji wake kuwa shilingi bilioni 46 kwa ajili ya kununua na kusambaza mbolea. Tani 25,000 zimenunuliwa na kusambazwa kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku katika mikoa 26.

Mheshimiwa Spika, madeni ya mwaka 2015/2016 ya mawakala wa pembejeo za kilimo yenye thamani ya shilingi bilioni 42.38 yamelipwa, madeni ya wazabuni wa pamba ya shilingi bilioni 22.09 yamelipwa, kati ya madeni ya shilingi bilioni 78.1 yaliyokuwa yamehakikiwa na kukubaliwa mwaka 2023. Aidha, wanunuzi wa pamba wamelipwa shilingi bilioni 20.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la uwekezaji wa kujenga na kukarabati miundombinu ya umwagiliaji, jumla ya shilingi bilioni 361.5 zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi 780 ya umwagiliaji ikiwemo kukamilisha miradi 133 iliyoanza katika mwaka wa fedha 2022/2023 na kuanza utekelezaji miradi 647 iliyopangwa kutekelezwa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili, 2024 jumla ya miradi 231 kati ya 788 iliyopangwa kutekelezwa mwaka 2022/2023 na 2023/2024 imeendelea kutekelezwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika skimu 20 kati ya 25 umefika asilimia 40; ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji katika skimu 29 kati ya 30 umefika 35%; ujenzi wa mabwawa 14 ya umwagiliaji umefika 50%; upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mabonde matano kati ya 22 yenye hekta 300,005 umekamilika; upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa skimu 14 zenye jumla ya hekta 35,000 kati ya skimu 44 umekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ujenzi wa miundombinu ya skimu mpya tisa zenye ukubwa wa hekta 14,000 kati ya skimu 28 umeanza; ukarabati wa miundombinu ya skimu tatu zenye jumla ya hekta 2800 kati ya 18 umeanza; ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya pamoja matatu kati ya sita unaendelea; wakandarasi sita wamepatikana kwa ajili ya kuanza ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika skimu kumi zenye ukubwa wa hekta 14,000 na mabonde mawili ya kimkakati; upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mabwawa 18 umekamilika, mabwawa19 unaendelea na mabwawa 53 upo katika hatua za kusaini mikataba; upembuzi

yakinifu na usanifu wa kina wa skimu 14 kati ya 240 zenye ukubwa wa hekta 14,000 umekamilika; mapitio ya skimu 13 kati ya 255 za ukarabati yenye hekta 21,000 umekamilika na ujenzi wa Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili na Ukusanyaji wa Ada kwa huduma za *NIRC* umekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu uanzishwaji wa vituo jumuishi vya kutoa huduma za zana za kilimo, jumla ya shilingi bilioni moja zilitengwa kwa ajili uanzishwaji wa vituo vitatu vya kutoa huduma za zana kilimo, ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa ujenzi wa kituo cha kutoa huduma ya zana za kilimo kwa wakulima Mtanana, Kongwa umefika 9% wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa vituo jumuishi vya zana za kilimo vitano katika katika Halmashauri za Chamwino, Madaba, *Songea DC,* Itilima, Mbarali na Korogwe wamepatikana, Bodi ya Pamba pamoja na Chama cha Wachambuaji wa Pamba wamenunua matrekta 200.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la kuongeza ajira; katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ilipanga kutengeneza ajira 428,000 kupitia mpango wa *BBT* ikiwa na malengo ya kuongeza ajira, mitaji, teknolojia na umilikishaji wa ardhi. Ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara imeanza kutekeleza programu ya *BBT* kupitia miradi minne ambayo ni mashamba makubwa ya pamoja, upatikanaji wa mitaji, visima kwa wakulima wadogo na *BBT* ya *extension,* utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alipozindua programu ya *BBT* mwezi Machi, 2023, ardhi kwa ajili ya programu hiyo ilikuwa na ukubwa wa ekari 300. Ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi kufikia Aprili, 2024 utekelezaji wa programu hiyo ni kama ifuatavyo:-

(i) Ekari 340,465.28 zimepatikana kwa ajili ya programu ya *BBT;*

(ii) Ekari 5,700 kati ya ekari 11,430 katika shamba la Mlazo/Ndogowe zimesafishwa;

(iii) Ekari 1,000 katika shamba la Mlazo/Ndogowe zimetengwa kwa ajili ya kuwapatia wanakijiji wanaolima maeneo yanayozunguka;

(iv) Mashamba matatu ya Chinangali/Ndogowe, Mapogoro yenye ukubwa wa ekari 65,000 yameanza kuendelezwa;

(v) Nyumba 46 katika shamba la Chinangali II na nyumba 53 katika shamba la Mlazo/Ndogowe zimejengwa kwa ajili ya makazi ya vijana na wanawake;

(vi) Visima tisa na mabwawa matatu yamejengwa katika shamba la Chinangali II;

(vii) Visima 12 na mabwawa matano yamechimbwa katika shamba la Mlazo kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji; na

(viii) Vijana na wanawake 268 wamepatiwa mashamba katika shamba la Chinangali kwa ajili ya kuanza uzalishaji ambapo katika msimu wa kilimo cha 2023/2024 ekari 620 zimepandwa zao la alizeti.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la mitaji mikopo ya riba nafuu ya 4% yenye thamani ya shilingi milioni 950 imetolewa kupitia Mfuko wa *AGITF* kwa ajili ya kuwawezesha vijana na wanawake 118 waliopo kwenye mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imeboresha utendaji wa Mfuko wa *AGITF* ambapo hadi kufika Aprili, 2024 mfuko umekusanya shilingi bilioni 1.5 na kati kiasi hicho shilingi bilioni 1.4 ni marejesho ya fedha za mkopo na shilingi milioni 75 ni riba ya mkopo.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Sokoine imetekeleza programu ya *BBT – Agricultural Extension Entrepreneurship Scheme* yenye lengo la kukuza ujuzi wa vijana wahitimu wa vyuo vya kilimo na wanatumika kutoa ushauri wa kitaalam kwa wakulima. Hadi Aprili, 2024 wahitimu 230 kutoka vyuo

vya kilimo wamechaguliwa na wanaendelea kutoa huduma za ugani katika kata 40 zinazozalisha zao la pamba kwa kushirikiana na sekta binafsi katika Mikoa ya Shinyanga, Tabora, Simiyu, Mara, Mwanza na Pwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi visima 22 vimechimbwa kwa wakulima wadogo katika Mikoa ya Dodoma na Mbeya na miundombinu ya umwagiliaji kwa kila eneo la ekari 2.5 imewekwa, aidha, magari mawili ya kuchimbia visima yamenunuliwa na jumla ya ajira 475,000 zimezalishwa kutokana na miradi inayotekelezwa na Wizara ikiwemo miradi ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la kuhamasisha matumizi ya mazao yaliyoongezewa virutubisho, Taifa letu linakabiliwa na tatizo la lishe ambapo katika kutatua tatizo hilo Wizara inatekeleza mpango kazi wa lishe, pamoja na mambo mengine mpango huo unalenga kuimarisha upatikanaji wa ndani wa mazao yaliyoongezewa virutubisho ili kupunguza utegemezi wa misaada ya mazao hayo kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa vipando 250,000 vya mbegu za awali za viazi lishe vimezalishwa na kusambazwa kwa wakulima na wakulima 2,200, mashamba darasa 100 yakiwemo 50 ya maharage na 50 ya mahindi lishe yameanzishwa, mafunzo kuhusu lishe bora na uzalishaji wa maharage, viazi na mahindi lishe yametolewa kwa Maafisa Ugani.

Mheshimiwa Spika, ili kulinda jamii yetu Wizara itaendelea kuwekeza kwenye eneo la utafiti na uzalishaji wa mbegu zilizoongezewa virutubishi ili kutosheleza mahitaji ya mbegu hizo nchini. Aidha, kama Serikali hatutaruhusu uagizaji wa mazao ya kilimo ama nafaka kutoka nje ya nchi yaliyoongezewa virutubisho ili kulinda wananchi wetu na kizazi kijacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika eneo la masoko, shilingi bilioni 4.75 zilitengwa, ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa zabuni kwa ajili ya ujenzi wa masoko ya Busoka, Kabanga, Murongo, Mkwenda

na Sirari zipo katika hatua ya upekuzi. Mkataba wa ujenzi wa masoko ya Endashangwet, Kibakwe, Losirwa upo katika hatua ya upekuzi, usanifu wa soko la kuuzia ndizi la Mamsera – Rombo umekamilika, mnada wa chai umeanzishwa, mkataba wa kuzalisha tumbaku kilo 213,000 kwa msimu wa 2023/2024 umesainiwa.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo ya kuongeza mauzo ya mazao ya kilimo nje ya nchi Wizara katika mwaka 2023/2024 ilipanga kuongeza mauzo nje ya nchi. Ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili, 2024 mauzo ya mazao ya kilimo nje ya nchi yameongezeka kutoka dola za Marekani bilioni 1.2 hadi dola za Marekani bilioni 2.3 ambayo ni sawa sawa na 91.7%.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la upatikanaji wa mitaji naomba kutoa taarifa katika Bunge lako Tukufu katika mwaka wa fedha 2023/2024 jumla ya mikopo iliyotolewa na taasisi za fedha ilikuwa shilingi trilioni 33, kati ya hizo shilingi trilioni 3.317 sawa na 10% ya mikopo yote imetolewa kwa ajili ya shughuli za kilimo ikilinganishwa na shilingi trilioni 2.287 katika mwaka wa fedha 2022.

Mheshimiwa Spika, kwa kipekee ninapenda kuishukuru Wizara ya Fedha, Benki Kuu na Wizara ya Mipango na Uwekezaji kukubali kama Taifa tuanze kuandaa sera ya mkopo katika sekta ya kilimo na bima kwa ajili ya kilimo. Kukamilika kwa sera hizo kutatoa mwongozo utakaopunguza masharti ya mikopo kwa sekta za uzalishaji ikiwemo kilimo. Vilevile bima ya mazao itawezesha wakulima kupata fidia zinazotokana na majanga katika sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu hadi kufikia Aprili, 2024 Wizara imesajili jumla ya wakulima 3,910,556, waingizaji wa mbolea 31, mawakala wa mbolea 4,167 na vyama vya ushirika 776. Masuala mengine mtambuka ambayo Wizara imetekeleza moja ni kuandaa Mpango wa Mageuzi ya Kilimo *(Agricultural Transformation Masterplan)* ya mwaka 2050 wenye lengo la kuhakikisha kwamba *Vision 2050* inahusisha sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, pia kuendelea na maboresho ya sera ya maendeleo ya ushirika kuanza, marekebisho ya Sheria ya Tasnia ya Korosho Na.18 kwenye Sheria ya Fedha ya mwaka 2024 na kuanza marekebisho ya Sheria ya Chai Na. 3 ya mwaka 1997 kwenye Sheria ya Fedha ya mwaka 2024.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa bajeti wa mwaka 2024/2025 umezingatia Dira ya Maendeleo ya mwaka 2025, Mpango wa Maendeleo wa Taifa, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi, Sera ya Kilimo, Mpango wa Maendeleo, Sera ya Maendeleo ya Ushirika na Mkakati wa Ukuzaji wa Sekta ya Kilimo (Ajenda 10/30). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpango umezingatia Malengo Endelevu *(SDGs),* Mwongozo na Mpango wa Bajeti wa mwaka 2024/2025, Mkakati wa Kuongeza Fedha za Kigeni, Mpango wa Mageuzi ya Kilimo, maoni na ushauri wa Kamati za Kudumu, Maoni ya Baraza la Rais la Ushauri wa Kilimo, wadau wa maendeleo na masuala mtambuka ya jinsia, mazingira, lishe, mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara itaendelea kutekeleza vipaumbele vitano iliyoanza kutekelezwa mwaka 2023/2024 kwa kukamilisha miradi iliyoanza mwaka 2022/2023, 2023/2024 na kuanza miradi mipya. Aidha, Wizara itaongeza kipaumbele kimoja na hivyo kufanya vipaumbele vya mwaka 2024/2025 kuwa sita vitakavyotekelezwa kwa mikakati 27. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tathmini ya sensa ya watu na makazi iliyofanyika mwaka 2022 imeonesha kuwa idadi ya Watanzania ni milioni 61.7, kati ya hao Watanzania milioni 31.7 ni wanawake sawa na 51% ambapo kati yao milioni 11.2 wanaishi mijini na milioni 20.5 wanaishi vijijini na wanaume ni milioni 30 sawa na asilimia 49% ambapo kati yao milioni 10.3 wanaishi mijini na milioni 19.7 wanaishi vijijini. Kwa Tanzania Bara, takwimu zinaonesha kuwa 65.5% ya Watanzania wanaishi vijijini ambapo shughuli za kilimo zinafanyika na 34.4% wanaishi mjini.

Mheshimiwa Spika, kati ya Watanzania wanaoishi vijijini, 39.0% ni vijana wenye umri wa miaka 14 mpaka 40 ambao ni nguvu kazi ya Taifa. Kati hao vijana 51.4% ni wanawake na 48.6% ni wanaume. Aidha, kwa mujibu wa takwimu za *IFAD* ya mwaka 2019, vijana wanaojishughulisha na kilimo ni 59% na wanaishi vijijini. Ni muhimu kuzitazama takwimu hizi zilizotokana na sensa ya watu na makazi na takwimu za *IFAD* ili kuweza kufanya maamuzi ya mabadiliko ya ugawaji wa rasilimali hususani kwenye sekta za uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara inalenga ukuaji wa sekta ya kilimo kwa upande wa mazao kufikia 5%, kuchangia 20% katika Pato la Taifa, kuendelea kuchangia 100% ya upatikanaji wa chakula na kuongeza mauzo ya mazao nje ya nchi hadi kufikia dola za Marekani bilioni tatu. Malengo hayo yatafikiwa kwa kutekeleza vipaumbele sita na mikakati 27.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele chetu cha kwanza katika mwaka 2024/2025 hadi mwaka 2050 kitakuwa ni kuongeza tija na uzalishaji. Kipaumbele hiki hakitabadilika isipokuwa mabadiliko yanaweza kufanyika kwenye mikakati ya kufikia kipaumbele hicho.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele cha pili, ni kuongeza ajira zenye staha na ushiriki wa vijana; cha tatu, ni kuimarisha usalama wa chakula na lishe; cha nne, ni kuimarisha upatikanaji wa masoko mitaji na mauzo ya nje; cha tano, ni kuimarisha maendeleo ya ushirika; na cha sita ni kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika uendelezaji wa sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika eneo la utafiti Wizara itatumia shilingi bilioni 41.39 kwa ajili ya kutekeleza mambo mbalimbali baadhi ni kama ifuatavyo:-

(i) Kujenga Benki ya Mbegu *(Gene Bank)* katika kituo cha *TARI* Selian ili kuwa msingi mkuu wa utafiti wetu;

(ii) Kulinda mbegu zetu na usalama wa nchi, kama nchi kwa sasa hatuna uhifadhi mzuri wa vinasaba vya mbegu zetu

katika Taifa letu kutokana na vinasaba vya mbegu zetu kutapakaa maeneo mbalimbali na saa zingine kutegemea mataifa ya nje; na

(iii) Kujenga Kituo cha Sayansi za Kibaolojia *(Bioscience Lab)* katika kituo chetu cha *TARI* Mikocheni katika Wilaya ya Mkuranga;

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo muhimu kwa Taifa letu kwa ajili ya usalama wa nchi yetu na usalama wa utafiti.

(i) Kusomesha watafiti na wataalamu mbalimbali 485 kwa ajili ya kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ikiwemo kuhaulisha teknolojia na kutoa mafunzo kwa wakulima. Kati ya hao Shahada ya Uzamivu ni 33, Shahada ya Uzamili 124, Shahada 52, Stashahada mmoja na mafunzo ya ujuzi maalumu 274;

(ii) Kukarabati Kituo cha *TARI*, Tengeru na kukifanya kuwa kituo mahiri cha utafiti na uzalishaji wa mbegu za mazao ya bustani *(Horticultural Centre of excellence);*

(iii) Kuzalisha na kusambaza pingili za mihogo milioni 5.7 kwa maeneo ya uzalishaji ya zao hilo ikiwemo Mkoa wa Kigoma; na

(iv) Kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba 19 ya utafiti yenye jumla ya hekta 1120, kuanza ujenzi wa miundombinu mipya ya umwagiliaji yenye ukubwa wa hekta 1000, kuendelea na ujenzi wa maabara ya kuzalisha miche ya migomba kwa njia ya chupa katika Kituo cha Maruku na kuzalisha mbegu za awali za mpunga kilo 2000 zinazostahamili athari za chumvi.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la uzalishaji wa mbegu katika mwaka wa fedha wa 2024/2025 tutawezesha upatikanaji na usambazaji wa mbegu bora kwa wakulima kufikia tani 80,000 dhidi ya lengo la tani 120,000, miche milioni 47, pingili za mihogo 6.2 na vipando vya viazi 450,000. Aidha, tutaendelea kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya uzalishaji wa mbegu ya *ASA* yaliyoanza mwaka 2022/2023 na 2023/2024 yenye jumla ya hekta 1375.

Mheshimiwa Spika, pia tutaanza ujenzi wa miundombinu mipya ya umwagiliaji yenye jumla ya hekta 800, kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi ya miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya mbegu yenye ukubwa wa hekta 3,000, kuanza ujenzi wa uzio wa mashamba ya mbegu yenye ukubwa wa hekta 6000, kununua na kusimika mitambo miwili ya kuchakata mbegu yenye uwezo wa kuchakata tani nne kwa saa katika shamba letu la Mbozi na Namtumbo, kutenga jumla ya hekta 4917, ekari 12,285 za mashamba ya *ASA* na kuwapatia sekta binafsi ya Kitanzania kwa ajili ya uzalishaji wa mbegu.

Mheshimiwa Spika, kiasi cha shilingi bilioni 44.4 kinapendekezwa kutumika kwa ajili ya kuimarisha uzalishaji wa mbegu. Katika eneo la udhibiti wa mbegu, katika eneo hili yafuatayo yatatekelezwa:-

(i) Kuongeza idadi za mbegu zinazothibitishwa ubora kutoka 63,000 mpaka 8,000;

(ii) Kusajili wazalishaji wa miche ya parachichi ili kuwezesha ufuatiliaji;

(iii) Kununua mitambo miwili ya kuchapisha *label;*

(iv) Kuweka utaratibu wa kikanuni wa kusimamia bei ya mbegu; na

(v) Kutangaza bei elekezi ya mbegu kila tarehe moja Septemba ya kila msimu wa kilimo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwekezaji kwenye eneo la ruzuku ya mbolea; upatikanaji wa mbolea katika mwaka wa fedha 2022/2023 ulikuwa tani 819,000 na mwaka 2023/2024 ulifika tani 1,052,000. Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara kupitia *TRFA* inatarajia uagizwaji wa mbolea na uzalishaji wa ndani kufika tani milioni 1.5 za mbolea na kuzisambaza kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku utakaoendelea hadi mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, kadhalika katika mwaka wa fedha 2024/2025 *TFC* itatekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kununua tani 100,000 za mbolea na kusambaza kwa wakulima;

(ii) Kujenga kiwanda cha kuchanganya mbolea *(blending facility)* kwa kuzingatia taarifa ya afya ya udongo eneo husika chenye uwezo wa kuchanganya mbolea tani 120 kwa saa; na

(iii) Kiasi cha shilingi bilioni 300 kinapendekezwa kutumika kwa ajili ya ruzuku ya mbolea na kuiwezesha *TFC*.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la viuatilifu, mamlaka ya afya ya mimea itanunua jumla ya lita 95,000 za viuatilifu kwa ajili ya kudhibiti visumbufu ya mazao ya mimea ambavyo vitasambazwa kwa ruzuku. Pia *TPHPA* itanunua ndege nyuki 20 ili kuimaarisha kituo cha kilimo anga kwa ajili ya kupulizia.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la urasimishaji wa shughuli za kilimo, kwa kuwa Wizara ya Kilimo imechukua hatua ya kusajili wakulima ambapo hadi Aprili, 2024 wakulima 3,910,000 wamesajiliwa kwenye mfumo wa kuwatambua, usajili huo hautakamilika kama hatutachukua *coordinates* za *GPS* na wakulima kupatiwa hati za shamba lao.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara itaanza utoaji wa ruzuku ya upimaji wa mashamba ya wakulima

wadogo waliopo vijijini na kuwapatia hati ambapo ruzuku hiyo itaendelea hadi mwaka 2030. Upimaji wa mashamba ya wakulima na kuwapatia hati katika mwaka wa fedha 2024/2025 utatumia shilingi bilioni tano. Zoezi hili litahusisha Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kupitia Tume ya Matumizi Bora ya Ardhi, hatua hiyo ni ya msingi kwa urasimishaji wa shughuli ya kilimo na kulinda ardhi ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, suala la utambuzi wa wakulima haliwezi kukamilika bila kupima ardhi yake na kuhakikisha ardhi hiyo inapata haki miliki, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi itaanza kupimia ardhi wakulima 2,000 wa kwanza na kuhakikisha wanapatiwa hati hizo bila gharama yoyote ikiwa ni sehemu ya urasimishaji.

Mheshimiwa Spika, ikiwa ni sehemu ya *smart subsidies* Serikali itaanza kutoa ruzuku ya kutoa ardhi kwa wakulima wadogo na kuhakikisha wanapata hati za hakimiliki ili kukamilisha zoezi la usajili, zoezi hili litasaidia urasimishaji na utunzaji wa ardhi ya kilimo, kupata mikopo kutoka kwenye taasisi za fedha na kupunguza migogoro ya ardhi. Programu hiyo itaanza katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la ugani, yafuatayo yatatekelezwa:-

(i) Kununua pikipiki 600 na vipima afya 43 na kuvisambaza kwa Maafisa Ugani ili kukamilisha *package* ya pikipiki na vipima afya ya udongo;

(ii) Kuendelea kujenga nyumba 50 za Maafisa Ugani;

(iii) Kuendelea na ujenzi wa miundombinu kwenye Kiwanja cha Maonesho ya Wakulima ya Nanenane katika Viwanja vya Nzuguni na John Mwakangale, Mbeya; na

(iv) Kununua magari 50 kwa ajili ya Maafisa Kilimo ngazi za Wilaya. Wizara ya Kilimo tumeamua badala ya kununua

magari ya sisi viongozi katika ngazi ya Wizara tutaweka fedha kwa ajili ya kuwanunulia Maafisa Ugani katika ngazi ya Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la mafunzo; katika eneo hili changamoto kubwa iliyopo ni uwezo wa Serikali katika ajira za Maafisa Ugani. Sote tumekuwa tukiona upungufu wa Maafisa Ugani katika ngazi mbalimbali, ili kutatua tatizo hili katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara haitafanya jukumu la kusomesha Maafisa Ugani katika ngazi za Astashahada ya Awali, Astashahada na Stashahada ambao wanaenda kwa ajili ya kutafuta ajira. Jukumu la kusomesha Maafisa Ugani litabaki kuwa chini ya Wizara yenye dhamana ya masuala ya elimu.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo itavigeuza vyuo vyake vya *MATI* kuwa vituo vya mafunzo kwa ajili ya wakulima na Maafisa Ugani walioko kazini, kwa ajili ya marejea. Mwalimu Nyerere alipoanzisha vituo vya utafiti wa kilimo, pembeni mwa vituo hivyo alianzisha vyuo vya mafunzo ya kilimo ambapo msingi wake mkubwa ulikuwa ni kuwafundisha wakulima teknolojia zinazopatikana katika vituo vya utafiti. Aidha, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa wanafunzi ambao walidahiliwa mwaka 2023/2024 wataendelea na masomo yao katika vyuo vya ngazi ya stashahada na shahada.

Mheshimiwa Spika, aidha, hatutadahili wanafunzi wengine wa Astashahada na Stashahada; jukumu hili litabaki kusimamiwa na Wizara ya Elimu na Wizara yetu itabaki na jukumu la utafiti na kuhaulisha teknolojia hizo kwa wakulima moja kwa moja kupitia vyuo vyetu vya *MATI*. Katika eneo hili shilingi bilioni 17.07 zitatumika.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la upimaji wa afya Wizara itaendelea kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kukamilisha upimaji wa udongo katika mikoa nane ya Tanzania Bara. Hii ni Mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani, Ruvuma, Kigoma, Tabora na Dar es Salaam pamoja na kuandaa ramani inayoonesha afya ya udongo kwa kila

mkoa. Ninaomba nilitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa tukikamilisha hili ramani na taswira ya udongo nchi nzima itakuwa inatambulika na tutaacha kutumia mbolea *generic* badala yake tutatumia zile ambazo zinafaa katika eneo husika*; (Makofi)*

(ii) Tutaendelea kutoa huduma za upimaji wa afya ya udongo na tutanunua maabara ya udongo inayohamishika kwa ajili ya kupima afya ya udongo; na

(iii) Wizara itaendelea na jukumu la kupima afya ya udongo kwa mikoa iliyobaki kati ya 26 ili kuandaa ramani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu eneo la umwagiliaji; Tume ya Taifa ya Umwagiliaji katika mwaka wa fedha 2024/2025 itaendelea kutekeleza miradi 780 iliyoanza mwaka 2022/2023 na mwaka 2023/2024 kukamilisha utekelezaji wa miradi 113 kati ya miradi 133 iliyopangwa, ujenzi wa mabwawa 14 yenye ujazo wa lita milioni 131, ujenzi wa skimu 25 na upembuzi yakinifu wa skimu 17.

Mheshimiwa Spika, pia tutaendelea na utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji 647 iliyoanza mwaka wa fedha 2023/2024. Ujenzi wa skimu 28 zenye hekta 69,000, ukarabati wa skimu 18 zenye ukubwa wa hekta 40,000, ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya *block farm*, usanifu na upembuzi yakinifu wa mabwawa 100 ya kuvunia maji. Hali kadhalika, kufanya mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu wa skimu 255 zenye ukubwa wa hekta 290,000 pamoja na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, kwa ajili ya ujenzi wa skimu 240.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025 tutaendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mabonde ya kimkakati yenye takribani ya hekta 250,000 na kukarabati miundombinu ya umwagiliaji kwa skimu 33 yenye hekta 6,089. Vilevile kukamilishwa kwa miradi inayoendelea kutekelezwa na itakayoanza kujengwa katika mwaka wa fedha 2024/2025 kutaongeza eneo la umwagiliaji hadi kufikia hekta 543,366 na kufanya

jumla ya eneo linalomwagiliwa kufikia hekta 1,270,647 ambalo ni sawa na asilimia 105 ya lengo la Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2025. Aidha, eneo hili litakaloongezeka litatengeneza ajira za moja kwa moja milioni 2.1 ambazo zitatokana na uwekezaji katika kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha upatikanaji wa maji ya umwagiliaji katika maeneo yasiyopata mvua za kutosha, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na kwa kushirikiana na Wizara ya Maji itafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa kutumia maji ya Ziwa Victoria ili kuyafikisha katika Mkoa wa Simiyu, Shinyanga, Tabora na Singida, aidha, maji ya Ziwa Tanganyika yaweze kufika katika Mkoa wa Kigoma, Rukwa na Katavi, kwa ajili ya shughuli za kilimo. Vilevile tutaanza kutekeleza miradi midogo midogo kwa wakulima wanaozunguka Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Bonde la Mto Ngono na Bugwema umekamilika na hatua za kumtafuta mkandarasi wa kuanza ujenzi zinaendelea. Vilevile Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imekamilisha upembuzi yakinifu na upembuzi wa kina wa Bonde la Mto Rufiji ambapo katika mwaka wa fedha 2024/2025 itaendelea na ujenzi wa mabwawa mawili ya Mbakiamtuli na Ngorongo. Ujenzi huo utakamilika katika kipindi cha miaka mitatu.

Mheshimiwa Spika, vilevile tume kwa kushirikiana na Shirika la Reli Tanzania itafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na kisha ujenzi wa mabwawa sita ya Dabalo, Buigiri, Hombolo, Kimagae, Kidete na Ikoa. Mabwawa haya yatatumika kuzuia mafuriko katika reli ya kati na pia kutumika katika shughuli za kilimo cha umwagiliaji. Hekta 25,000 zitapatikana katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua changamoto inayowakabili wakulima katika Bonde la Mbarali na kufuatia maelekezo ya Mheshimiwa Rais na ya Chama Cha Mapinduzi aliyoyatoa Katibu Mkuu katika ziara yake ya Nyanda za Juu Kusini, Wizara kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za Serikali itakamilisha

mazungumzo na mwekezaji wa *Mbarali Estate* wa Kampuni ya *Highland Estate,* kwa ajili ya Serikali kuchukua shamba moja na kumlipa haki zake zote. Serikali italifanya shamba hilo kuwa sehemu ya mashamba ya wakulima wadogo waliohamishwa kutoka maeneo yenye vyanzo vya maji. Sambamba na hilo, Wizara itajenga mabwawa matano kwa ajili ya kuwahudumia wakulima wa Mbarali. Lengo la Serikali ni kumaliza mchakato huu na mwekezaji kabla ya mwaka 2025. Serikali itatumia kiasi cha shilingi bilioni 393 ambacho kinapendekezwa katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu eneo la uzalishaji wa mazao; uzalishaji wa mazao ya asili ya biashara yakiwemo pamba, kahawa, mkonge, korosho, tumbaku, pareto, sukari na chai unatarajiwa kuongezeka kutoka tani milioni 1.258 mwaka 2023/2024 hadi kufikia tani milioni 2.030 mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, tasnia ya chai nchini inapitia changamoto nyingi ambazo msingi wake ni sera yetu ya ubinafsishaji na hali ya mabadiliko ya soko la chai duniani. Wizara imeamua kuchukua hatua za msingi zifuatazo:-

(i) Serikali kuwekeza kwenye mtambo wa kuchanganya chai ili wanunuzi waweze kuchanganya *blended tea* na kuuza chai hiyo kupitia mnada wa chai Tanzania;

(ii) Kuanzisha viwanda viwili vya kusindika chai ya wakulima wadogo kati ya viwanda saba vinavyolengwa kujengwa nchini ili wakulima waanze kuuza chai nyeusi badala ya majani;

(iii) Kujenga vituo 30 na mizani kwenye maeneo mapya ya uzalishaji;

(iv) Kuwezesha upatikanaji wa hati ya Kimataifa kwa ajili ya uendeshaji wa mashamba ya Kilolo na Lupembe;

(v) Kujenga miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya chai ya wakulima wadogo katika Mkoa wa Njombe na kuanzisha maeneo 13 mapya kwa ajili ya uzalishaji wa miche; na

(vi) Vilevile Wizara itakamilisha majadiliano kuhusu mashamba ya chai ya Kampuni ya *Mohamed Enterprises Do Mercantile* na *DUN* ili yaendelee na uzalishaji. Aidha, pale itakapohitajika kuyatwaa mashamba hayo Serikali itafanya hivyo kwa kuzingatia sheria ili kulinda haki za wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, tasnia ya korosho imepitia changamoto nyingi sana kutokana na mabadiliko yaliyofanyika mwaka 2017/2018 katika Sheria ya Korosho Namba 18 kwa kuondoa ushuru wa korosho wa *export levy* kutoka Mfuko wa Korosho na fedha hizo kuingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Tangu kipindi hicho Serikali haikupeleka fedha kuhudumia zao la korosho hadi mwaka 2022, jambo ambalo limesababisha kushuka kwa uzalishaji na ubanguaji wa korosho, hivyo wakulima kukata tamaa na utafiti wa korosho kuathirika. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali ilichukua hatua ya kuanza kutoa ruzuku ya pembejeo ambazo zimesababisha kuongezeka kwa uzalishaji kutoka tani 189,000 mwaka 2022/2023 hadi tani 310,000 mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara itachukua hatua za ziada zifuatazo:-

(i) Kuendelea kutoa ruzuku ya pembejeo kwa wakulima wa korosho;

(ii) Kuendelea na zoezi la usajili;

(iii) Kubadili mfumo wa kuuza korosho kutoka mfumo wa kulaza debe hadi mfumo wa uwazi kwa kutumia *TMX; (Makofi)*

(iv) Kufanya marekebisho ya Sheria ya Fedha mwaka huu ili kuwezesha mapato yatokanayo na mauzo ya korosho 100% kwenda kwenye ununuzi wa pembejeo wa zao la korosho pamoja na kulipa madeni ya sekta; na

(v) Kuanzisha kitalu na kujenga maghala tisa yatakayosimamiwa na vyama vikuu vya ushirika.

Mheshimiwa Spika, Serikali ni lazima tuchukue hatua hizi za msingi ili kuimarisha uzalishaji wa zao la korosho na mapato ya wakulima wa korosho. Ninafahamu maamuzi haya ya kubadili mfumo wa kulaza debe yana mgogoro, lakini Serikali itakabiliana na changamoto zozote zitakazokuja huko mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zao la tumbaku; leo nchi yetu ni ya pili kwa uazalishaji wa zao la tumbaku. Serikali itachukua hatua za ziada zifuatazo:-

(i) Tutatoa ruzuku ya shilingi bilioni 13 kwa wakulima wa tumbaku ambapo mbolea ya *NPK 10:18:24* itaingizwa nchini na Kampuni ya Serikali ya *TFC;*

(ii) Serikali itatoa waraka kwa benki utakaodhibiti mfumo wa kujiamulia *exchange rate* ya dola za Marekani kwa ajili ya kuwalipa wakulima baada ya kuuza tumbaku ili mkulima afaidike na faida itokanayo na *exchange rate* pale ambapo shilingi inakuwa na udhaifu. Zoezi hili litasimamiwa na Tume ya Taifa ya Ushirika;

(iii) Wizara itatenga fedha kiasi cha shilingi bilioni mbili kwa lengo la kuipatia Bodi ya Tumbaku kama ruzuku ya kuwasaidia wakulima kwenye ujenzi wa mabani; na

(iv) Wizara itaendelea kuiwezesha *TORITA* kufanya jukumu lake.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025 baada ya zao la pamba kuongezeka na kufikia tani 285,000, Serikali imejiwekea lengo la kufika tani 500,000. Lengo hili litafikiwa kwa kutekeleza mambo yafuatayo:-

(i) Kununua, kuchakata na kusambaza mbegu bora za pamba;

(ii) Kununua ndege nyuki 40 na mitambo mikubwa ya kunyunyuzia dawa;

(iii) Kujenga kiwanda cha vifaa tiba katika Wilaya ya Maswa;

(iv) Kujenga kiwanda cha kusindika mafuta ya pamba katika Wilaya ya Bariadi;

(v) Kujenga *service industrial park* kwa ajili ya uwekezaji wa kuongeza thamani ya zao la pamba katika Mkoa wa Simiyu;

(vi) Kununua jozi nyingine ya mitambo ya kuchimbia mabwawa ya umwagiliaji ambayo itakuwa na *bulldozer* moja, *excavator* moja, *wheel loader* moja, *driller* moja na *motor grader* moja; na

(vii) Kununua na kusimika mitambo ya kuongeza thamani katika zao la pamba katika *AMCOS* kwenye vijiji vyenye uzalishaji mkubwa wa pamba ikiwemo mitambo miwili ya kuzalisha nishati ya kupikia itokanayo na masalia ya miche ya pamba, mitambo nane ya kusokota nyuzi za pamba na kuzalisha vikoi, mitandio na bidhaa nyingine za pamba.

Mheshimiwa Spika, katika mazao ya mafuta, Serikali imejiwekea lengo katika mwaka wa fedha 2024/2025 kuweza kuongeza uzalishaji kufikia tani milioni 2.2, kuwezesha upatikanaji wa mbegu bora kufikia tani 5,000, kuzalisha na kusambaza mbegu bora za karanga pamoja na kuzalisha na kusambaza miche milioni mbili ya chikichi. Vilevile

Serikali itanunua ardhi yenye ukubwa wa hekta laki moja kwenye Halmashauri za Kigoma na Kyela kwa ajili ya kuanzisha kilimo cha mashamba makubwa ya chikichi, kununua ardhi yenye ukubwa wa eka 50,000 kwa ajili ya kuanzisha kilimo cha mashamba makubwa ya alizeti na kufanya majadiliano na Wizara ya Fedha ili kuweka kodi kwenye mafuta yanayotoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu mazao ya bustani - zao la parachichi; katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara itaendelea kuhamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa zao la parachichi ili kuweza kufikia malengo ya ku-*export* tani 30,000. Hali kadhalika itashirikiana na wadau kuzalisha miche milioni sita ya miparachichi na kuisambaza kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku.

Mheshimiwa Spika, Wizara itachimba visima na kusaidia teknolojia rahisi ya kukusanya maji pamoja na kuweke miundombinu ya umwagiliaji kwa ajili ya wakulima wa parachichi. Pia Wizara itatoa ruzuku ya viuatilifu bure kwa wakulima wa zao la parachichi na itashirikiana na Kiwanda cha *Intercom* kufanya utafiti wa kuzalisha mbolea inayofaa kwa ajili ya zao hili na kuisambaza kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku.

Mheshimiwa Spika, vilevile Wizara itakamilisha majadiliano na *African Development Bank* kwa ajili ya Mradi wa *Agricultural Special Processing Zone* kwa mazao ya bustani yenye thamani ya dola milioni 75. Mradi huu utahusisha ujenzi wa *Dar es Salaam Multiple Commodity Centre* ili kuweza kusafirisha mazao yetu nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa eneo la ajira; tutawezesha upatikanaji wa ardhi katika Mradi wa *BBT,* lakini vilevile katika eneo hili yafuatayo yatatekelezwa:-

(i) Kutambua na kuainisha mashamba mapya 30;

(ii) Kujenga mabwawa na kuchimba visima kwenye mashamba ya *BBT* Chinangali na maeneo mengine;

(iii) Kuanza kutekeleza Mradi wa *BBT* katika halmashauri 100 zitakazotenga maeneo yenye ukubwa wa hekta 200 kwa kila halmashauri na kujenga miundombinu ya umwagiliaji katika maeneo hayo; na

(iv) Kukamilisha majadiliano na Benki ya Maendeleo ya Afrika ili kuweza kupata fedha kwa ajili ya Mradi wa *BBT* zenye kiwango cha dola milioni 130.

Mheshimiwa Spika, utambuzi wa vijana watakaomilikishwa ardhi utafanywa na halmashauri husika ambapo Wizara ya Kilimo itatoa mafunzo ya kilimo-biashara kwa vijana hao katika maeneo yao na kuwawekea miundombinu husika kwenye mashamba yao. Wizara ilijenga *Ward Resource Centre* na kuzikabidhi halmashauri, kwa ajili ya kuwafundishia wakulima. Hata hivyo katika maeneo mengi *Ward Resource Centre* hizo zimebadilishwa matumizi na kuwa Ofisi za Watendaji.

Mheshimiwa Spika, Wizara itavichukua vituo hivyo kwa ajili ya kufundishia vijana na wakulima ambao ni sehemu ya Mradi wa *BBT*. Vituo hivyo vitatumika kutoa huduma za zana za kilimo kwa kuweka matrekta na zana nyingine za kulimia kwa lengo la kuwakodishia wakulima.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu na kwa kuanzia, nataka niiambie Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali kuwa Kituo cha Chimala na Kituo cha Ubaruku vitatumika kufundishia wakulima vijana wanaotoka Wilaya ya Mbarali ambao wanafaidika na Programu ya *BBT* katika eneo lao. Vilevile vitatumika kukodisha zana za kulimia kwa wakulima hao. Tayari nimemuagiza Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo kufanya mawasiliano na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kutekeleza jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu ninaomba niseme kwamba halmashauri zote ambazo zimegeuza matumizi ya vituo hivyo watafute eneo lingine na Wizara itaajiri vijana kusimamia vituo hivyo kwa mwaka ujao wa fedha. Kupitia Bunge lako Tukufu tayari

nimemwelekeza Katibu Mkuu, Wizara ya Kilimo aanze mchakato na Chuo Kikuu cha Sokoine kwa ajili ya kupata vijana 200 watakaokwenda kusimamia Vituo vya *Ward Resource Centre* vilivyotapakaa nchi nzima. Katika eneo hili kiasi cha shilingi bilioni 53.14 kinapendekezwa kutumika.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la kuwapatia wakulima wadogo mitaji kupitia Mfuko wa Pembejeo, Wizara imepanga kutoa mikopo ya riba nafuu ya 4.5% yenye thamani ya shilingi bilioni kumi kwa wakulima wadogo ambao ni vijana na wanawake, wanaojishughulisha na kilimo katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, kusimamia *AGITF* na *TADB* kukamilisha makubaliano na kutumia mfumo wa dhamana ili kuzisaidia taasisi za fedha kuwakopesha vijana. Wizara itakamilisha majadiliano na *IFAD* kwa ajili ya kuanzisha mradi wa upatikanaji wa mtaji kwa wakulima wadogo waliopo kwenye Programu ya *BBT* kwa kutumia Mfuko wa Pembejeo wenye thamani ya dola milioni 40.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itachimba visima 1,000 na kufunga vifaa vya umwagiliaji kwa ajili ya wakulima wadogo katika halmashauri 178 kwenye lengo la kufikia visima 67,000. Wizara inatoa rai kwa wazawa wanaopata fursa kukamilisha miradi hiyo kwa ufanisi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, dakika tano, malizia.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine muhimu yatakayotekelezwa na Wizara, kwa ufupi ni kama ifuatavyo:-

(i) Kukamilisha uanzishwaji wa mpango wa mageuzi ya kilimo *(Agricultural Transformation Master Plan)* wa mwaka 2050;

(ii) Kuendelea na utaratibu wa kutunga Sheria ya Kilimo;

(iii) Kuendelea kufanya marekebisho ya Sheria ya Korosho na Sheria ya Sukari;

(iv) Kuendelea na maboresho ya Sera ya Ushirika;

(v) Kufanya mapitio ya Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji;

(vi) Kuendelea kufanya marekebisho ya Sheria ya Tasnia ya Korosho;

(vii) Kuendelea na marekebisho ya Sheria ya Chai; na

(viii) Kuanzisha *compact* itakayosainiwa na Wizara ya Kilimo na wadau wa maendeleo ambao watatakiwa kutekeleza miradi ya vipaumbele vya Serikali kupunguza upotevu wa rasilimali na kupunguza fedha zinazotumika kwenye *capacity building.*

Mheshimiwa Spika, nitumie Bunge lako Tukufu kuwaambia wadau wa maendeleo wote kuwa yeyote anayetaka kuweka fedha katika kilimo ni lazima afuate kipaumbele cha Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bajeti yetu ya mwaka 2024/2025 inalenga kuendeleza miradi ya mwaka 2022/2023 na 2023/2024 na kuanza utekelezaji wa maeneo makubwa ya kimkakati ikiwemo kufanya upembuzi yakinifu, kuendelea kuimarisha utafiti, kuendelea kufanya juhudi za urasimishaji wa sekta ya kilimo. Maelezo ya ziada yako ukurasa wa 190. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais na Serikali nzima ya Chama Cha Mapinduzi kwa kuendelea na safari ya kuwekeza katika sekta ya kilimo na kukubali uwekezaji huu kwenye maeneo ya msingi kwa kuongeza bajeti ya kilimo kutoka shilingi bilioni 294 hadi leo tunapokwenda kuomba Bunge lako Tukufu liidhinishe bajeti ya shilingi 1,000,248,000,000. Uwekezaji huu umechochea ukuaji wa sekta ya kilimo kukua kutoka

2.7% mwaka 2024 hadi 4%.2 mwaka huu. Mauzo ya nje kutoka dola bilioni 1.2 hadi dola bilioni 2.3 na utoshelevu wa chakula kwa 100%.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais kwa kuweka fedha nyingi kwenye eneo la umwagiliaji kwa kipindi cha miaka mitatu. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuiwezesha *NFRA* kuwa mnunuzi mkuu wa mazao ya nafaka kutoka kwa wakulima. Pia niwahakikishie wakulima wote kuwa kuanzia tarehe 1 Julai, *NFRA* itaanza kununua mazao kwa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Rais kuweka fedha kwenye *TFC*. Maamuzi ya kuwekeza kwenye sekta ya kilimo yanamaanisha kuwa *rural transformation* inaweza kutokea katika nchi yoyote duniani. Kwa hatua zinazochukuliwa kwenye kilimo, *REA, TARURA* na maji vijijini zinathibitisha kuwa Serikali ya Awamu ya Sita imejipambanua kwa vitendo kuleta maendeleo vijijini na kujenga uchumi jumuishi.

Mheshimiwa Spika, ninayashukuru mashirika na taasisi za kimataifa, Benki ya Dunia, *African Development Bank,* Taasisi ya *USAID, IMF, IFAD, UNDP* na taasisi zote za kimataifa. Ninawashukuru sana wakulima wa nchi hii kwa kuendelea kufanya kazi katika mazingira magumu na kuendelea kulinda uchumi wa nchi yetu na usalama wa chakula. Ninawashukuru sana kundi la wafanyakazi katika sekta ya umma na sekta binafsi ambao wameanza kuwekeza katika sekta ya kilimo. Kundi hilo limeanza kukopa mikopo ya mishahara na kuwekeza kwenye kilimo. Ninaomba niwambie shambani kuna changamoto, lakini hatma ya kesho ya dunia hii ni kilimo. Hivyo Serikali itaendelea kushirikiana nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha, Wizara katika mwaka wa fedha 2024/2025 inatarajia kukusanya kiasi cha shilingi 10,600,254,000 kupitia Fungu 43 na Fungu 05. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni saba zitakusanywa kutokana na ukaguzi wa mazao, kodi za majengo na uuzaji wa nyaraka za kupitia Fungu 43 na shilingi bilioni 3.6 kutokana na ada za umwagiliaji na ukodishaji wa mitambo kupitia Fungu 05.

Mheshimiwa Spika, fedha za matumizi kwa mafungu yote; katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ya Kilimo inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 1,248,961,680,000 kupitia Fungu 43, Fungu 05 na Fungu 24.

Mheshimiwa Spika, kwa Fungu 43 katika mwaka wa fedha 2024/2025, shilingi 824,069,158,000 zinaombwa. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 700 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ambapo shilingi bilioni 500 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 174 ni fedha za nje. Aidha, shilingi bilioni 123 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 69 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 53 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo ya Wizara na Bodi.

Mheshimiwa Spika, kwa Fungu 05 katika mwaka wa fedha 2024/2025 Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 403. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 331 ni fedha za maendeleo na shilingi bilioni 71.884 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, shilingi bilioni 284 ni fedha za ndani na bilioni 43 ni fedha za nje. Aidha, kati ya shilingi 71 ya fedha za matumizi ya kawaida zinazoombwa, shilingi bilioni 64 ni kwa ajili ya matumizi ya *OC* na shilingi bilioni saba ni kwa ajili ya *PE* ya watumishi.

Mheshimiwa Spika, kwa Fungu 24 katika mwaka wa fedha 2024/2025 Tume ya Maendeleo ya Ushirika inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 21. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 20 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo shilingi bilioni 11 ni mishahara na shilingi bilioni nane ni matumizi mengineyo. Aidha, kiasi fedha cha shilingi milioni 800 zinaombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**2 MEI, 2024**

**HOTUBA YA WAZIRI WA KILIMO, MHESHIMIWA HUSSEIN MOHAMED BASHE (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA KILIMO KWA MWAKA 2024/2025**

## 1 UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu baada ya kuzingatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, sasa lijadili na kukubali kupitisha utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka 2023/2024 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka 2024/2025.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kufikia siku ya leo tukiwa na afya njema ili tuweze kujadili bajeti hii ya Sekta ya Kilimo ambayo inagusa maisha ya wakulima kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu. Ninapenda kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kusimamia shughuli za kilimo nchini. Ninamuahidi Mheshimiwa Rais na Watanzania kuwa nitatumia uwezo wangu wote kwa uaminifu na uadilifu mkubwa kuhakikisha kuwa kilimo kinachangia kikamilifu katika kuhakikisha usalama wa chakula na lishe nchini, kulisha wengine kibiashara, kuongeza ajira na kuinua pato la mkulima ili kupunguza umasikini.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaungana na Wabunge wote kutoa pole kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa msiba mkubwa tulioupata wa kuondokewa na aliyekuwa Rais mstaafu wa Awamu ya Pili, Hayati Alhaji Ali Hassan Mwinyi. Ninatoa pole pia kwa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, watoto na ndugu wote wa Hayati Alhaji Ali Hassan Mwinyi na watanzania wote. Tutaendelea kuenzi mchango mkubwa wa Rais wetu wa Awamu ya Pili katika ujenzi wa Taifa letu kwa kuongoza mageuzi ya kiuchumi kutoka uchumi hodhi kuwa uchumi unaoongozwa na nguvu za soko. Hatua hiyo iliwezesha kuimarisha

ushirikiano na mashirika ya kimataifa kama vile Benki ya Dunia na Shirika la Fedha Duniani ambayo yameendelea kuwa miongoni mwa wabia wa maendeleo katika kilimo; kuhamasisha ushiriki wa Sekta Binafsi katika kuendeleza kilimo; na kuhamasisha ushiriki wa vijana katika kilimo na yeye kuwa mkulima wa mfano.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** ninatoa pole kwa Mheshimiwa Rais, Watanzania wote na familia kwa kuondokewa na aliyekuwa Waziri Mkuu mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Mhe. Edward Ngoyai Lowassa. Tutaendelea kumkumbuka kwa umahiri wake mkubwa katika usimamizi, uwajibikaji, ujasiri, ushupavu na ufanyaji wa maamuzi katika kuleta maendeleo kwa Taifa. Na mimi binafsi ninamshukuru kwa dhati kwa kunilea na kunikuza kisiasa na kiuongozi. Mafunzo yake ya msingi yanatujenga kuwa na utii kwa Taifa letu, Chama chetu na viongozi wetu wakuu. Aidha, yanatufundisha kuwa, Kiongozi anapaswa kuwa na maono, kufanya maamuzi, kuyasimamia maamuzi hayo na kuwa na msimamo kwenye mambo ya msingi kwa maendeleo ya Taifa letu. Daima tutaendelea kumkumbuka.

5. Kadhalika, ninatoa pole kwa familia na wananchi wa Jimbo la Mbarali kwa kuondokewa na aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo Mhe. Francis Leornad Mtega. Vilevile, ninatoa pole kwa familia na wananchi wa Jimbo la Kwahani Zanzibar kwa kuondokewa na aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo Mhe. Ahmed Yahya Abdulwakil. Ninaungana na Mheshimiwa Spika, wabunge wenzangu na watanzania kwa ujumla katika kuomboleza misiba hii mikubwa.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** ninatoa pole sana kwa wananchi wakiwemo wakulima wa Wilaya za Rufiji, Karatu, Mlimba na Hanang' pamoja na maeneo mengine yaliyopatwa na maafa. Wizara ya Kilimo imelichukulia suala hilo kwa uzito mkubwa kwa kutuma timu ya wataalam kufanya tathmini ya ardhi na mazao ya kilimo yaliyoathiriwa na mafuriko, kuainisha mahitaji ya chakula na pembejeo za kilimo, kutoa elimu kupitia Maafisa ugani kuhusu kilimo cha mazao ya muda mfupi na pia kuhakikisha wadau wanafikisha

misaada ya chakula na pembejeo za kilimo kwa wakulima ili kurejea katika shughuli zao za uzalishaji.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa kipaumbele katika uendelezaji wa Sekta ya Kilimo. Hatua hiyo imewezesha kuongeza hamasa ya wadau wa kilimo kuwekeza katika maeneo mbalimbali ya mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye pamoja na majukumu yake makubwa aliyonayo, amekuwa mstari wa mbele katika kusisitiza kilimo endelevu na kinachozingatia utunzaji wa mazingira, kuimarisha usalama wa chakula na kupambana na umasikini na yeye mwenyewe kufanya shughuli za kilimo kama mkulima.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, ninapenda kutumia fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.) kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa hapa Bungeni wakati wa kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2024/2025. Hotuba hiyo imetoa maelezo na maelekezo kuhusu maendeleo ya Sekta ya Kilimo hususan katika uendelezaji wa kilimo cha umwagiliaji, maendeleo ya Ushirika na upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo. Ninamhakikishia kuwa maelekezo yake yote yamezingatiwa katika mpango na bajeti ya Wizara ya Kilimo katika mwaka 2024/2025. Vilevile, ninamshukuru kwa dhati kwa mchango anaoutoa katika Sekta hii ya kilimo kwa kufuatilia utekelezaji wa shughuli za kilimo na yeye kuwa mkulima.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** pia nitumie fursa hii kumpongeza Mhe. Dkt. Dotto Mashaka Biteko (Mb.) kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninaamini kupitia yeye uratibu wa shughuli za kilimo utaendelea kuimarika na kuwezesha kufikiwa kwa malengo yaliyowekwa. Ninamuahidi kumpa ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yake.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** nikupongeze wewe binafsi kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (Inter Parliamentary Union - IPU), Naibu Spika Mheshimiwa Mussa Azan Zungu (Mb.) pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa uongozi wenu wenye weledi, ujuzi na ustadi mkubwa ambao umewezesha utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya nchi ikiwemo Sekta ya Kilimo. Aidha, ninawapongeza Mhe. Deodatus Philip Mwanyika Mbunge wa Jimbo la Njombe na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo pamoja na Mhe. Dkt Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Jimbo la Madaba na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kwa kuchaguliwa na Bunge kuwa wenyeviti wa Bunge.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** pia ninaipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa ushauri, maoni na miongozo mbalimbali ya kuendeleza Sekta ya Kilimo. Niihakikishie Kamati kuwa maoni na ushauri wao umezingatiwa katika kipindi chote cha utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2023/2024 na maandalizi ya mpango wa mwaka 2024/2025. Aidha, ninawapongeza wabunge wote kwa umahiri wenu mkubwa katika kuchangia mijadala inayoendelea katika Mkutano wa 15 wa Bunge hili la Bajeti.

12. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee ninampongeza Mhe. David Ernest Silinde Mbunge wa Jimbo la Mbozi Magharibi kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Kilimo. Ninamshukuru sana kwa ushirikiano anaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara ya Kilimo. Vilevile, ninampongeza aliyekuwa Naibu Waziri wa Kilimo Mhe. Anthony Peter Mavunde (Mb.) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Madini. Ninamshukuru sana kwa ushirikiano wake katika kipindi chote alichofanya kazi katika Wizara ya Kilimo na ninamtakia mafanikio katika utekelezaji wa majukumu yake mapya.

13. Pia, ninamshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Bw. Gerald Geofrey Mweli, Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Hussein Mohamed Omar, pamoja na Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi, Bodi na Wakala zilizo chini ya Wizara na watumishi wote kwa kazi nzuri na ushirikiano

mkubwa wanaoutoa katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

14. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya kipekee ninawashukuru wakulima wote nchini na Sekta binafsi, kwa mchango wao mkubwa katika kuhakikisha nchi inakuwa na usalama wa chakula na kuongeza uuzaji wa mazao nje ya nchi. Pia, ninawashukuru kwa dhati taasisi za fedha, wabia wa maendeleo na Asasi zisizo za Serikali kwa mchango wao katika kukuza Sekta ya Kilimo nchini.

15. ***Mheshimiwa Spika,*** ninatoa shukrani za pekee kwa wananchi wa Jimbo la Nzega Mjini kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kipindi chote cha kuwawakilisha hapa Bungeni. Aidha, ninawapongeza kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali ambazo zinalenga kuleta maendeleo katika Jimbo letu. Pia, ninawashukuru sana Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi, Madiwani na watumishi wa Halmashauri ya Mji wa Nzega kwa ushirikiano wao wanaoendelea kunipatia katika utekelezaji wa majukumu yangu. Ninawaahidi kuendelea kuwatumikia kwa juhudi na uaminifu mkubwa kwa lengo la kuliletea maendeleo Jimbo letu la Nzega Mjini.

## 2 HALI YA KILIMO

### 2.1 Mchango wa Kilimo katika Uchumi

16. ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Kilimo katika mwaka 2023 ilikua kwa asilimia 4.2 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.3 mwaka 2022. Vilevile, Sekta ya Kilimo imechangia asilimia 26.5 katika Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 26.2 mwaka 2022, imetoa ajira kwa wananchi kwa wastani wa asilimia 65.6 na kuchangia asilimia 65 ya malighafi za viwanda. Sekta ya Kilimo kwa upande wa mazao ilikua kwa asilimia 4.2 mwaka 2023 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 2.7 mwaka 2022; imechangia asilimia 16.1 kwenye Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 15 mwaka 2022; na imeendelea kuchangia asilimia 100 ya upatikanaji wa chakula.
Vilevile, mauzo ya mazao ya kilimo nje ya nchi katika mwaka 2022/2023 yamefikia takribani Dola za Marekani Bilioni 2.3

ikilinganishwa na takriban Dola za Marekani Bilioni 1.2 katika mwaka 2019/2020.

**2.2 Hali ya Chakula**

17. ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa mazao ya chakula katika msimu wa kilimo wa 2022/2023 ulifikia tani 20,402,014 ikilinganishwa na tani 17,148,290 katika msimu wa kilimo wa 2021/2022 sawa na ongezeko la asilimia 19. Katika kipindi hicho, uzalishaji wa mazao ya nafaka ulikuwa tani 11,448,757 ikilinganishwa na tani 9,233,298 msimu wa kilimo 2021/2022 sawa na ongezeko la asilimia 23.9 na uzalishaji wa mazao yasiyo nafaka ulikuwa tani 8,953,258 ikilinganishwa na tani 7,914,992 katika msimu wa kilimo 2021/2022 sawa na ongezeko la asilimia 13.1.

18. Aidha, uzalishaji wa mahindi katika msimu wa kilimo wa 2022/2023 ulikuwa tani 8,010,949 ikilinganishwa na tani 6,417,356 zilizozalishwa katika msimu wa kilimo wa 2021/2022 sawa na ongezeko la asilimia 24.83. Aidha, uzalishaji wa mchele katika kipindi hicho ulikuwa tani 2,332,188 ikilinganishwa na tani 1,708,369 zilizozalishwa katika msimu wa kilimo wa 2021/2022 sawa na ongezeko la asilimia 36.52. Uzalishaji wa mazao mengine ni kama unavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 1.**

19. ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa chakula kwa msimu wa kilimo wa 2022/2023 ulitosheleza mahitaji ya chakula ya tani 16,390,404 kwa mwaka 2023/2024 na kuwepo kwa ziada ya tani 4,011,611. Kutokana na hali hiyo, Taifa limejitosheleza kwa chakula kwa asilimia 124 ikilinganishwa na utoshelevu wa asilimia 114 mwaka 2022/2023. Aidha, utoshelevu wa chakula unatarajiwa kufikia asilimia 130 ifikapo mwaka 2025.

**Jedwali Na. 1:** Uzalishaji wa Mazao ya Chakula kwa Msimu 2022/2023 (Tani) na upatikanaji wa chakula kwa mwaka 2023/2024 – Tathmini Ya Awali (Juni, 2023)

| **Nafaka** | **Mahindi** | **Mtama & Malezi** | **Mchele** | **Ngano** | **Nafaka Jumla** |
|---|---|---|---|---|---|
| Uzalishaji | 8,010,949 | 1,019,098 | 2,332,188 | 86,522 | 11,448,757 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Mahitaji | 6,648,698 | 2,298,101 | 1,168,282 | 312,247 | 10,427,327 |
| Uhaba(-)/Ziada (+) | 1,362,251 | -1,279,003 | 1,163,907 | -225,725 | 1,021,430 |
| **Utoshelevu/SSR(%)** | **120** | **44** | **200** | **28** | **110** |
| | | | | | |
| **Yasio nafaka** | **Mikunde** | **Ndizi** | **Muhogo** | **Viazi** | **Yasiyo nafaka jumla** |
| Uzalishaji | 2,802,839 | 1,224,144 | 2,575,453 | 2,350,821 | 8,953,258 |
| Mahitaji | 964,739 | 1,095,624 | 2,735,480 | 1,167,234 | 5,963,077 |
| Uhaba(-)/Ziada (+) | 1,838,100 | 128,520 | 160,027 | 1,183,587 | 2,990,181 |
| **Utoshelevu/SSR(%)** | **291** | **112** | **94** | **201** | **150** |
| | | | | | |
| **Jumla** | **Nafaka** | **Yasio nafaka** | | | **Jumla** |
| Uzalishaji | 11,448,757 | 8,953,258 | | | 20,402,014 |
| Mahitaji | 10,427,327 | 5,963,077 | | | 16,390,404 |
| Uhaba(-)/Ziada (+) | 1,021,430 | 2,990,181 | | | 4,011,611 |
| **Utoshelevu/SSR(%)** | **110** | **150** | | | **124** |

**Chanzo:** *Wizara ya Kilimo, 2023*

20. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na Taifa kujitosheleza kwa chakula, Halmashauri 19 zilibainika kuwa na upungufu wa chakula katika vipindi tofauti. Katika kukabiliana na upungufu huo, Wizara kupitia NFRA imetoa tani 481.9 za chakula cha msaada katika Halmashauri za Muleba (tani 23.16), Shinyanga Manispaa (tani 4.776), Geita DC, Geita Mji na Nyangh'wale (tani 33.4), Kakonko (tani 5.184), Temeke (tani 25), Kinondoni (tani 25), Ubungo (tani 25), Kigamboni (tani 25), Rufiji (tani 20), Bahi (tani 8.1), Kibiti (tani 20), Hanang' (tani 14.4), Moshi Manispaa (tani 20), Hai (18.6), Same (tani 44.28) na Kilosa (tani 20). Aidha, Halmashauri za Kibiti, Rufiji na Hanang' zilipewa unga wa mahindi tani 50, 100 na 14.4; mtawalia. Pia, Wizara kupitia NFRA imeidhinisha mauzo ya tani 500 za mahindi ya bei nafuu kwenda katika Halmashauri ya Liwale.

### 2.3 Hali ya Umwagiliaji

21. ***Mheshimiwa Spika,*** eneo linalomwagiliwa katika mwaka 2023/2024 ni hekta 727,280.6. Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imeendelea kujenga na kukarabati miundombinu ya umwagiliaji ambapo katika mwaka 2022/2023 ilianza ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji yenye jumla ya hekta 95,005 na katika mwaka 2023/2024 ilianza ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji yenye jumla ya hekta 161,180.46. Miradi hiyo ikikamilika itaongeza eneo la umwagiliaji kwa hekta 256,185.46 hivyo kufanya eneo linalomwagiliwa kufikia jumla ya hekta 983,466.06 ambazo ni sawa na asilimia 81.95 ya lengo la hekta 1,200,000 ifikapo mwaka 2025 kama ilivyoelekezwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 - 2025.

### 2.4 Hali ya Ushirika

22. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa kushirikiana na Wizara za kisekta, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Wadau wa ushirika imeendelea na uhamasishaji na uanzishaji wa Vyama vya Ushirika katika sekta mbalimbali za kiuchumi ikiwemo Kilimo, Uvuvi, Mifugo, Fedha, Viwanda na Madini. Hadi Aprili 2024, Vyama vya Ushirika vilivyosajiliwa vimefikia 7,522 ikilinganishwa na vyama 7,300 mwaka 2023. Kati ya hivyo, 78 ni Vyama vya Upili, 4,391 ni Vyama vya Ushirika wa Kilimo na Masoko (AMCOS), 2,074 ni Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS), kimoja (1) ni Shirikisho la Vyama vya Ushirika, 978 ni Vyama vinavyojishughulisha na umwagiliaji, mbogamboga, ufugaji, uvuvi, viwanda na madini.

## 3. MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2023/2024

### 3.1 Makusanyo ya Maduhuli

**Fungu 43**

23. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara ilikadiria kukusanya mapato ya Shilingi **6,677,254,000** kupitia Fungu 43, kutokana na vyanzo mbalimbali. Hadi Aprili 2024, Wizara imekusanya Shilingi **4,558,250,017.09** sawa na asilimia 68.3 ya makadirio. Inatarajiwa kuwa malengo yaliyowekwa yatafikiwa ifikapo mwisho wa mwaka 2023/2024.

**Fungu 05**
24. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara ilikadiria kukusanya mapato ya Shilingi **10,000,000,000** kupitia Fungu 05, kutokana na vyanzo mbalimbali. Hadi Aprili 2024, Wizara imekusanya Shilingi **1,914,783,657.5** sawa na asilimia 19.2 ya makadirio.

**3.2 Fedha Zilizoidhinishwa kwa Mafungu Yote (43, 24 na 05)**
25. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/ 2024, Wizara ya Kilimo ilitengewa jumla ya Shilingi **970,785,619,000** kupitia Fungu 43, Fungu 05 na Fungu 24. Kati ya fedha hizo, Shilingi **767,835,139,000** ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na Shilingi **202,950,480,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

**Fedha zilizotolewa.**
26. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2024, Shilingi **522,157,771,839** sawa na asilimia 53.8 ya fedha zilizoidhinishwa zimetolewa. Kati ya fedha hizo, Shilingi **421,700,267,306** ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na Shilingi **100,457,504,534** ni kwa ya matumizi ya kawaida.

**4 MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2023/2024**
27. ***Mheshimiwa Spika,*** ninawasilisha hotuba hii wakati huu ambapo Serikali yetu ya Awamu ya Sita (6) inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imetimiza miaka mitatu (3) ya uongozi. Katika Bajeti ya mwaka 2023/2024, Wizara ya Kilimo ilikuja mbele ya Bunge lako Tukufu kuomba kuidhinishiwa Shilingi Bilioni 970.8 ambapo fedha hizo zilikuwa zinalenga utekelezaji wa vipaumbele vitano (5) ambavyo ni kuongeza uzalishaji na tija, kuongeza ajira zenye staha na ushiriki wa vijana na wanawake katika kilimo, kuimarisha usalama wa chakula na lishe, kuimarisha upatikanaji wa masoko, mitaji na mauzo ya mazao nje ya nchi na kuimarisha maendeleo ya ushirika. Vipaumbele hivyo, vimetekelezwa kupitia mikakati 27. Leo mbele ya Bunge lako Tukufu ninawasilisha mafanikio ya utekelezaji wa Bajeti hiyo kama ifuatavyo:-

### 4.1 Kuongeza Uzalishaji na Tija

28. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na kutofautiana kwa takwimu za mazao zinazopatikana katika mifumo mbalimbali ya Serikali, na kwa kuwa shughuli za kilimo msingi wake mkubwa ni kukuza uchumi wa nchi na kuondoa umasikini, Wizara imeyagawa mazao ya kilimo katika makundi mapya manne (4) ambayo ni mazao ya chakula, mazao ya bustani (horticulture), mazao ya mafuta na mazao asilia ya biashara ili takwimu hizo ziweze kushabihiana na mifumo ya Serikali ikiwemo mifumo ya Benki Kuu, Mamlaka ya Mapato Tanzania na Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa kuzingatia makundi hayo, hivyo kuongeza ufanisi katika kupanga mipango ya kuendeleza Sekta ya Kilimo.

29. ***Mheshimiwa Spika,*** eneo la uzalishaji wa mazao ya chakula lina jumla mazao 12 ambayo yanatengeneza kundi la mazao ya chakula (food basket) **Jedwali Na. 2.** Uzalishaji wa mazao ya chakula msimu wa 2022/2023 umeongezeka hadi tani 20,402,014 kutoka tani 17,148,290 msimu wa kilimo wa 2021/2022 sawa na ongezeko la asilimia 19 dhidi ya lengo la tani 24,245,684. Uzalishaji wa tani 20,402,014 za mazao ya chakula umewezesha utoshelevu wa chakula kwa mwaka 2023/2024 kufikia asilimia 124 ikilinganishwa na lengo la asilimia 150 ifikapo 2030. Ongezeko hilo linatokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya chakula katika msimu wa kilimo 2022/2023 ukilinganisha msimu wa kilimo wa mwaka 2021/2022 ambapo uzalishaji wa mahindi uliongezeka kutoka tani 6,417,000 hadi tani 8,010,949, sawa na ongezeko la asilimia 24.8; mchele kutoka tani 1,708,000 hadi tani 2,332,188, sawa na ongezeko la asilimia 36.5; ngano kutoka tani 61,698 hadi tani 86,522, sawa na ongezeko la asilimia 40.2; na mazao ya jamii ya mikunde kutoka tani 2,498,559 hadi tani 2,802,839, sawa na ongezeko la asilimia 12.2.

**Jedwali Na. 2:** Mwenendo wa Uzalishaji wa Mazao ya Chakula (Tani '000') Msimu 2020/2021 -2022/2023.

| Na. | Zao | 2020/2021 | 2021/2022 | 2022/2023 |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mahindi | 7,039 | 6,417 | 8,011 |
| 2 | Mchele | 2,688 | 1,708 | 2,332 |
| 3 | Ngano | 70 | 62 | 87 |
| 4 | Mtama | 807 | 768 | 738 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 5 | Ulezi | 76 | 62 | 61 |
| 6 | Uwele | 195 | 216 | 221 |
| 7 | Muhogo | 2,486 | 2,411 | 2,575 |
| 8 | Maharage | 1,287 | 1,269 | 1,484 |
| 9 | Mikunde | 947 | 1,099 | 1,319 |
| 10 | Ndizi | 1,443 | 1,290 | 1,224 |
| 11 | Viazi Vitamu | 1,254 | 1,415 | 1,798 |
| 12 | Viazi Mviringo | 373 | 431 | 552 |
| | **Jumla** | **18,665** | **17,148** | **20,402** |

***Chanzo:*** *Wizara ya Kilimo 2023*

30. ***Mheshimiwa Spika,*** katika eneo la mazao asilia ya biashara, uzalishaji wa mazao hayo katika mwaka 2023/2024 umeongezeka kutoka tani 1,123,477.92 mwaka 2022/2023 hadi tani 1,260,321.1 sawa na asilimia 78.05 ya lengo la kuzalisha tani 1,614,758 na uzalishaji unaendelea. Ongezeko hilo limechangiwa na uzalishaji wa korosho ambao umefikia tani 254,500 ikilinganishwa na tani 189,113.79 mwaka 2022/2023 sawa na ongezeko la asilimia 63.6 ya lengo la kuzalisha tani 400,000 mwaka 2023/2024; uzalishaji wa pamba umefikia tani 282,510 ikilinganishwa na tani 174,486 mwaka 2022/2023 sawa na asilimia 80.7 ya lengo la kuzalisha tani 350,000 mwaka 2023/2024; na uzalishaji wa sukari umefikia tani 392,724 ikilinganishwa na tani 460,048.94 mwaka 2022/2023 sawa na asilimia 85.4 ya lengo la kuzalisha tani 445,000.

31. Kadhalika, ongezeko hilo limechangiwa na uzalishaji wa kahawa ambao umefikia tani 66,071.8 ikilinganishwa na tani 82,000 mwaka 2022/2023 sawa na asilimia 77.7 ya lengo la kuzalisha tani 85,000; uzalishaji wa pareto ambao umefikia tani 4,238 ikilinganishwa na tani 3,150 mwaka 2022/2023 sawa na asilimia 121.08 ya lengo la kuzalisha tani 3,500; uzalishaji wa mkonge ambao umefikia tani 56,732.7 ikilinganishwa na tani 48,359.49 mwaka 2022/2023 sawa na asilimia 94.55 ya lengo la kuzalisha tani 60,000; uzalishaji wa chai ambao umefikia tani 13,525 ikilinganishwa na tani 26,753 mwaka 2022/2023 sawa na asilimia 45 ya lengo la kuzalisha tani 30,000; uzalishaji wa tumbaku ambao umefikia tani 178,521 ikilinganishwa na tani 125,592 mwaka 2022/2023; na uzalishaji wa kakao umefikia tani 9,729.2 ikilinganishwa na tani 13,972.7 mwaka 2022/2023 sawa na

asilimia 64.9 ya lengo la kuzalisha tani 15,000. Uzalishaji wa mazao hayo ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 3.**

**Jedwali Na. 3:** Mwenendo wa Uzalishaji wa Mazao Asilia ya Biashara Mwaka 2021/2022 Hadi 2023/2024 (Tani).

| Na | | Uzalishaji kwa miaka iliyopita | | Uzalishaji mwaka 2023/2024 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **MAZAO** | **2021/2022** | **2022/2023** | **Lengo** | **Uzalishaji** | **Asilimia** |
| 1 | Korosho | 240,158 | 189,113.79 | 400,000 | 254,500* | 62.6 |
| 2 | Pamba | 144,792 | 174,486 | 350,000 | 282,510 | 80.6 |
| 3 | Pareto | 2,694 | 3,150 | 3,500 | 4,238 | 121.1 |
| 4 | Kahawa | 66,837 | 82,000 | 85,000 | 66,071* | 77.7 |
| 5 | Tumbaku | 70,699 | 125,592 | 226,000 | 178,521* | 78.9 |
| 6 | Chai | 24,825 | 26,754 | 30,000 | 13,525* | 42.6 |
| 7 | Mkonge | 44,151 | 48,359.49 | 60,000 | 56,732.7* | 94.6 |
| 8 | Sukari | 379,280 | 460,048.94 | 445,000 | 392,724 | 85.4 |
| 9 | Kakao | 9,741 | 13,973.70 | 15,000 | 11,499.4* | 64.9 |
| | **JUMLA** | **983,177** | **1,123,477.92** | **1,614,758** | **1,260,321.1** | **78.05** |

***Chanzo:*** *Wizara ya Kilimo 2024*
**Uzalishaji/Ununuzi unaendelea*

32. ***Mheshimiwa Spika,*** katika eneo la mazao ya bustani uzalishaji umefikia tani 8,438,273.98 mwaka 2022/2023 ikilinganishwa na tani 7,902,047.7 mwaka 2021/2022 sawa na ongezeko la asilimia 6.7 ya lengo la tani 6,264,346.86. Uzalishaji wa mazao ya bustani ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 4**.

**Jedwali Na. 4:** Mwenendo wa Uzalishaji wa Mazao ya Bustani (Tani) Mwaka 2020/2021 hadi 2022/2023

| Na. | Mazao | 2020/2021 | 2021/2022 | 2022/2023 |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Matunda | 7,210,586 | 6,335,642 | 6,530,302 |
| 2. | Maua | 592 | 489.5 | 576.9 |
| 3. | Mboga | 2,007,182.90 | 1,450,022.10 | 1,777,878.49 |
| 4. | Viungo | 117,321.90 | 115,894.10 | 129,516.59 |
| | **Jumla** | **9,335,682.8** | **7,902,047.7** | **8,438,273.98** |

***Chanzo:*** *Wizara ya Kilimo 2023*

33. ***Mheshimiwa Spika,*** katika eneo la mazao ya mafuta uzalishaji umefikia tani 2,143,098.7 ikilinganishwa na tani 1,703,950.93 mwaka 2021/2022 sawa na ongezeko la asilimia 25.8 ya lengo la tani 3,033,266. Kwa mfano, uzalishaji wa alizeti umeongezeka kutoka tani 425,653.1 msimu wa 2021/2022 hadi tani 1,132,298.34 msimu wa 2022/2023 sawa na ongezeko la asilimia 166 na ufuta umeongezeka kutoka tani 79,170.43 msimu wa 2021/2022 hadi tani 266,694 mwaka 2022/2023 sawa na ongezeko la asilimia 237.2. Mwenendo wa uzalishaji wa mazao ya mafuta ni kama unavyoonekana katika **Jedwali. Na. 5**

**Jedwali Na. 5:** Mwenendo wa Uzalishaji wa Mazao ya Mafuta (Tani) Mwaka 2020/2021 Hadi 2022/2023

| **Na.** | **Mazao** | **2020/2021** | **2021/2022** | **2022/2023** |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Alizeti | 478,900 | 425,653.10 | 1,132,298.34 |
| 2. | Ufuta | 236,162 | 79,170.43 | 266,994 |
| 3. | Nazi | 192,238.90 | 201,538.50 | 95,465.20 |
| 4. | Chikichi | 58,791 | 60,789.90 | 62,125.00 |
| 5. | Karanga | 895,219 | 936,799 | 586,216.09 |
| | **Jumla** | **1,861,311** | **1,703,950.93** | **2,143,098.70** |

**Chanzo:** *Wizara ya Kilimo, 2023*

34. ***Mheshimiwa Spika,*** ongezeko la uzalishaji limechangiwa pia na kuongezeka kwa tija ambapo katika kipindi hicho tija ya mazao ya kilimo imeongezeka kama ifuatavyo:- tija ya zao la mahindi imeongezeka kutoka tani 1.9 kwa hekta hadi tani 2.0 kwa hekta sawa na asilimia 33 ya uwezekano wa tija ya kuzalisha tani 6 kwa hekta; tija ya zao la mpunga imeongezeka kutoka tani 1.25 kwa hekta hadi tani 4 kwa hekta sawa na asilimia 80 ya uwezekano wa tija ya kuzalisha tani 5 kwa hekta; tija ya maharage imeongezeka kutoka tani 0.8 kwa hekta hadi tani 1.6 kwa hekta sawa na asilimia 53 ya uwezekano wa tija ya kuzalisha tani 3 kwa hekta; na tija ya ngano imeongezeka kutoka tani 1 kwa hekta hadi tani 1.4 kwa hekta sawa na asilimia 28 ya uwezekano wa tija ya kuzalisha tani 5 kwa hekta.

35. Kadhalika, tija ya uzalishaji wa korosho imeongezeka kutoka tani 0.5 kwa hekta hadi tani 0.7 kwa hekta sawa na asilimia 35 ya uwezekano wa tija ya kuzalisha tani 2 kwa hekta; tija ya zao la pamba imeongezeka kutoka tani 0.6 kwa hekta hadi tani 1.34 kwa hekta sawa na asilimia 45 ya uwezekano wa tija ya kuzalisha tani 3 kwa hekta; tija ya zao la miwa imeongezeka kutoka tani 82.04 kwa hekta hadi tani 93.70 kwa hekta sawa na asilimia 93.7 ya uwezekano wa tija ya kuzalisha wastani tani 100 kwa hekta; na tija ya zao la tumbaku imeongezeka kutoka tani 1.38 kwa hekta hadi tani 1.5 kwa hekta sawa na asilimia 60 ya uwezekano wa tija ya kuzalisha tani 2.5 kwa hekta.

36. Vilevile, tija ya zao la kahawa imeongezeka kutoka tani 0.3 kwa hekta hadi tani 1 kwa hekta sawa na asilimia 67 ya uwezekano wa tija ya kuzalisha tani 1.5 kwa hekta; tija ya zao la chai imeongezeka kutoka tani 1.1 kwa hekta hadi tani 1.5 kwa hekta sawa na asilimia 43 ya uwezekano wa tija ya kuzalisha tani 3.5 kwa hekta; tija ya zao la mkonge imeongezeka kutoka tani 1.2 kwa hekta hadi tani 1.38 kwa hekta sawa na asilimia 55 ya uwezekano wa tija ya kuzalisha tani 2.5 kwa hekta; na tija ya zao la pareto imeongezeka kutoka tani 0.75 kwa hekta hadi tani 0.8 kwa hekta sawa na asilimia 64 ya uwezekano wa tija ya kuzalisha tani 1.25 kwa hekta.

37. ***Mheshimiwa Spika,*** tija ya zao la alizeti imeongezeka kutoka tani 0.8 kwa hekta hadi tani 1 kwa hekta sawa na asilimia 30 ya uwezekano wa tija ya kuzalisha tani 4 kwa hekta; na tija ya zao la ufuta imeongezeka kutoka tani 1.49 kwa hekta hadi tani 1.6 kwa hekta sawa na asilimia 0.64 ya uwezekano wa tija ya kuzalisha tani 2.5 kwa hekta.

38. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kufikia mafanikio hayo Wizara imetekeleza Mikakati ifuatayo:-

**4.1.1 Kuimarisha utafiti wa mbegu Utafiti na ugunduzi wa teknolojia**

39. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya Shilingi Bilioni 40.73 zilitengwa kwa ajili ya kuimarisha utafiti wa mbegu.

40. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TARI katika mwaka 2023/2024 ilipanga kufanya utafiti wa teknolojia 25 zikiwemo utafiti wa mbegu aina kumi (10) za mazao ya kimkakati ya nafaka, jamii ya mikunde na mafuta; teknolojia mpya kumi (10) za kanuni bora za kilimo katika nyanja za afya ya udongo, magonjwa, wadudu na viuatilifu; teknolojia tano (5) za kuongeza thamani ya mazao ya maharage, miwa, soya, viazi lishe na korosho; na kutoa mafunzo ya matumizi ya teknolojia bora 3,000 za kilimo kwa maafisa ugani 5,000 na wakulima 2,000,000.

41. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2024 TARI imegundua teknolojia 64 sawa na asilimia 256 ya lengo la teknolojia 25. Teknolojia hizo ni aina 53 za mbegu bora, nane (8) za kanuni bora za kilimo na tatu (3) za kuongeza thamani. Kati ya aina 53 za mbegu bora zilizogunduliwa, aina sita (6) zimethibitishwa kwa ajili ya matumizi zikiwemo tano (5) za zabibu na moja (1) ya tumbaku. Mbegu hizo ni TARIZAB1, TARIZAB2, TARIZAB3 (kwa ajili ya matunda), TARIZAB4 (kwa ajili ya kukausha), TARIZAB5 (kwa ajili ya mvinyo) na TRBS23. Mbegu za zabibu zilizogunduliwa zina sifa ya kutoa mavuno kwa wingi (tani 7.5 – 27.5/hekta), kinzani dhidi ya wadudu na kuhifadhiwa kwa muda mrefu (siku 14 – 21) baada ya kuvuna ikilinganishwa na aina nyingine ambazo huharibika baada ya siku saba (7).

42. Vilevile, aina 47 kati ya 53 zilizogunduliwa zimewasilishwa Taasisi ya Uthibiti wa Ubora wa Mbegu Tanzania (Tanzania Official Seed Certification Institute - TOSCI) kwa ajili ya majaribio na kuidhinisha matumizi. Mbegu hizo ni pamoja na maharage (6), choroko (10), korosho (4), mpunga (6), migomba (6), mahindi (9), tumbaku (3) na biringanya (3).

43. ***Mheshimiwa Spika*** teknolojia nane (8) za kanuni bora za kilimo zilizogunduliwa zikiwemo tatu (3) za kudhibiti wadudu na tano (5) za fangasi katika zao la korosho zimependekezwa kwa ajili ya matumizi. Kadhalika, aina tatu (3) za teknolojia za kuongeza thamani zilizogunduliwa ambazo ni mvinyo wa beetroot, achali ya mchanganyiko wa mbogamboga na maembe, juisi ya tunda la pasheni na maembe zimependekezwa kwa ajili ya matumizi. Vilevile,

TARI kwa kushirikiana na Shirika la NYUMBU imebuni mashine ya kuchakata miwa kwa ajili ya wakulima wadogo, mashine hiyo ipo katika hatua ya majaribio. Pia, mafunzo kuhusu matumizi ya teknolojia za kilimo na kanuni za kilimo bora cha mazao yametolewa kwa wakulima 139,079 na Maafisa ugani 473 ambapo teknolojia 580 zimesambazwa.

44. ***Mheshimiwa Spika,*** TARI ilipanga kuzalisha mbegu mama tani 28, mbegu za awali tani 450 na mbegu za msingi tani 6,973. Aidha, TARI kupitia mradi wa AFDP ilipanga kuzalisha tani 53.2 za mbegu za awali na tani 5.6 mbegu mama za mazao ya mahindi, alizeti na maharage; na kusafisha na kuzalisha mbegu za asili tani 10 za mazao ya nafaka, jamii ya mikunde na mbogamboga.

45. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi Aprili 2024 Wizara kupitia TARI :-

i. Imezalisha jumla ya mbegu za utafiti tani 787.08 ikiwemo mbegu mama tani 16.85, mbegu za awali tani 206.93 na mbegu za msingi tani 563.59;

ii. Imezalisha tani 203.48 za mbegu zilizothibitishwa;

iii. Imesafisha aina 15 za mbegu bora za mpunga zilizozalisha tani 3.9 za mbegu za awali na usafishaji wa aina nne (4) za mbegu bora za ngano (lumbesa, mbayuwayu, chiriku na sifa) unaendelea; na

iv. Imesafisha aina 54 za mbegu za asili za mpunga, mbili (2) za bamia (pusa na sawani), mbili (2) za nyanya (tanya na tengeru), mbili (2) za mchicha (akheri na nguruma) na aina 10 za mbegu za maharage.

46. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TARI ilipanga kuhifadhi vizazi vya mbegu katika vituo vya TARI vya Dakawa, Hombolo, Ifakara na Selian kwa ajili ya utafiti.

47. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2024 TARI imeendelea kutunza vinasaba 28,977 vya mazao ya mpunga (1,798), mtama (248), uwele (41), ulezi (215), ngano (57), zabibu (36), migomba (157), maharage (355), muhogo (433), korosho (22,773), mahindi (342), shayiri (313), viazi vitamu (212), viazi mviringo (6), miwa (142), minazi (7), pareto (380), chikichi (3), ufuta (555), pamba (828), parachichi (62) na matunda na miti ya dawa (14) kwa ajili ya kuendeleza utafiti na uhifadhi wa mbegu katika vituo vyake vya utafiti ikiwa ni pamoja na TARI Dakawa, Hombolo, Ifakara na Selian. **Kuimarisha Miundombinu ya Utafiti**

48. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TARI katika mwaka 2023/2024, ilipanga kujenga miundombinu ya umwagiliaji; kukarabati majengo ya ofisi katika vituo 17; kujenga ghala sita (6) zenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani 2,490 za mbegu na zenye vyumba vya ubaridi katika vituo sita (6) vya TARI Uyole, Ilonga, Ukiriguru, Maruku, Ifakara na Kihinga; na kukamilisha ujenzi wa ghala tano (5) zenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani 2,075 katika vituo vitano (5) vya TARI vya Naliendele, Tumbi, Selian, Hombolo na Dakawa.

49. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2024, utekelezaji ni kama ifuatavyo:-

i. Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji katika vituo 12 vya utafiti vyenye ukubwa wa hekta 874.9 umefikia wastani wa asilimia 37.5;

ii. Ujenzi wa ghala tano (5) katika vituo vya TARI Naliendele, TARI Tumbi, TARI Selian, TARI Hombolo na TARI Dakawa umefikia wastani wa asilimia 45; na

iii. Ujenzi wa ghala mpya sita (6) katika vituo vya TARI Uyole, TARI Ilonga, TARI Ukiriguru, TARI Maruku, TARI Ifakara na TARI Kihinga zabuni ipo katika hatua ya kusaini mkataba.

50. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilipanga kukamilisha ujenzi wa ofisi na nyumba nne (4) za watumishi katika kituo cha TARI Kihinga – Kigoma;

kuendelea na ujenzi wa ofisi za TARI Makao Makuu – Dodoma; na kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Utafiti wa Kahawa cha Mwayaya (Buhigwe).

51. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi Aprili, 2024 ujenzi wa ofisi na nyumba nne (4) za watumishi katika kituo cha TARI Kihinga umefikia asilimia 95; ujenzi wa ofisi ya TARI Makao Makuu umefikia asilimia 65; na ujenzi wa kituo cha utafiti wa kahawa cha Mwayaya kilichopo Buhigwe katika Mkoa wa Kigoma umekamilika.

52. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TARI ilipanga kujenga maabara mpya ya kuzalisha miche kwa njia ya chupa (*tissue culture*) katika kituo cha TARI Maruku kwa ajili ya kuzalisha miche bora ya migomba na maabara ya utambuzi na udhibiti wa visumbufu vya zao la korosho katika kituo cha TARI Naliendele; kujenga maabara ya kuzalisha miche ya mkonge kwa njia ya chupa (tissue culture) katika kituo cha TARI Mlingano na kuimarisha miundombinu ya maabara ya udongo ya TARI Mlingano.

53. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2024, utekelezaji umefikia hatua zifuatazo:

i. Ujenzi wa maabara ya kuzalisha miche ya mkonge kwa njia ya chupa (tissue culture) katika kituo cha TARI Mlingano umefikia asilimia 98. Maabara hiyo itakapokamilika itaongeza uwezo wa kuzalisha miche bora kutoka miche 500,000 hadi miche 10,000,000
ii. Ukarabati wa maabara ya udongo ya TARI Mlingano umefikia asilimia 80 na itakapokamilika itakuwa na uwezo wa kupima sampuli za udongo 20,000 kwa mwaka; na
iii. Zabuni kwa ajili ya ujenzi wa maabara za TARI Maruku na TARI Naliendele zipo katika hatua ya makabidhiano ya eneo la ujenzi.



***Picha Na.1:*** *Jengo la Maabara ya Tissue Culture - TARI Mlingano*

54. ***Mheshimiwa Spika,*** TARI ilipanga kununua vifaa vya maabara ya udongo ya TARI Mlingano ili kuiwezesha kupata ithibati (accreditation); na kununua vitendanishi vya maabara za tissue culture za TARI Uyole, Tengeru na Mikocheni ili kuongeza uwezo wa kuzalisha miche.

55. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2024, TARI imenunua vifaa na vitendanishi vya maabara ya TARI Mlingano. Kupitia mradi wa *Biosecurity* na TARI Tengeru imenunua madawa na vitendanishi vya maabara ikiwemo *MS – Media, Aga, Benzel Amminopurine* (BAP), *Indole Butric Acid* (IBA) kwa ajili ya uzalishaji kwenye maabara ya tissue culture. Vilevile, kupitia ufadhili wa COSTECH na BMGF, TARI Mikocheni imenunua madawa na vitendanishi ikiwemo *MS – Media, Vitamins, Sucrose, Aga, PCR kit, DNA extraction kit* na *Primwer* kwa ajili ya maabara ya *tissue culture*.

56. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024 Wizara ilipanga kuviwezesha vituo vya utafiti vya TARI kupata hati miliki ya maeneo yao; kuendelea kujenga uzio katika kituo cha TARI Uyole (hekta 1,042); kuanza ujenzi wa uzio wa mashamba katika vituo vingine 16 vya TARI na vituo vidogo 18. Kadhalika, Wizara ilipanga

kuiwezesha Taasisi ya Utafiti wa Chai Tanzania (Tea Research Institute of Tanzania-TRIT) kukamilisha utaratibu wa kupata Ithibati (ISO 17025 Accreditation) ya maabara ya udongo na mimea iliyopo Wilaya ya Mufindi kwa lengo la kuimarisha utafiti wa chai na kupima afya ya udongo.

57. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2024 utekelezaji ni kama ifuatavyo :-

i. TARI imepata hati miliki za mashamba saba (7) katika vituo vya TARI vya Uyole, Naliendele, Dakawa, Ukiriguru, Tumbi, Mlingano na Kihinga;
ii. Ujenzi wa uzio katika mashamba ya vituo vya TARI Uyole yenye ukubwa wa hekta 1,042 umefikia asilimia 40;
iii. Zabuni ya manunuzi ya wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa uzio katika vituo vingine imetangazwa;
iv. Ukaguzi wa awali kwa ajili ya kuiwezesha maabara ya udongo na mimea ya TRIT kupata ithibati umefanywa na wakaguzi wa *Southern Africa Develepment Community Accreditation Services* (SADCAS) ambapo ukamilishaji wa ithibati upo katika hatua ya mwisho. Hivyo, ni matarajio ya Wizara kuwa kazi hiyo itakamilika katika mwaka 2024/2025.

58. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TORITA ilipanga kukarabati na kujenga majengo mapya ya utawala na maabara; kuimarisha upatikanaji wa vitendea kazi; kununua vifaa na vitendanishi vya maabara; kujenga miundombinu ya umwagiliaji kwa ajili ya kuzalisha tani 1.2 za mbegu za ziada za tumbaku; kununua mashine ya kufungasha mbegu; na kujenga aina mpya za mabani manne (4) ya mfano kwa wakulima yenye uwezo wa kukausha tani 2.4 za majani ya tumbaku kwa kutumia nishati mbadala ili kulinda mazingira.

59. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2024 utekelezaji ni kama ifuatavyo:-

i. Mkataba wa ununuzi wa vifaa na vitendanishi vya maabara umesainiwa;

ii. Utafiti wa upembuzi wa awali (reconnaissence survey) umefanyika katika kituo kidogo cha utafiti cha TORITA kilichopo Mtanila - Chunya
kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji;
iii. Mkataba kwa ajili ya ununuzi wa mashine ya kufungasha mbegu za tumbaku umesainiwa; na
iv. Ujenzi wa mabani manne (4) ya kufundishia wakulima kutumia nishati ya kuni na nishati mbadala (organic briquettes - vitofali) umekamilika katika vituo vya Tumbi - Tabora (2) na Mtanila - Chunya (2). Mabani hayo yanauwezo wa kukausha tani 2.4 za majani ya tumbaku kwa siku tano (5) hadi 10 kila moja.

60. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kahawa Tanzania (Tanzania Coffee Reaserch Institute - TaCRI) ilipanga kuzalisha mbegu bora za kahawa tani 1.8 zikiwemo tani 1.5 za Arabika na tani 0.3 za Robusta; kuzalisha miche chotara 20,000,000 kwa kushirikiana na Bodi ya Kahawa; kutoa mafunzo kuhusu kilimo bora cha kahawa kwa maafisa ugani 511, wakulima viongozi 483 na wakulima wadogo 3,393 katika Halmashauri zinazozalisha kahawa; na kununua magari manne (4).

61. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2024 TaCRI kwa kushirikiana na Bodi ya Kahawa Tanzania imezalisha mbegu bora aina ya Arabika tani 1.5 na Robusta tani 0.3 sawa na asilimia 100 ya lengo. Vilevile, TaCRI imezalisha miche 21,899,560 sawa na asilimia 109.5 ya lengo kwa ajili ya kusambaza kwa wakulima katika maeneo ya uzalishaji wa kahawa. Aidha, TaCRI imetoa mafunzo kuhusu kilimo bora cha zao la kahawa kwa Maafisa ugani 126, wakulima viongozi 137 na wakulima wadogo 2,987.

62. ***Mheshimiwa Spika,*** TARI kupitia miradi ya Kuwezesha Upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo Tanzania (Tanzania Agriculture Input Support Project – TAISP) na Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi (Agriculture and Fisheries Development Programme – AFDP), ilipanga kuwajengea uwezo watafiti watano (5) katika Shahada ya Uzamivu na watafiti wanne (4) wa Shahada ya Uzamili.

63. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2024 watumishi watano (5) wanasoma shahada ya uzamivu. Aidha, watumishi 115 wanaendelea na masomo ya muda mrefu katika vyuo mbalimbali. Kati ya hao, 28 wanasoma shahada ya uzamivu, 48 shahada ya uzamili, 33 shahada ya kwanza na astashada mmoja (1). Pia, TARI imenunua magari 15, matrekta nane (8) na mashine za kuvunia mbili (2).



***Picha Na. 2****: Ujenzi wa ofisi za Kituo cha TARI Kihinga mkoani Kigoma*

### 4.1.2 Uzalishaji wa mbegu na miche bora pamoja na usambazaji wa mbegu na miche ya ruzuku

64. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya Shilingi Bilioni 43.03 zilitengwa kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji na usambazaji wa mbegu na miche bora.

65. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili, 2024 upatikanaji wa mbegu bora umefikia tani 68,473.67 ikilinganishwa na tani 64,152.11 mwaka 2022/2023. Upatikanaji huo ni sawa na asilimia 54 ya mahitaji ya tani 127,650 kwa mwaka. Aidha, uzalishaji wa mbegu bora ndani ya nchi umefikia tani 49,414 sawa na ongezeko la asilimia 11.4 ikilinganishwa na tani 44,344.4 zilizozalishwa mwaka 2022/2023. Uzalishaji wa mbegu bora ndani ya nchi umechangiwa na ASA, TARI na Sekta binafsi.
Upatikanaji na uzalishaji wa mbegu bora nchini ni kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na.6.**

**Jedwali Na. 6:** Upatikanaji wa Mbegu Bora Nchini mwaka 2023/2024

| Na. | Zao | Uzalishaji wa Ndani(Tani) | Bakaa (Tani) | Uagizaji toka Nje(Tani) | Jumla (Tani) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mahindi | 23,083 | 2,029.03 | 15,122.15 | 40,234 |
| 2 | Mpunga | 322 | 41.074 | - | 363 |
| 3 | Mtama | 426 | 21.238 | 16.65 | 464 |
| 4 | Alizeti | 1,078 | 39.349 | 164.16 | 1,282 |
| 5 | Mbegu za Mboga | 73 | 92.467 | 701.89 | 867 |
| 6 | Peas | - | - | - | - |
| 7 | Malisho | - | 3.76 | - | 4 |
| 8 | Maharage | 43 | - | 30.19 | 73 |
| 9 | Pamba | 23,750 | - | - | 23,750 |
| 10 | Choroko | 0.75 | - | - | 0.75 |
| 11 | Mbaazi | 2 | - | - | 2 |
| 12 | Karanga | 9 | - | - | 9 |
| 13 | Ufuta | 43 | 4.59 | - | 47 |
| 14 | Ngano | 378 | 117.325 | - | 496 |
| 15 | Kunde | 0.25 | - | - | 0.25 |
| 16 | Njugu mawe | - | - | - | - |
| 17 | Ulezi | 1 | | - | 1 |
| 18 | Tumbaku | - | 0.286 | - | 0 |
| 19 | Maharage ya Soya | 204 | - | 675.89 | 880 |
| **Jumla** | | **49,414** | **2,349.12** | **16,710.93** | **68,474** |

**Chanzo:** *Wizara ya Kilimo, 2024*

66. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia ASA ilipanga kuzalisha na kusambaza tani 5,000 za mbegu bora za alizeti na ngano kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku. Hadi Aprili, 2024 jumla ya tani 3,593.4 zimepatikana ambapo tani 1,619 ni za ngano na tani 1,974.4 ni za alizeti. Vilevile, tani 1,015 kati ya tani 1,619 za ngano zimesambazwa kwa mpango wa ruzuku katika mikoa ya Njombe, Rukwa, Mbeya, Manyara, Arusha na Kilimanjaro. Aidha, tani 725 kati ya tani 1,974.4 za mbegu za alizeti zimesambazwa kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku katika mikoa ya Singida, Dodoma, Manyara, Arusha, Tanga, Kilimanjaro, Ruvuma, Rukwa, Katavi na Geita.

67. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia ASA, TARI na Bodi za mazao ilipanga kuzalisha miche 37,500,000 ya mazao mbalimbali. Hadi Aprili,

2024, jumla ya miche 29,261,780 ya mazao ya kahawa (21,899,560), chai (3,048,000), mkonge (2,413,277), korosho (239,762), chikichi (307,588), parachichi (647,724), zabibu (338,101), minazi (75,000), viazi (278,155), miwa (4,543) na migomba (10,070) imezalishwa na kusambazwa kwa wakulima katika mikoa ya Songwe, Kagera, Kilimanjaro, Njombe, Iringa, Tanga, Morogoro, Kigoma, Tabora na Mbeya. Vilevile, pingili za muhugo 4,438,170 zimezalishwa na kusambazwa kwa wakulima 267,145 katika mikoa ya Mara, Morogoro, Pwani, Mwanza, Geita, Kigoma, Katavi, Tabora, Singida, Mtwara, Lindi na Ruvuma.




***Picha Na.3:*** *Kitalu cha Miche ya Chikichi katika shamba la mbegu Msimba - Morogoro*

68. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2023/2024 ilipanga kuimarisha uzalishaji na upatikanaji wa mbegu bora nchini kwa kuendelea kuiwezesha ASA kujenga na kukamilisha miundombinu ya umwagiliaji yenye jumla ya hekta 3,304.8 ifikapo mwaka 2025 katika mashamba yote ya mbegu ya ASA ya Kilimi (hekta 300), Msimba (hekta 400), Bugaga (hekta 100), Mbozi (hekta 400), Luhafwe (hekta 400), Dabaga (hekta 300), Namtumbo (hekta 500), Arusha (hekta 100), Kilangali (hekta 300), Mazizi (hekta 4.8), Msungura (hekta 100) na Mwele (hekta 400). Aidha, ilipanga kuiwezesha ASA kununua vitendea kazi vikiwemo matrekta kumi (10) na zana zake.

69. ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa ASA imeendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji yenye ukubwa wa hekta 805.5 iliyopangwa katika mwaka 2022/2023 na hekta 795 zilizopangwa katika mwaka 2023/2024.

70. Hadi Aprili, 2024 utekelezaji umefikia hatua zifuatazo:-

i. Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji wa hekta 220 kati ya 400 katika shamba la Kilimi umekamilika. Aidha, ukamilishaji wa eneo la hekta 180 katika shamba hilo unaendelea;
ii. Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika shamba la Arusha (hekta 200) umefikia asilimia 55;
iii. Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika Shamba la Msimba (hekta 200) umefikia asilimia 45;
iv. Ujenzi wa bwawa lenye ujazo wa lita milioni 45 katika shamba la mbegu Arusha umekamilika;
v. Ujenzi wa bwawa lenye ujazo wa lita milioni 45 katika shamba la Msimba umefikia asilimia 70; na
v. Uwekaji wa miundombinu ya umwagiliaji kwa njia ya matone katika shamba la Tengeru lenye ukubwa wa hekta 5.5 umekamilika;
vi. Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika shamba la Namtumbo (hekta 300) utekelezaji upo katika hatua ya kumpata mshauri elekezi; na
vii. Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya Mbozi (hekta 100), Arusha (hekta 100) na Msimba (hekta 100) utekelezaji upo katika hatua za kusaini mkataba.

71. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, ASA imeendelea na upembuzi yakinifu kwa ajili ya kutekeleza miradi ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya mbegu yenye ukubwa wa hekta 3,000. Mashamba hayo ni Mwele (hekta 500), Namtumbo (hekta 900), Kilimi (hekta 200), Msungura (hekta 100), Mbozi (hekta 500) na Msimba (hekta 800). Hadi Aprili, 2024 utekelezaji wa ujenzi wa miundombinu upo katika hatua ya tathmini ya kumpata mshauri elekezi.

72. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilipanga kuiwezesha ASA kujenga ghala katika mashamba ya Arusha, Mbozi, Namtumbo, Msungura na Kilangali; kununua na kufunga mitambo miwili (2) ya kuchakata

mbegu katika mashamba ya mbegu ya Mbozi na Namtumbo; na kulipa fidia ya mashamba mapya ya mbegu ya Tanganyika (Luhafwe), Namtumbo na Chalinze (Msungura na Mazizi). Hadi Aprili, 2024 taratibu za manunuzi ya wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa ghala la Arusha zimefikia hatua ya kusaini mkataba na mshauri elekezi. Aidha, taratibu za ununuzi wa mitambo miwili (2) ya kuchakata mbegu katika mashamba ya mbegu ya Mbozi na Namtumbo zipo katika hatua ya tathmini.

73. ili kuzuia uvamizi wa mashamba ya mbegu, ASA imekamilisha ujenzi wa uzio katika mashamba ya Msimba – Kilosa (hekta 2,600) na Kilimi – Nzega (hekta 1,102). Aidha, ujenzi wa uzio katika shamba la Arusha (hekta 600) utekelezaji upo katika hatua ya tathmini ya kumpata mkandarasi. Pia, ASA imenunua magari matatu (3), pikipiki nne (4), mashine za kupandia mpunga mbili (2) na matrekta mapya tisa (9) na zana zake kwa ajili ya kurahisisha shughuli za uzalishaji katika mashamba ya mbegu.

74. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia ASA ilipanga kuendelea kufungua maeneo mapya katika mashamba ya Mwele (hekta 300), Luhafwe (hekta 400), Msimba (hekta 300), Kilimi (hekta 200), Namtumbo (hekta 200) na Mbozi (hekta 200). Hadi Aprili 2024, jumla ya hekta 1,619 sawa na asilimia 101.2 ya lengo zimefunguliwa katika mashamba ya mbegu ya Kilimi (hekta 260), Namtumbo (hekta 389), Msimba (hekta 540), Dabaga (hekta 100) na Mwele (hekta 330). Eneo hili litaongeza uzalishaji wa mbegu wa takribani tani 3,000 kwa kuipatia sekta binafsi. Vilevile, utumiaji wa eneo hilo unaongeza ulinzi dhidi ya uvamizi wa mashamba.

**Uthibiti wa Ubora wa Mbegu**

75. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Taasisi ya Uthibiti wa Ubora wa Mbegu (Tanzania Official Seed Certification Institute - TOSCI) ilipanga kusimamia majaribio ya utambuzi (Distinctness, Uniformity and Stability - DUS) kwa aina 150 za mbegu; majaribio ya umahiri kwa aina mpya 25 za mbegu; kukagua mashamba ya mbegu ya umma na binafsi hekta 55,000; maduka 2,220 na ghala 114 za mbegu.

76. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2024 aina mpya za mbegu 16 zimefanyiwa majaribio ya utambuzi (DUS) na kufaulu. Aina hizo ni

mazao ya malisho ya mifugo aina nne (4), mahindi aina mbili (2), soya aina mbili (2), choroko aina nne (4), pilipili hoho aina moja (1), tikiti maji aina moja (1), kabeji aina moja (1) na ngogwe aina moja (1). Pia, jumla ya majaribio ya aina mpya za mbegu 13 yamepandwa na uchukuaji wa taarifa katika maeneo ya majaribio ya TOSCI makao makuu na Kanda ya Kaskazini, Arusha unaendelea. Majaribio hayo ni kwa mazao ya bamia aina moja (1), "butternut" aina moja (1), tango aina moja (1), nyanya aina saba (7) na alizeti aina tatu (3).

77. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hicho, TOSCI imepanda mbegu kwa ajili ya Majaribio ya Umahiri ya Kitaifa (NPT) ya aina mpya za mbegu yaliyokamilisha taratibu za maombi katika maeneo ya malisho ya mifugo (Uyole-Mbeya), tumbaku (Chunya), mahindi (Milundikwa-Sumbawanga, Mbimba-Mbozi, Mtwango-Njombe, Kilolo, Seatondale-Iringa, GairoMorogoro) na alizeti (Gairo Morogoro). Vilevile, TOSCI imekagua jumla ya hekta 45,659.3 za mashamba 680 ya mbegu ambapo hekta zote zimekidhi viwango vya ubora wa kanuni bora za kilimo na utenganisho wa mashamba ya mbegu (Isolation Distance) kwa ajili ya uzalishaji wa mbegu bora.

78. TOSCI imefanya ukaguzi wa maduka ya mbegu 2,097 katika Mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Tabora, Kigoma, Mwanza, Shinyanga, Mara, Kagera, Iringa, Ruvuma, Njombe, Mbeya, Songwe, Dar es Salaam na Morogoro. Ukaguzi huo umebaini uwepo wa baadhi ya mbegu ambazo hazijafanyiwa vipimo vya ubora, mbegu zilizoingizwa nchini kinyume cha sheria na mbegu ambazo zimepimwa na kukutwa hazina ubora kutokana na utunzaji mbaya. Aidha, mbegu hizo zimeteketezwa na wahusika kufikishwa kwenye vyombo vya sheria.

79. Kadhalika, ili kuimarisha ubora wa mbegu TOSCI imechukua jumla ya sampuli 1,131 za mbegu na kufanya vipimo katika maabara za TOSCI. Kati ya hizo, sampuli 978 sawa na asilimia 86.47 zilifaulu na sampuli 61 sawa na asilimia 5.40 hazikufaulu. Aidha, sampuli 92 sawa na asilimia 8.13 zinaendelea kufanyiwa vipimo vya maabara.

80. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuboresha shughuli za uthibiti na udhibiti ubora wa mbegu, TOSCI imeanzisha mfumo wa kielektroniki *TOSCI Online Application System* (TOAS) ambao unawezesha huduma zote kutolewa kupitia mfumo huo zikiwemo, usajili wa wauzaji wa mbegu bora, ukaguzi wa mashamba ya mbegu, vibali vya kuagiza na kuuza mbegu bora, kuomba lebo na vipimo vya maabara. Hadi Aprili, 2024 vibali 1,937 vimetolewa kupitia mfumo huo kwa vituo vya utafiti na kampuni za uzalishaji na uuzaji wa mbegu kwa ajili ya kuagiza tani 16,710.93 za mbegu kutoka nje ya nchi. Pia, vibali 70 vya kuuza mbegu tani 3,065 nje ya nchi zenye thamani ya Shilingi Bilioni 67.43 vimetolewa na wauzaji wa mbegu bora 6,617 wamesajiliwa.

81. Vilevile, katika kupunguza udanganyifu wa wafanyabiashara wanaouza mbegu zisizo na ubora nchini, TOSCI imeanzisha huduma ya utoaji wa lebo za kielektroniki ambapo hadi Aprili 2024, jumla ya lebo 13,240,899 zimetolewa.

82. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha miundombinu ya uthibiti na udhibiti wa mbegu, TOSCI imetekeleza yafuatayo:-

i. Kukamilisha ujenzi wa maktaba ya rejea za nasaba za mimea (Genetic Reference Library) kwa ajili ya kutunzia taarifa za vinasaba vya aina mbalimbali za mimea ya mazao; na
ii. Kukamilisha ujenzi wa jengo la kuhifadhia mbegu za rejea katika hali ya ubaridi (Coldroom Building) lililopo TOSCI Makao Makuu; na
iii. Kukamilisha ukarabati wa maabara na Ofisi za Kanda ya Nyanda za Juu Kusini zilizopo Njombe kwa ajili kuimarisha huduma za upimaji wa ubora wa mbegu kwa wazalishaji wa mbegu katika Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

83. ***Mheshimiwa Spika,*** maabara kuu ya mbegu ya Taifa iliyopo katika Mkoa wa Morogoro imehuishiwa ithibati ya ISTA (International Seed Testing Association) ambayo imewezesha kujumuishwa kwa makundi muhimu ya mazao yanayozalishwa nchini. Makundi hayo ni mazao ya nafaka, jamii ya mikunde, mbogamboga na mazao mengineyo. Vilevile, TOSCI imejiunga na makundi muhimu ya Skimu za Mbegu za Organization for Economic Cooperation and Development - OECD ambazo ni za mazao ya nafaka, mahindi, mtama na uwele, mbogamboga,

malisho na mikunde na mazao ya mafuta na nyuzi. Hatua hiyo, itawezesha Tanzania kufanya biashara ya mbegu kimataifa na kuliongezea taifa fedha za kigeni.

84. Kadhalika, ili kuhakikisha wazalishaji na wafanyabiashara wa mbegu wanazingatia Sheria na Kanuni, TOSCI imetoa mafunzo kuhusu sheria na kanuni za mbegu pamoja na uthibiti na udhibiti wa ubora wa mbegu kwa wafanyabiashara 302 wa mbegu. Pia, imetoa mafunzo kwa wakulima 200 kuhusu uzalishaji wa mbegu kwa mfumo wa Ubora wa Mbegu Uliobainishwa na Mkulima (UMBEGU).

**4.1.3 Uwekezaji kwenye Huduma za Ugani**

85. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya Shilingi Bilioni 15 zilitengwa kwa ajili ya kuimarisha huduma za ugani nchini. Kazi zilizopangwa katika mwaka 2023/2024 ni kununua na kusambaza magari 55, visanduku vya ugani 4,000, sare 4,000, *soil scanner* 45 na vishikwambi 1,500 na kusambaza kwa maafisa ugani ili kuongeza ufanisi wa utoaji huduma za ugani kwa wakulima.

86. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2024 Wizara imenunua vishikwambi 4,446 sawa na asilimia 296.4 ya lengo. Kati ya hivyo vishikwambi 946 vimesambazwa katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Tanga kwa ajili ya ukusanyaji wa takwimu na taarifa za kilimo (ARDS) na usambazaji unaendelea. Vilevile, leseni za kudumu 143 zimenunuliwa ili kuwezesha vifaa vya kupima afya udongo (soil scanner) kufanya kazi iliyokusudiwa. Aidha, Wizara imenunua na kusambaza visanduku vya ugani 1,000 kwa maafisa ugani kilimo 1,000 katika mikoa ya Mbeya, Songwe, Njombe, Iringa, Ruvuma, Rukwa na Katavi sawa na asilimia 25 ya lengo. Kadhalika, magari 51 na pikipiki 550 kwa ajili ya maafisa ugani ngazi ya Mkoa na Halmashauri yamelipiwa na Wakala wa Manunuzi ya Serikali anakamilisha taratibu za manunuzi.

87. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imetoa mafunzo kuhusu matumizi ya vifaa vya kupima afya ya udongo kwa Maafisa Ugani 497 kutoka katika mikoa 26 nchini. Mafunzo hayo yamewezesha jumla ya wakulima 12,737 kupima sampuli 8,339 za udongo kutoka kwenye mashamba yao kwa kutumia *soil scanners* na kupatiwa hati za matokeo ya afya ya udongo za mashamba yao.

88. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilipanga kuimarisha Mfumo wa M-Kilimo na matumizi ya Kituo cha Huduma kwa Wateja ili kuwawezesha wadau kupata huduma kupitia ujumbe mfupi, mitandao ya kijamii na barua pepe, kuwezesha na kusimamia matumizi sahihi ya vitendea kazi zikiwemo pikipiki pamoja na kukarabati vituo sita (6) vya rasilimali za kilimo vya Kata (WARCs) katika Mikoa ya Kigoma, Pwani, Lindi, Morogoro, Simiyu na Tanga.

89. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kukiwezesha kituo cha Huduma kwa Wateja kufanya kazi kwa muda wa siku saba (7) za wiki kuanzia saa 1:30 asubuhi hadi saa 4:00 usiku ambapo hadi Aprili, 2024 kituo hicho kimepokea simu 21,754 za wadau kuhusu vibali vya kusafirisha mazao, mbolea ya ruzuku, visumbufu vya mazao na uendelezaji wa mazao ya kilimo. Vilevile, Wizara imeendelea kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji wa matumizi sahihi ya pikipiki katika utoaji wa huduma kwa wakulima. Aidha, taratibu za manunuzi ya mkandarasi kwa ajili ya kukarabati vituo sita (6) vya rasilimali za kilimo vya Kata katika Mikoa ya Kigoma, Pwani, Lindi, Morogoro, Simiyu na Tanga zipo katika hatua ya kusaini mkataba.

**Maonesho ya Kilimo ya Kimataifa ya Nanenane**

90. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2023/2024 ilipanga kuimarisha viwanja viwili (2) vya maonesho ya kilimo vya John Mwakangale (Mbeya) na Nzuguni (Dodoma) kuwa na hadhi ya Maonesho ya Kilimo ya Kimataifa. Hadi Aprili, 2024, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika viwanja vya John Mwakangale na Nzuguni umekamilika ambapo ramani na mchoro vimeandaliwa kwa ajili ya kuanza taratibu za ujenzi.

91. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuwezesha upatikanaji wa teknolojia za kisasa za kilimo, Wizara imeratibu Maonesho ya Kimataifa na Sikukuu za Wakulima – Nanenane ya mwaka 2023 yaliyofanyika katika Viwanja vya John Mwakangale Jijini Mbeya. Katika maonesho hayo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan alizindua ugawaji wa seti ya vifaa vya kupima afya ya udongo (soil scanner, kompyuta, *printer*, *lamination* mashine na vishikwambi) kwa Maafisa Ugani.

92. Vilevile, Mheshimiwa Rais alizindua mpango wa kuchimba visima kwa wakulima wadogo kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji katika eneo lenye ukubwa wa ekari 2.5. Kadhalika, alizindua ugawaji wa vifaa vya kutengeneza vihenge vya chuma kwa vijana 420 wa Tanzania bara na Visiwani na ghala 14 za kuhifadhi nafaka zilizojengwa chini ya Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu Tanzania (TANIPAC). Aidha, katika maonesho hayo tuzo kwa watafiti bora watano (5) na Mikoa mitano (5) iliyoongoza kwa uzalishaji wa mazao ya chakula zilitolewa.



***Picha Na.4:*** *Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akizindua ugawaji wa Vifaa vya Ugani (Extension KIT) kwa Maafisa Ugani Katika Siku ya Kilele cha Maadhimisho ya Maonesho ya Kimataifa ya Kilimo ya NaneNane ya mwaka 2023.*

**Mafunzo ya Kilimo**

93. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2023/2024, ilipanga kudahili wanafunzi 3,000 katika ngazi ya Astashahada ya Awali, Astashahada na Stashahada za kilimo. Kati ya hao, wanafunzi 2,500 watagharamiwa mafunzo kwa vitendo katika Halmashauri na Wilaya ili kuwajengea uzoefu wa kufanya kazi shambani na kuwawezesha kuajiriwa na kujiajiri. Vilevile, Wizara ilipanga kuwawezesha vijana 260 waliohitimu katika vyuo vya Kilimo hapa nchini kupata mafunzo ya kilimo katika mashamba makubwa nchini Israel. Kadhalika, Wizara ilipanga kugharamia mafunzo ya muda mrefu na mfupi ya watumishi 22 katika vyuo vya ndani kwa lengo la kuwaongezea maarifa na ujuzi wa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

94. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2024 Wizara imedahili wanafunzi 3,372 (Astashahada ya Awali 1,279; Astashahada 1,164; na Stashahada 929) katika Vyuo 14 vya Mafunzo ya Kilimo vya Umma katika fani za Kilimo. Udahili umeongezeka kutokana na ukarabati wa miundombinu ya vyuo na kuwezesha upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Aidha, jumla ya wanafunzi 2,400 wa stashahada na astashahada wanatarajiwa kuanza mafunzo kwa vitendo Mei, 2024 katika Halmashauri na viwanda kuendana na mpango wa programu ya mafunzo katika mwaka 2023/2024. Aidha, vijana 258 wanaendelea kupata mafunzo ya kilimo nchini Israel ili kuwawezesha kujiajiri na kutoa huduma na ushauri kwa wakulima kwa vitendo wataporejea nchini.

95. ***Mheshimiwa Spika,*** watumishi nane (8) wa shahada ya uzamili na mmoja (1) wa shahada ya kwanza wanaendelea na masomo katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (Sokoine University of Agriculture – SUA) na Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini. Kadhalika, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kilimo Endelevu Tanzania (Sustainable Agriculture Tanzania - SAT) imetoa mafunzo ya mbinu za ufundishaji kwa wakufunzi 124 yaliyolenga kuimarisha ubora wa elimu na kuwezesha wakufunzi kutoa mafunzo bora kwa wanafunzi na wakulima; mafunzo ya utungaji mitihani kwa wakufunzi 63 na mafunzo ya saikolojia na ushauri kwa walezi wa wanafunzi 56.

96. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilipanga kukarabati na kujenga miundombinu ya Vyuo sita (6) vya MATI Uyole, KATRIN, Inyala, Igurusi, Mtwara, Mlingano pamoja na Vituo vinne (4) vya Mafunzo kwa Wakulima vya Bihawana, Mkindo, Themi na Ichenga na kuvipatia Vyuo vya Mafunzo ya Kilimo Mlingano, HORTI Tengeru, Inyala, Maruku, Mubondo, Mtwara, Bihawana FTC, Ichenga FTC na Mkindo FTC vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

97. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2024 wakandarasi kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa baadhi ya miundombinu katika Vyuo vya Kilimo vya Uyole, KATRIN, Inyala, Igurusi, Mtwara, Mlingano pamoja na vituo vya Mafunzo ya Wakulima vya Bihawana, Mkindo, Themi na Ichenga wamepatikana. Vilevile, ununuzi wa magari matatu (3), matrekta matatu (3), vifaa vya TEHAMA na samani upo katika hatua mbalimbali za manunuzi.

98. Kadhalika, Wizara ilipanga kuendelea kushirikiana na SAT kupitia Mradi wa Kuwezesha Utekelezaji wa Mitaala Katika Vyuo vya Mafunzo ya Kilimo Awamu ya Pili kuandaa vitini vitatu (3) vya kufundishia moduli za kilimo; kuandaa vitabu vitatu (3) vya kiada kuhusu Kilimo Hai, Jinsia katika Kilimo na Utunzaji wa Mazingira; kuandaa miongozo mitatu (3) ya mafunzo kwa vitendo kwa ajili ya kufundishia moduli za Kilimo Hai, Jinsia katika Kilimo na Utunzaji wa Mazingira; na kutoa mafunzo rejea kwa wakufunzi kulingana na mahitaji yatakayoibuliwa.

99. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2024 vitini vitatu (3) vinavyohusu huduma za ugani, utunzaji wa udongo na maji na masoko ya kilimo vimeandaliwa ambapo nakala 1,800 zimechapishwa kwa ajili ya usambazaji katika vyuo vya mafunzo ya kilimo. Aidha, uandaaji wa vitabu vitatu (3) vya kiada kuhusu Kilimo Hai, Jinsia katika Kilimo na Utunzaji wa Mazingira unaendelea.

**4.1.4 Kuanza kujenga nyumba za maafisa ugani**

100. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2023/2024 ilipanga kuanza kujenga nyumba za Maafisa ugani ili kusogeza huduma za ugani karibu na wakulima na kurahisisha utoaji wa ushauri wa kitalaam wa kilimo. Hadi Aprili, 2024 mchoro wa nyumba za Maafisa Ugani umekamilika na taratibu za ujenzi wa nyumba 50 katika Halmashauri 46 zilizopo kwenye mikoa 18 nchini zimeanza.

**4.1.5 Upimaji wa afya ya udongo na utoaji wa ruzuku ya mbolea na viuatilifu**

101. ***Mheshimiwa Spika***, jumla ya Shilingi Bilioni 174.3 zilitengwa kwa ajili ya kutoa ruzuku ya mbolea na kupima afya ya udongo katika mashamba mapya 30 yenye ukubwa wa hekta 200,000 katika mikoa ya Pwani (hekta 60,000), Morogoro (hekta 50,000), Njombe (30,000), Songwe (hekta 30,000) na Tanga (hekta 30,000).

**Upimaji wa afya ya udongo**

102. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi Aprili 2024, mashamba yenye ukubwa wa hekta 438,666.86 yamepimwa afya ya udongo katika mikoa ya Tanga (hekta 116,610.16), Manyara (hekta 125,645.59), Simiyu (hekta 11,070) na mashamba ya BBT (hekta 136,186.11). Pia, hekta 49,155 za mashamba ya wakulima walipimiwa afya ya udongo kwa

kutumia *soil scanners* nchi nzima kwa lengo la kubaini upatikanaji wa virutubishi katika ardhi ya kilimo. Matokeo ya upimaji wa afya ya udongo hususan kuhusu upatikanaji wa virutubishi kwenye udongo yaliwasilishwa kwa wakulima na kutoa mapendekezo ya aina ya mbolea na mazao yanayofaa kuzalishwa katika maeneo husika.



***Picha Na.5:*** *Wataalam wa Wizara ya Kilimo wakipima afya udongo wilaya ya Bukoba katika Mkoa wa Kagera*

**Ruzuku ya Mbolea**

103. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/ 2024, Wizara ilipanga kuendelea kuratibu upatikanaji na usambazaji wa mbolea nchini kwa kutoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima. Hadi Aprili, 2024 upatikanaji wa mbolea umefikia tani 1,052,218.4 ikilinganishwa na tani 819,442 mwaka 2022/2023 sawa na asilimia 123.95 ya makadirio ya mahitaji ya mbolea ya tani 848,884 kwa mwaka. Upatikanaji huo umetokana na tani 114,223 zilizozalishwa ndani ya nchi, tani 611,651.4 zilizoingizwa kutoka nje ya nchi na tani 326,344 bakaa ya msimu wa 2022/2023 (**Jedwali Na. 7**). Aidha, tani 471,839.9 zenye thamani ya ruzuku ya Shilingi 136,495,898,332 zimesambazwa kwa wakulima kupitia mpango wa ruzuku ambapo tani 92,134.65 zenye thamani ya Shilingi Bilioni 13.7 zimetolewa kama ruzuku kwenye zao la tumbaku.

**Jedwali Na. 7:** Upatikanaji wa Mbolea nchini mwaka 2023/2024 (Tani)

| Aina ya Mbolea | Bakaa Msimu 2022/2023 | Uzalishaji wa Ndani | Uagizaji Kutoka Nje | Jumla ya Upatikanaji | Mahitaji ya Mbolea 2023/2024 |
|---|---|---|---|---|---|
| UREA | 49,824 | 0 | 200,166 | 249,990 | 230,429 |
| DAP | 90,495 | 0 | 54,498 | 144,993 | 176,227 |
| NPKs | 34,365 | 512 | 90,860 | 125,737 | 134,315 |
| CAN | 36,013 | 0 | 97,986 | 133,999 | 116,719 |
| SA | 17,300 | 0 | 111,852 | 129,152 | 58,407 |
| Fomi | 12,732 | 41,046 | 0 | 53,778 | 11,434 |
| Minjingu | 16,780 | 28,856 | 0 | 45,636 | 9,498 |
| TSP | 0 | 0 | 3,200 | 3,200 | 6,946 |
| MoP | 1,968 | 0 | 16,365 | 18,333 | 13,333 |
| NPS | 28,651 | 0 | 0 | 28,651 | 26,878 |
| NPSZn | 32,820 | 0 | 0 | 32,820 | 20,895 |
| Other N | 1,590 | 2,662 | 15,090 | 19,342 | 10,979 |
| Lime | 305 | 8,628 | 0.2 | 8,933 | 1,100 |
| Dolomite | 4 | 2,762 | 0 | 2,766 | 3,000 |
| Gypsum | 0 | 512 | 0.2 | 512 | 2,089 |
| Other Fertilizers | 3,497 | 29,245 | 21,634 | 54,376 | 26,635 |
| **Jumla** | **326,344** | **114,223** | **611,651.4** | **1,052,218.4** | **848,884** |

**Chanzo:** *Wizara ya Kilimo, 2024*

104. ***Mheshimiwa Spika***, uzalishaji wa ndani wa tani 114,223 umetokana na uzalishaji wa viwanda vya ndani kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 8**. Vilevile, kiwanda cha kuchanganya mbolea cha ITRACOM kimesimika mitambo itakayokuwa na uwezo wa kuzalisha tani 800,000 za mbolea kwa mwaka. Aidha, kiwanda hicho kikikamilika kitakuwa na uwezo wa kuzalisha mbolea tani 1,000,000 kwa mwaka.

**Jedwali Na. 8:** Uzalishaji wa Mbolea Ndani ya Nchi mwaka 2023/2024

| Na. | Jina la Kampuni | Tani |
|---|---|---|
| 1 | ITRACOM | 41,046 |
| 2 | Minjingu | 28,856 |
| 3 | YARA | 26,305 |
| 4 | ABM | 6,836 |

| | | |
|---|---|---|
| 5 | ETG | 4,535 |
| 6 | Dodoma Cement | 4,190 |
| 7 | Keen feeders | 1,082 |
| 8 | HSSL | 850 |
| 9 | Mtali | 245 |
| 10 | Sianga | 170 |
| 11 | Input Agri | 54 |
| 12 | Amka | 20 |
| 13 | Fahari | 15 |
| 14 | Juanco | 11 |
| 15 | Farm Access | 8 |
| **Jumla** | | **114,223** |

***Chanzo:*** *Wizara ya Kilimo, 2024*

**Usajili wa wakulima na wafanyabiashara wa mbolea**

105. ***Mheshimiwa Spika***, katika kurahisisha usambazaji wa mbolea kwa wakulima nchini, Wizara ya Kilimo imeongeza idadi ya waingizaji wakubwa wa mbolea kutoka 28 mwaka 2022/2023 hadi 31 mwaka 2023/2024; mawakala wadogo 3,265 mwaka 2022/2023 hadi 3,500 mwaka 2023/2024; na kusajili vyama vya ushirika 776 kwa ajili ya kuwa mawakala wa kusambaza mbolea. Pia, ghala 987 zenye uwezo wa kuhifadhi tani 458,610 zimeainishwa nchini kwa ajili ya kuhifadhi mbolea.

106. Vilevile, Wizara kupitia TFRA ilipanga kuendelea na usajili wa wakulima katika mfumo wa kidigiti ili kuwa na uhakika wa takwimu na taarifa za wakulima na hivyo kuiwezesha Serikali kupanga mipango sahihi ya kuendeleza kilimo nchini; kutoa mafunzo ya ukaguzi wa ubora wa mbolea; kusajili aina mpya za mbolea na visaidizi vyake 85; na kutoa leseni 2,100. Hadi Aprili, 2024 wakulima 3,910,556 wamesajiliwa kwenye kanzidata *https://ruzuku.tfra.go.tz*. Usajili huo utakamilika kwa kuchukua *coordinates* (GPS) za mashamba ya wakulima wadogo na mkulima kupatiwa hati ya shamba lake.

107. Vilevile, TFRA imetoa mafunzo kuhusu ukaguzi wa ubora wa mbolea kwa wataalam 20 katika Mikoa ya Tabora, Mbeya Mtwara, Kilimanjaro, Manyara, Singida, Morogoro, Kigoma, Simiyu, Dodoma, Njombe, Lindi na Dar es Salaam ili kuimarisha shughuli za udhibiti na ukaguzi wa mbolea. Pia, TFRA imesajili aina mpya za

mbolea na visaidizi vyake 50 na imetoa vibali 339 vya kuagiza mbolea nje ya nchi.

108. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara katika mwaka 2023/2024, ilipanga kuiwezesha Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC) kiasi cha Shilingi Bilioni 40 kama mtaji na kuufanya mtaji wake kuwa Shilingi Bilioni 46 kwa ajili ya kununua mbolea na kununua ardhi ya kujenga kiwanda cha kuchanganya mbolea (Blending Facilities) kwa kushirikiana na Sekta Binafsi.

109. ***Mheshimiwa Spika***, ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara imetekeleza yafuatayo:-

i. Kuiwezesha TFC kiasi cha Shilingi Bilioni 40 kwa ajili ya ununuzi wa tani 25,000 na kusambazwa kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku katika mikoa 26 hapa nchini;
ii. Kuendelea kukamilisha taratibu za ununuzi wa mbolea tani 50,000 zenye thamani ya Shilingi Bilioni 70 kupitia Mradi wa Kuwezesha Upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo (TAISP);
iii. Kuiwezesha TFC kununua na kusambaza jumla ya tani 4,000 za mbolea ya kupandia baada ya kuingia makubaliano ya usambazaji wa mbolea na Kampuni ya OCP AFRICA;
iv. Kupata eneo lenye ukubwa wa ekari 14 katika Wilaya ya Kisarawe na ekari tano (5) eneo la Bandari Kavu Kwala katika Mkoa wa Pwani kwa ajili ya ujenzi wa ghala la kuhifadhi pembejeo za kilimo;
v. Kununua magari matano (5) kwa ajili ya usimamizi wa biashara ya pembejeo;
vi. Kufungua vituo vipya vya mauzo katika mikoa ya Iringa, Kilimanjaro, Kigoma, Singida, Mara, Tanga, Manyara, Morogoro, Ruvuma na Katavi; na
vii. Kuingia makubaliano ya usambazaji wa mbolea na Vyama vya Ushirika 29 na Mawakala wa pembejeo 500 kwa ajili ya kusambaza mbolea.



***Picha Na. 6:*** *Mbolea iliyoagizwa na Kampuni ya Mbolea Tanzania TFC kutoka nje ya nchi ikishushwa kwenye Meli katika bandari ya Dar es Salaam na kupakiwa kwenye Lori kwa ajili ya kusambazwa kwa wakulima*

110. Kadhalika, Wizara imelipa madeni yenye thamani ya kiasi cha Shilingi Bilioni 42.38 kwa mawakala wa pembejeo za kilimo kwa msimu wa 2015/2016. Pia, Serikali imelipa Shilingi 22,098,632,846.30 ikiwa ni sehemu ya Shilingi 78,410,372,041.60 ya madeni ya wazabuni wa pamba yaliyohakikiwa na kukubaliwa mwaka 2023/2024.

**Upatikanaji wa Viuatilifu na Udhibiti wa Visumbufu vya Mazao Viuatilifu**

111. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara katika mwaka 2023/2024, kupitia Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu (Tanzania Plant Health and Pesticide Authority – TPHPA) ilipanga kununua viuatilifu lita 101,000 kwa ajili ya kudhibiti viwavijeshi, kweleakwelea, nzige, nzi wa matunda na panya; kusavei na kuainisha maeneo ya mazalia ya visumbufu vya mazao na mimea na kudhibiti visumbufu; na kuimarisha udhibiti wa ubora wa viuatilifu vinavyozalishwa nchini na vinavyoingizwa kutoka nje ya nchi.

112. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2024 zabuni ya ununuzi wa lita 108,020 za viuatilifu imetangazwa kwa ajili ya udhibiti wa visumbufu vya nzige (lita 4,000), kweleakwelea (lita 12,000), viwavijeshi (lita 90,000) na nzi wa matunda (lita 2,020). Aidha, kupitia Bodi ya Pamba Tanzania kwa kushirikiana na Vyama Vikuu vya Ushirika imeratibu ununuzi wa viuatilifu vya pamba chupa/ekapaki 16,500,000 vyenye thamani ya Shilingi Bilioni 82 na kusambazwa kwa wakulima.

113. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia TPHPA kwa kushirikiana na Shirika la kudhibiti Nzige wa Jangwani (DLCO – EA) imedhibiti malalo na mazalia ya kwelea kwelea katika Halmashauri za Kibaha, Chalinze, Babati, Mlimba, Kondoa, Kongwa, Mbarali na Chamwino na kuokoa tani 42.35 za mazao ya mtama, mpunga na alizeti katika eneo lenye jumla ya hekta 809. Vilevile, TPHPA kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Udhibiti wa Nzige Wekundu (International Red locust Control Organisation for Central and Southern Africa – IRCO - CSA) imedhibiti nzige katika bonde la mto Malagarasi katika eneo lenye ukubwa wa hekta 1,800.

114. Vilevile, imedhibiti nzige (tree locust) kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta 1,248 katika Wilaya ya Mpwapwa. Kadhalika, TPHPA imedhibiti milipuko ya viwavijeshi vamizi katika eneo la uzalishaji lenye ukubwa wa hekta 24,600 katika Halmashauri za Arusha, Mbogwe, Makete, Kilindi, Kondoa, Kongwa, Lushoto, Liwale, Mpwapwa, Ludewa, Ruangwa, Babati mji, Mbulu, Njombe, Singida, Nkasi, Mpanda, Kilosa, Chamwino, Madaba, Kyela, Meru na Iramba. Aidha, TPHPA imedhibiti milipuko ya panya katika mikoa ya Morogoro, Pwani, Tanga, Dodoma, Mtwara, Lindi, Manyara, Kigoma na Arusha katika kaya 602,644 na kuokoa hekta 97,217 za mazao ya wakulima.

115. Kadhalika, kupitia Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushirikiana na Vyama Vikuu vya Ushirika, Serikali imeratibu ununuzi wa viuatilifu lita 2,679,520 na salfa tani 65,539.6 vyenye thamani ya Shilingi Bilioni 189 na kusambazwa kwa wakulima. Pia, kupitia Bodi ya Tumbaku Tanzania na Vyama Vikuu vya Ushirika imeratibu ununuzi wa viuatilifu vya zao la tumbaku Deltamethrin chupa 3,490,050, Imidacloprid pakti 1,661,929 na Flumetralin lita 166,193 zenye thamani ya Shilingi 27,630,472,800.

116. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mradi wa Kuimarisha Huduma za Afya ya Mimea na kuhakikisha Usalama wa Chakula nchini Tanzania (Strengthening Plant Health Services in Tanzania for Enhanced Food Safety - STREPHIT) imewezesha upatikanaji wa magari nane (8), pikipiki 19, vishikwambi 41, kompyuta za mezani 34 na majokofu 17 kwa ajili ya kuimarisha ukaguzi na udhibiti wa visumbufu vya mimea na mazao.

117. Vilevile, kwa kushirikiana na wadau wa kilimo imenunua ndege nyuki 63 kwa ajili ya kuimarisha ukaguzi na udhibiti wa visumbufu vya mazao nchini. Ndege nyuki hizo zikijumuishwa na zilizonunuliwa na Bodi ya Pamba Tanzania na TPHPA kwa mwaka 2022/2023 zinafikia jumla ya ndege nyuki 103. Aidha, awamu ya kwanza ya ununuzi wa ndege maalum kwa ajili ya udhibiti wa milipuko ya visumbufu vya mimea na mazao imefikia hatua ya kuwapata watengenezaji wa ndege hiyo na mkataba wa ununuzi umefikia hatua ya upekuzi.

**4.1.6 Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Umwagiliaji**

118. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya Shilingi Bilioni 361.5 zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi 780 ya umwagiliaji ambapo miradi hiyo ilikuwa ni kukamilisha miradi 133 iliyoanza mwaka 2022/2023 na kuanza utekelezaji wa miradi 647 iliyopangwa katika mwaka 2023/2024. Kati ya miradi 133 iliyoanza mwaka 2022/2023, 69 ni miradi ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji inayohusisha skimu mpya (25), ukarabati wa skimu (30) zenye jumla ya hekta 95,005 na ujenzi wa mabwawa (14) yenye mita za ujazo 131,535,000. Aidha, miradi 64 ni ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa skimu 42 na mabonde ya kimkakati 22.

119. ***Mheshimiwa Spika***, Aidha, katika mwaka 2023/2024, Tume ilipanga kuanza utekelezaji wa miradi 647 inayohusisha:-

a) Ujenzi na ukarabati wa skimu 46 (skimu mpya 28 - hekta 69,505 na kukarabati skimu 18 - hekta 40,497) zenye jumla ya hekta 110,002;
b) Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mabonde ya kimkakati;
c) Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina pamoja na kuanza ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba makubwa ya pamoja sita (6) yenye jumla ya hekta 79,518.46 kupitia

programu ya BBT katika mikoa ya Kigoma, Mbeya, Kagera, Njombe, Singida na Dodoma;

d) Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa skimu mpya 240;
e) Mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu wa skimu 255 za kukarabati zenye ukubwa wa hekta 290,095; na
f) Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mabwawa mapya 100 pamoja na kuanza ujenzi wa mabwawa hayo yenye takribani mita za ujazo 936,535,700.



***Picha Na.7:*** *Ujenzi wa tuta la bwawa katika Mradi wa Umwagiliaji - Membe Dodoma*

120. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili, 2024 jumla ya miradi 231 kati 780 iliyopangwa kwa mwaka 2022/2023 na 2023/2024 imeendelea kutekelezwa. Kwa miradi iliyoanza 2022/2023, miradi 20 kati ya 25 ya ujenzi wa skimu mpya utekelezaji wake umefikia wastani wa asilimia 40; miradi 29 kati ya 30 ya ukarabati wa skimu za umwagiliaji utekelezaji wake umefikia wastani wa asilimia 35; na ujenzi wa mabwawa 14 ya umwagiliaji unaendelea ambapo utekelezaji wake umefikia wastani wa asilimia 50. Utekelezaji wa miradi ni kama unavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 1, 2 na 3.**

121. Vilevile, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa miundombinu ya umwagiliaji katika mabonde matano (5) kati ya 22 umekamilika sawa na asilimia 23 ya lengo. Mabonde hayo ni Mkomazi (hekta 3,140), Kasinde (hekta 15,000), Umba (hekta 5,560),

Mtambo (hekta 7,000) na Lukuledi (4,680). Aidha, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika mabonde 17 ya kimkakati yaliyobaki unaendelea kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 4.**

122. Kadhalika, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa skimu 15 kati ya skimu 42 zilizopangwa sawa na asilimia 33 umekamilika. Skimu hizo ni Legeza mwendo (Kalambo-hekta 5,500), Kisese (Kondoa-hekta 3,000), Nyamgongwa (Geita-hekta 2,000), Nyanzwa (Kilolo-hekta 9,000), Igaka-Bundala (Sengerema-hekta 3,000), Mgambalenga (Kilolo-hekta 3,000), Mangalali (Iringa-hekta 750), Luganga/ Magozi/Mkombilenga (Iringa-hekta 2,500), Lipuli (Iringa -hekta 560), Rudewa (Kilosa -hekta 1,000), Itipingi (Njombe -hekta 162), Arusha Chini (Nanyamba -hekta 120), YongomaNdungu (Same-hekta 2,000) na Tyme Masagi (hekta 2,100). Aidha, upembuzi yakinifu na usanifu katika skimu 28 zilizobaki unaendelea kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 5.**

123. ***Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa miradi iliyopangwa katika mwaka 2023/2024 ni kama ifuatavyo :-

i. Ujenzi wa skimu mpya tisa (9) kati ya skimu 28 zilizopangwa umeanza sawa asilimia 32.1 ya lengo. Skimu hizo ni Nanganga (Ruangwa), Rutamba (Lindi), Itipingi (Njombe), Nambalapi (Ruvuma), Mgambalenga (Iringa), Lwafi Katongolo (Nkasi), Msange (Singida), Narunyu (Lindi). Aidha, skimu 19 zipo katika hatua mbalimbali za manunuzi kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 6.**

ii. Ukarabati wa skimu tatu (3) za Ndungu (Same), Naming'ong'o (Momba) na Kihurio (Same) kati ya skimu 18 zilizopangwa sawa na asilimia 16.6 ya lengo umeanza kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 7**;

iii. Wakandarasi sita (6) kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya skimu 10 katika mabonde mawili (2) ya kimkakati wamepatikana. Skimu hizo ni Mapalagwe (hekta 1,200), Ndanda (hekta 650), Nanganga (hekta 1,000), Narunyu (hekta 3,499), Kinyope (hekta 200), Rutamba (hekta 300), Chekelei (hekta 2,000), Mtambo (hekta 2,000);

iv. Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya pamoja matatu (3) kati ya sita (6) unaendelea; na

v. Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mabwawa 18 umekamilika, 19 unaendelea na 63 upo katika hatua za kusaini mikataba kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 8**;

vi. Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa skimu mpya 14 zenye jumla ya hekta 14,310 kati ya skimu 240 zilizopangwa umekamilika. Aidha, skimu 226 zilizobaki zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 9**; na

vii. Mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati wa skimu 13 zenye jumla ya hekta 21,150 kati ya skimu 255 yamekamilika. Aidha, skimu 242 zilizobaki zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na.10**.

124. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha Vyama vya Umwagiliaji Tume ilipanga kutoa mafunzo kwa Vyama vya Umwagiliaji 430 vilivyosajiliwa ili kusimamia uendeshaji na matunzo ya skimu za umwagiliaji; kuanzisha na kusajili Vyama vya Umwagiliaji 200; na kuwezesha matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa usajili na ukusanyaji wa ada ya huduma za umwagiliaji katika skimu.

125. ***Mheshimiwa Spika***, hadi Aprili, 2024 yafuatayo yametekelezwa :-

i. Kusajiliwa kwa vyama vipya vya umwagiliaji 244 na hivyo kufanya vyama vilivyosajiliwa kufikia 730. Hatua hiyo inawezesha kuvitambua vyama hivyo, kurahisisha utoaji wa huduma za umwagiliaji na kuimarisha ukusanyaji wa ada ya huduma za umwagiliaji;
ii. Kutoa mafunzo ya ukusanyaji wa ada za umwagiliaji kwa vyama 333 katika mikoa 25; na
iii. Kukamilika kwa ujenzi wa mfumo wa kielektroniki wa usajili na ukusanyaji wa ada ya huduma za umwagiliaji (NIRC iMIS) ambao unapatikana kupitia kiunganishi cha *https://imis.nirc.go.tz*.

Mfumo huo utawezesha upatikanaji wa taarifa sahihi za wakulima katika skimu za umwagiliaji na ukusanyaji wa ada ya huduma za umwagiliaji.

126. ***Mheshimiwa Spika***, Tume ilipanga kununua magari kwa ajili ya ofisi za za umwagiliaji za wilaya, kukamilisha usanifu wa ofisi 25 za mikoa na kuendelea kujenga ofisi za Tume Makao Makuu. Hadi Aprili, 2024 Tume imetekeleza yafuatayo :-

i. Imenunua magari 21 na hivyo kufanya Tume kuwa na jumla ya magari 48 yaliyonunuliwa na taratibu za manunuzi ya magari mengine 12 na pikipiki 23 zinakamilishwa;
ii. Imekamilisha usanifu kwa ajili ya ujenzi wa ofisi 25 za umwagiliaji za mikoa na taratibu za manunuzi kwa ajili ya kuwapata wakandarasi wa kujenga ofisi hizo zinaendelea; na
iii. Ujenzi wa jengo la ofisi ya makao makuu iliyopo Njedengwa (Dodoma) unaendelea na umefikia asilimia 50.

**4.1.7 Uanzishwaji wa vituo jumuishi vya kutoa huduma za zana za kilimo (Mechanization Centres)**

127. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya Shilingi Bilioni moja (1) zilitengwa kwa ajili kuanzisha vituo vitatu (3) vya kutoa huduma jumuishi za zana za kilimo katika mashamba makubwa ya pamoja na kujenga karakana tatu (3) kwa ajili ya kuhifadhi na kuhudumia zana za kilimo katika mashamba hayo.

128. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili, 2024 Wizara kwa kushirikiana na Kampuni za TATA Holding Ltd na John Deere imeanza ujenzi wa kituo kimoja cha kutoa huduma ya zana za kilimo kwa wakulima kilichopo eneo la Mtanana katika Wilaya ya Kongwa ambapo ujenzi umefikia asilimia 90; na imeanzisha vituo vya kutoa huduma ya zana za kilimo kwenye mashamba ya BBT ya Mlazo/Ndogowe na Chinangali II ambapo taratibu za manunuzi zinaendelea.

129. Vilevile, Wizara inaendelea na taratibu za ujenzi wa Vituo jumuishi vya zana za kilimo (mechanization centres) vitano (5) katika Halmashauri za Chamwino, Madaba, Songea, Itilima,

Mbarali na Korogwe ambapo wakandarasi wamepatikana kwa ajili ya kuanza ujenzi.

130. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na uhamasishaji wa matumizi ya zana bora na za kisasa za kilimo, katika mwaka 2023/2024, Sekta binafsi imeingiza nchini jumla ya matrekta makubwa 2,783 na matrekta madogo 4,254 kwa ajili ya kilimo na kufanya idadi ya matrekta makubwa kuongezeka kutoka 22,849 mwaka 2022/2023 hadi 25,632 mwaka 2023/2024 na matrekta madogo kuongezeka kutoka 11,379 mwaka 2022/2023 hadi 15,633 mwaka 2023/2024.

131. Vilevile, kwa kushirikiana na Chama cha Wachambuaji wa Pamba (Tanzania Ginners Association - TGA) jumla ya matrekta 200 yamenunuliwa na kusambazwa katika Kata 40 zinazozalisha pamba kwa wingi katika mikoa ya Simiyu, Tabora, Shinyanga, Mara, Katavi, Mwanza na Kigoma. Kati ya hayo, 100 yamenunuliwa na TGA na 100 na yamenunuliwa na Bodi ya Pamba. Mashine na zana za kilimo nyingine zilizoingizwa nchini ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na.9**.

**Jedwali Na. 9:** Mashine na zana za kilimo nyingine zilizoingizwa nchini 2023/2024

| Na. | Mashine na Zana | Idadi |
|---|---|---|
| 1. | Mashine za kuvuna | 114 |
| 2. | Plau za matrekta | 1,506 |
| 3. | Haro za matrekta | 391 |
| 4. | Mashine za kupura | 122,826 |
| 5. | Zana za kupandia | 17,193 |
| 6. | Majembe ya kukokotwa na wanyamakazi | 1,082,517 |

**Chanzo:** *TRA, 2023*

**Uendelezaji wa Mazao ya Kimkakati Zao la Mkonge**

132. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha uzalishaji wa zao la mkonge, Wizara kupitia Bodi ya Mkonge Tanzania kwa kushirikiana na TARI imezalisha miche 2,413,227 ya mkonge kwa ajili ya kusambaza kwa wakulima; imetoa mafunzo ya kilimo bora cha mkonge na ubora wa singa kwa Maafisa Ugani 100 na wakulima 20,215 katika mikoa ya Tanga, Morogoro, Kilimanjaro, Mbeya, Njombe na Tabora; na imetoa mafunzo kwa watafiti/wataalam 20

wa maabara ya udongo. Aidha, wakulima 1,350 kutoka AMCOS za Magunga, Mwelya, Ngombezi, Magoma na Hale wameunganishwa na soko la ndani la mkonge. Vilevile, Bodi imeagiza korona mbili (2) kati ya lengo la kununua korona tano (5) kwa ajili ya viwanda vya kuchakata mkonge.

**Zao la Chai**

133. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Chai Tanzania imeendelea kuimarisha uzalishaji wa zao la chai ambapo miche bora 3,500,000 ya chai imezalishwa na kusambazwa kwa wakulima. Aidha, Bodi kwa kushirikiana na wabia wa maendeleo wameanzisha kiwanda kidogo cha chai Sakare katika Wilaya ya Korogwe chenye uwezo wa kusindika chai kilo 200 kwa siku kwa ajili ya uongezaji thamani wa zao la chai kwa wakulima wadogo; kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imekamilisha utafiti na kuandaa ramani ya maeneo yanayofaa kwa kilimo cha chai kwa njia ya umwagiliaji katika Mkoa wa Njombe; imefufua mashamba ya chai yenye ukubwa wa hekta 150 katika Wilaya ya Kilolo na ufufuaji unaendelea katika mashamba mengine.

134. Kadhalika, mnada wa chai Tanzania umeanzishwa ambapo katika mnada wa kwanza uliofanyika tarehe 13 Novemba, 2023 kilo 31,294 ziliuzwa kwa bei ya wastani wa Dola za Marekani 0.77 kwa kilo. Pia, Bodi inaratibu uanzishwaji wa viwanda viwili (2) vya kuchakata chai kwa ajili ya wakulima wadogo wa Wilaya za Kilolo na Tarime ambapo utaratibu wa kumpata mkandarasi na manunuzi ya mitambo ya kuchakata majani mabichi ya chai unaendelea. Viwanda hivyo vitakuwa na uwezo wa kusindika tani 4 za majani mabichi ya chai kwa siku.

**Zao la Pareto**

135. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Pareto Tanzania kwa kushirikiana na TARI imezalisha na kusambaza tani 1.4 za mbegu bora za pareto kwa wakulima. Aidha, TARI imezalisha miche 770,000 ya pareto itakayozalisha tani 1.5 za mbegu zitakazosambazwa kwa wakulima na uzalishaji unaendelea. Pia, mafunzo ya kilimo bora cha zao la pareto yametolewa kwa wakulima 5,600 na Maafisa Ugani 16 kutoka katika Halmashauri 16 zinazozalisha zao la pareto.

**Zao la Tumbaku**

136. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha uzalishaji wa zao la tumbaku, Wizara kupitia Bodi ya Tumbaku Tanzania imesimamia utiaji saini wa mikataba ya uzalishaji baina ya wanunuzi na wakulima ambapo mikataba ya kuzalisha tani 226,258 imesainiwa msimu wa kilimo 2023/2024. Aidha, Kampuni za ununuzi wa tumbaku zimeongezeka kutoka kampuni tatu (3) msimu wa 2019/2020 hadi kampuni 12 msimu wa 2022/2023 na hivyo kuongeza ushindani. Hatua hiyo, imewezesha kuongezeka kwa bei ya tumbaku kutoka wastani wa Shilingi 3,255 kwa kilo msimu wa 2019/2020 hadi Shilingi 5,825 kwa kilo msimu wa 2022/2023.

**Zao la Pamba**

137. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Pamba Tanzania imeendelea kuimarisha uzalishaji wa zao la pamba kwa kusambaza tani 24,318 za mbegu za pamba sawa na asilimia 110 ya lengo la kusambaza tani 22,146 kwa wakulima katika mikoa yote inayolima pamba. Vilevile, chupa/ekapaki 16,500,000 zimenunuliwa kati ya hizo chupa 7,000,000 zimesambazwa kwa wakulima na usambazaji unaendelea. Vilevile, wataalam 230 wa kilimo wameajiriwa katika Kata hizo ili kutoa elimu ya kanuni za kilimo bora cha pamba kwa wakulima. Aidha, kilimo cha pamba katika maeneo hayo kitafanyika kwa utaratibu wa kilimo cha mkataba. Pia, ununuzi wa mitambo ya kuchimba mabwawa kwa ajili ya umwagiliaji upo katika hatua ya tathmini ya zabuni. Mitambo hiyo ni *buldozer* moja (1), *excavator* moja (1), *whell loder* moja (1) na *motor grader* moja (1).



***Picha Na.8:*** *Mhe. David E. Silinde (Mb), Naibu Waziri wa Kilimo akikagua maendeleo ya zao la pamba – Bariadi katika Mkoa wa Simiyu*

**Zao la Kahawa**

138. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Kahawa Tanzania imeendelea kuimarisha uzalishaji wa zao la kahawa kwa kuratibu uzalishaji na usambazaji wa miche bora ya kahawa 21,899,560 kwa wakulima. Vilevile, Bodi imeanzisha mashamba ya mfano ya kahawa 18 katika Mikoa ya Ruvuma, Mbeya, Songwe, Kagera na Kilimanjaro kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa vitendo kwa wakulima wa zao la kahawa. Aidha, Bodi imewezesha ukarabati wa miti ya kahawa kwenye mashamba 86 katika mikoa ya Kagera, Kilimanjaro, Ruvuma na Songwe; na kutoa mafunzo kuhusu kilimo bora cha kahawa, ubora na masoko kwa vyama vya ushirika 65 katika maeneo ya uzalishaji.

139. Vilevile, Wizara kupitia Bodi imekamilisha upimaji wa maji chini ya ardhi na miamba (Hydrological Survey and Geophysical Survey) kwa ajili ya uchimbaji wa visima vya kuwawezesha wakulima kumwagilia mashamba ya kahawa katika Wilaya ya Mbozi. Kadhalika, Bodi imeendelea kuimarisha upatikanaji wa masoko ya kahawa kwa kupitia ushiriki wa maonesho ya kimataifa ya kahawa Japan (SCAJ) na Adis Ababa Ethiopia (AFCA) ambapo soko la Japan limepatikana na tani 11,602.72 za kahawa zimeuzwa katika soko hilo.

**Zao la Korosho**

140. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha uzalishaji wa zao la korosho, Wizara kupitia Bodi ya Korosho Tanzania imetoa mafunzo

kuhusu udhibiti ubora wa korosho ghafi kwa viongozi wa vyama vya msingi 483 na viongozi 225 kutoka katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Morogoro na Tanga. Vilevile, Bodi imeanzisha mashamba darasa ya kilimo cha korosho 30 kwa ajili ya kutoa mafunzo ya kilimo bora cha korosho kwa vitendo kwa wakulima. Aidha, ili kuimarisha ubora wa korosho zinazozalishwa na wakulima katika Wilaya ya Manyoni na kusogeza huduma za ugani karibu na wakulima, Bodi imekamilisha ujenzi wa ghala lenye uwezo wa kuhifadhi tani 3,000 za korosho na nyumba mbili (2) za watumishi. Kadhalika, ujenzi wa ofisi za Bodi na ofisi za wasimamizi wa mashamba ya pamoja ya korosho katika Wilaya ya Manyoni umefikia wastani wa asilimia 95.

**Zao la kakao**

141. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa kushirikiana na Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (Warehouse Receipts Regulatory Board - WRRB), Soko la bidhaa Tanzania (Tanzania Mercantile Exchange - TMX), COPRA na wadau imeendelea kuratibu na kusimamia mfumo wa ukusanyaji na ununuzi wa kakao kupitia vyama vya ushirika katika mikoa ya Mbeya na Morogoro. Hadi Aprili 2024, tani 11,499.4 za kakao zenye thamani ya Shilingi 129,085,758,200 zimekusanywa na kuuzwa ikilinganishwa na tani 8,868.51 zenye thamani ya Shilingi 37,919,884,675 zilizouzwa mwaka 2022/2023. Aidha, bei ya kakao imeendelea kuongezeka kutoka wastani wa Shilingi 7,000 kwa kilo msimu wa 2022/2023 hadi wastani wa Shilingi 29,000 kwa kilo msimu wa 2023/2024.

**a) Mazao ya Mafuta Zao la Ufuta**

142. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha uzalishaji wa zao la ufuta kwa kusambaza mbegu bora za ufuta tani 24 kwa wakulima katika mikoa ya Lindi (tani 10), Mtwara (tani 10), Ruvuma (tani 2) na Pwani (tani 2). Vilevile, Wizara kupitia TARI imezalisha mbegu za msingi za ufuta tani 0.3 ambazo zitatumika kuzalisha tani 60 za mbegu zilizothibitishwa. Aidha, mafunzo ya kilimo bora cha zao la ufuta kwa wakulima 65 na Maafisa Ugani 62 yametolewa kwa wakulima katika mkoa wa Mtwara.

**Zao la Karanga**
143. ***Mheshimiwa Spika*** Wizara katika mwaka 2023/2034 kupitia TARI imetoa mafunzo kuhusu kilimo bora cha karanga kwa Maafisa Ugani 175 na wakulima 640 kupitia mashamba ya mfano 124 katika mikoa ya Tabora, Katavi, Shinyanga, Tanga, Kigoma, Simiyu, Mwanza, Geita na Mara. Aidha, katika kuimarisha utafiti wa mbegu bora za karanga, TARI imeandaa ekari 50 kwa ajili ya kuzalisha mbegu za msingi katika kituo cha TARI Naliendele na vituo vidogo vya Suluti na Nachingwea.

**b) Mazao ya Bustani**
**Zao la Parachichi**
144. ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa zao la parachichi zinazouzwa nje ya nchi (exportable varieties) umeongezeka kutoka tani 17,711.49 mwaka 2021/2022 hadi tani 26,826.3 mwaka 2022/2023. Ongezeko hilo limetokana na kuimarika kwa soko la ndani na nje ya nchi. Vilevile, katika kuimarisha utafiti wa mbegu bora za parachichi, TARI imekusanya vinasaba vya aina 13 za parachichi ambazo ni Hass, Fuerte, Weisal, Ikulu, Booth 7, Mwaikokesya, Uyole line 1, Uyole line 2, Choquate, Pinkerton, Nabal, Simmonds na Duke na kuvihifadhi kwenye benki ya vinasaba katika kituo cha TARI Uyole.

145. Vilevile, aina saba (7) za vinasaba vimepelekwa katika mikoa ya Rukwa, Mbeya, Songwe, Arusha, Kilimanjaro, Iringa, Ruvuma, Morogoro, Dodoma na Pwani kwa ajili ya kufanya majaribio ya maeneo ambayo yanaweza kustawi na kuzaa vizuri ambapo Booth 7 imeonekana kufanya vizuri katika maeneo yenye joto na Uyole line 1, Uyole line 2 zinafanya vizuri katika maeneo ya baridi na joto.

**Zao la Zabibu**
146. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha uzalishaji wa zao la zabibu ambapo katika mwaka 2023/2024 mafunzo ya kanuni bora za kilimo cha zabibu, teknolojia za kuchakata na kusindika zabibu kwa wakulima 687 na Maafisa Ugani 10 katika Mkoa wa Dodoma yametolewa. Kadhalika, nakala 400 za vipeperushi vya kanuni za kilimo bora cha zabibu pamoja na nakala 200 za Mwongozo wa Kilimo Bora cha zabibu zimeandaliwa na kusambazwa kwa wadau wa zao hilo. Aidha, TARI imeendelea

kukusanya vinasaba vya zao la zabibu kwa ajili ya utafiti ambapo vinasaba vya zao hilo vimeongezeka kutoka aina 26 hadi 36.

**Zao la Ndizi**

146. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha uzalishaji wa zao la ndizi, Wizara imetoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha migomba kwa wakulima 5,000 na Maafisa Ugani 46 katika Mkoa wa Kagera. Pia, katika kuweka mazingira wezeshi ya uuzaji wa ndizi, Wizara imekamilisha usanifu wa ujenzi katika kituo cha kuuzia ndizi Mamsera (Rombo) na taratibu za usanifu na ujenzi wa vituo vingine zinaendelea.

**c) Mazao yenye utegemezi kutoka nje ya nchi**

148. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara katika mwaka 2023/2024 ilipanga kuzalisha tani 445,000 za sukari; kukamilisha upembuzi yakinifu wa mabwawa ya Mandela na Wembele; kuongeza upatikanaji wa mbegu bora za miwa kwa kuanzisha kitalu cha hekta 400 katika bonde la Kilombero; kusambaza tani 5,000 za mbegu za alizeti kwa mpango wa ruzuku zenye uwezo wa kuzalisha takribani tani 1,000,000 za alizeti; kuzalisha mbegu za awali za alizeti tani 186 zenye uwezo wa kuzalisha mbegu zilizothibitishwa tani 7,440; kuzalisha mbegu za awali za ngano tani 2,500; kuongeza uzalishaji wa ngano kufikia tani 150,000; na kutambua na kupima maeneo yote yanayofaa kwa kilimo cha ngano nchini.

149. ***Mheshimiwa Spika***, ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi Aprili, 2024 utekelezaji umefikia hatua zifuatazo:-

**Zao la Miwa na Uzalishaji wa sukari**

150. ***Mheshimiwa Spika***, uzalishaji wa miwa umefikia tani 4,215,555.27 ambazo zimezalisha sukari tani 392,724 sawa na asilimia 88.25 ya lengo. Vilevile, Bodi ya Sukari kwa kushirikiana na Halmashauri imetambua maeneo yanayofaa kuwekeza katika miradi mipya ya sukari ambapo baadhi ya maeneo hayo ni Rufiji - Mkoa wa Pwani na Kasulu- Kigoma ambayo yamepata wawekezaji ambao wapo katika hatua mbalimbali za kuanza utekelezaji wa miradi ya sukari.

151. Kadhalika, kitalu cha uzalishaji wa mbegu za miwa (ekari 8) ambazo zitasambazwa kwa wakulima kimeanzishwa katika Bonde

la Turiani- Mtibwa - Morogoro. Aidha, Bodi imeingia makubaliano na Shirika la uzalishaji mali la Magereza kuanzisha kitalu cha mbegu chenye ukubwa wa hekta 400 kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa mbegu kwa wakulima wadogo wa Kilombero.

152. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuongeza tija na uzalishaji wa miwa, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa ya umwagiliaji (Mandela na Wembele) umefikia wastani wa asilimia 50 na upembuzi yakinifu kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji katika zao la miwa kwa wakulima wadogo wa Kilombero umefikia asilimia 25.

153. Vilevile, ili kudhibiti wadudu waharibifu wa miwa na magonjwa jumla ya hekta 800 za mashamba ya miwa zimekaguliwa na kudhibiti visumbufu vya miwa katika mashamba hayo. Aidha, ili kuwatambua na kutambua uzalishaji wa wakulima wadogo wa miwa, Bodi imewasajili kwenye mfumo wakulima 1,501 katika maeneo ya uzalishaji wa miwa. Pia, wakulima 7,807 katika mikoa ya Pwani, Morogoro, Kagera, Manyara na Kilimanjaro wamepatiwa mafunzo kuhusu afya ya udongo na udhibiti wa visumbufu vya zao la miwa.

**Upatikanaji wa Sukari nchini**

154. ***Mheshimiwa Spika***, wakati wa utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2023/2024 Serikali ilikabiliwa na tatizo la upungufu wa sukari ambao ulitokana na mvua za EL-Nino na tabia za wafanyabiashara kutengeneza uhaba wa sukari (*artificial scarcity*) kwa kutokuingiza sukari ya kuziba pengo (gap sugar) kulingana na vibali vya uagizaji walivyopatiwa na hivyo kupandisha bei ya sukari. Aidha, kiasi cha sukari walichoingiza nchini hawakukisambaza kama ilivyokusudiwa ili kutatua changamoto ya upatikanaji wa sukari.

155. ***Mheshimiwa Spika,*** hali hiyo ilisababisha kupanda kwa bei ambapo hadi tarehe 22 Januari, 2024 wastani wa bei ya jumla kwa wazalishaji wakubwa nchini ilikuwa ni kati ya Shilingi 3,800 na 4,000, wauzaji wa jumla kati ya Shilingi 4,500 na 5,000 na bei ya rejareja kati ya Shilingi 6,000 na 10,000 kwa kilo moja katika maeneo mengi, hali ambayo ilikuwa inahatarisha usalama wa nchi na uchumi wetu.

156. ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na changamoto hiyo, Wizara ilichukua hatua zifuatazo:-

i. Kutangaza bei elekezi ya sukari nchi nzima kupitia Gazeti la Serikali Na. 3. Toleo la 105 la tarehe 23 Januari, 2024. Bei elekezi iliyotangazwa ni kati ya Shilingi 2,600 na 2,900 kwa jumla na kati ya Shilingi 2,700 na 3,200 kwa rejareja;
ii. Kupitia NFRA ilitoa idhini ya uingizaji wa sukari tani 410,000 ambapo uingizaji wa sukari umeanza Januari 2024 na utakamilika ifikapo Desemba, 2024. Uingizaji wa sukari hiyo utaratibiwa na Serikali kwa kuzingatia ugavi na mahitaji na uwezo wa viwanda vya sukari kurudi katika uzalishaji;
iii. Kufanya marekebisho ya kanuni ya NFRA na kuiweka sukari kuwa sehemu ya usalama wa chakula;
iv. Kuanza marekebisho ya Sheria ya Sukari Na.6 ya mwaka 2001 kwenye sheria ya fedha ya mwaka 2024 ili kuiwezesha NFRA kununua sukari na kuhifadhi sukari kwenye hifadhi ya chakula ya Taifa kunusuru hali ya upatikanaji wa sukari inapotokea tatizo la aina yoyote. Hatua hiyo inalenga kuondoa uhodhi kwa baadhi ya wenye viwanda bila kuathiri dhamira ya Serikali ya kulinda viwanda vya ndani.

   ***"Serikali itaendelea kuvilinda viwanda vya ndani na kuwalinda wakulima wa miwa lakini ulinzi huo hautakuwa kwa gharama ya kuwatesa Watanzania milioni 61.7"***

   ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Bunge lako Tukufu ninaomba niwaambie wamiliki wa viwanda vya sukari nchini kuwa sukari ni chakula cha watanzania masikini na ni suala la usalama wa nchi, hivyo ***"Serikali haitavumilia wala haitaruhusu tena tatizo lililotokea kujirudia, ni wajibu wetu kuvilinda viwanda vya ndani lakini ni wajibu wetu pia kuwalinda watanzania na usalama wa nchi"***

157. ***Mheshimiwa Spika***, kupitia Bunge lako Tukufu ninawaambia wenye viwanda wafanye mabadiliko ya chama chao cha wazalishaji (Tanzania Sugar Producers Associations) ili kuhakikisha umoja huo unakuwa na uwakilishi wa wazalishaji wakubwa na wadogo kama ambavyo Serikali inawaelekeza.

**Zao la Alizeti**
158. ***Mheshimiwa Spika***, uzalishaji wa alizeti katika msimu wa 2022/2023 umefikia tani 1,132,298.34 ikilinganishwa na tani 425,653.10 msimu wa 2021/2022 sawa na ongezeko la asilimia 166. Ongezeko hilo limetokana na upatikanaji na matumizi ya pembejeo za kilimo hususan mbegu bora na mbolea. Aidha, Wizara imetoa mafunzo kuhusu mbinu za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ikiwemo, utunzaji wa unyevu mashambani, afya ya udongo na matumizi ya mbolea na kanuni za uzalishaji wa mbegu bora za alizeti kwa Maafisa Ugani 20, wakulima 826 na Kampuni za kitanzania 22 zinazozalisha mbegu za alizeti.

159. Kadhalika, mbegu bora za alizeti tani 1,974.4 zimepatikana ambapo hadi Aprili 2024, tani 725 za mbegu zimesambazwa kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku katika mikoa ya Singida, Dodoma, Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Ruvuma, Rukwa, Katavi na Geita. Aidha, Wizara kupitia TARI, imezalisha mbegu za awali za alizeti tani 81.8 zenye uwezo wa kuzalisha mbegu zilizothibitishwa tani 8,180; na imekusanya aina 13 za mbegu za alizeti kutoka kwa wakulima ambapo jumla ya vinasaba 52 vimeendelea kutunzwa kwa ajili ya utafiti.

**Zao la Ngano**
160. ***Mheshimiwa Spika***, uzalishaji wa ngano katika msimu wa 2022/2023 umefikia tani 86,522 sawa na asilimia 57.68 ya lengo. Vilevile, tani 1,616 za mbegu bora za ngano zimepatikana ambapo kati ya hizo tani 1,015 zimesambazwa kwa mpango wa ruzuku na usambazaji unaendelea katika mikoa ya Njombe, Rukwa, Mbeya, Manyara, Arusha na Kilimanjaro. Aidha, Wizara kupitia TARI imezalisha mbegu za msingi za ngano tani 205.2 zenye uwezo wa kuzalisha tani 4,275.22 za mbegu zilizothibitishwa.

**4.2 Kuongeza Ajira zenye Staha na Ushiriki wa Vijana na Wanawake kwenye Kilimo**
161. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ilipanga kutengeneza ajira 428,571 kwa mwaka 2023/2024 kupitia mipango na mikakati mbalimbali ikiwemo Programu ya Jenga Kesho iliyo Bora (BBT). Ili kufikia malengo hayo, Wizara imeendelea kutekeleza Programu ya Jenga Kesho iliyo Bora kwa vijana na wanawake yenye malengo ya

kuongeza ajira zenye staha, kuongeza tija, kubakiza wakulima katika sekta (retention of farmers) na kupunguza umaskini.

162. ***Mheshimiwa Spika***, ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi Aprili, 2024 ajira 475,025 zimezalishwa katika Sekta ya kilimo sawa na asilimia 110 ya lengo la kuzalisha ajira 428,571 kwa mwaka 2023/2024. Baadhi ya miradi na Programu iliyotekelezwa ni Programu ya Jenga Kesho iliyo Bora kwa vijana na wanawake, miradi ya umwagiliaji na miundombinu ya uhifadhi na masoko.

163. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024 Serikali katika Bunge lako Tukufu iliahidi uanzishwaji wa Programu ya BBT ikiwa na malengo manne (4) ambayo ni kuongeza ajira, mitaji, teknolojia na umilikishaji wa ardhi. Program hiyo imetekelezwa kupitia miradi minne (4) ambayo ni mashamba makubwa ya pamoja (Block Farms), utoaji wa mikopo yenye riba nafuu (4.5%) - BBT Financing; visima kwa wakulima wadogo (boreholes) na BBT – Ugani.

164. ***Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa baadhi ya miradi na programu ni kupitia mikakati ifuatayo;

**4.2.1 Kuwezesha upatikanaji wa ardhi ya kilimo na uanzishaji wa mashamba makubwa ya pamoja**

165. ***Mheshimiwa Spika***, jumla ya Shilingi Bilioni 10.5 zilitengwa kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa ardhi ya kilimo na uanzishaji wa mashamba makubwa ya pamoja kwa lengo la kuwezesha upatikanaji wa ajira na kuwabakiza wakulima katika Sekta ya kilimo hususan vijana na wanawake.

166. Mheshimiwa Rais alipozindua program ya BBT Machi 2023, ardhi kwa ajili ya program hiyo ilikuwa na ukubwa wa ekari 300. Ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili, 2024 jumla ya ekari 340,465.28 zimepatikana kwa ajili ya program ya BBT katika mikoa ya Dodoma, Kigoma, Mbeya, Singida, Pwani, Tanga, Njombe na Kagera. Aidha, mashamba matatu (3) ya Chinangali II – Chamwino (ekari 1,772), Ndogowe – Chamwino (ekari 11,430) na Mapogoro – Chunya (ekari 52,000) yameanza kuendelezwa na tathmini ya athari za mazingira na kijamii imefanyika na kupatiwa cheti cha EIA kutoka NEMC.

### 4.2.2 Kuimarisha Ushiriki wa Vijana na Wanawake katika Kilimo kupitia Program ya Jenga Kesho Iliyo Bora

167. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha ushiriki wa vijana na wanawake kwenye kilimo, Wizara imetoa mafunzo kuhusu kilimo biashara na kuwapatia mashamba vijana na wanawake 268 katika awamu ya kwanza kwa ajili ya kuanza uzalishaji wa mazao ambapo jumla ya ekari 620 zimepandwa zao la alizeti katika msimu wa 2023/2024. Aidha, alizeti itakayozalishwa katika shamba hilo itanunuliwa na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko.

168. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imejenga nyumba 46 katika shamba la Chinangali II kwa ajili ya makazi ya vijana na wanawake wanaotekeleza programu ya BBT na kuchimba visima tisa (9) na mabwawa matatu (3) kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.



***Picha Na.9:*** *Kijana mnufaika wa Programu ya BBT akifurahia maendeleo ya zao la alizeti katika shamba la BBT la Chinangali Wilaya ya Chamwino - Dodoma*

169. ***Mheshimiwa Spika***, jumla ya ekari 5,700 kati ya ekari 11,430 katika shamba la Mlazo/Ndogowe zimesafishwa na visima 12 na mabwawa matano (5) yamechimbwa kwa ajili ya kuhifadhi maji ya umwagiliaji. Aidha jumla ya ekari 1,000 katika shamba hilo zimetengwa kwa ajili ya kuwapatia wanakijiji wanaolima maeneo yanayozunguka shamba hilo. Pia, nyumba 53 zimejengwa katika shamba hilo kwa ajili ya makazi ya vijana na wanawake wa BBT.

**Programu ya BBT mitaji kwa vijana na wanawake**

170. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuwezesha upatikanaji wa mitaji kwa vijana na wanawake kupitia program ya BBT, Wizara imeuwezesha Mfuko wa Pembejeo za Kilimo *Agricultural Input Trust Fund* -AGITF kiasi cha Shilingi Bilioni 2.8 kwa ajili ya kutoa mikopo nafuu yenye riba isiyozidi asilimia 4.5 kwa vijana na wanawake waliopo kwenye mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo ili kupunguza umasikini na kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo. Hadi Aprili 2024, mikopo ya riba nafuu yenye thamani ya Shilingi Milioni 950 kwa ajili ya kuwawezesha vijana na wanawake 118 imetolewa.

**4.2.3 Kuhamasisha vijana kutoa huduma za ugani**

**BBT – Ugani (BBT Agricultural Extension Entrepreneurship Scheme)**

171. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2023/2024 ilipanga kupitia upya miongozo ya ugani iliyopo na kuandaa mfumo wa kisheria utakaoruhusu uanzishwaji wa kampuni za ugani za vijana ili kuongeza upatikanaji wa ajira kwa wahitimu wa kozi mbalimbali za kilimo nchini na kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma za ugani katika Sekta ya Kilimo.

172. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili, 2024 Wizara kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) imeanzisha BBT – *Agricultural Extension Enterpreneurship Scheme* (BBT – Ugani) ambayo inalenga kukuza ujuzi wa vijana wahitimu wa vyuo vya kilimo kwa kutumika kutoa ushauri wa kitaalam (huduma za ugani) kwa wakulima.

173. Wahitimu 230 kutoka Vyuo vya Kilimo wamechaguliwa na wanaendelea kutoa huduma za ugani katika Kata 40 zinazozalisha zao la pamba kwenye mikoa ya Shinyanga, Tabora, Simiyu, Mara, Mwanza na Pwani. Programu hiyo inagharamiwa na Serikali na Chama cha Wachambuaji wa Pamba (Tanzania Ginners Association – TGA) na uzalishaji katika Kata hizo utafanyika kwa utaratibu wa kilimo cha mkataba. Aidha, matokeo ya programu hiyo ni kuwawezesha vijana kuona fursa na kujiajiri kwa kuanzisha kampuni za ugani zinazotoa huduma binafsi.

**Mradi wa visima kwa wakulima wadogo (boreholes)**

174. ***Mheshimiwa Spika***, kwa kutambua changamoto zinazowakabili wakulima wadogo ikiwemo mabadiliko ya tabianchi, Wizara ilipanga kuanza programu ya kuchimba visima 68,000 iliyozinduliwa Agosti, 2023 na Mheshimiwa Rais katika viwanja vya Nanenane – Mbeya.

175. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili, 2024 jumla ya visima 22 vimechimbwa katika mikoa ya Dodoma na Mbeya kwa ajili ya wakulima na kuwawekea miundombinu ya umwagiliaji kwa kila eneo la ekari 2.5. Vilevile, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imenunua magari mawili (2) maalum kwa ajili ya kuchimbia visima. Aidha, lengo la programu hii ni kuwawezesha wakulima wadogo kuzalisha mazao mwaka mzima.

176. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuwajengea uzoefu, uelewa wa fursa zilizopo katika masuala ya Mifumo ya Chakula katika ngazi ya Kimataifa, Wizara imewawezesha vijana 4 wajasiliamali wa Kilimo kushiriki Jukwaa la Mifumo ya Chakula (WFF) lililofanyika mwezi Oktoba 2023 Rome nchini Italia.

177. Vilevile, pamoja na kuwajengea uelewa wa fursa za kimataifa na uwezo wa kutangaza biashara zao, vijana hao wamepata fursa mbalimbali. Kupitia Jukwaa hilo, Kampuni ya Vijana ya Mazaohub inayojihusisha na matumizi ya TEHAMA katika kutoa huduma za Ugani imeweza kukutana na kufanya mashirikiano ya Kibiashara na Kampuni ya The Catalyst Fund na Zephyr Acorn za Marekani, Digital Green ya India na Proparco ambazo tayari wameanzisha Ubia wa biashara kwa ajili ya kuimarisha huduma za Ugani Kidigiti na tayari wamewekeza zaidi ya Dola za Marekani 650,000. Fursa zingine zilizopatikana kutokana na ushiriki wa vijana hao ni kupata fursa ya kwenda kuwajengea uwezo vijana wa Sudan Kusini kuhusu fursa za kilimo na kuunganishwa na Galilee Export kwa ajili ya soko la parachichi zinazozalishwa na Kampuni ya vijana ya Kikombo Avocado Farm ya Njombe.

### 4.3 Kuimarisha Usalama wa Chakula na Lishe

#### 4.3.1 Uwekezaji kwenye miundombinu ya uhifadhi kuweza kufikia uwezo wa kuhifadhi tani 3,000,000 ifikapo 2030

178. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya Shilingi Bilioni 11.6 zilitengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa ghala 38 zenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani 33,000 katika Mikoa ya Ruvuma (28) na kukamilisha ujenzi wa ghala na vihenge vyenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani 165,000 katika kanda za Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula nchini (National Food Reserve Agency – NFRA) za Songea, Mbozi, Makambako, Dodoma na Shinyanga kupitia Mradi wa Kuongeza Uwezo wa Kuhifadhi unaotekelezwa na NFRA. Kadhalika, kupitia mradi wa TANIPAC, Wizara ilipanga kuandaa Mwongozo wa Usimamizi na Uendeshaji wa Ghala.

179. ***Mheshimiwa Spika***, hadi Aprili, 2024 ujenzi wa ghala 28 umefikia wastani wa asilimia 75. Ghala hizo zenye uwezo wa kuhifadhi tani 1,000 kila moja zinajengwa katika mkoa wa Ruvuma katika Halmashauri za Songea (11), Madaba (9), Namtumbo (7) na Manispaa ya Songea (1). Vilevile, mradi wa ujenzi wa ghala na vihenge kupitia NFRA katika kanda za Songea, Makambako, Mbozi, Dodoma na Shinyanga umefungwa na usuluhishi kwa njia ya kidiplomasia umekamilika.

180. Kadhalika, Wakala umemtaarifu Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu hatma iliyofikiwa kwenye majadiliano kama alivyoelekeza. Wakala pia, umefuatilia ongezeko la muda wa matumizi ya mkopo kutoka Poland ambapo Serikali kupitia Wizara ya Fedha imeridhia na kuwasilisha ombi hilo nchini Poland kwa kuridhia na kusaini *Addendum*. Pia, Mwongozo wa Usimamizi na Uendeshaji wa Ghala umekamilika na umeanza kutumika katika uendeshaji wa ghala zilizojengwa kupitia mradi wa TANIPAC.

#### 4.3.2 Kuiongezea NFRA uwezo wa kununua mazao ya wakulima ili kuongeza hifadhi hadi kufikia tani 500,000

181. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024 Wizara ilipanga kununua tani 400,000 za nafaka ambapo Shilingi Bilioni 14 zilizotokana na bajeti na Shilingi Bilioni 274 zilizotokana na vyanzo vya NFRA na idhini ya hazina kutumia taasisi za fedha kuchukua fedha kwa ajili ya kununua mazao.

182. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili, 2024 NFRA imenunua tani 294,069.216 za nafaka na ununuzi unaendelea. Kiasi kilichonunuliwa kikijumuishwa na bakaa ya msimu wa 2022/2023 kinafanya NFRA kuhifadhi jumla ya tani 337,672.868 katika ghala zake.

**4.3.3 Kuanza matumizi ya mfumo wa *Crop Stock Dynamic Systems***

183. ***Mheshimiwa Spika,*** moja ya changamoto kubwa inayolikabili Taifa letu ni ukosefu wa taarifa sahihi za mazao ya kilimo katika maeneo ya sokoni, ghala za kijamii na vituo vya ukaguzi wa mazao. Aidha, Serikali imekuwa ikitoa taarifa kuhusu hifadhi ya chakula inayopatikana kwa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA). Hata hivyo, dhana pana ya usalama wa chakula ni hifadhi iliyopo Serikalini, kwa wafanyabiashara, ghala binafsi na masoko na taarifa sahihi ya biashara ya mazao yanayoingia na yanayotoka.

184. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilipanga kuanza kutumia mfumo wa kidigiti (Crop Stock Dynamics Systems) kwa ajili ya usajili wa wafanyabiashara, masoko, ghala za umma na binafsi.

185. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, mafunzo kuhusu matumizi ya mfumo wa Crop Stock Dynamics Systems katika kukusanya bei za mazao ya kilimo katika masoko na kusajili masoko, ghala, vituo vya uuzaji na ununuzi wa mazao ya kilimo yametolewa kwa Maafisa Ugani 149 nchini. Vilevile, mafunzo hayo yalihudhuriwa na wataalam kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, TanTrade, Kampuni ya *Multics Tanzania* na Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Aidha, ghala 1,215, masoko 196 na vituo vya ukaguzi 93 vimesajiliwa katika mikoa yote na usajili unaendelea.

**4.3.4 Kuratibu Mkutano wa Mifumo ya Chakula Afrika - 2023**

186. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na wadau wa Sekta ya Kilimo nchini katika mwaka 2023/2024, ilipanga kuratibu na kushiriki Mkutano wa Mifumo ya Chakula Afrika 2023 (Africa Green Revolution Forum (AGRF) - Africa Food System Summit) kwa lengo la kuongeza uwekezaji katika Sekta ya Kilimo nchini, upatikanaji wa mitaji, kukuza utalii, kuimarisha biashara ya mazao ya kilimo na teknolojia.

187. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali yetu ilikuwa mwenyeji wa Mkutano wa Mifumo ya Chakula Afrika 2023 uliofanyika tarehe 05 hadi 08 Septemba, 2023 katika Ukumbi wa Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere Dar es Salaam na kuhudhuriwa na washiriki 5,400 kutoka nchi 90 Duniani. Katika Mkutano huo Sekta ya Kilimo imefanikiwa kupata Dola za Marekani Milioni 600 kutoka Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, IFAD, AGRA na USAID kwa ajili ya kutekeleza miradi ya mifumo ya chakula.

188. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia mkutano huo hati za makubaliano tatu (3) kwa ajili ya kushirikiana katika kuendeleza Sekta ya Kilimo zimesainiwa. Hati hizo ni;

i. Hati ya Makubaliano kati ya Wizara ya Kilimo na Kampuni ya Agricom kwa ajili ya kuwezesha programu ya BBT (huduma za zana za kilimo katika mashamba ya Chinangali);
ii. Hati ya Makubaliano kati ya Wizara ya Kilimo na CRDB kwa ajili ya mikopo ya kilimo himilivu (Green fund); na
iii. Hati ya Makubaliano kati ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) na Taasisi ya Utafiti wa Kibaolojia na Uchumi ya Norway (Norwegean Institute Bioeconomy Research - NIBIO) katika eneo la utafiti na teknolojia za kilimo.

Aidha, kiasi cha Shilingi Bilioni 2.4 kimepatikana kwa ajili ya kuwezesha utafiti na uendelezaji wa teknolojia za kilimo.




***Picha Na. 10:*** *Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan (katikati) akuzungumza kwenye mjadala uliowahusisha wakulima vijana kwenye Mkutano wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF) uliofanyika jijini Dar es Salaam mwezi Septemba 2023*

### 4.3.5 Kuhamasisha matumizi ya mazao yaliyoongezewa virutubishi ili kukabiliana na matatizo ya lishe nchini

189. ***Mheshimiwa Spika,*** Taifa linakabiliwa na tatizo la lishe ambapo katika kutatua tatizo hilo Serikali imekuwa ikitekeleza Mpango Kazi wa Lishe katika Kilimo (Nutrition Sensitive Agriculture Action Plan – NSAAP). Hata hivyo, Serikali imekuwa ikipokea misaada ya baadhi ya mazao yaliyoongezwa virutubishi kutoka nje ya nchi.

190. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2023/2024 ilipanga kuwezesha Maafisa Ugani kuanzisha mashamba darasa 100 na mashamba ya mfano 28; kuzalisha vipando 390,150 vya mbegu za awali za viazi lishe; kutoa mafunzo kwa wakulima 2,000 na Maafisa Ugani 725 kuhusu uzalishaji wa maharage na mahindi lishe ambayo yanatokana na mbegu zilizofanyiwa utafiti na taasisi zetu.

191. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili, 2024 mashamba darasa 100 yakiwemo 50 ya maharage na 50 ya mahindi lishe yameanzishwa na maafisa ugani 50 na wakulima 2,700 wamepatiwa mafunzo kuhusu lishe bora na uzalishaji wa maharage, viazi na mahindi lishe katika mikoa ya Geita, Kagera, Mwanza, Simiyu, Mbeya, Tanga, Rukwa na Mara. Vilevile, vipando 250,000 vya mbegu za awali za viazi lishe vimezalishwa na kusambaza kwa wakulima na wakulima 2,200 kutoka mikoa ya Geita, Kagera, Mwanza, Simiyu na Mara wamepatiwa mafunzo ya uzalishaji wa vipando vya viazi lishe na lishe bora.

192. Vilevile, Wizara kupitia mradi wa AGRI - Connect ilipanga kuanzisha majiko lishe 100. Hadi Aprili, 2024 majiko lishe 51 yameanzishwa katika mikoa ya Mbeya, Rungwe, Iringa na Njombe kwa lengo la kuelimisha jamii kuhusu namna ya kuandaa milo inayozingatia mahitaji ya lishe kwa watoto wadogo, wagonjwa na mama wajawazito na wanao nyonyesha. Mwongozo wa namna ya kuunda Majiko lishe katika ngazi ya jamii umekamilika na mafunzo ya namna ya kuendesha majiko lishe hayo yametolewa kwa wakulima viongozi 100 katika mikoa ya Mbeya, Rungwe, Iringa na Njombe.

193. ***Mheshimiwa Spika***, Pia, Wizara kupitia Programu ya Agri-Connect ilipanga kuanzisha miradi ya bustani katika shule za msingi 100 kutoka Mikoa ya Njombe (40) Songwe (25) na Iringa (35) kwa lengo la kuhamasisha uzalishaji na matumizi ya mazao hayo mashuleni ili kuboresha lishe. Vilevile, Wizara kupitia mradi wa Beyond Cotton ilipanga kujenga matenki matatu (3) ya kuvuna na kuhifadhi maji ya mvua kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji wa bustani za mboga na matunda ili kuongeza upatikanaji wa mazao hayo na kuboresha lishe miongoni mwa wakulima wa pamba.

194. ***Mheshimiwa Spika***, hadi Aprili, 2024 Wizara kupitia mradi wa AGRI – Connect imewezesha shule 100 kutoka mikoa ya Njombe (40) Iringa (35) na Songwe (25) kuanzisha klabu za afya na lishe ambapo kila klabu ina wanafunzi 50 (25 wa kike na 25 wa kiume). Elimu ya uzalishaji na matumizi ya mazao ya kuongeza virutubishi imetolewa kwa wanafunzi 5,000 kutoka katika klabu hizo. Mbegu zilizozalishwa ni pamoja na Mahindi lishe (kilo 115) Maharage lishe (kilo 402) na viazi lishe (vipando 750,000). Aidha, shule 4 (Igingilanyi, Luganga, Kimande na Ilolo Mpya) kutoka mkoa wa Iringa zimewezeshwa kwa kuwekewa miundombinu ya umwagiliaji ili kusaidia uzalishaji wa mboga na matunda kwa lengo la kuboresha lishe kwa wanafunzi shuleni.

195. Vilevile, Wizara kupitia mradi wa Beyond Cotton imetoa mafunzo ya lishe kwa nadharia na vitendo katika SACCOS tisa (9) katika Wilaya za Misungwi (3), Magu (3) na Kwimba (3). Aidha, katika kujihakikishia upatikanaji wa maji kwa ajili ya uzalishaji wa mboga na matunda, imekamilisha ujenzi wa matenki tisa (9) ya kuvunia maji ya mvua katika shule tatu (3) za msingi zilizopo Wilaya za Misungwi, Magu na Kwimba

***"Ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa ili kulinda jamii yetu Wizara itaendelea kuwekeza kwenye eneo la utafiti na uzalishaji wa mbegu zilizoongezewa virutubishi ili kutosheleza mahitaji ya mbegu hizo nchini. Aidha, baada ya kujitosheleza kwa upatikanaji wa mbegu hizo, Wizara ya Kilimo haitaruhusu mazao yaliyoongezewa virutubishi kutoka nje ya nchi kuingia ndani ya nchi na kusambazwa".***

### 4.4 Kuimarisha Upatikanaji wa Masoko, Mitaji na Mauzo ya Mazao nje ya Nchi

#### 4.4.1 Kujenga miundombinu ya masoko ya mazao ya kilimo

196. ***Mheshimiwa Spika***, jumla ya Shilingi Bilioni 4.75 zilitengwa kwa ajili ya kutekeleza yafuatayo:

**Ujenzi wa Masoko ya Kimkakati**

196. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara katika mwaka 2023/2024 ilipanga kuendeleza ujenzi wa masoko matano (5) ya kimkakati yaliyokuwa chini ya mradi wa DASIP katika Halmashauri za Kahama (Busoka), Ngara (Kabanga), Kyerwa (Nkwenda na Murongo), na Tarime (Sirari). Hadi Aprili, 2024 zabuni kwa ajili ya ujenzi wa masoko ya Kahama (Busoka), Ngara (Kabanga), Kyerwa (Murongo) na Tarime (Sirari) zipo katika hatua ya tathmini. Aidha, zabuni kwa ajili ya soko la Kyerwa (Nkwenda) imetangazwa. Ujenzi wa masoko hayo utawezesha kuendeleza biashara ya mazao ya mchele, muhogo (Busoka); ndizi na maharage (Nkwenda); ndizi na parachichi (Kabanga); ndizi na viazi mviringo (Murongo); na mchele na mahindi (Sirari) katika mipaka ya nchi za Uganda, Kenya, Rwanda na Burundi.

**Ujenzi wa Vituo vya Masoko (Market sheds)**

198. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara katika mwaka 2023/2024 ilipanga kujenga vituo vitatu (3) vya masoko ya kilimo (*market sheds)* ili kuwezesha wakulima kukusanya na kuuza mazao yao sehemu rasmi inayotambulika na mamlaka husika. Hadi Aprili, 2024, mkataba wa ujenzi wa masoko ya Endashangwet (Karatu), Kibakwe (Mpwapwa), Losirwa (Monduli), Ushirika na Parking (Nzega mji) umewasilishwa kwa mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya upekuzi.

**Kuimarisha COPRA na kuiwezesha CPB kununua mazao**

199. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024 Wizara ilipanga kuiwezesha Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (Cereal and Other Produce Regulatory Authority - COPRA) kuimarisha usimamizi wa uhifadhi na biashara ya mazao ya nafaka na mazao mchanganyiko ili kukidhi vigezo vya soko. Vilevile, Wizara ilipanga kuiwezesha Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (Cereal and Other Produce of Board – CPB)

kununua tani 115,000 za mazao ya mahindi, mpunga, ngano, maharage, alizeti na mtama mweupe.

200. ***Mheshimiwa Spika***, hadi Aprili, 2024 Mkurugenzi Mkuu wa COPRA ameteuliwa; Muundo wa Taasisi umepitishwa na kikao cha Kamati ya Rais ya Utekelezaji (Presidential Implementation Committee - PIC); COPRA imetambuliwa na kusajiliwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa namba TR 267; Bodi ya Wakurugenzi wa COPRA imezinduliwa; Nembo ya COPRA imezinduliwa na imeanza kutumika; Notisi ya kutangaza Mazao Mchanganyiko yatakayosimamiwa na COPRA imetolewa kwenye Gazeti la Serikali; Rasimu ya Kanuni na Miongozo kwa ajili wa usimamizi vimeandaliwa; na COPRA kwa kushirikiana na Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala, Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania pamoja na Soko la Bidhaa Tanzania (Tanzania Mercantile Exchange - TMX) imeanza kutoa miongozo ya kusimamia biashara ya nafaka na mazao mchanganyiko.

201. Kadhalika, CPB imenunua tani 49,331.89 za nafaka na mazao mengine kutoka kwa wakulima zinazojumuisha mahindi tani 44,352.28, mtama tani 56.74, mpunga tani 1,754.05, ngano tani 2,443.74 na maharage tani 211. Vilevile, Serikali ya Tanzania kupitia CPB kwa kushirikiana na WFP inaendelea kusindika mahindi kwa ajili ya kuzalisha unga wa kupeleka nchini Malawi. Aidha, Wizara ipo katika hatua za mwisho za majadiliano na Serikali za Zambia, Zimbabwe na Malawi kuwauzia mahindi kupitia NFRA na CPB.
***“Serikali inatoa rai kwa wafanyabiashara wa mazao nchini kuuza mazao ya chakula katika nchi hizo kutokana na fursa ya soko la mazao hayo”***

202. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuwezesha upatikanaji wa bei nzuri ya mazao yanayozalishwa nchini, Wizara kupitia Bodi ya Chai Tanzania imeanzisha mnada wa chai ambapo katika mnada wa kwanza uliofanyika tarehe 13 Novemba, 2023 kilo 31,294 ziliuzwa kwa bei ya wastani wa Dola za Marekani 0.77 kwa kilo. Aidha, Wizara kupitia Bodi ya Tumbaku Tanzania imesimamia utiaji saini wa mikataba ya uzalishaji baina ya wanunuzi na wakulima ambapo mikataba ya kuzalisha kilo 213,077,306 imesainiwa msimu wa kilimo 2023/2024.

**4.4.2 Kuimarisha uongezaji thamani na uhifadhi wa mazao ya kilimo**

203. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya Shilingi Bilioni 28.23 kwa ajili ya kutekeleza yafuatayo: **Ujenzi wa Vituo Jumuishi**

204. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2023/2024, ilipanga kujenga Vituo Jumuishi (common use facilities) vitatu (3) vya kukusanya, kuchambua, kupanga madaraja, kufungasha na kusafirisha mazao ya bustani katika mikoa ya Iringa, Kilimanjaro na Dar es Salaam. Vituo hivyo, vitawezesha kupunguza upotevu wa mazao ya bustani, kuongeza ubora na mauzo ya mazao hayo ndani na nje ya nchi. Hadi Aprili, 2024 mkataba wa ujenzi wa vituo jumuishi vya Iringa – Mufindi (1) na Mbeya – Rungwe (1) umewasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya upekuzi.

**Ujenzi wa Kiwanda cha Kusindika Zabibu Ghafi**

205. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2023/2024 ilipanga kujenga kiwanda chenye uwezo wa kusindika zabibu tani 200 kwa mwaka ambazo zitazalisha mchuzi wa zabibu lita 150,000 katika Mkoa wa Dodoma ili kuongeza thamani ya zao la zabibu, kupunguza upotevu na kuwaongezea wakulima soko. Hadi Aprili, 2024 ujenzi wa kiwanda cha kusindika zabibu katika mkoa wa Dodoma umefikia wastani wa asilimia 60.

**Ujenzi wa Kiwanda cha Kubangua Korosho**

206. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Korosho katika mwaka 2023/2024 ilipanga kuiwezesha Sekta binafsi kujenga kiwanda cha kubangua korosho. Hadi Aprili, 2024 Bodi imeanzisha Kongani ya Viwanda katika eneo lenye ukubwa wa ekari 1,572 lililopo kijiji cha Maranje, Wilaya ya Nanyamba mkoani Mtwara ambapo eneo la ekari 373 limefanyiwa tathmini, fidia imelipwa kwa wananchi wanaohusika na eneo hilo limesafishwa na maandalizi ya kuanza kuweka miundombinu ya barabara, maji na umeme yanaendelea. Aidha, ubanguaji wa korosho umeongezeka kutoka tani 11,976 msimu wa 2022/2023 hadi tani 26,656 msimu wa 2023/2024.

**Ujenzi wa Kituo Mahiri Cha Usimamizi wa Mazao**

207. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia mradi wa TANIPAC katika mwaka 2023/2024 ilipanga kukamilisha ujenzi wa Kituo Mahiri cha Usimamizi wa Mazao Baada ya Kuvuna (Mtanana – Kongwa) na Maabara Kuu ya Kilimo Jijini Dodoma. Hadi Aprili, 2024 ujenzi wa Kituo Mahiri Cha Usimamizi wa Mazao baada ya kuvuna umefikia wastani wa asilimia 95 na ujenzi wa Maabara kuu ya Kilimo umefikia asilimia 48. Kukamilika kwa miundombinu hiyo kutawezesha usambazaji wa teknolojia bora za usimamizi wa mazao baada ya kuvuna nchini.

**Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko**

208. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia CPB katika mwaka 2023/2024, ilipanga kusindika mahindi tani 40,500; kukamua alizeti tani 5,000; kukoboa mpunga tani 20,000; kusindika ngano tani 15,000; na kuchakata korosho tani 115 kwa ajili ya kuzalisha jibini (cashewnut butter). Hadi Aprili, 2024 Bodi imesindika mahindi tani 3,112.36, mafuta ghafi ya alizeti tani 47.20, mpunga tani 1,001.99, ngano tani 79.63 na siagi ya korosho tani 0.20 na usindikaji unaendelea.

**4.4.3 Kuongeza mauzo ya mazao ya kilimo nje ya nchi**

209. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2023/2024 ilipanga kuongeza mauzo ya mazao mbalimbali kwa asilimia tano (5) kufikia Dola za Marekani Bilioni 1.457. Pamba kutoka Dola za Marekani Milioni 227.1 hadi Dola za Marekani Milioni 238.46 na tumbaku kutoka Dola za Marekani Milioni 355 hadi Dola za Marekani Milioni 372.75. Vilevile, katika kufungua masoko nje ya nchi Wizara ilipanga kuboresha maabara za afya ya mimea za TPHPA ili ziweze kupata ithibati na kuwezesha kutoa vyeti vya ubora vinavyokubalika kimataifa.

210. ***Mheshimiwa Spika***, ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili, 2024 mauzo ya mazao ya kilimo nje ya nchi yameongezeka kutoka Dola za Marekani Bilioni 1.2 mwaka 2019/2020 hadi Dola za Marekani Bilioni 2.3 mwaka 2022/2023 sawa na ongezeko la asilimia 91.7 kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 11.** Ongezeko hilo limechangiwa na mauzo ya Kahawa, Tumbaku, Korosho, Mchele, ufuta, mazao jamii ya

mikunde na mazao ya bustani. Ongezeko la mauzo kwa baadhi ya mazao ni kama ifuatavyo:-

i. Mauzo ya parachichi yameongezeka kutoka tani 17,711.49 zenye thamani ya Dola za Marekani Milioni 51 mwaka 2021/2022 hadi tani 26,826.30 zenye thamani ya Dola za Marekani Milioni 77.3 mwaka 2022/2023;
ii. Mauzo ya pamba nje ya nchi yameongezeka kutoka tani 32,608.8 zenye thamani ya Dola za Marekani Milioni 15.6 mwaka 2021/2022 hadi tani 65,771.38 zenye thamani ya Dola za Marekani Milioni 33.5 mwaka 2022/2023; na
iii. Mauzo ya tumbaku nje ya nchi yameongezeka kutoka tani 8,376.8 zenye thamani ya Dola za Marekani Milioni 35.2 mwaka 2021/2022 hadi tani 32,587.29 zenye thamani ya Dola za Marekani Milioni 142.4 mwaka 2022/2023.

211. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia TPHPA kwa kushirikiana na FAO na EU imempata mkandarasi wa ukarabati wa maabara katika vituo 36 vya mipakani ikiwemo maabara ya Kurasini, Tengeru na TPHPA makao makuu. Vilevile, zabuni za ununuzi wa vifaa vya maabara `kwa ajili ya kuboresha maabara za afya ya mimea za Kurasini, Kibaha, Tengeru na TPHPA makao makuu ili ziweze kupata ithibati na kuwezesha kutoa vyeti vya ubora vinavyokubalika kimataifa zimetangazwa.

212. Kadhalika, maabara ya TPHPA makao makuu Arusha imepata ithibati ya Kimataifa ya ISO/IEC 17025:2017 kwa ajili ya kupima viwango vya mabaki ya kemikali kwenye mazao. Pia, kufuatia hatua za Serikali za kufungua soko la parachichi nchini China, zao hilo linatarajiwa kuanza kuuzwa China kuanzia Mei, 2024. Kadhalika, taratibu za ufunguzi wa masoko ya mazao mengine ikiwemo soko la tangawizi nchini Marekani, soko la pilipili na mahindi nchini China na soko la ndizi (plantain) nchini Afrika Kusini zinaendelea.

#### 4.4.4 Kuimarisha upatikanaji wa mitaji (Agricultural finance)

213. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) katika mwaka 2023/2024 ilipanga kuongeza idadi ya taasisi za fedha zinazotumia mfuko wa dhamana kutoka taasisi 15 hadi 21 ili kurahisisha utoaji wa mikopo;

kuwezesha miradi mipya 40, ununuzi wa matrekta 42 pamoja na *combine harvesters* 10; kutoa mikopo ya pembejeo kwenye miradi 20 ya kilimo; na kuwajengea uwezo wakulima wadogo 1,400 kuhusu elimu ya fedha. Hadi Aprili, 2024 utekelezaji umefikia hatua zifuatazo.

214. ***Mheshimiwa Spika***, taarifa ya Benki Kuu ya mwaka 2023 imeonesha kuwa jumla ya mikopo iliyotolewa na taasisi za fedha nchini ni Shilingi **Trilioni 33.159** ilitolewa. Kati ya hiyo, Shilingi **Trilioni 3.317** ilitolewa kwenye Sekta ya Kilimo sawa na asilimia 10 ya mikopo yote. Miongoni mwa taasisi za fedha zilizotoa mikopo hiyo ni TADB Shilingi Bilioni 138.119, CRDB Shilingi Trilioni 1.41 na NMB Shilingi Trilioni 1.7 na kiasi kilichobaki kimetolewa na taasisi nyingine za fedha.

215. Kadhalika, TADB imeongeza taasisi mbili (2) za fedha zinazotumia mfuko wa dhamana ambazo ni *Self Micro Finance* na *Exim Bank Tanzania*. Hatua hiyo, imewezesha utoaji wa mikopo yenye thamani ya Shilingi Bilioni **138.119** kwenye Sekta ya Kilimo Mazao kwa njia ya moja kwa moja na Shilingi Bilioni **41.817** kupitia mfuko wa dhamana ya mikopo kwa wakulima wadogo. Kupitia mikopo hiyo, TADB imewezesha miradi mipya 31 sawa na asilimia 77.5 ya lengo la miradi 40. Aidha, TADB imewezesha ununuzi wa magari mawili (2) ya baridi, matrekta 44, *combine harvesters* 20 na *power tiller* 150.

216. Vilevile, imetoa mafunzo kuhusu elimu ya fedha kwa wakulima 1,851 sawa na asilimia 132.2 ya lengo la wakulima 1,400; kuzindua huduma ya mikopo kwa wanawake na vijana; na kampeni ya kuwashawishi vijana kushiriki katika kilimo.

217. ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na changamoto ya uwepo wa madeni chechefu, Serikali imeboresha utendaji wa Mfuko wa Pembejeo za Kilimo (AGITF) kwa kumteua Mtendaji Mkuu mpya wa Mfuko na kuanza kukusanya fedha za madeni zilizotolewa taarifa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG). Hadi Aprili, 2024 mfuko umekusanya Shilingi 1,526,164,540.96. Kati ya kiasi hicho, Shilingi 1,450,873,342.05 ni marejesho ya fedha ya mikopo (principal) na Shilingi 75,291,198.91 ni riba ya mikopo. Vilevile, ili kuongeza ufanisi wa upatikanaji wa mikopo AGITF imeingia

mkataba wa makubaliano ya mashirikiano na TADB na Benki ya Ushirika.

218. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kipekee ninapenda kuishukuru Wizara ya Fedha, Benki Kuu na Wizara ya Mipango na Uwekezaji kukubali kama Taifa kuanza kuandaa Sera ya mikopo na Sera ya Bima katika Sekta ya Kilimo na bima ya kilimo. Kukamilika kwa sera hizo kutatoa mwongozo utakaopunguza masharti ya mikopo kwa sekta za uzalishaji ikiwemo kilimo. Vilevile, bima ya mazao itawezesha wakulima kupata fidia zinazotokana na majanga katika kilimo.

**4.5 Kuimarisha Maendeleo ya Ushirika (Strengthening Cooperative Development)**

219. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume katika mwaka 2023/2024 ilipanga kuimarisha usimamizi na udhibiti wa Vyama vya Ushirika, kuwezesha Vyama vya Ushirika kujiendesha kibiashara, kuimarisha na kupitia upya mifumo ya upatikanaji wa viongozi wa Vyama vya Ushirika na kuendelea kupitia upya Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya Mwaka 2013.

220. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili, 2024 yafuatayo yametekelezwa:-

**4.5.1 Kuimarisha Usimamizi na Udhibiti wa Vyama vya Ushirika**

221. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Maendeleo ya Ushirika ilipanga kuratibu uanzishwaji wa Benki ya Taifa ya Ushirika kwa kuhamasisha ununuaji wa hisa ili kupata mtaji wa Shilingi Bilioni 20; kuratibu uanzishwaji wa Mfuko wa Bima ya Akiba na Amana za wanachama wa SACCOS utakaotumika kama kinga ya akiba na amana za wanachama.

222. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume imeendelea kuratibu uanzishwaji wa Benki ya Taifa ya Ushirika kwa kuhamasisha ununuaji wa Hisa. Hadi Aprili 2024, Hisa zimeongezeka kutoka Shilingi Bilioni 4.7 mwaka 2022/2023 hadi Shilingi Bilioni 17.1 sawa na asilimia 85.5 ya mtaji hitajika wa shilingi Bilioni 20.

223. Katika mtaji uliopatikana, Vyama vya Ushirika vimewekeza jumla ya Shilingi Bilioni 8.6 sawa na asilimia 84.31 ya kiasi cha Shilingi

Bilioni 10.2 kilichotengwa kwa ajili ya Vyama vya Ushirika kuwekeza na kumiliki Hisa kwa asilimia 51. Aidha, kampuni, taasisi na watu binafsi zimewekeza kiasi cha Shilingi Bilioni 8.5 sawa na asilimia 86.73 ya kuwekeza Shilingi Bilioni 9.8.

224. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume imeendelea kuratibu uanzishwaji wa Mfuko wa Bima ya Akiba na Amana za wanachama wa SACCOS ambapo kwa kushirikiana na wadau imeandaa rasimu ya Kanuni zinazosimamia Vyama vya Ushirika wa Kifedha ambazo zimejumuisha masuala ya uanzishwaji, uendeshaji, usimamizi na ukaguzi wa mfuko wa Kinga ya Akiba na Amana za Wanachama (SDGS). Lengo la kanuni hizo ni kuwezesha usimamizi na ukaguzi wa mfuko kama takwa la Kisheria.

225. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ilipanga kuweka mifumo rasmi na jumuishi ya biashara na masoko kwa mazao mchanganyiko ambayo hayana bodi za usimamizi na kuhamasisha matumizi ya mizani ya kidigiti kwa mazao yenye mifumo rasmi ya biashara.

226. Hadi Aprili, 2024 Tume kwa kushirikiana na Bodi ya Usimamizi wa Ghala, Soko la Bidhaa Tanzania na wadau wengine imeratibu na kusimamia mauzo ya mazao ya wakulima kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala. Jumla ya tani 1,656,410.28 za mazao zenye thamani ya Shilingi 1,977,744,859,472.50 zilikusanywa na kuuzwa kupitia mfumo rasmi wa Ushirika ikilinganishwa na tani 1,841,363.98 zilizouzwa kwa thamani ya Shilingi 1,755,121,090,813 mwaka 2022/2023. Thamani ya mauzo imeongezeka kwa asilimia 12.7 kutoka Shilingi 1,755,121,090,813 mwaka 2022/2023 hadi Shilingi 1,977,744,859,472.50 mwaka 2023/2024 kama inavyoonekana kwenye **Kiambatisho Na. 12**.

227. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume imesimamia upatikanaji wa Mizani ya Kidigiti 1,178 yenye thamani ya Shilingi 3,534,000,000.00 kupitia Vyama Vikuu vya Ushirika vya KCU (1990) Ltd, KDCU Ltd, KACU Ltd na Ushirika wa mradi wa pamoja wa korosho (KCJE) Ltd. Mizani hiyo imesambazwa kwenye Vyama vya Ushirika vya Msingi (AMCOS) vinavyojishughulisha na mazao ya kahawa, korosho, ufuta, soya, mbaazi, kakao na tumbaku katika Mikoa ya Kagera, Lindi, Mbeya, Tabora, Mtwara, Ruvuma na Pwani.



***Picha Na.11:*** *Mizani ya Kidigiti inayotumiwa na Vyama vya Ushirika kupima mazao*

228. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ilipanga kusimamia na kudhibiti Vyama vya Ushirika kwa kukagua vyama 7,300; kuwajengea uwezo Maafisa Ushirika, viongozi na watendaji wa Vyama vya Ushirika; na kusambaza na kusimamia matumizi ya Mfumo wa Usimamizi wa kielektroniki wa Vyama vya Ushirika (MUVU).

229. Hadi Aprili, 2024 Vyama vya Ushirika 3,679 sawa na asilimia 50.4 ya lengo la vyama 7,300 vimekaguliwa. Ukaguzi huo umebaini baadhi ya vyama havijatambua na kuthaminisha mali kama Sheria inavyoelekeza, uandishi mbovu wa vitabu vya hesabu na baadhi ya viongozi wa vyama kukosa uadilifu.
Vilevile, Tume imetoa mafunzo kuhusu ukaguzi na usimamizi wa vyama, maadili, rushwa, afya ya akili na udhibiti wa msongo wa mawazo kwa maafisa ushirika 57 kutoka katika mikoa ya Tabora, Katavi, Rukwa, Mbeya na Njombe. Aidha, katika kuimarisha uwezo wa viongozi na watendaji wa kusimamia Vyama vya Ushirika Tume kwa kushirikiana na TFC, SCCULT COASCO na MoCU imetoa mafunzo kuhusu uandishi wa vitabu vya hesabu na mfumo wa MUVU kwa wanachama 40,253, viongozi 5,553 na watendaji 7,517.

230. Hatua mbalimbali zimechukuliwa ikiwemo kuunda kamati za elimu za mikoa zinazojumuisha COASCO, MoCU na Ofisi za Warajis wasaidizi wa mikoa ambazo zitatoa mafunzo kwa vyama, Kuziondoa Bodi na Watendaji madarakani na baadhi ya taarifa za Vyama kuwasilishwa TAKUKURU na Jeshi la Polisi kwa lengo la

kuchukua hatua za kisheria kwa wahusika hususan kwenye maeneo ya wizi, ubadhilifu na rushwa kwa fedha na mali zingine za Vyama.

231. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume imesajili wanachama 1,492,838 na vyama vya ushirika 6,183 katika mfumo wa MUVU kati ya vyama 7,522 vilivyo kwenye Daftari la Usajili wa Vyama. Lengo la usajili huo ni kuimarisha usimamizi, kuboresha ufanisi na kurahisisha upatikanaji wa takwimu sahihi kwa ajili ya mipango mbalimbali ya maendeleo katika kukuza sekta ya Ushirika kwa ujumla. Aidha, mfumo huo umeunganishwa na Mfumo Mkuu Unganishi wa Serikali (GovESB), Mfumo wa Mizani ya Kielektroniki wa Upimaji wa Mazao (Mkulima Hub), Mfumo Jumuishi wa Usimamizi wa Rasilimali (ERMS), Mfumo wa Ukusanyaji wa Malipo ya Serikali Kielektroniki (GePG) na Mfumo wa Usajili wa Watu kwa njia ya Mtandao chini ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).

232. Kadhalika, Tume imetoa mafunzo kuhusu matumizi ya Mfumo wa MUVU kwa Maafisa ushirika 104 na Watendaji wa Vyama 1,243 kutoka vyama 874 vya mikoa ya Dar es Salaam, Songwe, Mwanza, Kagera, Tabora, Lindi, Mara na Kigoma.

233. ***Mheshimiwa Spika,*** COASCO ilipanga kukagua Vyama vya Ushirika 5,000 ambapo hadi Juni, 2023 Vyama 3,911 vimekaguliwa sawa na asilimia 78 ya lengo. Kati ya vyama vilivyokaguliwa, vyama 479 (asilimia 12.25) vilipata hati inayoridhisha, vyama 2,475 (asilimia 63.28) vilipata hati yenye shaka, vyama 830 (asilimia 21.22) vilipata hati mbaya na vyama 127 vilipata hati isiyo na maoni (asilimia 3.25).

**4.5.2 Kuwezesha Vyama vya Ushirika kujiendesha Kibiashara**

234. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ilipanga kuratibu uanzishwaji wa viwanda ikiwemo kiwanda cha kubangua korosho cha TANECU Ltd na Kiwanda cha vifungashio kinachojengwa na SONAMCU Ltd; kuratibu ufufuaji wa vinu vya kuchakata pamba vya Sola (Simiyu), Mugango na Buyagu (Mara) na Manawa (Mwanza); na kuimarisha uwekezaji wa mali za ushirika katika uzalishaji kwa kuvijengea uwezo Vyama vya Ushirika na kufuatilia na kutambua mali za Vyama vya Ushirika.

235. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume imewezesha uanzishwaji wa viwanda vipya viwili (2) ikiwemo cha kukamua mafuta ya Mbegu cha Chama cha RUNALI na cha kubangua korosho cha TANECU LTD ambacho kinaendelea kukamilishwa. Aidha, kiwanda cha kuchambua na kuchakata pamba cha SOLA (SIMCU Ltd Simiyu) kimefufuliwa. Ufufuaji na uanzishwaji wa viwanda hivyo umefanya jumla ya viwanda vinavyomilikiwa na Vyama vya Ushirika kufikia 328.



***Picha Na.12:*** *Kiwanda cha kubangua korosho cha chama cha ushirika cha TANECU kilichopo katika mkoa wa Mtwara*

236. Kadhalika, Vyama Vikuu na Miradi ya Pamoja 63 na SACCOS 79 zenye Leseni zimefanya utambuzi wa mali 647 zisizohamishika zenye thamani ya Shilingi 5,124,287,849,967 kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 10**.

**Jedwali Na. 10:** Mali za Vyama Zilizothaminishwa mwaka 2023/2024

| Na | AINA YA MALI | IDADI | THAMANI |
|---|---|---|---|
| 1 | Majengo | 158 | 1,423,311,498,653.00 |
| 2 | Mashamba | 54 | 253,294,188,419.00 |
| 3 | Viwanda | 6 | 69,405,899,425.00 |
| 4 | Mashine na Mitambo | 78 | 46,515,741,590.00 |
| 5 | Viwanja | 122 | 176,947,668,429.00 |
| 6 | Vyombo vya Moto | 134 | 35,533,816,677.00 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 7 | Maghala | 52 | 76,398,170,042.00 |
| 8 | Mali zisizoshikika | 43 | 3,042,880,866,732.00 |
| | **JUMLA KUU** | **647** | **5,124,287,849,967.00** |

**Chanzo:** *Wizara ya Kilimo, 2024*

237. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ilipanga kuhamasisha watu 20,000 (wanawake, vijana na watu wenye ulemavu) kuanzisha au kujiunga na vyama vya Ushirika kwenye Sekta mbalimbali ikiwemo kilimo, mifugo, uvuvi, madini, usafirishaji na uchukuzi pamoja na ushirika wa fedha; na kujengea uwezo Vyama vya Ushirika 121 kujitafutia pembejeo, masoko na miundombinu ya kuhifadhi mazao.

238. Hadi Aprili, 2024 Vyama vya Ushirika vya mbogamboga 41 vyenye jumla ya wanachama 2,157 vimesajiliwa katika mikoa ya Arusha (14), Mbeya (4), Njombe (5), Manyara (3), Iringa (10), Kilimanjaro (2) na Songwe (3). Vilevile, Vyama vya Ushirika nane (8) vya vijana vimesajiliwa katika mikoa ya Rukwa (1), Singida (4), Kilimanjaro (1) na Dodoma (2). Aidha, Wananchi 1,516 waliopo kwenye makundi maalum wamehamasishwa kujiunga na ushirika.

**4.5.3 Kuimarisha na kupitia upya Mifumo ya Upatikanaji wa Viongozi wa Vyama vya Ushirika**

239. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ilipanga kuimarisha usimamizi wa rasilimali watu katika Vyama vya Ushirika kwa kupitia upya sifa za watendaji katika Vyama vya Ushirika na kuratibu ajira zote katika vyama.

240. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2024 Tume ilifanya ukaguzi wa sifa za watendaji wakuu (Leadership Audit) wa Vyama Vikuu vyote vya Mazao na miradi ya pamoja 50 na kubaini kuwa asilimia 65 ya watendaji hawakuwa na sifa za kiongozi katika nafasi zao. Kutokana na hali hiyo, Tume ilivielekeza vyama kuajiri watendaji wenye sifa. Tume imetoa maelekezo ikiwemo vyama kuajiri viongozi wenye sifa stahiki, na viongozi wa Vyama wasio na sifa wakiwemo wahasibu wakuu ambao hawana CPA kujiendeleza ndani ya miaka mitatu (3).

241. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume imeandaa Taratibu za Msingi za Uendeshaji (Standard Operating Procedures) tatu (3) ambazo ni Usimamizi wa Rasilimali Watu kulingana na Taratibu za Usimamizi wa Ajira, Taratibu za Uendeshaji wa Mashauri ya Kinidhamu Pamoja na Taratibu za Upunguzaji Kazi Wafanyakazi kwa Sababu za Kiuendeshaji (Termination based on operational requirements). Aidha, Tume imewezesha upatikanaji wa watendaji wakuu wa Vyama Vikuu Vitatu (3) vya NCU, SHIRECU na SIMCU ambao ni watumishi wa Umma ili kuimarisha uwezo wa kiutendaji wa vyama hivyo. Watumishi hao wamehamishiwa katika vyama hivyo kwa utaratibu wa kushikizwa kwa muda (Secondment).

242. Kadhalika, Tume imeendelea kusimamia upatikanaji wa watendaji wakuu wenye sifa stahiki kwa Vyama vingine vya Ushirika vya IGEMBENSABO, PMCU, ACU, KICU, KYECU, CHUTCU, SORECU, TAMCU, MAMCU, TANECU, RIVACU, SIFACU na LATCU.

### 4.5.4 Kuendelea Kupitia upya Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya Mwaka 2013

243. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ilipanga kupitia na kuboresha Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya Mwaka 2013 ili iweze kuendana na wakati. Hadi Aprili, 2024 Tume imekamilisha mapitio ya Rasimu ya Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013 ili kuimarisha usimamizi na udhibiti wa Ushirika na kutatua changamoto za Vyama vya Ushirika.

244. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume imekamilisha mapitio ya Rasimu ya Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya mwaka 2002 kwa kujumuisha maoni mbalimbali ya wadau na kuhakikisha kuwa rasimu ya Sera inaakisi mwelekeo wa sasa wa ushirika.

## MAENEO MENGINE MUHIMU YALIYOTEKELEZWA NA WIZARA

### i. Urasimishaji, Uboreshaji na Uendeshaji wa Shughuli za Kilimo

245. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara katika mwaka 2023/2024, ilipanga kufanya tathmini ya mahitaji ya taasisi za Wizara ya Kilimo ili kuziunganisha itakapohitajika; kuimarisha usajili wa wadau wa kilimo ikiwa ni pamoja na wafanyabiashara wa mazao ya kilimo na watoa huduma nyingine katika shughuli za kilimo ikiwa ni pamoja na huduma za ugani na bima ya mazao.

246. ***Mheshimiwa Spika***, hadi Aprili, 2024 Serikali imekamilisha tathmini ya utendaji wa taasisi mbalimbali ikijumuisha taasisi za Sekta ya Kilimo nchini. Kwa upande wa Sekta ya Kilimo tathmini hiyo ilipendekeza kuunganishwa kwa taasisi za utafiti wa Chai (TRIT), Utafiti wa Tumbaku (TORITA) na Utafiti wa Kahawa (TaCRI) kuwa sehemu ya muundo wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) bila kuathiri majukumu ya msingi ya taasisi hizo; Bodi ya Chai Tanzania kuunganishwa na Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai (TSHTDA) ili kuwa bodi moja (Bodi ya Chai); na Bodi ya Pareto kufutwa na majukumu yake kuhamishiwa katika Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA).

247. Kadhalika, wakulima 3,910,556, waingizaji wa mbolea 31 na mawakala wa mbolea 4,167 wamesajiliwa kwenye mfumo wa kidigiti kwa ajili ya kupata ushauri wa kitaalam ikiwemo kupata taarifa za pembejeo za kilimo.

**ii. Kuongeza Matumizi ya Teknolojia na Mbinu za Kilimo Kinachohimili Mabadiliko ya Tabianchi**

248. ***Mheshimiwa spika,*** ili kuongeza uhimilivu wa kilimo kutokana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi Wizara ilipanga kuhuisha Mpango wa Kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika Sekta ya Kilimo pamoja na kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Mazingira ambapo maeneo mbalimbali yametekelezwa.

249. ***Mheshimiwa spika,*** hadi Aprili, 2024 tathmini ya athari za mazingira na jamii imefanyika katika mradi wa mifumo himilivu ya chakula pamoja na mashamba makubwa ya pamoja ya BBT na Kituo cha mafunzo ya wakulima cha Bihawana. Mashamba yaliyofanyiwa tathmini ni pamoja na Ikang'asi, Mapogoro, Ndogowe, Chinangali pamoja na Kituo cha Bihawana, ambapo vyeti vinne (4) vya tathmini ya mazingira na jamii vya mashamba hayo vimepatikana.

250. Vilevile, elimu kuhusu kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi, masoko, utunzaji wa mazingira na miundombinu ya umwagiliaji ilitolewa kwa vijana 57 waliopo katika programu ya BBT. Pia, ulifanyika ufuatiliaji wa ujumuishwaji wa masuala ya mazingira na kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi katika bajeti na

mipango ya Halmashauri za Itigi, Iramba, Manyoni na Ikungi ambapo ilibainika masuala hayo kuzingatiwa.

251. ***Mheshimiwa spika,*** Wizara kupitia mradi wa mifumo himilivu ya chakula imeanzisha madawati ya kusimamia masuala ya mazingira na jamii kwenye taasisi za TARI, ASA na TOSCI pamoja na mfumo wa kushughulikia malalamiko kuanzia ngazi ya jamii hadi Wizara. Aidha, Wizara inaandaa Mfumo wa Usimamizi wa Mazingira na Kijamii (ESMF) na Mpango Husishi wa Usimamizi wa Wadudu (IPMP) kwenye mradi wa kuwezesha Upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo Tanzania ili kuhakikisha mradi unatekelezwa kwa kuzingatia hifadhi ya mazingira. Pia, Wizara kupitia mradi huo imetoa mafunzo kuhusu utunzaji wa mazingira kwa Maafisa mazingira na kilimo katika Halmashauri 56 zinazotekeleza mradi.

252. ***Mheshimiwa spika,*** Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imekamilisha tathmini ya athari za mazingira na jamii kwenye miradi 29 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa skimu za umwagiliaji na mabwawa. Vilevile, Wizara kupitia Programu ya Uhimilivu wa Mifumo ya Chakula Tanzania imeandaa mipango ya Usimamizi wa Mazingira na jamii (ESMPs) katika skimu za umwagiliaji 23 ili kuwezesha uhifadhi wa mazingira.

253. Vilevile, Wizara kupitia Mradi wa Kuboresha Usimamizi wa Maliasili na Kukuza Utalii Kusini mwa Tanzania (REGROW) imetoa mafunzo kuhusu matumizi sahihi ya viuatilifu na mfumo wa kuwasilisha na kushughulikia malalamiko kwa wakulima 182 kwenye skimu za Gonakuvagogolo, Chosi, Herman, Makangarawe, Mbuyuni Kimani, Madibira, Matebete, Isenyela na Uturo katika mkoa wa Mbeya.

254. Pia, Wizara kupitia TARI imesambaza jumla ya miche 10,209 ya mazao ya miti ya kudumu ya mazao ya korosho, parachichi, michikichi, minazi, maembe, machungwa na miti ya matunda mbalimbali kwa wakulima 3,300 katika mikoa ya Tabora, Mbeya, Singida, Shinyanga na Simiyu kwa ajili ya kupunguza, kukabiliana na kuhimili mabadiliko ya tabianchi nchini.

**iii. Jinsia**

255. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara katika mwaka 2023/2024, ilipanga kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara katika ngazi ya viongozi na wataalam kwa kuwapatia mafunzo kuhusu masuala ya kijinsia; kufanya uchambuzi wa masuala ya jinsia katika Sekta ya Kilimo; na kuandaa mwongozo utakaowezesha kuandaa miradi itakayozingatia masuala ya jinsia katika udhibiti wa sumukuvu kwa lengo la kuleta ufanisi na udhibiti endelevu.

256. ***Mheshimiwa Spika***, hadi Aprili, 2024 Wizara imewajengea uwezo watumishi 67 wa Wizara katika ngazi ya viongozi na wataalam kwa kuwapatia mafunzo kuhusu masuala ya kijinsia. Vilevile, imeandaa Mwongozo wa Kujumuisha Masuala ya Jinsia katika mradi wa Kudhibiti Sumukuvu na kutoa mafunzo kuhusu ujumuishaji na uzingatiaji wa masuala ya jinsia katika mnyororo wa thamani wa mazao ya alizeti, ngano na mpunga kwa Halmashauri 57. Pia, Uchambuzi wa Kijinsia katika mikoa 14 inayotekeleza Mradi wa TAISP kwenye mnyororo wa thamani wa alizeti, ngano na mpunga kwa lengo la kubaini hali halisi, changamoto na fursa za kijinsia zilizopo unaendelea.

**iv. VVU na UKIMWI**

257. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara katika mwaka 2023/2024, ilipanga kuendelea kutoa huduma ya lishe na dawa kwa watumishi wanaoishi na VVU na UKIMWI; kuendelea kutoa elimu ya VVU, UKIMWI na magonjwa sugu yasiyoambukiza (MSY) na kuweka vifaa kinga katika majengo yote ya Wizara pamoja na Taasisi zake.

258. ***Mheshimiwa Spika***, hadi Aprili, 2024 Watumishi wanne (4) wanaoishi na VVU na UKIMWI wamewezeshwa kupata huduma ya ushauri nasaha, lishe na dawa. Vilevile, huduma ya vifaa kinga (kondomu) 33,600 imetolewa katika Ofisi za Wizara na Taasisi zake; na Wizara imezindua kamati 13 za kudhibiti VVU, UKIMWI na MSY mahala pa kazi katika Taasisi zake.

**Masuala mengine yaliyotekelezwa na Wizara**

259. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa vipaumbele na mikakati iliyowekwa na Wizara yapo maeneo mbalimbali yaliyotekelezwa ili yawezeshe ufikiwaji wa malengo. Maeneo hayo ni:-

i. Kuandaa Mpango wa Mageuzi ya Kilimo (Agricultural Transformation Masterplan - 2050) utakaoongoza Maendeleo ya Sekta ya Kilimo kwa kipindi cha miaka 25. Mpango huo utasimamia mabadiliko ya kisera, kimuundo na kimkakati;
ii. Kufanya marekebisho ya Sheria ya Sukari Na.6 ya mwaka 2001 kwenye sheria ya fedha ya mwaka 2024 kwa ajili ya kuiwezesha NFRA kununua na kuhifadhi sukari kwenye Hifadhi ya Chakula ya Taifa ili kunusuru hali ya upatikanaji wa sukari inapotokea kudorora kwa soko la sukari;
iii. Kufanya marekebisho ya Sheria ya Tasnia ya Korosho Na.18 ya mwaka 2009 kwenye Sheria ya Fedha ya mwaka 2024 ili kuwezesha mapato yanayotokana na mauzo ya korosho ghafi (export levy) asilimia 100 kwenda kwenye ununuzi wa pembejeo za zao la korosho pamoja na kulipa madeni ya pembejeo; na
iv. Kuanza marekebisho ya Sheria ya Chai Na.3 ya mwaka 1997 kwenye Sheria ya Fedha ya mwaka 2024 ili kuiwezesha Bodi kuwa na mapato kwa ajili ya kujiendesha; na
v. Kufanya mapitio ya Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji Na.4 ya Mwaka 2013.

**5 MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2024/2025**

260. ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango na Bajeti ya Wizara katika mwaka 2024/2025, umezingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa (2025); Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano Awamu ya Tatu (2021/2022 – 2025/2026); Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Sera ya Taifa ya Kilimo ya mwaka 2013; Sera ya Taifa ya Umwagiliaji ya mwaka 2010; Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya Mwaka 2002 na Mkakati wa Ukuzaji wa Sekta ya Kilimo (Ajenda 10/30 investment roadmap).

261. Vilevile, Mpango umezingatia Malengo Endelevu ya Maendeleo (SDGs); Mwongozo na Mpango wa Bajeti wa Mwaka 2024/2025; Mkakati wa Kuongeza Fedha za Kigeni; Mpango wa Mageuzi ya Kilimo wa Mwaka 2050 (Tanzania Agricultural Masterplan); Maoni na ushauri wa Kamati za Kudumu za Bunge; Maoni ya Baraza la Rais la Ushauri wa Kilimo, wadau wa maendeleo na masuala mtambuka ya jinsia, mazingira, lishe, mabadiliko ya tabianchi, vijana, kutokomeza ajira kwa watoto katika Sekta ya Kilimo, VVU na UKIMWI.

262. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Wizara itaendelea kutekeleza vipaumbele vitano (5) vya mwaka 2023/2024 kwa kukamilisha miradi iliyoanza mwaka 2022/2023, 2023/2024 na kuanza miradi mipya. Aidha, Wizara itaongeza kipaumbele kimoja (1) na hivyo kufanya vipaumbele vya mwaka 2024/2025 kuwa sita (6) vitakavyotekelezwa kupitia mikakati 27.

263. ***Mheshimiwa Spika,*** tathmini ya sensa ya watu na makazi iliyofanyika mwaka 2022 imeonesha kuwa idadi ya watanzania ni milioni 61.7. Kati ya hao, watanzania milioni 31.7 ni wanawake sawa na asilimia 51 ambapo kati yao milioni 11.2 wanaishi mijini na milioni 20.5 wanaishi vijijini na wanaume ni milioni 30 sawa na asilimia 49 ambapo kati yao milioni 10.3 wanaishi mijini na milioni 19.7 wanaishi vijijini. Kwa Tanzania Bara, takwimu zinaonesha kuwa asilimia 65.6 ya watanzania wanaishi vijijini ambako ndipo shughuli za kilimo zinafanyika na asilimia 34.4 wanaishi mijini.

264. Kati ya watanzania wanaoishi vijijini, asilimia 39.0 ni vijana wenye umri kati ya miaka 14 hadi 40 ambao ni nguvu kazi ya Taifa. Kati ya Vijana hao, asilimia 51.4 ni wanawake na asilimia 48.6 ni wanaume. Aidha, kwa mujibu wa takwimu za IFAD za mwaka 2019, asilimia 59 ya vijana wanaoishi vijijini wanajishughulisha na kilimo.

265. ***Mheshimiwa Spika,*** ni muhimu kuzitazama takwimu hizo zilizotokana na sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022 na takwimu za IFAD ili kuwezesha kufanya maamuzi ya mabadiliko na ugawaji wa rasilimali hususani kwenye kilimo.

266. ***Mheshimiwa Spika,*** kitabu kinachoitwa *How the Current Variables Shape the Future 2030* kimeeleza wazi umuhimu wa ongezeko la idadi ya watu na namna ambavyo Afrika inaweza kuitumia sekta ya kilimo kuleta mapinduzi ya kiuchumi. Dhana ya muda mrefu ya kuamini kuwa maendeleo ya kiuchumi Duniani yataletwa na Sekta ya huduma kwa Afrika haiwezekani, hivyo ni lazima Afrika ifanye mapinduzi ya viwanda ambayo yatawezeshwa na Sekta ya Kilimo kwa asilimia 100 ili kujenga Sekta nyingine.

267. Vilevile, kitabu cha *The last drop: Solving the World's Water Crisis* (2023) kilichoandikwa na Tim Smedley kimeeleza moja ya

tatizo kubwa linaloathiri ukuaji wa uchumi wa Dunia ni upungufu wa maji. Hivyo, Wizara ya kilimo tunapopanga mipango yetu leo na kesho kama taifa ni lazima tutambue athari za upungufu wa maji katika kilimo na mambo mengine yanayotuzunguka. Na sisi kama Wizara hatujafumbia macho viashiria vyote vinavyotuzunguka huku tukitambua kwamba mwaka 2030 Taifa hili linakadiriwa kuwa na idadi ya watu milioni 79 na mwaka 2050 Taifa linakadiriwa kuwa na idadi ya watu milioni 135 ambao watahitaji chakula takriban tani milioni 20.7 na milioni 35.4; mtawalia.

268. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025 Wizara inalenga ukuaji wa Sekta ya Kilimo kwa upande wa mazao kufikia asilimia 5 kuchangia asilimia 20 katika Pato la Taifa, kuendelea kuchangia asilimia 100 ya upatikanaji wa chakula na kuongeza mauzo ya mazao nje ya nchi hadi kufikia Dola za Marekani Bilioni 3. Malengo hayo yatafikiwa kwa kutekeleza vipaumbele sita na mikakati 27.

269. ***Mheshimiwa Spika,*** kipaumbele chetu cha kwanza katika mwaka 2024/2025 hadi mwaka 2050 kitakuwa ni Kuongeza tija na uzalishaji (Increase Productivity and Production). Kipaumbele hiki hakitabadilika isipokuwa mabadiliko yanaweza kufanyika kwenye mikakati ya kufikia kipaumbele hicho; kipaumbele cha pili ni kuongeza ajira zenye staha na ushiriki wa vijana na wanawake kwenye kilimo; cha tatu ni kuimarisha usalama wa chakula na lishe; cha nne kuimarisha upatikanaji wa masoko, mitaji na mauzo ya mazao nje ya nchi; cha tano kuimarisha maendeleo ya ushirika; na cha sita ni kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika uendelezaji wa Sekta ya Kilimo.

270. ***Mheshimiwa Spika***, vipaumbele na mikakati ni kama ifuatavyo:-

**i. Kuongeza Tija na Uzalishaji (Increase Productivity and Production); Mikakati:-**

a) Utafiti wa mbegu;
b) Uzalishaji na usambazaji wa mbegu na miche bora na kutoa ruzuku ya mbegu na miche bora kwa baadhi ya mazao;
c) Uwekezaji kwenye utoaji wa ruzuku ya mbolea na viuatilifu;
d) Usajili wa wakulima na urasimishaji wa shughuli za kilimo;
e) Kuwekeza kwenye ujuzi kwa wataalam wa ndani;

f) Uwekezaji kwenye huduma za ugani;
g) Kupima afya ya udongo kwa wakulima wadogo na wakubwa;
h) Uendelezaji wa kilimo cha umwagiliaji; na
i) Uanzishaji wa vituo Jumuishi vya Kutoa Huduma za Zana za Kilimo.

**ii. Kuongeza ajira zenye staha na ushiriki wa vijana na wanawake kwenye kilimo (Increase Decent Jobs And Enhancing Youth And Women Participation In Agriculture Sector) Mikakati**:-

a) Kuwezesha upatikanaji wa ardhi ya kilimo na uanzishaji wa mashamba makubwa ya pamoja;
b) Kuimarisha ushiriki wa vijana na wanawake katika kilimo kupitia programu ya Jenga Kesho iliyo Bora; na
c) Kuimarisha ushiriki wa wazawa katika miradi ya kilimo (Local Content).

**iii. Kuimarisha Usalama wa Chakula na Lishe (To Improve Food and Nutrition Security); Mikakati:-**

a) Uwekezaji kwenye miundombinu ya uhifadhi kuweza kufikia uwezo wa kuhifadhi tani 3,000,000 ifikapo mwaka 2030;
b) Kuiongezea NFRA uwezo wa kununua mazao ya wakulima ili kuongeza hifadhi ya chakula;
c) Kuimarisha matumizi ya mfumo wa kidigiti wa *Crop Stock Dynamic Systems*; na
d) Kuhamasisha matumizi ya mazao yaliyoongezewa virutubishi ndani ya nchi ili kukabiliana na matatizo ya lishe nchini.

iv. **Kuimarisha upatikanaji wa masoko, mitaji na mauzo ya mazao nje ya nchi (Strengthen access to market, agriculture financing and crop exports);**

**Mikakati:-**

a) Kujenga miundombinu ya masoko ya mazao ya kilimo kwa ajili ya wakulima katika Halmashauri mbalimbali;
b) Kuimarisha uongezaji thamani na uhifadhi kwa kushirikisha Sekta Binafsi;
c) Kuongeza mauzo ya mazao ya kilimo ndani na nje ya nchi;
d) Kuimarisha upatikanaji wa mitaji ; na
e) Kuziwezesha maabara za Serikali na Sekta Binafsi kufikia viwango vya ubora unaotakiwa kimataifa.

**v. Kuimarisha Maendeleo ya Ushirika (Strengthening Cooperative Development)**

a) Kuwezesha uwekezaji katika mifumo ya kidigiti kwenye Vyama vya Ushirika na Mamlaka za Usimamizi;
b) Kuimarisha usimamizi na udhibiti wa Vyama vya Ushirika;
c) Kuwezesha Vyama vya Ushirika kujiendesha kibiashara na kuvisaidia kupata mitaji; na
d) Kuhamasisha Ushirika kwenye Sekta mbalimbali na Makundi Maalum.

**vi. Kuimarisha Matumizi ya Mifumo ya TEHAMA katika Uendelezaji wa Sekta ya Kilimo (Agriculture Digitalization)**

a) Kuimarisha mifumo ya kidigiti itakayowezesha upatikanaji wa taarifa sahihi kwa wakati; na
b) Kuwekeza kwenye matumizi ya mifumo ya kidigiti katika Sekta ya Kilimo.

**KAZI ZITAKAZOTEKELEZWA KWA KUZINGATIA MIKAKATI YA VIPAUMBELE VYA MWAKA 2024/2025**

**5.1 Kuongeza Tija na Uzalishaji**

**5.1.1 Utafiti wa mbegu**

271. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia TARI katika mwaka 2024/2025 imepanga kuendelea na utafiti wa visumbufu vya mazao mbalimbali ikiwemo utafiti wa magonjwa, wadudu na minyoo fundo ya migomba (Sigatoka, mnyauko fusari, bungua wa migomba, fukusi wa migomba, minyoo ya migomba, virusi vya migomba) ili kupata aina za migomba yenye ukinzani wa visumbufu hivyo na mavuno mengi.
Vilevile, TARI itaendelea na utafiti wa ukinzani wa kutu jani (soybean rust) katika zao la soya na utafiti wa magonjwa ya virusi (cassava mosaic disease na cassava brown streak disease) katika zao la muhogo ili kupata mbegu zenye ukinzani na magonjwa hayo. Aidha, TARI itaendelea na utafiti wa magonjwa ya Cashew Leaf and Nut Blight, Ubwiri unga na mnyauko fusari katika zao la korosho ili kuongeza uzalishaji wa zao hilo.

272. ***Mheshimiwa Spika***, ili kupata aina bora za mbegu za soya zinazokidhi soko la kimataifa, TARI itaendelea na utafiti wa mbegu za soya zenye viwango vya protini na mafuta. Aidha, itaendelea na utafiti wa mbegu za ngano katika maeneo ya joto ili kupata

mbegu zinazostahimili hali ya joto kwa lengo la kuongeza uzalishaji na kukidhi mahitaji ya ngano nchini.

273. Kadhalika, TARI itafanya utafiti wa ladha ya mvinyo wa zabibu za hapa nchini na athari zinazotokana na matumizi ya mbolea za asili na za viwandani katika ladha ya mvinyo ili kuboresha na kupata ushindani katika soko la kimataifa. Pia, TARI itahaulisha teknolojia ya matumizi ya Rafiki Planter inayotumika katika upandaji wa mbegu za pamba ili iweze kutumika katika kupanda mazao ya ufuta, mtama na mahindi.

274. ***Mheshimiwa Spika,*** TARI itaendelea kukamilisha upatikanaji wa Ithibati ya Kimataifa ya Maabara ya Afya ya Udongo na Mimea iliyopo katika Wilaya ya Mufindi; kuanzisha shamba la vinasaba kwa kukusanya vinasaba vyote vya chai nchini kwa ajili ya utafiti; na kuanzisha mashamba mawili (2) ya mbegu kwa ajili ya utafiti wa aina bora za chai katika mikoa ya Iringa na Tanga.

275. ***Mheshimiwa Spika,*** TARI itaendelea na utafiti wa viwango, aina na mbinu za matumizi ya mbolea ya chokaa ili kuongeza uzalishaji wa mazao katika maeneo yaliyoathiriwa na tindikali nchini; itaendelea kukusanya taarifa za afya ya udongo na kuandaa kanzidata na ramani za kidigiti za udongo unaofaa kwa mazao mbalimbali nchini; na itaendelea na utafiti wa aina za wanga wa muhogo kwa ajili ya matumizi ya viwanda hapa nchini ili kupunguza uagizaji wa wanga kutoka nje ya nchi na kuimarisha soko la wakulima wa ndani.

276. ***Mheshimiwa Spika,*** TARI itafanya utafiti wa zao la pareto ili kupata aina za mbegu zenye sifa za mavuno mengi (kilo 1,500 hadi 2,300 kwa hekta), ubora wa maua (pyrethrum content, 1.9 – 2.2), na ukinzani wa ugonjwa wa mizizi (root rot), na itafanya uhaulishaji wa teknolojia zikiwemo mbegu bora za ngano (TARIwheat1 na TARIwheat2) zenye mavuno mengi, uhimilivu wa magonjwa na kiwango cha *protein* aina ya gluten kinachohitajika kwa uokaji; na teknolojia za mazao yaliyoongezewa virutubishi kibaiolojia kwenye maeneo yenye udumavu. TARI pia, itahaulisha teknolojia za zana za kilimo ikiwemo Rafiki *Planter*, matumizi ya chokaa, kitalu mkeka katika kuongeza ufanisi wa uzalishaji wa zao la mpunga.

277. Kadhalika, itaendelea kusafisha na kutunza aina 24 za mbegu za asili kwa mazao ya mpunga (11), maharage (4), mtama (3) na mbogamboga (6). Pia, TARI itafanya utafiti wa aina ya chai ya zambarau (purple tea) na ugonjwa unaokausha mashina ya chai na namna ya kudhibiti kuenea kwa vimelea vya *Armillaria mellea.* Aidha, TARI itazalisha na kusambaza pingili za muhogo 5,760,000 aina ya TARICASS4 zenye uwezo wa kuzalisha tani 40 hadi 60 kwa hekta kwa wakulima katika maeneo ya uzalishaji wa zao hilo ikiwemo mkoa wa Kigoma.

278. Vilevile, TARI kwa kushirikiana na *Indonesia Palm Oil Association* (IPOA) itakusanya vinasaba 11,400 vya chikichi ndani ya nchi na kutoka Indonesia kwa ajili ya kufanya utafiti na kupata aina za mbegu zenye mavuno mengi, wingi wa mafuta na ukinzani wa magonjwa. Pia, Kukusanya vinasaba (*germplasms*) 240 vya kakao na kuanzisha mashamba ya kutunza vinasaba katika Mkoa wa Morogoro. Pia, itawajengea uwezo watafiti sita (6) wa TARI kuhusu kilimo bora cha chikichi katika nchi ya Indonesia.

279. ***Mheshimiwa Spika,*** TARI itazalisha tani 1,518 za mbegu za mazao ya nafaka, jamii ya mikunde, mafuta na mbogamboga. Kati ya hizo tani 28 ni mbegu mama, tani 280 ni mbegu za awali na tani 800 mbegu za msingi. Vilevile, itazalisha tani 420 za mbegu zilizothibitishwa za mazao hayo. Pia, mbegu za awali na msingi zitasambazwa kwa ASA na Sekta binafsi kwa ajili ya kuzalisha mbegu zilizothibitishwa.

280. Vilevile, TARI itazalisha mbegu za awali za pamba tani 30 ambazo zitazalisha tani 370 za mbegu za msingi zitakazozalisha tani 17,000 hadi 20,000 za mbegu zilizothibitishwa kwa ajili ya wakulima wa pamba nchini.

281. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na changamoto za athari za chumvi kwenye udongo, Wizara kupitia TARI itazalisha mbegu za awali za mpunga tani 2 (SATO1 tani 1 na SATO9 tani 1) zinazostahimili athari hizo katika mikoa ya Iringa, Kilimanjaro, Tanga, Mbeya, Shinyanga na Katavi. Mbegu hizo zina uwezo wa kuzalisha mbegu za msingi tani 120 ambazo zitazalisha tani 7,200 za mbegu zilizothibitishwa ambazo zitatosheleza kupandwa kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta 2,400.

282. ***Mheshimiwa Spika,*** TARI itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya utafiti wa mbegu ulioanza katika mwaka 2022/2023 na mwaka 2023/2024 yenye jumla ya hekta 1,120.9. Mashamba hayo ni TARI Hombolo (hekta 70), TARI Kihinga (hekta 150), TARI Ilonga (hekta 200), Selian (hekta 120), Uyole (hekta 120), Kifyulilo (hekta 20), Seatondale (hekta 6.5), Kibaha (hekta 20), Maruku (hekta 32), Tengeru (hekta 50), Dakawa (hekta 50), Ifakara (hekta 36.4), Tumbi (hekta 60), Bagamoyo (hekta 20), Mlingano (hekta 20), Mkuranga (hekta 40), Naliendele (hekta 37), Ukiriguru (hekta 47) na Isimani (hekta 22).

283. Vilevile, TARI itaanza ujenzi wa miundombinu mipya ya umwagiliaji yenye ukubwa wa hekta 1,000 katika mashamba ya utafiti ya TARI Ilonga (hekta 150), Kihinga (hekta 100), Tumbi (hekta 100), Ukiriguru (hekta 250), Dakawa (hekta 100), Ifakara (hekta 100) na Uyole (hekta 200). Aidha, TARI itajenga kituo cha Sayansi za Kibaolojia (Bioscience) katika kituo cha TARI – Mikocheni (Mkuranga) kwa ajili ya kutoa huduma za kisasa za kisayansi katika utafiti wa mbegu, wadudu, magonjwa, uhimilivu wa tabianchi, udongo, uhandisi wa kibaolojia (bioengineering) na kanzi data za taarifa za kibaolojia (bioinformatics).

284. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha uhifadhi wa mbegu, kuendeleza na kuwa na msingi mkuu wa utafiti na usalama wa nchi, TARI itajenga Benki ya mbegu (Gene Bank) katika kituo cha TARI Selian. Vilevile, TARI itaendelea na ujenzi wa maabara ya kuzalisha miche ya migomba kwa njia ya chupa katika kituo cha TARI – Maruku ili kuongeza uwezo wa kuzalisha miche bora ya migomba na kukabiliana na visumbufu vya zao hilo kama fungashada ya migomba (Banana Bunchy Top Disease – BBTD); na ujenzi wa maabara ya patholojia ya TARI – Naliendele kwa ajili ya utafiti wa magonjwa ya mazao. Vilevile, Wizara itakarabati kituo cha TARI – Tengeru na kukifanya kuwa kituo mahiri cha utafiti na uzalishaji wa mbegu za mazao ya bustani.

285. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kulinda uvamizi wa mashamba ya utafiti TARI itaanza ujenzi wa uzio katika mashamba ya utafiti ya vituo vya TARI Mlingano, Tumbi, Tengeru, Mikocheni (Mkuranga na Bagamoyo) Ilonga na Ukiriguru. Vilevile, itaendelea na ujenzi wa uzio ulioanza mwaka 2022/2023 na 2023/2024 katika vituo vya utafiti

vya TARI Uyole (hekta), Kifyulilo (hekta), Hombolo (hekta), Maruku (hekta), Kihinga, Dakawa na Ifakara. Aidha, TARI italipa fidia kwa wananchi katika shamba la Uyole ili kupisha ujenzi wa uzio.

286. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TARI itaendelea na ujenzi wa ghala 11 zenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani 4,565 za mbegu ulionza mwaka 2022/2023 na 2023/2024 katika vituo vya utafiti vya TARI Uyole, Ilonga, Ukiriguru, Maruku, Ifakara, Kihinga, Naliendele, Tumbi, Selian, Hombolo na Dakawa; na kukamilisha upatikanaji wa ithibati kwa maabara ya udongo ya TARI Mlingano itakayotumika kupima afya ya udongo na kupunguza gharama za kupima udongo nje ya nchi. Vilevile, TARI itanunua vifaa na kuwapatia mafunzo wataalam wa maabara za kuzalisha miche kwa njia ya chupa na udongo za TARI Mlingano ili kuimarisha upimaji wa afya ya udongo kutoka wastani wa sampuli 5,000 hadi sampuli 20,000 kwa mwaka na kuongeza uzalishaji wa miche ya mkonge kutoka miche 500,000 hadi miche 10,000,000 kwa mwaka.

287. Wizara kupitia kituo cha utafiti wa Tumbaku, itazalisha kilo 300 za mbegu za tumbaku ya mvuke aina ya K326; itafanya utafiti wa utambuzi na kuthibitisha hali ya udongo unaozalisha tumbaku; na itakarabati maabara ya utafiti wa zao la tumbaku iliyopo Tumbi katika mkoa wa Tabora.

288. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TARI itazalisha mbegu bora za kahawa tani 9.8 zikiwemo tani 6.5 za arabika na tani 3.3 za robusta. Mbegu hizo zitazalisha miche 20,000,000 ya kahawa itakayosambazwa kwa mpango wa ruzuku kwa wakulima katika mikoa 17 inayozalisha kahawa.

289. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwenye tasnia ya kahawa, Wizara kupitia TARI itaendelea na tafiti za kubaini aina za kahawa zenye tija kubwa, ukinzani wa visumbufu vya mmea wa kahawa, muonjo (cup quality) na ustahimilivu wa ukame. Pia, TARI itaendelea na tafiti za kanuni bora za kilimo cha kahawa ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Wizara kupitia TARI itaendelea na ujenzi wa nyumba nne (4) za watumishi, jiko, hosteli, uzio na kuchimba kisima katika Kituo cha Utafiti wa Kahawa cha Mwayaya (Buhigwe).

### 5.1.2 Uzalishaji na usambazaji wa mbegu na miche bora na kutoa ruzuku ya mbegu na miche bora kwa baadhi ya mazao

290. ***Mheshimiwa Spika***, mahitaji ya mbegu bora kwa mwaka ni tani 127,650. Katika mwaka 2024/2025, upatikanaji wa mbegu bora nchini unatarajiwa kuwa tani 80,000 zikihusisha tani 8,568 za mbegu zitakazozalishwa na ASA na tani 71,432 zitazalishwa na Sekta binafsi. Kati ya tani 8,568 zitakazozalishwa na ASA, tani 2,412 (alizeti), tani 1,500 (ngano), tani 200 (soya), tani 2,500 (mahindi), tani 1,200 (mpunga), tani 120 (maharage), tani 400 (mtama), tani 150 (ufuta), tani 50 (choroko), tani 30 (fiwi) na tani 6 (mbogamboga).

291. Ili kufikia lengo la upatikanaji wa mbegu bora, ASA itaendelea kuwapatia Sekta binafsi mashamba yenye ukubwa wa hekta 4,914 kwa ajili ya kuzalisha mbegu za mazao. Kadhalika, ASA itaendelea na marekebisho ya tindikali ya udongo kwa kuweka chokaa katika mashamba matano ya mbegu ya Msimba (hekta 2,000), Dabaga (hekta 970), Kilimi (hekta 864.5), Mbozi (hekta 260) na Kilangali (hekta 1,000).

292. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuimarisha uzalishaji wa mbegu bora kwa mwaka mzima ASA itaendelea kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya uzalishaji wa mbegu bora ulioanza katika mwaka 2022/2023 yenye ukubwa wa hekta 580 kati ya hekta 805.5 katika mashamba ya Msimba (hekta 200), Arusha (hekta 200) na Kilimi (hekta 180); na kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya uzalishaji wa mbegu bora ulioanza katika mwaka 2023/2024 yenye ukubwa wa hekta 795 katika mashamba ya Namtumbo (hekta 300), Msimba (hekta 195), Mbozi (hekta 100), Arusha (hekta 100) na Kilimi (hekta 100). Vilevile, ASA itaendelea kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya mbegu yenye jumla ya hekta 3,000 katika mashamba ya Namtumbo (hekta 900), Msimba (hekta 800), Mwele (hekta 500), Msungura (hekta 100), Mbozi (hekta 500) na Kilimi (hekta 200).

293. Vilevile, ASA itaanza ujenzi wa miundombinu mipya ya umwagiliaji katika maeneo yenye jumla ya hekta 800 katika mashamba ya mbegu ya Mwele (hekta 300), Namtumbo (hekta 300), Msungura (hekta 100) na Bugaga (hekta 100); kuanza ujenzi

wa uzio katika mashamba ya mbegu ya Arusha (hekta 600), Kilangali (hekta 1,200), Namtumbo (hekta 3,580.4) na Mwele (hekta 874) ili kuzuia uvamizi wa mashamba hayo; kujenga miundombinu minne (4) ya kukausha na kuhifadhi mbegu katika mashamba ya mbegu ya Arusha, Kilimi, Msungura na Namtumbo; na kujenga ghala moja (1), karakana moja (1) na ofisi moja (1) katika shamba la Kilimi na kukarabati karakana moja (1) katika shamba la Msimba.

294. Ili kuboresha mazingira ya watumishi, ASA itajenga na kukarabati nyumba 49 za watumishi katika mashamba ya mbegu ya Mwele, Kilimi, Msimba, Kilangali, Namtumbo, Mbozi, Arusha, Luhafwe na Msungura.

295. ***Mheshimiwa Spika,*** ASA itanunua vitendea kazi ikiwemo matrekta matatu (3), magari madogo mawili (2), malori matatu (3), mtambo wa kuvunia mbegu (combine harvester), pikipiki mbili (2) na mitambo miwili (2) ya kuchakata mbegu.

296. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Wizara kupitia Bodi za mazao, Wakala na Taasisi zake kwa kushirikiana na Sekta binafsi itazalisha na kusambaza jumla ya miche 47,500,000 ya mazao mbalimbali ikiwemo miche ya kahawa (20,000,000), korosho (1,000,000), zabibu (500,000), minazi (10,000,000), migomba (2,000,000), parachichi (6,000,000), chikichi (2,000,000), chai (3,000,000) na mkonge (3,000,000). Pia, itazalisha na kusambaza pingili za muhogo 6,290,000 na vipando vya viazi vitamu 450,000 katika maeneo ya uzalishaji wa mazao hayo.

297. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia TOSCI itaendelea kusimamia na kuthibiti ubora wa mbegu zinazozalishwa nchini na zinazoagizwa nje ya nchi ambapo katika mwaka 2024/2025 itaongeza idadi ya mbegu zinathibitishwa ubora kutoka tani 63,424 mwaka 2023/2024 hadi tani 80,000. Vilevile, TOSCI itakagua mashamba ya mbegu yenye ukubwa wa hekta 55,285 ili kuhakiki vigezo vinavyohitajika katika uzalishaji wa mbegu bora.

298. Ili kuhakikisha mbegu zinazouzwa nchini zinakidhi ubora, TOSCI itachukua sampuli 4,185 za mbegu kwa ajili ya vipimo vya maabara; kukagua maduka ya mbegu 2,420 na ghala 130 za kuhifadhi mbegu ili kuimarisha uthibiti wa mbegu bora kwa

kuzingatia Sheria na Kanuni za Mbegu. Aidha, wafanyabiashara wote watakaokutwa na makosa hayo, watachukuliwa hatua za kisheria ikiwemo kufutiwa usajili wao kama wafanyabiashara wa mbegu.

299. ***Mheshimiwa Spika***, TOSCI itasajili wazalishaji wa miche ya parachichi nchini ili kuwezesha ufuatiliaji, usimamizi na uthibiti ubora wa miche ya parachichi inayozalishwa; na kusajili kampuni 30 kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa mbegu bora nchini na wafanyabiashara 500 kwa ajili ya kuuza mbegu bora. Aidha, TOSCI itatoa lebo 32,000,000 za mbegu bora na kutoa mafunzo kwa wakaguzi wa mbegu 50 na wakaguzi wa mbegu walioidhinishwa (ASI's) 40 katika mikoa 25 ya Tanzania Bara. Ili kuwezesha upatikanaji wa lebo kwa wakati, TOSCI itanunua mitambo miwili (2) ya kuchapisha lebo zinazotumika katika vifungashio vya mbegu.

300. Vilevile, TOSCI itafanya majaribio ya utambuzi wa aina mpya za mbegu (DUS tests) kwa aina 150 za mbegu na majaribio ya kitaifa ya umahiri wa aina mpya za mbegu (NPT) kwa aina 50 za mbegu ili kuimarisha uthibiti wa ubora wa mbegu nchini. Pia, TOSCI itafanya majaribio ya uhalisia wa mbegu zilizopo katika uzalishaji (Control plot testing) kwa sampuli za mazao 250 ili kuhakiki kama mbegu husika inaendelea kutunza uhalisia wake.

301. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kusimamia udhibiti wa upandishaji holela wa bei za mbegu za mazao ya kilimo, Wizara itaweka utaratibu wa kikanuni wa kusimamia bei ya mbegu na kutangaza bei elekezi tarehe 01 Septemba ya kila mwaka.

### 5.1.3 Uwekezaji kwenye utoaji wa ruzuku ya mbolea na viuatilifu

**Upatikanaji wa mbolea**

302. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2024/2025 itaendelea kutoa ruzuku ya mbolea na viuatilifu kupitia mpango wa ruzuku kwa mazao yote. Hivyo, kupitia TFRA, Serikali itaratibu uingizwaji wa tani 1,086,115 za mbolea na kuzisambaza kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku utakaoendelea hadi mwaka 2025/2026; itakamilisha vigezo muhimu katika mfumo wa usajili wa wakulima; na itasajili wakulima, waagizaji na wasambazaji wa mbolea katika mfumo wa kielektroniki kwa lengo la kuimarisha usambazaji wa mbolea nchini.

303. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, TFC itanunua tani 100,000 za mbolea na kusambaza kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku. Vilevile, itajenga kiwanda cha kuchanganya mbolea (Bulk Blending Facilities) kwa kushirikiana na Kampuni ya Serikali ya Morocco (OCP Group Africa) ambacho kitachanganya mbolea kwa kuzingatia afya ya udongo ya eneo husika. Aidha, kiwanda hicho kinatarajiwa kuwa na uwezo wa kuchanganya tani 120 za mbolea kwa saa.

304. Kadhalika, itanunua magari matano (5) yenye uwezo wa kubeba tani 15 kila gari kwa ajili ya kuwezesha usambazaji wa mbolea na kukarabati ghala saba (7) zenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani 100,000 katika mikoa ya Mwanza, Tabora, Ruvuma, Rukwa, Njombe, Mbeya na Mtwara kwa ajili ya uhifadhi wa mbolea.

305. ***Mheshimiwa Spika,*** TFC itaingia Makubaliano na kiwanda cha *Tanzania Biotech Products Limited* (TBPL) ambayo ni kampuni tanzu iliyochini ya Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) kwa ajili ya kuanza kuzalisha na kusambaza mbolea zisizo na kemikali (Bio- fertilizers) zinazozalishwa kwa kushirikiana na wataalamu kutoka nchini Cuba. Vilevile, TFC itaunda mfumo wa kidijiti (ICT) kwa kushirikiana na Taasisi ya Serikali Mtandao kwa ajili kusimamia na kuhakiki mauzo ya mbolea na viuatilifu katika vituo vya mauzo na mawakala. Mfumo huo utafungwa katika ghala/vituo vya mauzo ya mbolea.

306. Kadhalika, ili kuhakikisha mauzo ya mbolea yanakusanywa ipasavyo, Wizara itaiwezesha TFC kununua *Point of Sale* (POS) 40 ambazo zitasambazwa kwenye vituo vya mauzo vya TFC ili kurahisisha ukusanyaji wa mapato na ufuatiliaji wa maduhuli.

**Upatikanaji wa Viuatilifu na Udhibiti wa Visumbufu vya mazao na mimea**

307. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TPHPA itanunua na kusambaza lita 95,000 za viuatilifu zikiwemo lita 10,000 za Fenthion 60% ULV kwa ajili ya kudhibiti ndege waharibifu wa mazao aina ya kwelea kwelea, lita 4,000 za Fenitrothion 96% ULV kudhibiti Nzige, lita 77,000 na Sulphur 80 Wg za Profenofos + Emamectin Benzoate, Imidacloprid+ cypermethrin kudhibiti viwavijeshi vamizi, lita 1,500 za

Bromadiolone kudhibiti panya na lita 2,500 za Methyl Eugenol 98% kudhibiti inzi wa matunda na kilo 1,000 za Mancozeb+metalax kwa ajili ya kudhibiti visumbufu vya parachichi. Vilevile, TPHPA itaendelea kuimarisha kituo cha Kilimo Anga cha udhibiti wa visumbufu vya mimea na mazao kwa kununua vitendea kazi ambavyo ni magari saba (7) na ndege nyuki 20.

308. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TPHPA katika mwaka 2024/2025, itaimarisha matumizi ya njia za kibaolojia kwa kuzalisha wadudu rafiki na kusajili viuatilifu hai kwa ajili ya udhibiti wa wadudu waharibifu wa mazao kama njia mbadala ya matumizi ya viuatilifu vya viwandani. Vilevile, TPHPA itanunua vifaa vya maabara ya karantini ya Taifa ya mimea na maabara ya uchambuzi wa viuatilifu zilizopo katika mkoa wa Arusha na kukarabati ofisi mbili (2) za kanda (Kurasini na Tengeru) na kununua maeneo matatu (3) kwa ajili ya kujenga ofisi katika mikoa ya Njombe, Mtwara na Tabora. Aidha, itajenga ofisi pamoja na maabara ndogo 12 kwenye vituo vya ukaguzi mipakani ili kuwezesha biashara ya mazao kimataifa na kudhibiti kuingia kwa visumbufu hatarishi vya mimea na mazao.

309. Vilevile, TPHPA itakagua vifaa vya kunyunyizia viuatilifu katika maduka ya pembejeo za kilimo; itaimarisha usajili wa miundo mipya ya vifaa vya kunyunyizia viuatilifu na ufuatiliaji wa athari za viuatilifu kwa binadamu na mazingira. Aidha, TPHPA itaendelea kuimarisha ukusanyaji, uhifadhi na utumiaji wa rasilimali za kijenetiki za mimea; kuimarisha usimamizi na uratibu wa kudhibiti milipuko ya visumbufu vya mimea; na kuimarisha kituo cha ufuatiliaji wa magonjwa (BBTD observatory system) ili kudhibiti visumbufu vya mimea na mazao kwa wakati.

310. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TPHPA kwa mwaka 2024/2025 itaendelea kupima masalia ya mabaki ya viuatilifu katika mazao ya bustani na nafaka (mahindi). Lengo ni kutengeneza kanzidata ya mabaki ya viuatilifu katika mazao ya bustani na nafaka itakayotumika kushauri mbinu za kuboresha matumizi ya viuatilifu na kuwezesha upatikanaji wa masoko ya mazao husika nje ya nchi.

311. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TPHPA kwa mwaka 2024/2025 itakagua maduka 4,000 ya viuatilifu nchini ili kudhibiti ukiukwaji wa Sheria Na.4 ya Afya ya Mimea ya Mwaka 2020 na kukabiliana na uwepo wa viuatilifu bandia na chakavu nchini; na itatoa mafunzo ya matumizi sahihi ya Viuatilifu na Afya ya Mimea kwa wakulima 4000, wafanyabiashara 500 kwa ajili ya kupunguza athari za viuatilifu kwenye afya ya binadamu na mazingira na kuongeza tija katika kilimo.

**5.1.4 Usajili wa Wakulima na Urasimishaji wa Shughuli za Kilimo**

312. ***Mheshimiwa Spika,*** suala la utambuzi wa mkulima haliwezi kukamilika bila kupima ardhi yake na kuhakikisha ardhi hiyo inapata hati za hakimiliki. Katika mwaka 2024/2025, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi itaanza kupima ardhi ya wakulima wadogo 2,000 na kuhakikisha wanapatiwa hati za hakimiliki bila gharama yoyote ikiwa ni sehemu ya urasimishaji. Programu hiyo itaanza katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

313. Aidha, Wizara itaendelea kusajili wadau wa kilimo wakiwemo wafanyabiashara wa mazao ya kilimo na watoa huduma za ugani, ghala, bima ya mazao na pembejeo za kilimo ili kuweka utaratibu wa kisheria utakaosimamia shughuli zote za wadau hao.

**5.1.5 Kuwekeza kwenye ujuzi kwa wataalam wa ndani**

314. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kuwajengea uwezo wataalamu wa Wizara na Taasisi zilizopo chini yake kwa lengo la kuwawezesha wataalam hao kuendana na teknolojia na maendeleo ya kisasa katika kilimo, kuongeza ujuzi na maarifa na hivyo kuleta ufanisi katika utendaji hususan kutatua changamoto za wakulima na kuongeza tija na uzalishaji.

315. Katika mwaka 2024/2025, Wizara imepanga kuwawezesha jumla ya wataalam 485 kupata mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi. Kati ya hao Shahada ya Uzamivu (33), Shahada ya Uzamili (124), Shahada (52), Stashahada (1) na mafunzo ya ujuzi maalum (275). Lengo la mafunzo hayo ni kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ikiwemo kuhaulisha teknolojia na kutoa mafunzo kwa wakulima.

### 5.1.6 Uwekezaji kwenye Huduma za Ugani

316. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara katika mwaka 2024/2025, itaendelea kuimarisha huduma za ugani kwa kuendelea kununua na kusambaza vitendea kazi kwa Maafisa Ugani ikiwemo pikipiki 600, vipima afya ya udongo 43, magari na kuendelea kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji wa vitendea kazi wanavyogawiwa maafisa ugani katika Halmashauri mbalimbali; kuimarisha utoaji wa huduma za ugani kupitia mfumo wa M-Kilimo kwa kuunganisha mfumo huo na mfumo wa usajili wa wakulima.

317. Vilevile, itaendelea na ujenzi wa miundombinu kwenye viwanja vya maonesho ya wakulima ya Nanenane katika viwanja vya Nzuguni (Dodoma) na John Mwakangale (Mbeya) ili kuvifanya viwanja hivyo kuwa endelevu na hadhi ya kimataifa; kuendelea kujenga nyumba 50 za Maafisa Ugani; na kujenga na kukarabati vituo vitano (5) vya rasilimali za kilimo vya Kata (Ward Resource Centres - WARCs) katika mikoa ya Singida, Dodoma na Iringa.

318. Kadhalika, TARI itaimarisha vituo nane (8) mahiri vya usambazaji wa teknolojia (AgriTech Hubs) katika viwanja vya maonesho ya kilimo Nanenane kwa kuweka miundombinu ya umwagiliaji ili kuwezesha shughuli za kilimo na mafunzo ya kilimo kwa wakulima kufanyika mwaka mzima.

319. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kununua magari kwa ajili ya Maafisa ugani ngazi ya Mkoa na Halmashauri ili kurahisisha utekelezaji wa shughuli za kilimo.

***Mafunzo ya Kilimo***

320. ***Mheshimiwa Spika***, kwa muda mrefu Wizara imekuwa ikigharamia mafunzo ya kilimo kuanzia ngazi ya Astashahada ya Awali, Astashahada na Stashahada katika Vyuo vya Mafunzo ya Kilimo (MATI). Katika mwaka 2024/2025, Wizara itaanza kufanya mabadiliko ya mfumo wa utoaji wa mafunzo katika Vyuo vya Mafunzo ya Kilimo (MATI) kwa kutoa mafunzo ya kilimo biashara kwa wakulima viongozi kulingana na ikolojia ya mazao. Wakulima hao watatoa mafunzo kwa wakulima wenzao ili kuongeza upatikanaji wa huduma za ugani kwa wakulima. Aidha, jukumu la kutoa mafunzo ngazi ya Astashahada ya Awali, Astashahada na

Stashahada litabaki kuwa chini ya Wizara yenye dhamana na masuala ya Elimu.

***"Mwalimu Nyerere alipoanzisha vituo vya utafiti wa kilimo, pembeni mwa vituo hivyo alianzisha vyuo vya mafunzo ya kilimo ambapo msingi wake mkubwa ulikuwa ni kuwafundisha wakulima teknolojia zinazopatikana katika vituo vya utafiti"***

321. Aidha, wanafunzi ambao wamedahiliwa katika mwaka wa masomo 2023/2024 na wanaendelea na masomo katika Vyuo hivyo ngazi ya Astashahada na Stashahada wataendelea na masomo yao hadi watakapohitimu. Pia, Vyuo na vituo vitatumika kutoa mafunzo rejea kwa Maafisa ugani ili kuendana na teknolojia na mbinu za kisasa.

*"**Hatutadahili wanafunzi wengine wa Astashahada na Stashahada, jukumu hili litabaki kusimamiwa na Wizara yenye dhamana na masuala ya Elimu na Wizara yetu itabaki na jukumu la utafiti na kuhaulisha teknolojia hizo kwa wakulima kupitia vyuo vya MATI**"*

322. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara itaandaa Mkakati wa Mafunzo kwa Wakulima (Farmers' Training Strategy) ili kuhakikisha teknolojia zinazogunduliwa na watafiti zinawafikia wakulima kwa njia ya mafunzo kupitia vyuo na vituo vyake vya mafunzo ya kilimo. Pia, itaandaa na kutekeleza program za uhaulishaji wa teknolojia zinazogunduliwa na watafiti wa kilimo ambapo wakulima 5,000 watanufaika.

323. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara itaendelea kutoa mafunzo ya kilimo biashara kwa kuzingatia ikolojia ya kilimo kwa vijana 1,000 kupitia programu ya BBT katika vyuo na vituo vya mafunzo ya kilimo. Kadhalika, ili kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia, Wizara itaendelea kukarabati miundombinu katika vyuo na vituo vya mafunzo ya kilimo vya KATRIN, Inyala, Igurusi, Mtwara, Mlingano, HORTI Tengeru, Maruku, Mubondo, Bihawana FTC, Ichenga FTC na Mkindo FTC

**5.1.7 Kupima Afya ya Udongo kwa wakulima wadogo na wakubwa**

324. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara itapima afya ya udongo katika maeneo mapya ya uwekezaji yatakayoainishwa katika mikoa ya Simiyu, Mara, Geita, Tabora, Songwe na Tanga kwa kuhusisha maeneo kwa ajili ya vijana na wanawake kupitia Programu ya BBT;

kuendelea kutoa huduma ya kupima afya ya udongo kwa wakulima wakubwa na wadogo bure kwa kutumia vifaa vya kupima afya ya udongo vilivyosambazwa katika Halmashauri; na itabuni na kuhamasisha matumizi ya teknolojia sahihi za utunzaji wa maji na udongo mashambani ili kulinda vyanzo vya maji kwa ajili ya umwagiliaji katika mikoa ya Morogoro, Iringa na Mbeya. Vilevile, Wizara itanunua *mobile soil laboratory van* kwa ajili ya kupima afya ya udongo.

325. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara itakamilisha upimaji wa afya udongo katika mikoa nane (8) iliyobaki kati ya 26 ya Tanzania bara ya Mtwara, Lindi, Pwani, Tanga, Ruvuma, Kigoma, Tabora na Dar es Salaam ili kuandaa ramani inayoonesha afya ya udongo kwa kila mkoa itakayosaidia shughuli za matumizi ya teknolojia sahihi katika maeneo ya uzalishaji.

**5.1.8 Uendelezaji wa kilimo cha umwagiliaji**

326. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji katika mwaka 2024/2025 itaendelea na utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji 780 iliyoanza kutekelezwa mwaka 2022/2023 na 2023/2024 kama ifuatavyo:-

i. Kukamilisha utekelezaji wa miradi 69 ya ujenzi na ukarabati ambayo ilianza mwaka 2022/2023 inayojumuisha ujenzi wa mabwawa 14 yenye mita za ujazo milioni 131.5; ujenzi wa skimu mpya 25 zenye jumla ya hekta 53,234; na ukarabati wa skimu 30 zenye jumla ya hekta 41,771. Aidha, itakamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa skimu 28 kati ya 42 na mabonde ya kimkakati 17 kati 22 yaliyopangwa mwaka 2022/2023;

ii. Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji 647 ambayo ilianza kutekelezwa mwaka 2023/2024. Miradi hiyo ni:-
    a) Ujenzi wa skimu mpya 28 zenye jumla ya hekta 69,505;
    b) Ukarabati wa skimu 18 zenye jumla ya hekta 40,497;
    c) Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya pamoja (Block farms) sita (6) yenye jumla ya hekta 79,518.46;
    d) Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mabonde 22 ya kimkakati;

e) Usanifu na ujenzi wa mabwawa 100 ya kuvunia maji kwa ajili ya umwagiliaji;
f) Kufanya mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati wa skimu 255 zenye ukubwa wa hekta 290,095; na
g) Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa skimu mpya 240. Aidha, ujenzi wa skimu hizo utafanyika baada ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

327. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itafanya ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji katika skimu 33 zenye jumla ya hekta 6,089 zitakazonufaisha wakulima 4,693 kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na.13**. Pia, Tume itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mabonde ya kimkakati yenye takribani hekta 255,181.

328. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha upatikanaji wa maji ya umwagiliaji kwenye maeneo yasiyopata mvua za kutosha, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa kutumia maji ya ziwa Victoria (mikoa ya Simiyu, Shinyanga, Tabora na Singida) na ziwa Tanganyika (mikoa ya Kigoma na Katavi) kwa ajili ya shughuli za kilimo ili kuongeza tija na uzalishaji. Vilevile, Wizara inakamilisha tathmini ya uwezekano wa kutumia maji kutoka kwenye maziwa hayo kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji hususan katika maeneo yaliyo pembezoni na maziwa.

329. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa bonde la mto Ngono na Bugwema umekamilika na sasa hatua za kumtafuta mkandarasi kwa ajili ya ujenzi zinaendelea. Vilevile, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itakamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa bonde la Mto Rufiji ambapo katika mwaka 2024/2025 itaanza ujenzi wa mabwawa mawili (2) ya Mbakiamtuli na Ngorongo. Ujenzi huo utakamilika kwa kipindi cha miaka mitatu (3). Vilevile, Tume kwa kushirikiana na Shirika la Reli Tanzania itafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa sita (6) ya Dabalo, Buigiri, Hombolo, Kimagae, Kidete na Ikowa. Mabwawa

hayo yatatumika kuzuia mafuriko katika reli ya kati na kutumika kwa shughuli za kilimo cha umwagiliaji.

330. ***Mheshimiwa Spika,*** kukamilika kwa miradi ya ujenzi inayoendelea kutekelezwa na itakayoanza kujengwa mwaka 2024/2025 kutaongeza eneo la umwagiliaji kwa hekta 543,366.46 na kufanya eneo linalomwagiliwa kufikia hekta 1,270,647.06 ambayo ni sawa na asilimia 105.89 ya lengo la kufikisha hekta 1,200,000 ifikapo mwaka 2025 kama inavyoelekezwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020. Aidha, eneo litakaloongezeka litatengeneza ajira takribani 2,173,466 zitokanazo na uwekezaji katika kilimo cha umwagiliaji.

331. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2024/2025, Tume imepanga kuanza ujenzi wa ofisi 19 na ukarabati wa ofisi sita (6) za Umwagiliaji za Mikoa. Ujenzi wa ofisi hizo unalenga kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa watumishi na kusogeza huduma kwa wadau. Aidha, Tume imepanga kununua magari 13 na pikipiki 477 kwa ajili kuimarisha usimamizi wa shughuli mbalimbali za umwagiliaji katika ofisi za Wilaya. Vilevile Tume imepanga kununua mitambo ya kuchimba visima ambapo katika mwaka 2024/2025 itaanza na ununuzi wa mitambo 30. Mitambo hiyo itatumika katika uchimbaji wa visima katika Halmashauri mbalimbali nchini. Pia, Tume itanunua mitambo mitatu (3) kwa ajili ya uchimbaji wa mabwawa ya umwagiliaji.

332. Vilevile, ili kuhakikikisha miundombinu ya umwagiliaji inakuwa endelevu na kuleta tija iliyokusudiwa, Tume itatoa mafunzo ya uendeshaji na matunzo ya miundombinu ya umwagiliaji pamoja na ukusanyaji wa ada ya huduma za umwagiliaji kwa wakulima viongozi 10,000 katika skimu 1,230. Aidha, Tume itasajili vyama vipya vya umwagiliaji 500, kusimamia na kufanya ufuatiliaji wa vyama vilivyosajiliwa kupitia mfumo wa kielekroniki wa NIRCiMIS na POS.

333. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua changamoto inayowakabili wakulima katika bonde la Mbarali na kufuatia maelekezo ya Mheshimiwa Rais, Wizara itakamilisha mazungumzo na mwekezaji wa Mbarali Estates wa Kampuni ya *Highland Estates* kwa ajili ya Serikali kuchukua shamba moja na kumlipa haki zake zote na kulifanya shamba hilo kuwa sehemu ya wakulima wadogo

waliohamishwa katika maeneo ya vyanzo vya maji. Sambamba na hilo Serikali itajenga mabwawa matano (5) kwa ajili ya kuwahudumia wakulima hao.

### 5.1.9 Uanzishaji wa Vituo Jumuishi vya Kutoa Huduma za Zana za Kilimo

334. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2024/2025 itaanzisha vituo 10 vya kuhifadhi na kutoa huduma ya zana za kilimo kwa wakulima katika mikoa ya Dodoma, Njombe, Rukwa, Mwanza, Mara, Iringa, Katavi, Singida, Manyara na Mbeya; na kuendelea kuhamasisha watoa huduma ya zana za kilimo kuwekeza kwenye mashamba makubwa ya pamoja yatakayoanzishwa kupitia Programu ya BBT katika mikoa ya Dodoma, Njombe, Mbeya, Kagera, Kigoma, Shinyanga, Singida na Pwani.

### Uzalishaji wa Mazao kwa Mwaka 2024/2025

335. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara katika mwaka 2024/2025 itaendelea kusimamia mikakati ya kuongeza uzalishaji na tija kwa mazao mbalimbali yakiwemo mazao asilia ya biashara, mazao ya bustani, mazao ya chakula, mazao ya mafuta na mazao yenye mahitaji makubwa.

### Mazao Asilia ya Biashara

336. ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa mazao asilia ya biashara yakiwemo pamba, kahawa, mkonge, korosho, tumbaku, pareto, sukari na chai unatarajiwa kuongezeka kutoka tani **1,260,321.1** mwaka 2023/2024 hadi tani **2,030,000** mwaka 2024/2025 kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 11**.

**Jedwali Na. 11:** Matarajio ya Uzalishaji wa Mazao Asilia ya Biashara (Tani) katika Mwaka 2024/2025

| Na. | MAZAO | 2023/2024 | 2024/2025 |
|---|---|---|---|
| 1 | Korosho | 254,500 | 595,000 |
| 2 | Pamba | 282,510 | 500,000 |
| 3 | Pareto | 4,238 | 5,000 |
| 4 | Kahawa | 66,071 | 85,000 |
| 5 | Tumbaku | 178,521 | 200,000 |
| 6 | Chai | 13,525 | 30,000 |
| 7 | Mkonge | 56,732.7 | 80,000 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 8 | Sukari | 392,724 | 520,000 |
| 9 | Kakao | 11,499.4 | 15,000 |
| **JUMLA** | | **1,260,321.1** | **2,030,000** |

**Chanzo:** *Wizara ya Kilimo, 2024* **Zao la Pamba**

337. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Bodi ya Pamba Tanzania katika msimu wa kilimo wa 2024/2025 imepanga kuongeza uzalishaji wa pamba kutoka tani 282,510 msimu wa 2023/2024 hadi tani 500,000 na kuongeza ubora wa pamba kutoka asilimia 44.3 hadi asilimia 75 kwa madaraja ya juu. Lengo hilo litafikiwa kwa kununua, kuchakata na kusambaza mbegu bora za pamba tani 28,000, chupa (acrepacks) 7,000,000 na vinyunyizi 100,000 kwa wakulima wa pamba.

338. Kadhalika, Bodi itanunua ndege nyuki 40 na mitambo mikubwa ya kunyunyizia viuadudu (high pressure boom sprayers) 3,000, itanunua jozi nyingine ya mitambo ya kuchimba mabwawa ya umwagiliaji ambayo itakuwa na *buldozer* moja (1), *excavator* moja (1), *wheel loder* moja (1), *driller* moja (1) na *motor grader* moja (1). Vilevile, itanunua na kusimika mitambo ya kuongeza thamani katika zao la pamba katika AMCOS kwenye vijiji vyenye uzalishaji mkubwa wa pamba. Baadhi ya mitambo itakayonunuliwa na kusimikwa ni mitambo miwili (2) ya kuzalisha nishati ya kupikia inayotokana na masalia ya miche ya pamba, mitambo nane (8) ya kusokota nyuzi za pamba na kuzalisha vikoi, mitandio na bidhaa nyingine za nguo.

339. ***Mheshimiwa Spika***, jumla ya Shilingi Bilioni 100 zitatumika kutoa pembejeo za kilimo ikiwemo mbegu, viuatilifu na vinyunyizi kupitia Mfuko wa Wakfu wa kuendeleza zao la pamba. Hatua hiyo, imechukuliwa baada ya wakulima kushindwa kujinunulia pembejeo. Historia inaonesha kuwa Nchi zote zinazozalisha zao la pamba zinakopesha wakulima na kulipa wakati wa kuuza pamba yao. Kikao cha wadau kilichokutana mwezi Machi, 2024 kiliamua Mfuko wa kuendeleza zao la pamba uimarishwe ili uweze kuwahudumia wakulima kikamilifu.

340. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali itaendelea na juhudi za kuongeza thamani ya zao la pamba kwa kujenga kiwanda cha vifaa tiba vinavyotumia pamba kama malighafi Wilaya ya Maswa katika

Mkoa wa Simiyu. Aidha, kiwanda kikubwa cha kusindika mafuta ya pamba kitajengwa Wilaya ya Bariadi katika Mkoa wa Simiyu na Mkoa utaendelea na mipango ya kujenga serviced industrial park itakayokuwa na miundombinu ya umeme, maji na barabara kwa ajili ya uwekezaji na uongezaji thamani wa zao la pamba.

**Zao la Mkonge**

341. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Bodi ya Mkonge Tanzania itahamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa zao la mkonge kutoka tani 56,732.69 mwaka 2023/2024 hadi tani 80,000 mwaka 2024/2025. Lengo hilo litafikiwa kwa kununua zana za kilimo kwa ajili ya kuwezesha uendelezaji wa mashamba makubwa ya pamoja; kununua mashine ya kuchakata mkonge; kuendeleza miundombinu ya kituo cha uchakataji cha Handeni; kukarabati miundombinu ya shamba la Kibaranga; na kuwezesha umiliki wa ardhi ya kilimo yenye ukubwa wa hekta 6,000 kwa ajili ya kuanzisha mashamba makubwa ya pamoja katika mikoa ya Tanga, Singida na Morogoro. Aidha, Bodi itaratibu usambazaji wa miche ya mkonge 3,000,000 katika maeneo ya uzalishaji. Vilevile, TARI itatoa mafunzo kuhusu uzalishaji wa mkonge na fursa zitokanazo na zao hilo kwa wadau 100,000 na Maafisa Ugani 500.

342. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza matumizi ya mmea wa mkonge, Bodi kwa kushirikiana na Chuo Cha Sayansi na Teknolojia Cha Nelson Mandela (Nelson Mandera African Institute of Science and Technology), itajenga kituo cha uzalishaji wa Inzi chuma (Blacksoldier flies) kwa kutumia mabaki ya Mkonge (Sisal waste) ili kutengeneza *protein* kwa matumizi ya binadamu na mifugo (Wanyama, ndege na samaki).

343. Pia, Bodi itawezesha utafiti wa zao la mkonge utakaofanywa na watafiti kutoka Chuo Kikuu cha DarEs-Salaam (UDSM), TARI-Mlingano, Chuo Cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandera (NM-AIST) kwa kushirikiana na Kampuni ya Carbonovia UK ya Oxford Uingereza kuhusu uwezekano wa kuzalisha *protein* kutokana na hewa ukaa (Carbon dioxide) kutoka kwenye mabaki ya mkonge. Bodi kwa kushirikiana na Jeshi la Magereza na Chuo cha Mafunzo Zanzibar itaanzisha na kuimarisha utaalam wa uzalishaji wa bidhaa za mikono za Mkonge ili kutengeneza ajira kwa vijana na wanawake.

**Zao la Kahawa**

344. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Bodi ya Kahawa Tanzania katika mwaka 2024/2025 itahamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa zao la kahawa kutoka tani 66,071.8 mwaka 2023/2024 hadi tani 85,000. Lengo hilo litafikiwa na Bodi kwa kushirikiana na TARI kutoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha kahawa na mbinu za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa wakulima 48,000 na Maafisa Ugani 511 kwenye maeneo ya uzalishaji; kuzalisha na kusambaza miche 20,000,000 katika maeneo yanayozalisha kahawa; na kuboresha mfumo wa ununuzi wa kahawa kuwa wa kidigiti ili kupunguza gharama kwa wanunuzi na kurahisisha malipo kwa wakulima. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na wadau itaratibu na kushiriki Mkutano wa Tatu wa Kahawa Afrika (Third African Coffee Summitt), mkutano huo utawezesha ukuaji wa tasnia ya kahawa nchini.

345. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Bodi ya Kahawa Tanzania itajenga miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya kahawa yenye ukubwa wa hekta 4,000 katika wilaya za Karagwe na Misenyi zilizopo katika Mkoa wa Kagera. Aidha, Bodi kwa kushirikiana na TARI itasambaza miche bora ya kahawa kwa mpango wa ruzuku kwa wakulima katika mikoa 17 ikiwemo Mkoa wa Kagera. Lengo ni kuongeza uzalishaji wa kahawa na kuimarisha pato la wakulima.

**Zao la Chai**

346. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Bodi ya chai Tanzania katika mwaka 2024/2025 itahamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa chai kavu kutoka tani 13,525 mwaka 2023/2024 hadi tani 30,000. Lengo hilo litafikiwa kwa kuwezesha shughuli za mnada wa chai Tanzania na kununua mtambo wa kuchanganya chai; kujenga vituo 30 vya mizani kwenye maeneo mapya ya uzalishaji wa chai katika Wilaya za Kilolo, Ludewa, Njombe, Lushoto, Korogwe na Tarime; kuwezesha upatikanaji wa hati ya kimataifa kwa ajili ya uendeshaji wa mashamba ya Kilolo na Lupembe; kujenga miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya chai ya wakulima wadogo katika Mkoa wa Njombe; kuanzisha maeneo 13 mapya kwa ajili ya uzalishaji wa miche ya chai; na kutoa mafunzo kuhusu kilimo bora cha chai kwa wakulima wadogo wa chai 32,000

na kuhamasisha wakulima hao kutumia fursa ya mbolea ya ruzuku inayotolewa na Serikali katika uzalishaji wa zao la chai.

347. ***Mheshimiwa Spika***, Bodi kwa kushirikiana na wadau itaanzisha viwanda viwili (2) vya kusindika chai kati ya lengo la kuanzisha viwanda saba (7) nchini na kufufua mashamba ya chai yenye ukubwa wa hekta 150 katika Wilaya ya Kilolo pamoja na kuhamasisha wakulima kufufua mashamba yao. Vilevile, Wizara itakamilisha majadiliano kuhusu mashamba ya chai yaliyotelekezwa na Kampuni za MeTL, Dhow Mechantile na DL ili yaendelee na uzalishaji. Aidha, pale itakapohitajika kuyatwaa mashamba hayo, Serikali itafanya hivyo kwa kuzingatia taratibu za sheria ili kulinda haki za wawekezaji.

**Zao la Korosho**

348. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Bodi ya korosho Tanzania katika mwaka 2024/2025 itahamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa korosho kutoka tani 254,500 mwaka 2023/2024 hadi tani 595,000. Uzalishaji huo utafikiwa kwa kununua na kusambaza viuatilifu vya korosho tani 30,000 za *sulphur* na lita 3,800,000 za viuatilifu vya maji kwa mpango wa ruzuku. Aidha, Bodi kwa kushirikiana na TARI itazalisha miche 1,000,000 ya korosho na kusambaza katika mikoa ya Pwani, Lindi, Ruvuma, Dodoma, Mtwara, na Tanga. Pia, TARI itaanzisha kitalu cha Taifa cha uzalishaji wa miche ya korosho katika kituo cha TARI Naliendele chenye uwezo wa kuzalisha miche 10,000,000 kwa mwaka.

349. Pia, TARI itazalisha mbegu tani 100 na kusambaza katika Halmashauri zote zinazolima zao la korosho; itaendelea kusajili wakulima na kutambua mashamba yao; itabadili mfumo wa kuuza korosho kutoka mfumo wa kulaza debe hadi mfumo wa uwazi wa kutumia TMX; itatoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la korosho kwa wakulima 1,300 na maafisa 300 katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma, Songwe, Pwani, Manyara, Kigoma na Dodoma; na itaandaaa mashamba darasa 15 katika mikoa ya Pwani, Tanga, Mtwara, Lindi na Ruvuma.

350. ***Mheshimiwa Spika***, Bodi itaendelea na ujenzi wa viwanda vya kubangua korosho pamoja na kuongeza thamani bidhaa zingine zitokanazo na korosho kama vile mafuta ya ganda la korosho

(Cashewnut Shell Liquid – CSL) na viwanda vingine vya mazao ya mafuta katika kongani ya viwanda iliyopo Maranje Wilaya ya Nanyamba katika Mkoa wa Mtwara. Aidha, Bodi itakamilisha ujenzi wa ghala lenye uwezo wa kuhifadhi tani 3,000 za korosho katika Wilaya ya Manyoni. Pia, Bodi itajenga ghala zenye uwezo wa kuhifadhi tani 1,000 katika vyama vikuu vya ushirika vya MAMCU ghala tatu (3), TANECU ghala tatu (3) na CORECU ghala tatu (3) ili msimu unaofuata tuanze kufanya minada ya korosho katika vyama vya msingi.

**Zao la Tumbaku**

351. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Bodi ya Tumbaku Tanzania katika mwaka 2024/2025 itahamasisha wakulima kuzalisha tumbaku kutoka tani 178,521 mwaka 2023/2024 hadi kufikia tani 200,000. Uzalishaji huo utafikiwa kwa kuhamasisha wakulima kuzingatia kanuni za kilimo bora cha zao la tumbaku; kuhamasisha wakulima kujenga na kuboresha mabani ya kukaushia tumbaku; kuanzisha mashamba mawili (2) ya mfano katika Wilaya za Chunya na Uyui; na kutoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la tumbaku kwa Maafisa Ugani katika maeneo ya uzalishaji wa tumbaku. Vilevile, Bodi itakamilisha ujenzi na ununuzi wa vifaa katika ofisi ya Bodi iliyopo Tabora na kuanza ujenzi wa ofisi mpya za Bodi katika Wilaya za Urambo, Kaliua, Sikonge na Songea.

352. Vilevile, Bodi ya Tumbaku itaratibu upatikanaji wa tani 127,316 za mbolea na kusambaza kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku, viuatilifu lita 236,329 na pakiti 1,664,286, vifungashio belo 11,709 na nyuzi 166,429 kwa ajili ya kuimarisha uzalishaji wa tumbaku. Pia, mbolea ya NPK (10:18:24) itaagizwa na TFC na kusambazwa kwa wakulima wa zao la tumbaku.

353. Aidha, Serikali itatoa Waraka kwa Benki utakaodhibiti mfumo wa kujiamulia *exchange rate* ya Dola za Marekani kwa ajili ya kuwalipa wakulima baada ya kuuza tumbaku ili mkulima afaidike na faida inayotokana na *exchange rate* pale ambapo Shilingi inakuwa dhaifu na zoezi hili litasimamiwa na Tume ya Ushirika.

354. ***Mheshimiwa Spika***, Bodi ya Tumbaku Tanzania itajenga mabani ya kisasa 2,353 katika mikoa ya Tabora, Shinyanga, Geita, Kigoma, Ruvuma, Katavi, Mbeya, Songwe, Iringa, Morogoro na

Mara. Mabani hayo yatasaidia kupunguza upotevu wa majani, kuongeza ubora wa tumbaku na kutunza mazingira.

**Zao la Pareto**

355. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia COPRA katika mwaka 2024/2025 itahamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa zao la pareto kutoka tani 4,238 mwaka 2023/2024 hadi tani 5,000. Uzalishaji huo utafikiwa kwa kuratibu ujenzi wa makaushio 100 ya pareto katika wilaya za Mbeya (25), Makete (20), Ileje (20), Mbulu (15), Ludewa (10) na Arusha (10). Vilevile, Bodi itaendelea kutoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la pareto kwa wakulima 10,500 na wakaguzi wa pareto 25 katika maeneo ya uzalishaji wa zao hilo. Vilevile, COPRA itaratibu usambazaji wa mbegu bora kilo 5,300 na kuratibu vituo 450 vya ukaguzi wa pareto katika mikoa ya Mbeya, Songwe, Njombe, Iringa, Manyara na Arusha.

**Zao la kakao**

355. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa kakao itaendelea kuhamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa kakao kutoka tani 11,499.4 mwaka 2023/2024 hadi tani 15,000. Lengo hilo litafikiwa kwa kutoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora kwa wakulima na Maafisa Ugani katika Halmashauri za Kyela, Rungwe, Busokelo, Mlimba na Mvomero. Vilevile, Wizara kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa kushirikiana wadau itaendelea kufanya maboresho ya mfumo wa uuzaji kwa kuboresha uendeshaji wa minada ambayo itaongeza uwazi na uwajibikaji kwa lengo la kuhakikisha kuwa mkulima ananufaika na kilimo cha zao la kakao. Pia, Tume itaendelea kutoa elimu ya masoko na fedha kwa wanachama na wakulima 100,000 wa kakao.

**Mazao ya Chakula**

357. ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa mazao ya chakula unaohusisha mazao ya nafaka na yasiyo nafaka unatarajiwa kufikia takriban tani 31,489,630 katika msimu wa kilimo wa 2023/2024 ikilinganishwa na tani 20,402,014 katika msimu wa kilimo wa 2022/2023.

**Mazao yenye mahitaji makubwa**

358. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kuhamasisha uzalishaji na tija kwa mazao ya ngano, mafuta ya kula, miwa/sukari kwa lengo la kupunguza matumizi ya fedha za kigeni zinazotumika kuagiza mazao na bidhaa hizo kutoka nje ya nchi.

**Zao la ngano**

359. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2024/2025 itaendelea kuhamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa ngano kutoka tani 86,522 mwaka 2022/2023 hadi kufikia tani 150,000 mwaka 2023/2024 na kuendelea kuhamasisha uzalishaji hadi kufikia uwezo wa kujitosheleza wa tani 1,000,000 ifikapo mwaka 2027/2028. Lengo hilo litafikiwa kwa kutekeleza yafuatayo:

i. Kushirikiana na Sekta binafsi kuongeza upatikanaji wa mbegu bora kufikia tani 18,000 zilizothibitishwa ambazo zitazalisha takriban tani 375,000 za ngano kwa mwaka 2024/2025. Mbegu hizo zitatokana na tani 864 za mbegu za Msingi (basic) zitakazopatikana kutoka TARI

ii. Kuongeza upatikanaji wa mbegu bora kutoka tani 18,000 kufikia tani 30,000 zilizothibitishwa ambazo zitazalisha takriban tani 625,000 za ngano kwa mwaka 2025/2026. Mbegu hizo zitatokana na tani 1,440 za mbegu za Msingi (basic) zitakazopatikana kutoka TARI;

iii. Kuongeza upatikanaji wa mbegu bora kutoka tani 30,000 kufikia tani 36,000 zilizothibitishwa ambazo zitazalisha takriban tani 750,000 za ngano kwa mwaka 2026/2027. Mbegu hizo zitatokana na tani 1,728 za mbegu za Msingi (basic) zitakazopatikana kutoka TARI;

iv. Kuongeza upatikanaji wa mbegu bora kutoka tani 36,000 kufikia tani 48,000 zilizothibitishwa ambazo zitazalisha takriban tani 1,000,000 za ngano kwa mwaka 2027/28. Mbegu hizo zitatokana na tani 2,304 za mbegu za Msingi (basic) zitakazopatikana kutoka TARI;

v. TARI kutoa mafunzo ya uzalishaji wa mbegu za kuazimia ubora (QDS) kwa wakulima 500 katika Wilaya za Nkasi, Babati, Hanang, Songwe, Mbinga, Siha na Makete;

vi. Kuwezesha uwekezaji katika mashamba ya West Kilimanjaro na Hanang yenye jumla ya ekari 6,135.34 ili kuongeza maeneo ya uzalishaji wa mbegu;

vii. Kukamilisha taratibu za kuchukua mashamba yaliyo chini ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na kuyakabidhi kwa wazalishaji;

viii. Kutambua na kupima maeneo yenye ukubwa wa hekta 20,000 yanayofaa kwa kilimo cha ngano nchini;

ix. Kuimarisha soko la ngano inayozalishwa kwa kutambua na kuingia mikataba ya hakikisho la ununuzi wa ngano na kampuni kubwa zinazoagiza ngano nje ya nchi na kuanza utekelezaji kuanzia tarehe 01 Julai. 2024;

x. Kufanya Marekebisho ya sheria ya usalama wa chakula na kuanza kusimamia nafuu ya kodi wanayopewa waingizaji wa ngano kutoka nje ya nchi;

xi. Kuendelea kufanya utafiti wa mbegu za ngano zenye kukidhi sifa ya mahitaji ya soko na tija katika uzalishaji; na

xii. Kujenga miundombinu ya umwagiliaji kwenye mashamba ya utafiti na uzalishaji wa mbegu za ngano.

**Zao la Miwa**

360. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2024/2025 kupitia Bodi ya Sukari Tanzania itaongeza uzalishaji wa zao la miwa kutoka tani 4,215,555.27 zilizozalisha sukari tani 392,724 mwaka 2023/2024 hadi kufikia tani 5,200,000 za miwa zitakazozalisha sukari tani 520,000. Lengo hilo litafikiwa kwa kutekeleza yafuatayo:

i. Kusimamia uanzishaji wa vitalu vya kuzalisha miche ya miwa kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta 400 katika bonde la Kilombero kwa ajili ya wakulima wadogo wa miwa;

ii. Wizara itaweka mfumo wa kikanuni wa uagizaji wa sukari inayotumika viwandani;

iii. Kukamilisha majadiliano ya kuomba unafuu wa kodi kwa viwanda vitakavyozalisha *ethanol* ili kupunguza gharama za uzalishaji wa sukari;

iv. Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara itazalisha teknolojia ndogondogo za viwanda vidogo kwa ajili ya wakulima wadogo wa miwa;

v. Kuendelea kutenga maeneo yanayofaa kwa ajili ya kilimo cha miwa ili kuwezesha uwekezaji katika tasnia ya sukari. Aidha, itakapohitajika kulipa fidia kwenye maeneo hayo, Wizara itafanya hivyo;

vi. Kusimamia upanuzi wa kiwanda cha sukari cha Mtibwa na mashamba ya miwa ya Dakawa yenye ukubwa wa hekta 12,000 zinazofaa kwa kilimo cha miwa;

vii. Kusimamia upanuzi wa mashamba yenye ukubwa wa hekta 13,000 ya kiwanda cha sukari Kagera;

viii. Kusimamia kiwanda cha sukari cha TPC ili kuongeza uwezo wa kuchakata miwa kutoka tani 200 hadi tani 210 kwa saa, kuongeza eneo la kulimwa miwa la hekta 400 na kuendelea kusimika miundombinu ya umwagiliaji;

ix. Kusimamia upanuzi wa kiwanda cha sukari cha Kilombero ambapo kitaongeza uzalishaji wa sukari kutoka tani 130,000 hadi tani 271,000 mwaka 2027;

x. Kusimamia usimikaji wa miundombinu ya umwagiliaji kwenye eneo la ukubwa wa ekari 100 kwenye *block farm* za wakulima wadogo Kilombero;

xi. Kupitia TARI na kwa kushirikiana na wakulima kuzalisha miche ya miwa 2,520 kwenye mashamba yenye ukubwa wa hekta 56 katika Mikoa ya Kagera na Morogoro; na

xii. TARI itaanzisha vitalu vya mbegu za miwa katika eneo la ekari 20 kwa wakulima wanaozunguka mabonde hayo; na kutoa mafunzo ya kanuni za kilimo bora cha miwa kwa wakulima 8,000 kupitia maonesho na makongamano mbalimbali.

**Mazao ya Mafuta**

361. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2024/2025 itahamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa mazao ya mafuta yakiwemo alizeti, chikichi, karanga na ufuta kutoka tani 2,143,098.70 mwaka 2022/2023 hadi kufikia tani 2,200,000. Lengo hilo litafikiwa kwa kutekeleza yafuatayo:

i. Kuwezesha upatikanaji wa mbegu bora za alizeti tani 5,000 na kusambaza kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku;

ii. Kuzalisha na kusambaza mbegu bora za karanga tani 150 na mbegu za ufuta tani 150;

iii. Kujenga miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya mbegu za alizeti ya ASA yenye ukubwa wa hekta 800;

iv. Kuhamasisha wawekezaji kuwekeza katika mashamba ya pamoja (block farms) kwa ajili ya kilimo cha alizeti;

v. Wizara kwa kushirikiana na wadau itaendelea kuzalisha na kusambaza miche ya chikichi 2,000,000 kwa wakulima katika maeneo ya uzalishaji;

vi. Serikali itanunua ardhi yenye ukubwa wa hekta 100,000 kwenye Halmashauri za Kigoma na Kyela kwa ajili ya kuanzisha kilimo cha mashamba makubwa ya chikichi;

vii. Kununua ardhi yenye ukubwa wa hekta 50,000 kwa ajili ya kuanzisha kilimo cha mashamba makubwa ya alizeti;

viii. TARI itazalisha mbegu za ufuta tani 108. Kati ya hizo tani tatu (3) ni mbegu za awali na mbegu za msingi tani tano (5) na mbegu zilizothibitishwa tani 100;

ix. TARI kutoa mafunzo ya kilimo bora cha zao la ufuta kwa wakulima 2,000 na Maafisa Ugani 500 na kuandaa mashamba ya mfano 105 katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani, Songwe, Morogoro, Tanga, Kilimanjaro, Manyara, Dodoma, Singida, Tabora na Mbeya; na

x. Wizara itaendelea na majadiliano na Wizara ya Fedha kuweka kodi kwenye mafuta yanayotoka nje ya nchi ili kulinda viwanda vya ndani na wakulima.

**Mazao ya bustani**

362. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2024/2025 kwa kushirikiana na wadau wa kilimo itahamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa mazao ya bustani kutoka tani 8,438,273.98 mwaka 2022/2023 hadi tani 9,000,000. Aidha, Wizara itaendelea kuhamasisha na kusimamia utekelezaji wa mikakati ya kuendeleza uzalishaji na upatikanaji wa masoko ya mazao ya Bustani. Lengo hilo litafikiwa kwa Wizara kutekeleza yafuatayo:

i. Kushirikiana na wadau wa mazao ya bustani kutoa mafunzo rejea kuhusu kilimo bora cha mazao ya bustani kwa maafisa ugani na wakulima katika maeneo ya uzalishaji;

ii. Kushirikiana na wadau kuzalisha na kusambaza miche ya mazao ya viungo;

iii. Kuanzisha mashamba makubwa ya pamoja ya migomba kwa ajili ya kilimo cha kibiashara cha migomba. Kwa kuanzia mashamba hayo yataanzishwa katika Wilaya ya Rombo kwa kusanifu mashamba na kuweka mifumo ya umwagiliaji, kujenga viwanda vya kuchakata na kufungasha ndizi kwa ajili ya usafirishaji nje ya nchi;

iv. Kununua mashine za kuchimbia visima katika halmashauri 184 zitazokuwa na uwezo wa kuchimba visima vya kati vyenye urefu wa mita 150 hadi 200; na

v. Kukamilisha usanifu wa *Agricultural Special Processing Zones* wa mazao ya bustani wenye thamani ya Dola za Marekani

Milioni 75 utaanza kwa kutekelezwa na AFDB kwa kujenga *Dar es Salaam Multiple Commodity Centre* (DMCC).

**Zao ya Parachichi**

363. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Wizara itaendelea kuhamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa parachichi zinazouzwa nje ya nchi (exportable varieties) kutoka tani 26,826.3 mwaka 2022/2023 hadi tani 30,000 Ili kufikia malengo hayo Wizara itatekeleza yafuatayo:-

i. Kushirikiana na wadau kuzalisha miche 6,000,000 ya parachichi na kusambaza kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku;

ii. Kuwawezesha wakulima wa parachichi kwa kuwachimbia visima na kuwawekea miundombinu ya umwagiliaji ikiwemo kuwapatia vifaa vya umwagiliaji kama vile pampu za maji na mipira;

iii. Kutoa mafunzo kwa wazalishaji wa miche 450, wakulima 4,000 na Maafisa ugani 160 katika mikoa ya Mbeya, Songwe, Njombe, Iringa, Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Kagera, Ruvuma, Rukwa, Kigoma na Morogoro;

iv. Kutoa ruzuku ya viuatilifu kwa wakulima wa zao la parachichi;

v. Wizara kupitia COPRA itanunua na kusambaza vifaa vya kupima ubora wa parachichi (dry matter machines); na

vi. Wizara kupitia TARI kwa kushirikiana na kiwanda cha ITRACOM itafanya utafiti na kuzalisha aina ya mbolea inayofaa kwa ajili ya zao la parachichi na mbolea hiyo itasambazwa kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku.

**5.2 Kuongeza Ajira zenye Staha na Ushiriki wa Vijana na Wanawake kwenye Kilimo**

364. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kuwezesha upatikanaji wa ajira zenye staha na ushiriki wa vijana na wanawake kwenye kilimo kupitia utekelezaji wa Programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora (Building a Better Tommorrow – BBT) inayotekelezwa kupitia miradi mikuu minne (4) ambayo ni kuwezesha upatikanaji wa ardhi ya

kilimo na uanzishaji wa mashamba makubwa ya pamoja (Block farms) na umilikishaji wa ardhi, kuwezesha upatikanaji wa mitaji kwa vijana na wanawake (BBT - Mitaji), kuimarisha Huduma za Ugani (BBT – Ugani) na kuwezesha upatikanaji wa miundombinu ya umwagiliaji kwa wakulima wadogo (BBT – Visima). Kupitia miradi hiyo yafuatayo yatatekelezwa: -

**5.2.1 Kuwezesha upatikanaji wa ardhi ya kilimo na uanzishaji wa mashamba makubwa ya pamoja (*Block farms) BBT - Mashamba***

365. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kutekeleza mradi wa mashamba makubwa ya Chinangali, Chunya, Singida na Ndogowe kwa kujenga mabwawa na kuchimba visima kwenye mashamba ya BBT jumla ya hekta 186,086. Vilevile, Wizara itaanza kutekeleza mradi wa BBT katika Halmashauri 100 zitakazotenga maeneo yenye ukubwa wa hekta 200 kwa kila Halmashauri na kujenga miundombinu ya umwagiliaji katika maeneo hayo. Utambuzi wa vijana watakaomilikishwa ardhi utafanywa na Halmashauri husika ambapo Wizara ya Kilimo itatoa mafunzo ya kilimo biashara kwa vijana hao katika maeneo yao. Pia, Wizara itaendelea kutambua na kuainisha mashamba mapya 30 kwa ajili ya uwekezaji wa mashamba makubwa.

366. Kadhalika, Wizara itakamilisha majadiliano na AfDP kwa ajili ya mradi wa BBT wenye thamani ya Dola za Marekani Milioni 130.

***BBT –Mitaji***

367. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia AGITF katika mwaka 2024/2025 itaongeza mikopo yenye riba nafuu kwa vijana na wanawake waliopo kwenye shughuli za kilimo na uongezaji thamani mazao kutoka Shilingi Bilioni 2 mwaka 2023/2024 hadi Shilingi Bilioni 10. Vilevile, itasimamia AGITF na TADB kukamilisha makubaliano ya mashirikiano (MoU) na kutumia mifumo ya dhamana ili kuzisaidia taasisi za fedha ziweze kuwakopesha vijana kwa kutumia dhamana zitakazosimamiwa na TADB.

368. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia AGITF itakamilisha majadiliano na IFAD kwa ajili ya kuanzisha mradi wa upatikanaji wa mitaji wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 40.

***BBT – Ugani***

369. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Sekta Binafsi na Bodi za mazao itaendelea kutekeleza Mpango wa Ugani (BBT – Agricultural Extension Enterpreneurship Scheme) ambao utahusisha jumla ya vijana 300. Vijana hao watazalisha mazao maalum ikiwemo pamba, korosho, tumbaku na kahawa. Lengo la mpango huo ni kuwatengenezea ajira vijana, kuimarisha utoaji wa huduma za ugani na kukuza ujuzi wa vijana wahitimu wa vyuo vya kilimo kwa kutoa huduma za ugani kwa wakulima.

***BBT – Visima***

370. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2024/2025 kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itaanza uchimbaji wa visima 1,000 kati ya lengo la kuchimba visima 67,000 ifikapo mwaka 2030 kwa wakulima wadogo katika Halmashauri 178 na kufunga vifaa vya umwagiliaji. Visima hivyo vya awamu ya kwanza vitamwagilia jumla ya hekta 16,000 na kunufaisha wakulima takriban 16,000.

**5.2.2 Kuimarisha ushiriki wa vijana na wanawake katika kilimo kupitia Programu ya Jenga Kesho iliyo Bora**

371. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2024/2025, itadahili na kutoa mafunzo kwa vijana na wanawake 1,000 katika vyuo vya mafunzo ya kilimo kupitia programu ya BBT; na kuwezesha vijana na wanawake waliopo katika mashamba ya BBT kuendelea na uzalishaji wa mazao ya kilimo.

**5.2.3 Kuimarisha ushiriki wa wazawa katika miradi ya kilimo**

372. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inatambua umuhimu wa ushiriki wa wazawa na kampuni za wazawa katika miradi na shughuli mbalimbali zilizopo katika mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo. Ushiriki wa wazawa katika Sekta ya kilimo unaongeza chachu katika ukuaji wa uchumi kwa kuongeza ujuzi na uwezo wa mbinu mbalimbali za uzalishaji na masoko, kukuza teknolojia na ubunifu katika uzalishaji na uchakataji wa mazao ya kilimo, kupunguza utegemezi wa uingizaji wa mazao na bidhaa zitokanazo na kilimo ndani ya nchi, kutengeneza ajira, kuimarisha ubora wa bidhaa na huduma hasa maeneo ya vijijini.

373. Katika mwaka 2024/2025, Wizara itaongeza ushiriki wa wazawa katika utekelezaji wa miradi mbalimbali kutoka asilimia 75 mwaka 2023/2024 hadi asilimia 85. Miradi hiyo inahusisha umwagiliaji, uhifadhi, utafiti, ubunifu na teknolojia.
***"Wizara inatoa rai kwa wazawa wanaopata fursa hiyo kukamilisha miradi hiyo kwa ufanisi na wakati ili kuuthibitishia umma wa Watanzania kuwa wazawa tukipewa nafasi tunaweza***''

**5.3 Kuimarisha Usalama wa Chakula na Lishe;**
374. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha usalama wa chakula na lishe nchini, Wizara katika mwaka 2024/2025 itaendelea na mpango wa kuwekeza kwenye miundombinu ya uhifadhi wa chakula, kuiongezea NFRA uwezo wa kuhifadhi chakula, kuimarisha na kuendelea na matumizi ya mfumo wa kidigiti wa *Crop Stock Dynamics Systems*, na kuhamasisha uzalishaji na matumizi ya mazao yaliyoongezewa virutubishi ili kukabiliana na matatizo ya lishe nchini. Ili kufikia malengo hayo, Wizara itatekeleza yafuatayo;

**5.3.1 Uwekezaji kwenye miundombinu ya uhifadhi kuweza kufikia uwezo wa kuhifadhi tani 3,000,000 ifikapo mwaka 2030**
375. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha uhifadhi wa mazao ya chakula Wizara katika mwaka 2024/2025, itakamilisha ujenzi wa ghala 28 katika mkoa wa Ruvuma na ujenzi wa miundombinu ya uhifadhi yenye uwezo wa kuhifadhi tani 165,000 kupitia Mradi wa kuongeza uhifadhi wa nafaka unaotekelezwa na NFRA na itafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa vihenge na ghala. Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na wadau wa kilimo katika kuwekeza kwenye ujenzi wa ghala za kuhifadhi mazao nchini ili kuongeza hifadhi ya mazao ya chakula ndani ya nchi na kuuza ziada nje ya nchi.

**5.3.2 Kuiongezea NFRA uwezo wa kununua mazao ya wakulima ili kuongeza hifadhi ya chakula**
376. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia NFRA katika mwaka 2024/2025 itanunua tani 1,150,000 za nafaka kwa lengo la kuimarisha usalama wa chakula nchini. Pia, NFRA itaendelea kuuza chakula kwa maombi maalumu na kutoa chakula cha misaada pale itakapohitajika katika nchi za jirani na nje ya ukanda wa Afrika.

377. Kadhalika, Wizara kupitia NFRA itakamilisha majadiliano na Benki ya NBC kuanzisha Hati Fungani ya Usalama wa Chakula (Food Security Bond) ili kuongeza uwezo wa NFRA kuhifadhi chakula.

**5.3.3 Kuimarisha na kutumia mfumo wa kidigiti wa Crop Stock Dynamics Systems**

378. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuendelea kutatua changamoto ya ukosefu wa taarifa sahihi za mazao ya kilimo katika maeneo ya sokoni, ghala binafsi na vituo vya ukaguzi, katika mwaka 2024/2025, Wizara kupitia COPRA itaendelea kusajili vituo vya ununuzi wa mazao, ghala za Sekta ya umma, Sekta binafsi na Vyama vya Ushirika na kuzipa namba maalum ya utambulisho kwa lengo la kufuatilia kiasi cha mazao ya kilimo kilichohifadhiwa katika ghala na mwenendo wa bei za mazao. Aidha, COPRA itasajili wafanyabiashara wakiwemo wanunuzi kwenye mnyororo wa thamani wa nafaka na mazao mchanganyiko; na kutoa elimu kwa umma kuhusu shughuli za usimamizi wa nafaka na mazao mchanganyiko kwa kuchapisha majarida na kuandaa vipindi kwenye TV, Redio na Mitandao ya kijamii.

**5.3.4 Kuhamasisha matumizi ya mazao yaliyoongezewa virutubishi ndani ya nchi ili kukabiliana na matatizo ya lishe nchini**

379. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kukabiliana na matatizo ya lishe nchini, Wizara itaendelea kutekeleza Mpango Kazi wa Lishe katika Kilimo (Nutrition Sensitive Agriculture Action Plan – NSAAP); kwa kuhamasisha uzalishaji wa mazao ya kilimo yenye virutubisho kwa wingi yaliyofanyiwa utafiti na wataalam wa hapa nchini. Aidha, Wizara kupitia TARI, itazalisha mbegu mama 350,000 za viazi lishe zenye uwezo wa kuzalisha vipando 7,000,000 na kuvisambaza katika mikoa ya Mwanza, Geita, Tabora, Katavi, Kigoma, Shinyanga, Simiyu, Kagera na Mara.

380. Pia, Wizara itatoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora kwa wakulima wawezeshaji na wazalishaji wa mbegu 150 katika Wilaya za Bukombe, Geita, Misungwi, Misenyi na Bukoba. Pia, itahaulisha na kusambaza mbegu viazi lishe, mahindi na maharage zilizoongezewa viinilishe kibaiolojia kwenye ili kuboresha lishe kwa walaji.

### 5.4 Kuimarisha Upatikanaji wa Masoko, Mitaji na Mauzo ya Mazao nje ya Nchi

381. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuwezesha upatinakaji wa mitaji, masoko ya mazao ya kilimo ndani na nje ya nchi na kuimarisha mauzo ya mazao hayo nje ya nchi, Wizara imepanga kuwekeza kwenye miundombinu ya masoko ya mazao ya kilimo kwa ajili ya wakulima katika Halmashauri mbalimbali nchini; kuimarisha uongezaji thamani na uhifadhi pamoja na kuiwezesha Sekta binafsi kwa kuijengea miundombinu ya masoko; kuongeza mauzo ya mazao ya kilimo ndani na nje ya nchi; kuimarisha upatikanaji wa mitaji na kuziwezesha maabara za Serikali na Sekta binafsi ziweze kufikia viwango vya ubora vinavyotakiwa Kimataifa. Ili kufikia malengo hayo, Wizara itatekeleza yafuatayo: -

#### 5.4.1 Kujenga miundombinu ya masoko ya mazao ya kilimo kwa ajili ya wakulima katikaHalmashaurimbalimbali nchini

381. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2024/2025, itaendelea kuimarisha upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo ndani na nje ya nchi kwa kujenga masoko ya kimkakati mipakani na ujenzi wa vituo vya masoko (market sheds).

**Ujenzi wa Masoko ya Kimkakati**

383. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2024/2025 itaendelea na ujenzi wa masoko matano (5) ya kimkakati yaliyokuwa chini ya mradi wa DASIP katika Halmashauri za Manispaa ya Kahama (Busoka), Ngara (Kabanga), Kyerwa (Nkwenda na Murongo) na Tarime (Sirari). Ujenzi wa masoko hayo utawezesha kuendeleza biashara ya mazao ya kilimo katika mipaka ya nchi za Uganda, Kenya, Rwanda na Burundi.

**Ujenzi wa Vituo vya Masoko (Market sheds)**

384. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2024/2025 imepanga kujenga vituo vinne (4) vya masoko ya kilimo (market sheds) katika Halmashauri za Kigoma, Rombo (Mamsera), Ngara na Hai (Mula). Vituo hivyo vitawezesha wakulima kukusanya na kuuza mazao yao sehemu rasmi zinazotambulika na mamlaka husika. Vilevile, Wizara itafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika mipaka na Halmashauri nchini kwa ajili ya taratibu za kuanza ujenzi wa vituo vingine vya masoko (market sheds). Kadhalika, Wizara itafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina

kwenye mipaka yetu yote kwa nchi zinazotuzunguka kwa ajili ya kujenga miundombinu ya masoko.

385. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kuijengea uwezo COPRA kwa ajili ya kutoa huduma za usimamizi wa ubora na usalama wa nafaka na mazao mchanganyiko. Katika kufanikisha hilo Wizara itawezesha ununuzi wa magari manne (4), ununuzi wa samani na vitendea kazi vya watumishi; kuongeza watumishi 84, pamoja na kuanzisha Ofisi tano (5) za Kanda.

386. Vilevile, COPRA itakamilisha kanuni za usimamizi na kuanza kuratibu mnyororo wa thamani ya nafaka na mazao mchanganyiko kwa kuandaa miongozo mbalimbali ya kusimamia na kudhibiti viwango endelevu kuhusu uzalishaji, uchakataji, masoko na biashara ya nafaka na mazao mchanganyiko.

**5.4.2 Kuimarisha uongezaji thamani na uhifadhi kwa kushirikisha Sekta binafsi**

387. ***Mheshimiwa spika***, katika mwaka 2024/2025 Wizara itakamilisha ujenzi wa vituo jumuishi viwili (2) katika mikoa ya Iringa (Mufindi) na Mbeya (Rungwe). Vituo hivyo, vitawezesha ukusanyaji, uchambuaji, upangaji wa madaraja, ufungashaji uhifadhi na usindikaji wa mazao ya bustani. Pia, Wizara itakamilisha ujenzi wa kituo mahiri cha usimamizi wa mazao baada ya kuvuna kilichopo Kongwa katika Mkoa wa Dodoma. Kadhalika, Wizara itakamilisha ujenzi wa kiwanda cha kusindika zabibu katika Mkoa wa Dodoma ili kuongeza thamani ya zao la zabibu, kupunguza upotevu na kuwaongezea wakulima soko la zabibu.

388. Kadhalika, ili kupunguza upotevu, kuongeza thamani na kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi, Wizara itajenga miundombinu ya kukaushia muhogo katika Mkoa wa Kigoma; kujenga ghala na miundombinu ya kukaushia tangawizi katika Wilaya ya Buhigwe; na kujenga kiwanda cha kuchakata vanila katika kituo cha TARI Maruku Mkoa wa Kagera.

389. ***Mheshimiwa Spika***, CPB itasindika mahindi tani 40,500 zitakazozalisha unga wa mahindi tani 28,350 na pumba za mahindi tani 12,150; itakamua alizeti tani 5,250 na kuzalisha mafuta ya alizeti lita 1,575 na mashudu ya alizeti tani 3,675; itakoboa mpunga tani

15,000 zitakazozalisha mchele tani 10,500 na pumba za mpunga tani 4,500; itasindika ngano tani 15,000 zitakazozalisha unga wa ngano tani 10,500 na pumba za ngano tani 4,500.

390. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha usindikaji wa mazao ya chakula, CPB itakarabati miundombinu ya uchakataji wa mazao iliyopo katika mikoa ya Arusha (Unga Limited) na Iringa (Gangilonga) yenye uwezo wa kusindika mahindi na ngano tani 33,750 na tani 13,500 kwa mwaka mtawalia; itakarabati vihenge 23 vilivyopo Arusha na Iringa vyenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani 51,600 za nafaka; itajenga ghala mpya moja (1) yenye uwezo wa kuhifadhi nafaka tani 10,000 katika Wilaya ya Songea; na kusimika mitambo yenye uwezo wa kusafisha na kuchambua mbaazi na ufuta tani 200,000 kwa mwaka katika Mkoa wa Dar es Salaam.

**5.4.3 Kuongeza mauzo ya mazao ya kilimo ndani na nje ya nchi**

391. ***Mheshimiwa Spika***, katika kukabiliana na changamoto ya upatikanaji wa fedha za kigeni, Wizara itaendelea kuweka nguvu katika kufungua masoko na kuongeza mauzo ya nje ya nchi kutoka Dola za Marekani Bilioni 2.3 mwaka 2022/2023 hadi Dola za Marekani Bilioni 3 mwaka 2024/2025. Lengo hilo litafikiwa kwa kusimamia mikakati ya uzalishaji na kuendelea kuimarisha biashara ya mazao ya kilimo kwa kuweka mazingira wezeshi ya biashara ya mazao.

392. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia TPHPA, itawezesha kufungua masoko mapya 10 kwa ajili ya mazao ya nafaka, bustani, mikunde na tumbaku katika nchi za Malaysia (parachichi), Uturuki (nanasi na parachichi), Israel (parachichi), USA (parachichi), Vietnam (mbegu za matango na tikiti maji), China (pilipili, parachichi, mahindi meupe na pumba za ngano), Pakistan (tumbaku) na Afrika Kusini (ndizi). Vilevile, TPHPA, itaanzisha mfumo rasmi wa kufanya ufuatiliaji (crop traceability system) kwa mazao yote yanayosafirishwa nje ya nchi ili kulinda soko la mazao ya kilimo nje ya nchi.

393. Kadhalika, katika kuimarisha soko la ndani, CPB itanunua mahindi tani 41,300, mpunga tani 15,000, mtama tani 2,360, alizeti tani 5,250, maharage tani 4,100, choroko tani 20,000, ufuta tani 1,000, korosho tani 500 na karanga tani 150. Kadhalika, itanunua

ngano tani 15,000, itakayozalishwa na wakulima katika maeneo ya kimkakati ikiwemo Makete. Vilevile, CPB itaendelea na mashirikiano na kampuni za nje ya nchi zenye nia ya kununua mazao ya Tanzania. Kampuni hizo ni kutoka nchi za Zambia, Zimbabwe, Rwanda, Kenya, Sudani kusini, Falme za kiarabu na India. Pia, NFRA itauza mazao ya nafaka tani 500,000 nje ya nchi.

**5.4.4 Kuimarisha upatikanaji wa mitaji**

394. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025 Wizara itaendelea kushirikiana na taasisi za fedha ikiwemo Benki Kuu ya Tanzania katika kuimarisha utoaji wa mikopo yenye riba nafuu kwenye Sekta ya kilimo. Lengo ni kuhamasisha taasisi za fedha kuongeza kiwango cha mikopo inayotolewa kwenye sekta ya kilimo kutoka asilimia 10 mwaka 2023/2024 hadi asilimia 15 ifikapo mwaka 2030.

395. Katika kufikia lengo hilo, Wizara itaendelea kuimarisha miundombinu muhimu ya uzalishaji wa mazao ya kilimo ikiwemo ya umwagiliaji, uhifadhi na masoko ili kuwa na uhakika wa uzalishaji katika mnyororo wa thamani wa mazao kwa mwaka mzima. Hatua hiyo, itaongeza imani kwa taasisi za fedha na urasimishaji ili kuongeza mikopo inayotolewa katika Sekta ya Kilimo. Aidha, Wizara itaendelea kujadiliana na Wizara yenye dhamana na masuala ya fedha kuharakisha maandalizi ya Sera zitakazowezesha masharti ya Benki za Maendeleo kuwa tofauti na Benki za Biashara na upatikanaji wa Bima za mazao kwa wakulima.

396. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara itaratibu uanzishaji wa mfumo rasmi wa utoaji wa mikopo kwa wakulima katika tasnia ya pamba, tumbaku na korosho na kuimarisha mfumo wa *crop financing* kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania. Vilevile, Wizara kupitia COPRA itasimamia kilimo cha mkataba cha mazao yanayosimamiwa na Mamlaka hiyo.

397. ***Mheshimiwa Spika***, TADB itaongeza idadi ya taasisi za fedha zinazotumia mfuko wa dhamana kutoka taasisi 17 hadi 21 ili kurahisisha utoaji wa mikopo; itawezesha miradi mipya 34 ya uchakataji, sita (6) ya ghala, minne (4) ya vyumba vya ubaridi, miwili (2) ya miundombinu ya umwagiliaji, mawili (2) ya mashamba ya pamoja (block farms), ununuzi wa matrekta 20 pamoja na

*combine harvester* nane (8). Vilevile, TADB itatoa mikopo ya pembejeo kwenye miradi 24 ya kilimo, itawajengea uwezo wakulima wadogo 1,450 kwenye kanda nane (8) kuhusu elimu ya fedha na mikopo; itavijengea uwezo vikundi 16 vya wanawake na vijana na itaanzisha kampeni ya kuwashawishi vijana kushiriki katika kilimo.

**5.4.5 Kuziwezesha maabara za Serikali na Sekta binafsi ziweze kufikia viwango vya ubora vinavyotakiwa kimataifa**

398. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia TPHPA itaendelea kuimarisha maabara ya afya ya mimea iliyopo makao makuu kwa kununua na kufunga vifaa vya kisasa na kuifanya kuwa maabara ya rufaa ya afya ya mimea na viuatilifu. Pia, TPHPA itakamilisha usimikaji wa mashine na kununua vitendanishi vya Kituo cha Udhibiti wa Visumbufu vya Mimea Kibaiolojia (National Biological Control Unit) kilichopo Kibaha ili kuimarisha uzalishaji wa wadudu rafiki na usajili wa viuatilifu hai.

399. Vilevile, ili kuimarisha upimaji wa ubora wa mbegu TOSCI itafanya upanuzi wa maabara kuu ya mbegu ya Taifa iliyopo TOSCI Makao Makuu - Morogoro na kujenga maabara katika ofisi za kanda zilizopo katika mikoa ya Mwanza, Mtwara na Tabora. Pia, itakarabati maabara ya mbegu ya kanda ya kaskazini iliyopo katika Mkoa wa Arusha. Kadhalika, Wizara itaendelea kukamilisha ujenzi wa Maabara Kuu ya Kilimo Mtumba Dodoma ili kudhibiti ubora wa mazao.

**5.5 Kuimarisha Maendeleo ya Ushirika**

400. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha Vyama vya Ushirika, Wizara kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika katika mwaka 2024/2025 imepanga kuwezesha uwekezaji katika mifumo ya kidigiti kwenye Vyama vya Ushirika na Mamlaka za Usimamizi; kuimarisha usimamizi na udhibiti wa Vyama vya Ushirika; kuwezesha vyama vya ushirika kujiendesha kibiashara na kuviwezesha kupata mitaji; na kuhamasisha ushirika kwenye sekta mbalimbali na makundi maalum. Ili kufikia malengo hayo, Wizara kupitia Tume itatekeleza yafuatayo: -

**5.5.1 Kuwezesha Uwekezaji katika mifumo ya Kidigiti kwenye Vyama vya Ushirika na Mamlaka za Usimamizi**

401. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume itaendelea kuimarisha matumizi ya mifumo ya Kidigiti katika kusimamia na kuendesha vyama vya ushirika. Katika mwaka 2024/2025 Tume itanunua na kusambaza kompyuta mpakato 129 kwa Maafisa Ushirika ili kuwawezesha kutumia Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika. Aidha, Tume kwa kushirikiana na CRDB Foundation itawezesha Vyama vya Ushirika kupata mikopo yenye riba nafuu kwa ajili ya ununuzi wa mizani ya kidigiti 1,500 katika vyama vya ushirika wa mazao.

**5.5.2 Kuimarisha Usimamizi na Udhibiti wa Vyama vya Ushirika**

402. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume itaendelea kusimamia na kudhibiti Vyama vya Ushirika kwa kufanya kaguzi za mara kwa mara za Vyama vya Ushirika 5,482. Kadhalika, COASCO itakagua Vyama vya Ushirika 5,000. Vilevile, Tume itakagua sifa za watendaji kwenye Vyama Vikuu na SACCOS daraja 'B' 118 nchini ili kuhakikisha SACCOS hizo zinakuwa na watendaji wenye sifa zinazohitajika. Aidha, itaendelea kuratibu na kusimamia taratibu zote za ajira katika Vyama vya Ushirika ili kuhakikisha vyama vinapata watendaji wenye sifa stahiki.

**5.5.3 Kuhamasisha Vyama vya Ushirika kujiendesha kibiashara na kuviwezesha kupata mitaji**

403. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume itaratibu ukamilishaji wa kuanzisha Benki ya Taifa ya Ushirika kwa kuhamasisha vyama vya ushirika kuendelea kununua hisa ili kukamilisha mtaji hitajika wa Shilingi Bilioni 20. Benki hiyo itaanza kwa kufungua matawi matatu (3) katika mikoa ya Dodoma, Mtwara na Kilimanjaro. Pia, Benki hiyo itawezesha Vyama vya Ushirika kupata mikopo na kuongeza mitaji. Aidha, Tume kwa kushirikiana na Benki ya Taifa ya Ushirika pamoja na TADB, itatoa elimu kwa vyama kuhusiana na umuhimu wa mfuko wa Kinga za Akiba na Amana za SACCOS. Vilevile, itafunguliwa akaunti maalum itakayotumika kukusanya fedha za Mfuko kwa lengo la kuwasaidia wanachama wa SACCOS iwapo SACCOS hizo zitashindwa kutekeleza majukumu kwa mujibu wa Sheria ya Huduma ndogo za Fedha ya mwaka 2018 na kanuni zake za mwaka 2019.

404. Vilevile, Tume kwa kushirikiana na Bodi ya Usimamizi wa Leseni za Ghala, COPRA na Soko la Bidhaa Tanzania itaendelea kuimarisha mifumo rasmi na jumuishi ya biashara na masoko kwa mazao mbalimbali na kuhamasisha Vyama vya Ushirika kuendelea kuuza mazao ya kilimo nje ya nchi. Aidha, ili kuwezesha upatikanaji wa mbolea kwa wakulima kwa wakati, Tume kwa kushirikiana na TFRA itaendelea kuhamasisha Vyama vya Ushirika kuwa Mawakala wa kusambaza mbolea kwa mpango wa ruzuku.

405. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa na kuviwezesha vyama kujiendesha kibiashara, Tume itaendelea kuratibu na kusimamia Vyama Vikuu kujenga viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo. Tume itahamasisha ufufuaji wa kiwanda cha kuchambua pamba na kukamua mafuta cha Manawa kilichopo Wilayani Misungwi kinachomilikiwa na chama kikuu cha Ushirika Nyanza. Vilevile, Tume itaratibu na kusimamia ufufuaji wa kiwanda cha kuchambua pamba na kukamua mafuta kinachomilikiwa na Chama kikuu cha SHIRECU kilichopo Mhunze-Shinyanga.

406. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza uzalishaji na kuwezesha Vyama vya Ushirika kujiendesha kibiashara, Tume itaratibu utambuzi na uthaminishaji wa mali za vyama vya ushirika na kutafuta wawekezaji wa kimkakati kwa kushirikiana na Kituo cha Uwekezaji Tanzania. Hatua hiyo, itawezesha Vyama vya Ushirika kuwa na kumbukumbu za kiuhasibu za mali za vyama, kuongeza tija na kuvifanya kuwa shindani na endelevu.

### 5.5.4 Kuhamasisha Ushirika kwenye sekta mbalimbali na makundi maalum

407. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume itahamasisha vikundi 520 vinavyotekeleza shughuli mbalimbali za kiuchumi katika Sekta ya Kilimo, mifugo, uvuvi, madini, viwanda na fedha pamoja na wanawake, vijana na watu wenye ulemavu 20,000 ili kujiunga na kuanzisha Vyama vya Ushirika. Vilevile, Tume kwa kushirikiana na wadau itaviunganisha vyama vipya vya ushirika wa mbogamboga na wadau wa masoko pamoja na kuwajengea uwezo viongozi na wanachama wa Vyama hivyo kuhusu uendeshaji wa Vyama vya Ushirika na kuendelea kuhamasisha uanzishaji wa Vyama vya Ushirika vya mbogamboga.

**5.6 Kuimarisha Matumizi ya Mifumo ya TEHAMA katika Uendelezaji wa Sekta ya Kilimo (Agriculture Digitalization)**

408. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuimarisha utendaji kazi, matumizi bora ya rasilimali za kilimo, ufuatiliaji, kutoa tahadhari ya mapema kuhusu wadudu na magonjwa na udhibiti wa milipuko ya visumbufu vya mazao na mimea, kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma kwa wadau wa kilimo, Wizara katika mwaka 2024/2025 imepanga kutekeleza mikakati ifuatayo;

**5.6.1 Kuimarisha mifumo ya kidigiti itakayowezesha upatikanaji wa taarifa sahihi kwa wakati**

409. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025 Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari itaunganisha mifumo ya ndani ya Wizara na Taasisi zake na kuwa na mfumo mmoja ambao utaweza kusomana na mifumo ya nje ya Wizara ikiwemo mifumo ya NBS, Benki Kuu na TRA kwa lengo la kuongeza ufanisi katika ubadilishanaji wa taarifa.

**5.6.2 Kuwekeza kwenye matumizi ya mifumo ya kidigiti katika Sekta ya Kilimo**

410. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2024/2025 itatoa mafunzo kuhusu matumizi ya mifumo ya kidigiti kwa wadau wa kilimo ili kuwezesha matumizi ya mifumo hiyo. Kadhalika, Wizara itajenga miundombinu ya kisasa ya kidigiti kwa ajili ya uendelezaji wa kilimo kwa kutumia teknolojia kama vile *Internet of Things* (IoT), Akili Bandia (AI), vitambuzi visivyotumia waya (Sensor), na uchambuzi wa taarifa. Vilevile, Wizara itanunua vifaa vya TEHAMA kulingana na teknolojia mpya na ya kisasa ili kuongeza ufanisi wa mifumo ya kidigiti katika utoaji wa huduma. Aidha, Wizara itawawezesha vijana na wanawake kutumia elimu ya uvumbuzi katika kilimo na kusaidia kukuza teknolojia mpya za kilimo.

411. Kadhalika, katika kuwa na uendelevu wa kuibua na kuleta mawazo bunifu, Wizara itajenga kituo cha ubunifu wa teknolojia katika Mkoa wa Dodoma na kuweka teknolojia wezeshi ili kutoa fursa kwa vijana waweze kufanya ugunduzi, ubunifu na umaridadi wa mawazo bunifu ya teknolojia zitakazosaidia katika uendelezaji wa sekta ya kilimo.

**MAENEO MENGINE MUHIMU YATAKAYOTEKELEZWA NA WIZARA**

412. ***Mheshimiwa Spika,*** maeneo mengine muhimu yatakayotekelezwa ni pamoja na kupitia Sheria za Kilimo, urasimishaji wa shughuli za kilimo, kuongeza matumizi ya teknolojia na mbinu za kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi, jinsia na VVU na UKIMWI.

**i. Kupitia Sera, Sheria za Kilimo, Makubaliano na Miongozo ya uendeshaji wa shughuli za kilimo**

413. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kutekeleza kwa ufanisi vipaumbele na mikakati iliyowekwa na Wizara yapo maeneo mbalimbali yatakayotekelezwa ili yawezeshe ufikiwaji wa malengo yaliyowekwa. Kwa kuzingatia hayo, Wizara kwa mwaka 2024/2025 imepanga kuendelea na maboresho ya Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya mwaka 2002 na Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya Mwaka 2013; na kukamilisha uanzishwaji wa Mpango wa Mageuzi ya Kilimo (Agricultural Transformation Master Plan – 2050). Aidha, Wizara itaendelea na taratibu za kutunga Sheria ya Kilimo itakayowezesha kuwa na mfumo wa kisheria wa usimamizi na uratibu wa Sekta katika maeneo muhimu ikiwemo usimamizi na uendelezaji wa ardhi ya kilimo, kuhamasisha matumizi ya zana bora za kilimo na usimamizi wa kilimo cha mkataba.

414. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaanzisha *compact* ambayo tutasaini na wadau wa maendeleo ambao watatakiwa kutekeleza miradi ya vipaumbele vya Wizara ili kupunguza upotevu wa rasilimali za fedha zinazotumiwa na wadau wa maendeleo kwa gharama ya wakulima. Hivyo, wadau wote watatakiwa kusaini na ambaye hatasaini *compact* hiyo, Wizara itafuta makubaliano kati yake na mdau huyo.

**ii. Kuongeza Matumizi ya Teknolojia na Mbinu za Kilimo Kinachohimili Mabadiliko ya Tabianchi na Uhifadhi wa Mazingira**

415. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2024/2025, itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Mazingira katika Sekta ya Kilimo. Aidha, Wizara itaendelea kufanya tathmini ya athari za mazingira na jamii kwenye mashamba makubwa 10 yaliyo kwenye programu ya BBT na kuendelea na uhamasishaji wa kilimo chenye kutunza mazingira kwenye mashamba hayo. Pia, Wizara itasambaza mkakati wa kilimo ikolojia Hai kwa njia ya

mafunzo kwa maafisa ugani 120 katika Halmashauri 30 ili kuweza kuwafundisha wakulima kutumia mbinu za kilimo ikolojia kutunza mazingira na kuzalisha bidhaa zenye sifa ya kuingia katika masoko ya ndani na kimataifa ya kilimo hai.

416. Vilevile, Wizara kupitia mradi wa mifumo himilivu ya chakula itatoa mafunzo ya matumizi sahihi ya pembejeo za kilimo kwa wakulima 200 kwenye mashamba 13 ya ASA; itaandaa Mpango Husishi wa Usimamizi wa Wadudu (IPMP) kwenye mashamba ya ASA yaliyo chini ya mradi; na kuendelea na utekelezaji wa Mpango wa Usimamizi wa Mazingira na Jamii kwenye mradi wa kuwezesha upatikanaji wa pembejeo za kilimo.

417. Kadhalika, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itafanya tathmini ya athari kwa mazingira na jamii katika mabwawa 15 ya umwagiliaji, miradi 20 ya umwagiliaji na kufanya ukaguzi wa kimazingira katika miradi 30 ya umwagiliaji inayoendelea. Pia, Wizara itaandaa na kusambaza mpango wa mazingira na jamii katika skimu 30 pamoja na kuandaa na kusambaza mpango wa matumizi sahihi ya viuatilifu katika skimu 25 na kutoa mafunzo kwa wakulima 4,000 kuhusu utunzaji wa mazingira na njia sahihi za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi katika skimu za umwagiliaji 100.

418. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TARI imepanga kufanya tafiti mbalimbali kwa ajili ya kupata teknolojia za utunzaji wa mazingira ikiwemo utafiti kwa ajili ya kupata kanuni itakayosaidia kukadiria kiasi cha hewa ya ukaa kwenye mauzo ya kaboni kwa ajili ya utunzaji wa mazingira. Vilevile, TARI itaendelea kufanya tafiti ambazo zitazalisha teknolojia zinazostahimili mabadiliko ya tabianchi.

**iii.Jinsia**

419. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2024/2025 itaendelea kuhakikisha uzingatiaji wa masuala ya jinsia katika kilimo cha mazao mbalimbali. Wizara kupitia Mradi wa TAISP itawezesha uandaaji wa Mpango Kazi wa Kijinsia (Gender Action Plan) ambao utatekelezwa na Mradi. Aidha, Mradi utaendelea kuhakikisha kuwa masuala ya kijinsia yanazingatiwa katika utoaji wa pembejeo za kilimo ikiwemo utoaji wa ruzuku ya mbegu na mbolea pamoja na

utoaji wa mafunzo kupitia vikundi vya wakulima katika mashamba darasa ya Mradi. Kadhalika, Wizara kupitia Programu na Miradi mbalimbali ikiwemo BBT, AFDP, TANIPAC na TFSRP itaendelea kutekeleza shughuli zake kwa kuzingatia masuala ya jinsia.

**iv. VVU na UKIMWI**

420. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2024/2025 itaendelea kutoa huduma ya lishe na dawa kwa watumishi wanne (4) wanaoishi na VVU, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza (MSY). Vilevile, Wizara itaratibu vikao vinne (4) vya waelimisha rika kwa lengo la kubadilishana taarifa na kutathmini hali ya utekelezaji wa afua za VVU, UKIMWI na MSY mahala pa kazi katika Utumishi wa Umma. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara yenye dhamana ya masuala ya afya itaendelea kutoa elimu ya VVU, UKIMWI na MSY na kuweka vifaa kinga (kondomu) katika majengo yote ya Wizara na Taasisi zake ili kupunguza maambukizi mapya.

**Maeneo Mengine yatakayotekelezwa**

421. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa vipaumbele Wizara itaendelea kutekeleza yafuatayo :-

i. Kuendelea kuandaa Mpango wa Mageuzi ya Kilimo (Agricultural Transformation Masterplan - 2050) utakaoongoza Maendeleo ya Sekta ya Kilimo kwa kipindi cha miaka 25. Mpango huo utasimamia mabadiliko ya kisera, kimuundo na kimkakati;

ii. Kuendelea kufanya marekebisho ya Sheria ya Sukari Na.6 ya mwaka 2001 kwenye sheria ya fedha ya mwaka 2024 ili kuiwezesha NFRA kununua na kuhifadhi sukari kwenye Hifadhi ya Chakula ya Taifa ili kunusuru hali ya upatikanaji wa sukari inapotokea kudorora kwa soko la sukari;

iii. Kuendelea kufanya marekebisho ya Sheria ya Tasnia ya Korosho Na.18 ya mwaka 2009 kwenye sheria ya fedha ya mwaka 2024 ili kuwezesha mapato yanayotokana na mauzo ya korosho ghafi (export levy) asilimia 100 kwenda kwenye ununuzi wa pembejeo ya zao la korosho pamoja na kulipa madeni ya pembejeo; na

iv. Kuendelea na marekebisho ya Sheria ya Chai Na.3 ya mwaka 1997 kwenye sheria ya fedha ya mwaka 2024 ili kuiwezesha Bodi kuwa na mapato kwa ajili ya kujiendesha;

v. Kufanya mapitio ya Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji Na.4 ya Mwaka 2013 ili kuvipa nguvu ya kisheria vyama vya umwagiliaji;

vi. Wizara ya Kilimo itahakikisha inakamilisha mazungumzo na Wizara ya Uwekezaji na Wizara ya Fedha ili mashamba ya maua yaliyopo Arusha na mashamba yaliyokuwa yanamilikiwa na NAFCO yaanze kutumika; na

vii. Kuandaa mpango wa utoaji wa ruzuku ya mbegu bora kwa wakulima ambayo utekelezaji wake utaanza mwaka 2025/2026.

**Hitimisho na Shukrani**

422. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba nitumie fursa hii kuzishukuru Nchi na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa ambayo yamesaidia Wizara katika juhudi za kuendeleza kilimo. Baadhi yao kama ifuatavyo: Serikali za Japan, Marekani, Uingereza, China, Indonesia, Korea ya Kusini, India, Misri, Kuwait, Israel, Ubelgiji, Ujerumani, Finland, Norway, Brazil, Uholanzi, Ireland, Malaysia, Vietnam, Canada, Poland, Umoja wa Ulaya na Umoja wa Falme za Kiarabu.

423. ***Mheshimiwa Spika***, ninaomba nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais na Serikali nzima ya Chama Cha Mapinduzi kwa kuendelea na safari ya kuwekeza kwenye Sekta ya Kilimo na kukubali uwekezaji huu kwenye maeneo ya msingi kwa kuongeza Bajeti ya Kilimo kutoka Shilingi Bilioni 294 hadi leo tunapoenda kuomba kuidhinishiwa Bajeti ya Shilingi Trilioni 1.248. Uwekezaji huo umechochea ukuaji wa Sekta ya kilimo kutoka asilimia 2.7 mwaka 2022 hadi asilimia 4.2 mwaka 2023, mauzo ya nje ya nchi kutoka Dola za Marekani Bilioni 1.2 mwaka 2019/2020 hadi Dola za Marekani Bilioni 2.3 mwaka 2022/2023 na Utoshelevu wa chakula kutoka asilimia 114 mwaka 2021/2022 hadi asilimia 124 mwaka 2022/2023.

424. ***Mheshimiwa Spika***, ninamshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais kwa kuweka fedha nyingi kwenye eneo la umwagiliaji kwa kipindi

cha miaka mitatu (3) mfululizo kutoka Shilingi Bilioni 46.5 mwaka 2021/2022, Shilingi Bilioni 361.5 mwaka 2022/2023, Shilingi Bilioni 361.5 mwaka 2023/2024 na leo tunaomba kuidhinishiwa Shilingi Bilioni 393.3 kwa ajili ya miradi ya umwagiliaji. Kukamilika kwa miradi hiyo kutaongeza eneo la umwagiliaji lenye jumla ya hekta 543,366.46 na kutengeneza ajira takribani 2,146,887.

425. ***Mheshimiwa Spika***, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuiwezesha NFRA kuwa mnunuzi mkuu wa mazao ya nafaka kutoka kwa wakulima. Pia, ninamshukuru Mheshimiwa Rais na Bunge lako Tukufu kwa kukubali na kuamini kuwa uwekezaji wa kutoa ruzuku na baadaye kuyanunua mazao ya wakulima hususan ya chakula ni muhimu kwa uchumi wetu.

426. ***Mheshimiwa Spika***, ninamshukuru Mheshimiwa Rais na Bunge lako Tukufu kwa kukubali kuwekeza katika Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC) kutoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima na kukubali kuanza uhakiki kwa ajili ya kulipa madeni kwa wazabuni wa pembejeo za ruzuku msimu wa 2015/2016 na madeni ya Sekta ya pamba ya mwaka 2019/2020. Aidha, Serikali itaanza uhakiki wa madeni kwenye Sekta ya korosho na madeni ya pembejeo za ruzuku kwa msimu wa 2014/2015 ili kulipa madeni hayo.

427. ***Mheshimiwa Spika***, maamuzi ya kuwekeza kwenye Sekta ya kilimo yanamaanisha kuwa *rural transformation* inaweza kutokea katika nchi yoyote Duniani. Kwa hatua zinazochukuliwa kwenye kilimo, REA, TARURA na Maji vijijini, zinathibitisha kuwa Serikali ya Awamu ya Sita imejipambanua kutekeleza kwa vitendo kwa kuleta maendeleo vijijini ili kujenga uchumi jumuishi.

428. Ninayashukuru pia Mashirika na Taasisi za Kimataifa zifuatazo: Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Taasisi za Fedha, IMF, AU, IFAD, UNDP, FAO, JICA, EU, UNICEF, WFP, ENABEL, USAID, KOICA, ICRAF, AGRA, IITA, IRRI, ILRI, CABI, EAC, ILO ASARECA, CCARDESA, SADC, SAGCOT, TPSF, World Vegetable Centre, CIP, CIAT/ PABRA, UNEP, WARDA, Shirika la Kudhibiti Nzige wa Jangwani (DLCO-EA) na HELVETAS. Pia, Wadau wengine ni Shirika la Kudhibiti Nzige Wekundu (IRLCO-CSA), Bill and Melinda Gates Foundation, Gatsby Trust, TAHA, Rockfeller Foundation, Aga Khan Foundation, Unilever na Asasi zisizo za kiserikali nyingi ambazo hatuwezi kuzitaja zote

hapa. Ninaomba niwaambie wadau wa maendeleo mjiandae kusaini *compact* ili uwiano wa uwekezaji uwe kwa asilimia 80 kwenye miundombinu na asilimia 20 kujenga uwezo.

429. ***Mheshimiwa Spika,*** ninawashukuru sana wakulima wa nchi hii kwa kuendelea kufanya kazi katika mazingira magumu na kuendelea kulinda uchumi wa nchi yetu na usalama wa nchi. Aidha, ninawashukuru sana kundi la wafanyakazi katika sekta ya umma na binafsi ambao wameanza kuwekeza kwenye Sekta ya kilimo. Aidha, kundi hilo limeanza kukopa mikopo ya mishahara na kuwekeza kwenye kilimo. Ninaomba niwaambie shambani kuna changomoto lakini hatma ya kesho ya Dunia hii ni kilimo. Hivyo, Serikali itaendelea kushirikiana nao katika kutatua changamoto hizo.

## 6 MAOMBI YA FEDHA MWAKA 2024/2025 FUNGU 43, 24 na 05

### 6.1 Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli

430. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2024/2025 inatarajia kukusanya Shilingi **10,600,254,000** kupitia Fungu 43 na Fungu 05. Kati ya fedha hizo, Shilingi **7,000,254,000** zitakusanywa kutokana na ukaguzi wa mazao, kodi za majengo na uuzaji wa nyaraka za zabuni kupitia Fungu 43 na Shilingi **3,600,000,000** kutokana na ada za umwagiliaji na ukodishaji wa mitambo kupitia Fungu 05.

### 6.2 Fedha za Matumizi kwa Mafungu yote

431. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025 Wizara ya Kilimo inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi **1,248,961,680,000** kupitia Fungu 43, Fungu 05 na Fungu 24.

#### 6.2.1 Fedha kwa Fungu 43

432. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Shilingi **824,069,158,000** zinaombwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi **700,318,469,000** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya maendeleo ambapo Shilingi **525,642,532,000** ni fedha za ndani na Shilingi **174,675,937,000** ni fedha za nje. Aidha, Shilingi **123,750,689,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo Shilingi **69,894,933,000** ni kwa ajili ya mishahara na Shilingi **53,855,756,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo ya Wizara, Bodi na Taasisi.

**6.2.2 Fedha kwa Fungu 05**

433. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi **403,783,833,000**. Kati ya fedha hizo, Shilingi **331,899,223,000** ni fedha za Maendeleo na Shilingi **71,884,610,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha za maendeleo zinazoombwa, Shilingi **288,464,223,000** ni fedha za ndani na Shilingi **43,435,000,000** ni fedha za nje. Aidha, kati ya Shilingi **71,884,610,000** ya fedha za Matumizi ya Kawaida zinazoombwa, Shilingi **64,377,780,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na Shilingi **7,506,830,000** ni kwa ajili ya Mishahara (PE) ya watumishi wa Tume.

**6.2.3 Fedha kwa Fungu 24**

434. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Tume ya Maendeleo ya Ushirika inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi **21,108,689,000.** Kati ya fedha hizo, Shilingi **20,280,063,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo Shilingi **11,954,604,000** ni mishahara (PE) ya watumishi na Shilingi **8,325,459,000** ni Matumizi Mengineyo (OC). Aidha, fedha za ndani kiasi cha Shilingi **828,626,000** zinaombwa kutekeleza miradi ya Maendeleo.

435. ***Mheshimiwa Spika,*** hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara: *www.kilimo.go.tz*

436. ***Mheshimiwa Spika,*** NINAOMBA KUTOA HOJA**.**

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Mheshimiwa Waziri, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo na kwa niaba yake namwona Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Mariam Ditopile. *(Makofi)*

**MHE. MARIAM D. MZUZURI - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, naomba kuwasilisha taarifa kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Kwa sababu ya muda naomba taarifa hii iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa mezani.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na uhai kuweza kusimama kwa niaba ya Kamati ili kutoa taarifa hii. Pia napenda kutoa shukrani kwa niaba ya Kamati kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutekeleza masharti ya Kanuni ya 118(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii ina sehemu nne; sehemu ya kwanza ni utangulizi, sehemu ya pili inabainisha uchambuzi wa namna ya bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ilivyotekelezwa na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025; sehemu ya tatu inahusu maoni mapendekezo ya Kamati na sehemu ya nne inahusu hitimisho.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 6(1)(b) kikisomwa pamoja na kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 kimeipatia Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo jukumu la kushughulikia bajeti ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza jukumu hili tarehe 25 Machi, 2024 Kamati ilichambua taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na kufanya ulinganisho kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Fungu 43 - Wizara ya Kilimo, Fungu 24 - Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Fungu 05 - Tume ya Taifa ya Umwagiliaji. Aidha, Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti yanayotaka taarifa ya utekelezaji na makadirio ya Wizara hii, kuchambuliwa na Kamati kabla ya

kujadiliwa Bungeni. Naomba Bunge lijadili hoja ya Wizara ya Kilimo kwa pamoja na taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(2), baada ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati ilifanya uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ili kuliwezesha Bunge kushauri ipasavyo kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, mambo yaliyochambuliwa ni pamoja na ukusanyaji wa maduhuli, upatikanaji wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo na upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ya Kilimo ilijiwekea lengo la kukusanya jumla ya shilingi bilioni 6.8. Hadi kufikia mwezi Februari, 2024 Wizara ilikuwa imekusanya 68% ya lengo lililokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa makusanyo ya maduhuli unaonesha kwamba: -

(a) Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ukusanyaji wa maduhuli ulikuwa wa kuridhisha, kwani hadi kufikia mwezi Februari, 2024, Wizara na taasisi zake zilifikisha wastani wa 68% ya lengo; na

(b) Mwenendo huu wa makusanyo unaonesha kuwa lengo linaweza kufikiwa ifikapo mwisho wa mwaka wa fedha.

Mheshimiwa Spika, makusanyo ya maduhuli kwa Tume ya Umwagiliaji - Fungu 05; katika mwaka wa fedha 2023/2024 Tume ilijiwekea lengo la kukusanya jumla ya shilingi bilioni 10. Hadi kufikia mwezi Februari, 2024 ilikuwa imekusanya 17% ya lengo lililokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi unaonesha kwamba: -

(a) Makusanyo haya ya 17% hayaendani na matarajio na lengo la Wizara. Hivyo, kwa kipindi kilichobaki cha utekelezaji ni vigumu kufikia lengo kwa 75% kwa kuwa muda wa utekelezaji umekwishapita; na

(b) Mwenendo huu wa makusanyo unaleta shaka kwenye makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli iwapo ulikuwa na uhalisisa.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla mwenendo wa makusanyo ya maduhuli ya Wizara unatoa mwelekeo wa kufikia lengo. Changamoto kubwa ipo kwenye ukusanyaji wa maduhuli ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ambayo makusanyo yake hayaoneshi kufikia lengo.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi ya maendeleo; kwa madhumuni ya kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua miradi ifuatayo: -

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Ukarabati wa Maabara ya Udongo – *TARI* Mlingano; Kamati ilitembelea na kukagua Mradi wa Ukarabati wa Maabara ya Udongo ya *TARI* iliyopo Mlingano, Mkoani Tanga. Kituo hiki kina majukumu ya kuratibu na kufanya utafiti wa zao la mkonge na udongo. Kituo hiki pia kinawajibika kusambaza teknolojia zilizozalishwa, kuelimisha wakulima na wadau wengine kutumia teknolojia hizo.

Mheshimiwa Spika, mradi huu ulitengewa shilingi milioni 500 kwa ajili ya ukarabati. Hadi Kamati inautembelea, jumla ya shilingi milioni 350 sawa na asilimia 70 zilikuwa zimepokelewa ambapo ukarabati wa maabara ulikuwa umefikia 65%. Mradi huu ukikamilika utaongeza tija kwa kuimarisha maabara ya udongo ili iweze kupima na kutoa takwimu zenye ubora wa kutambulika kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kwamba ili mradi huu ulete tija iliyokusudiwa, Serikali iweke vipaumbele katika ukarabati wa maabara hizi za *TARI* ili kukamilisha maabara moja baada ya nyingine. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa Serikali inaendelea kukamilisha ithibati ili maabara itambulike kimataifa. Kamati inaona

pia kuwa ni vema Serikali ikaongeza kasi ya kukamilisha ithibati hiyo ili maabara ilete tija iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, mradi wa ukarabati wa ghala la Kipawa; Kamati ilitembelea na kukagua mradi wa ukarabati wa ghala uliopo eneo la Kipawa, Dar es Salaam. Ghala hili ni moja ya vyanzo vya mapato vya Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai. Kamati ilielezwa kuwa mradi huu una lengo la kuongeza na kuimarisha uwezo wa taasisi katika kutekeleza majukumu yake ambapo inatarajiwa kuchangia shilingi milioni 325.5 kama pato la ndani pamoja na kutoa ajira kwa washitiri watakaotumia ghala hili.

Mheshimiwa Spika, mradi huu ulitengewa jumla ya shilingi milioni 790 ambazo ni fedha za ndani kwa ajili ya shughuli ya ukarabati wa ghala. Hadi Kamati inatembelea mradi huu, shughuli ya ukarabati ilikuwa imekamilika. Kwa ujumla Kamati iliridhika na kazi iliyofanyika na kuitaka Serikali kuhakikisha inatumia ghala hilo kama ilivyokusudiwa ili kupunguza utegemezi wa taasisi kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa fedha ya matumizi ya kawaida; katika mwaka wa fedha 2023/2024 Fungu 43 - Wizara ya Kilimo iliidhinishiwa na Bunge bajeti ya shilingi bilioni 112 sawa na 13.9% ya bajeti yote kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Februari, 2024 Wizara ilipokea 66.6% ya bajeti iliyotengwa. Uchambuzi unaonesha kuwa hali ya upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida inaridhisha na hivyo kuleta matumaini ya kukamilisha lengo lililokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji - Fungu 05 iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 73.5 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia mwezi Februari, 2024, fedha iliyopokelewa ni 15% tu ya fedha iliyoidhinishwa. Uchambuzi unaonesha kuwa mwenendo huu wa upatikanaji wa fedha hauridhishi na hautoi mwelekeo wa ukamilishaji wa lengo lililokusudiwa. Miradi mingi ya umwagiliaji imeathirika kutokana na upatikanaji wa fedha usioridhisha.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Fungu 24 - Tume ya Maendeleo ya Ushirika iliidhinishiwa jumla ya shilingi

bilioni 17.4 kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na 88.8% ya bajeti ya Tume. Hadi kufikia Februari, 2024 Tume ilikuwa imepokea 46% tu ya bajeti ya matumizi ya kawaida iliyoidhinishwa. Uchambuzi unaonesha kwamba kwa ujumla wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida hauridhishi na hivyo unaonesha kwamba utekelezaji wa lengo unaweza usifikiwe kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kupitia na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Fungu 43 - Wizara ya Kilimo, Fungu 24 - Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Fungu 05 - Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Kamati ilishauri masuala mbalimbali ambayo Serikali iliyazingatia.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya ushauri wa Kamati uliozingatiwa ni kama ifuatavyo: -

(a) Serikali imeanza kuzingatia ushauri wa Kamati wa kuhakikisha kuwa Programu ya *BBT* inaanzishwa kikanda na katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo halmashauri. Serikali imeendelea kuainisha na kutambua mashamba kwa ajili ya *BBT* katika mikoa mbalimbali nchini ambapo hadi kufikia Februari, 2024 jumla ya ekari laki 3.4 zilikuwa zimebainishwa kwa ajili ya *BBT* katika mikoa mbalimbali ikiwemo Dodoma, Kigoma, Mbeya, Singida, Pwani, Tanga, Njombe na Kagera. Aidha, Serikali imeahidi kuziwezesha halmashauri ambazo zitatenga mashamba ya pamoja na kudahili vijana na wanawake kujenga miundombinu ya umwagiliaji;

(b) Serikali imeendelea kutoa elimu ya mpango wa ruzuku kupitia vikao vya wakuu wa mikoa, wilaya, maafisa kilimo vipindi vya redio na runinga. Aidha, kutokana na mpango huo, hadi kufikia mwezi Machi, 2024, jumla ya wakulima milioni 3.8 wamesajiliwa kati ya lengo la kusajili wakulima milioni saba ifikapo mwaka 2025/2026; na

(c) Ili kukabiliana na upotevu wa mazao baada ya mavuno, Serikali imeendelea na ujenzi wa miundombinu ya

kuhifadhi mazao ya kilimo baada ya kuvunwa ambapo hadi kufikia Februari, 2024, ujenzi wa ghala 28 umefikia wastani wa 75%. Maghala hayo yamejengwa maeneo mbalimbali ikiwemo Ruvuma katika Halmashauri ya Songea maghala 11, Madaba maghala tisa, Namtumbo maghala saba pamoja na ujenzi wa maghala 12 kupitia Mradi wa *TANIPAC* ambao umekamilika na kukabidhiwa *NFRA*.

Mheshimiwa Spika, katika hatua mbalimbali Kamati imeridhika kwamba ushauri wake unaendelea kuzingatiwa na Wizara pamoja na Tume katika utekelezaji wa majukumu yake. Aidha, upatikanaji wa fedha usioridhisha umeendelea kuwa kikwazo kwa Wizara na hivyo kushindwa kuzingatia ushauri wa Kamati. Hivyo Kamati inaisisitiza Serikali kutoa fedha kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya maduhuli; kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ya Kilimo - Fungu 43 inategemea kukusanya jumla ya shilingi bilioni saba, kiasi kinachotarajiwa kukusanywa ni ongezeko la asilimia tano ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi unaonesha kuwa: -

(a) Kwa ujumla makadirio ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2024/2025 yameongezeka kwa asilimia tano ikilinganishwa na lengo la makusanyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024; na

(b) Kutokana na mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kufikia 68% ndani ya robo tatu ya muda wa lengo, kuna uwezekano wa kufikia lengo la makusanyo lililowekwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kwa kuzingatia uzoefu wa makusanyo ya mwaka uliotangulia.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Fungu 05 - Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inakadiriwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 3.6 ambayo ni pungufu kwa 64% ya lengo la maduhuli kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Uchambuzi unaonesha kwamba kwa ujumla

makadirio ya maduhuli kwa mwaka 2024/2025 yameshuka kwa 64% ikilinganishwa na lengo la maduhuli ya mwaka wa fedha 2023/2024. Kamati inaona bado ni muhimu Tume ikajiwekea mikakati itakayoiwezesha kuongeza makusanyo ya maduhuli kwa mwaka huu wa fedha ili kuleta tija iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa matumizi ya kawaida; mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ya Kilimo, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na Tume ya Maendeleo ya Ushirika wanakadiria kutumia shilingi bilioni 215.9 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Fedha hizi ni ongezeko la matumizi ya kawaida kwa asilimia sita ikilinganishwa na bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, kufuatia ongezeko la asilimia sita kwenye bajeti ya matumizi ya kawaida, linatoa mwelekeo mzuri kwani fedha hizi zitaongeza msukumo wa kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa bajeti ya miradi ya maendeleo. Ongezeko hili la bajeti linategemewa kwenda sambamba na upatikanaji wake kwa wakati ili kutekeleza majukumu yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa programu za umwagiliaji, usambazaji wa mbolea pamoja na pembejeo za kilimo kwa wanachi kwa wakati, ufanisi wake unategemea upatikanaji wa fedha kwa kiwango stahiki na kwa wakati. Kama inavyoelekezwa katika ibara ya 37 ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, ibara hii imeahidi kusimamia kikamilifu hifadhi na matumizi endelevu ya maji, ardhi ya kilimo na mazingira, sambamba na kuongeza miundombinu ya umwagiliaji itakayoendeshwa kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ongezeko hilo la bajeti ya matumizi ya kawaida, Kamati inaona kuwa bado fedha iliyoongezwa haikidhi mahitaji kulingana na uzito wa majukumu makubwa yaliyopo katika kuhakikisha tija inaongezeka kwenye kilimo kwa kuboresha miundombinu ya umwagiliaji, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya hifadhi ya mazao, kuimarisha vituo vya utafiti, upatikanaji wa pembejeo, kuimarisha huduma za ugani pamoja na kuimarisha usimamizi na ukaguzi wa vyama vya ushirika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu makadirio ya matumizi kwa ajili ya miradi ya maendeleo; Kamati ilichambua makadirio ya jumla ya

shilingi trilioni 1.02 kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo inayopangwa kutekelezwa na Wizara ya Kilimo, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Makadirio hayo ni ongezeko la 24% ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa jumla unaonesha kwamba bajeti ya maendeleo kwa Wizara ya Kilimo, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na Tume ya Maendeleo ya Ushirika imeongezeka kwa 24% ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2023/2024. Nyongeza hii inaweza kuashiria mwelekeo wa kufikia malengo yaliyowekwa kwenye mpango wa kuendelea kuongeza tija na uzalishaji katika sekta ya kilimo. Aidha, nyongeza ya bajeti ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo inaweza kuleta tija kama Serikali itazingatia utoaji wa fedha hizo kwa mtiririko na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kulingana na uchambuzi huu, Wizara na taasisi zilizo chini yake zitaongeza uwezo wa utekelezaji wa miradi ikilinganishwa na utekelezaji ulivyokuwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati; baada ya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa bajeti pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Kilimo, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji pamoja na Tume ya Maendeleo ya Ushirika, ninaomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa Wizara ya Kilimo – Fungu 43:-

(a) Pamoja na Serikali kuendelea kuongeza bajeti ya kilimo, bado haikidhi mahitaji halisi ya sekta hii kwa kuzingatia matakwa ya utekelezaji wa Azimio la Maputo la mwaka 2003 na Malabo la mwaka 2014 linalozitaka nchi wanachama kutenga 10% ya bajeti ya Taifa kwa ajili ya sekta ya kilimo. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kutenga bajeti na fedha hizo kutolewa kwa wakati ili kuwezesha utekelezaji wa malengo na mikakati iliyokusudiwa.

(b) Uzalishaji duni na usio na tija wa mazao ya kilimo unatokana na kukosekana kwa mbolea ya kutosha na kwa wakati. Kamati inaishauri Serikali kuweka nguvu na kuchukua hatua za makusudi za kuzalisha pembejeo hapa nchini ikiwemo mbolea, mbegu na viuatilifu.

(c) Pamoja na Serikali kuweka mfumo mzuri wa utoaji wa mbolea ya ruzuku nchini, bado mfumo huo haujafahamika ipasavyo kwa wakulima wengi na hivyo kutoleta tija iliyokusudiwa. Kamati inaishauri Serikali kwamba:-

(i) Elimu iendelee kutolewa kuhusu uwepo wa mbolea ya ruzuku na namna ya kuipata ili kudhibiti mianya inayotumiwa na watu wachache ya kuuza mbolea kwa bei ya juu; na

(ii) Wizara iendelee kuongeza kasi ya kutoa elimu kwa wakulima kuhusu matumizi bora na sahihi ya mbolea pamoja na viuatilifu.

(d) Hakuna tija katika kilimo bila uwepo wa wataalamu wa kutosha yaani Maafisa Ugani ambapo mahitaji ni takribani wagani 20,000, lakini waliopo ni 35% tu ya mahitaji. Upungufu huu hauwezi kuleta matokeo yanayotarajiwa. Kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu wa kutenga bajeti na kuajiri Maafisa Ugani wa kutosha ili kutoa huduma za ugani na kuleta tija iliyokusudiwa.

(e) Hali ya upotevu wa mazao baada ya kuvunwa imeendelea kuwa kwenye tarakimu mbili (35%) ukilinganisha na shabaha ya kupunguza upotevu huo hadi 5% ifikapo mwaka 2030. Hali hii inaathiri usalama na upatikanaji wa chakula cha uhakika wakati wote nchini. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuimarisha miundombinu na kukamilisha ujenzi wa maghala ya kutosha katika ngazi za vijiji, kata na wilaya hasa kwenye maeneo yenye uzalishaji mkubwa wa mazao ya chakula.

(f) Mahitaji ya mbegu bora na za kutosha ni suala ambalo haliepukiki iwapo tunataka kuzalisha kwa tija na kuwanufaisha wakulima na wananchi kwa ujumla. Kamati inaishauri Serikali yafuatayo: -

(i) Kuendelea kuziwezesha taasisi zinazohusika na utafiti na uzalishaji wa mbegu kifedha, pamoja na kuimarisha miundombinu ya uzalishaji ili ziweze kuzalisha mbegu bora na za kutosheleza mahitaji yaliyopo nchini;

(ii) Kuweka mazingira ya kushirikisha sekta binafsi katika uzalishaji wa mbegu ili kupunguza matumizi ya fedha za kigeni zinazotumika kuagiza mbegu; na

(iii) Iweke mikakati ya kudhibiti mfumuko wa bei za mbegu kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo kuweka bei elekezi. Aidha, wananchi wapate taarifa sahihi kuhusu bei hizo na mbegu ziwafikie wakulima kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, ukosefu wa masoko ya uhakika ya mazao ya kilimo katika maeneo mengi ya wakulima nchini na nje ya nchi kumepelekea sekta ya kilimo kutochangia ipasavyo, lakini pia kuwakatisha wakulima tamaa ya kulima kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto hii, Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za makusudi kuhakikisha upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo hapa nchini na nje ya nchi unakuwa wa uhakika. Aidha, Serikali iweke mikakati mahsusi ya kuhakikisha kuwa mazao yanawekewa mnyororo wa thamani hapa nchini ili kuwanufaisha wakulima.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya sekta yoyote yanatokana na tafiti za kutosha kuhusu sekta husika. Sekta ya kilimo inahitaji kuziwezesha taasisi zake za utafiti ili kuongeza tija katika kilimo. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali: -

(i) Kuendelea kuimarisha miundombinu ya utafiti kwa kujenga miundombinu mipya na kukarabati iliyopo. Aidha, ukarabati uzingatie vipaumbele ili kukamilisha eneo moja baada ya lingine kuliko ilivyo sasa ambapo ukarabati unafanyika kwa sehemu katika vituo vingi na hivyo kukosa tija;

(ii) Kuendelea kuwekeza na kuimarisha Taasisi za Utafiti wa Kilimo nchini ikiwa ni pamoja na kuwaongezea rasilimali watu na rasilimali fedha kwa ajili ya utafiti na kuendelea kuwajengea uwezo watafiti wa kilimo ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi na kukuza sekta ya kilimo nchini; na

(iii) Kuongeza kasi katika kufufua uzalishaji wa mbegu za asili (mbegu za wakulima). Kuendeleza na kutunza mbegu hizi kutasaidia kulinda chanzo cha nasaba za mimea ambacho ni msingi wa tafiti zote, pia uzalishaji wa mazao ya asili utasaidia upatikanaji wa lishe bora katika chakula na kuchangia kujitosheleza kwa virutubisho na kupunguza ulazima wa virutubisho vya viwandani. Aidha, Serikali iweke mfumo wa kisheria utakaoruhusu uzalishaji na usambazaji wa mbegu za asili nchini.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Jenga Kesho Bora *(BBT)* imeanza kuonesha mwelekeo mzuri katika maeneo machache yaliyoanza kutekelezwa. Ili programu hii inufaishe vijana wengi zaidi, Kamati inaishauri Serikali yafuatayo: -

(i) Iboreshe mfumo wa upatikanaji wa vijana ili vijana wengi wapate fursa ya kushiriki. Naomba kurudia, iboreshe mfumo wa upatikanaji wa vijana ili vijana wengi wapate fursa ya kushiriki. *(Makofi)*

(ii) Ihakikishe fursa hii inawafikia vijana na wanawake katika halmashauri zao kwa kuanzisha mpango huu katika mikoa yote na halmashauri zote nchini;

(iii) Mikakati ya kuwawekea masoko ya uhakika iendelee ili kuwanufaisha vijana hao ili tija iliyokusudiwa iweze kufikiwa;

(iv) Iendelee kutekeleza mipango yake kwa kadiri ilivyojiwekea ili kutowakatisha tamaa vijana na wanawake; na

(v) Vijana waliopo na wanawake katika mashamba hayo, waendelee kuhamasishwa kulinda ajira hizo ili kuwa mfano kwa vijana wengine wenye mahitaji hayo na kujenga uwezo endelevu kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji – Fungu 05; kuhusu utekelezaji wa mipango ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Kamati inashauri yafuatayo: -

(a) Ukusanyaji hafifu wa maduhuli ya Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji unaipotezea Serikali mapato. Kamati inaishauri Tume ihakikishe inaweka utaratibu utakaohakikisha kuwa watumiaji wa maji wanalipa tozo za maji na kuiwezesha Tume kufikia malengo iliyojiwekea;

(b) Mchango mdogo wa kilimo cha umwagiliaji katika sekta ya kilimo unatokana na ufinyu wa bajeti na ucheleweshaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji pamoja na idadi ndogo ya wataalamu wa umwagiliaji. Kamati inashauri kuwa Serikali iendelee kuongeza bajeti ya kutosha kwa ajili ya umwagiliaji. Fedha hizo pia zitolewe kwa wakati ili kufikia malengo ya kufikisha eneo la umwagiliaji hekta milioni nane ambayo ni sawa na hekta milioni moja kwa mwaka ifikapo mwaka 2030. Hatua hizi zitawezesha kufikia lengo la kukuza sekta ya kilimo kwa asilimia kumi (Ajenda 10/30);

(c) Kutokuwepo kwa mfumo madhubuti wa miradi ya umwagiliaji inayolingana na mahitaji ya wakulima hasa kwenye maeneo ya vijijini, kumeendelea kuwa kikwazo cha kufikia malengo ya kuinua kilimo kwa njia ya umwagiliaji. Kamati inaishauri Serikali kuongeza juhudi katika kuweka mifumo imara na madhubuti katika miradi ya umwagiliaji katika maeneo yote nchini ikiwa ni pamoja na kuchimba mabwawa, kuvuna maji na kujenga

miundombinu ya umwagiliaji ili kufikia lengo lililokusudiwa; na

(d) Serikali iweke mazingira mazuri ili kuvutia sekta binafsi katika uwekezaji kwenye sekta ya umwagiliaji ili ardhi inayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji itumike kikamilifu na kuongeza tija.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Tume ya Maendeleo ya Ushirika – Fungu 24; mgawanyo wa majukumu na uwajibikaji katika Tume umepunguza ufanisi na kusababisha changamoto hasa za kiusimamizi na uwajibikaji wa Maafisa Ushirika. Kamati inaendelea kuitaka Serikali kukamilisha mapitio ya Sheria ya Ushirika ili kutatua changamoto zinazotokana na usimamizi na uwajibikaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wakala wa Ukaguzi wa Ushirika, Kamati inaishauri Serikali yafuatayo: -

(i) Iijengee uwezo *COASCO* ili iweze kufanya kazi kwa kujitegemea badala ya kufadhiliwa na Ushirika inayoikagua;

(ii) Iajiri watumishi wa kutosha na wenye uwezo katika sekta ya ushirika; na

(iii) Ihakikishe *COASCO* wanafanya ukaguzi ili kuvifikia Vyama vya Ushirika katika mikoa yote.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia njema ya Serikali kuanzisha Benki ya Ushirika kwa lengo la kuwawezesha wakulima kupata huduma za kifedha kwa karibu zaidi, bado Kamati inashauri yafuatao: -

(i) Kuendelea kuimarisha benki hii kwa kuhakikisha inapata mtaji toshelevu;

(ii) Iweke mfumo mzuri utakaoviwezesha Vyama Vikuu vya Ushirika pamoja na Vyama vingine vya Ushirika nchini kununua hisa za benki hii kama njia ya kuimarisha na kukuza mtaji;

(iii) Serikali iimarishe utendaji wa benki kwa kuwafanyia watumishi upekuzi *(vetting)* ya kutosha ili kuepuka kurudi kwenye anguko la awali la benki hii. Aidha, watumishi waliopelekea benki hii kufilisika wachukuliwe hatua za kisheria; na

(iv) Benki hii iendeshwe kibiashara ili iweze kushindana kwenye soko na benki nyingine za biashara ikizingatia kuwapa kipaumbele wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hitimisho, naomba kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, kwa ushirikiano waliouonesha katika kipindi chote cha uchambuzi wa bajeti ya Wizara ya Kilimo. Kutokana na ufinyu wa muda sitaweza kuwataja kwa majina, lakini naomba majina yao yaingizwe katika kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*).

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati tunaomba kutoa shukrani kwako wewe binafsi, lakini kwa Kamati ya Uongozi pamoja na *caucus* ya chama chetu chini ya Katibu wetu Mheshimiwa Rashid Shangazi, lakini kwa Bunge lote kwa ujumla kwa kumpendekeza na kumchagua Mheshimiwa Deo Mwanyika, Mwenyekiti wa Kamati yetu kuwa miongoni mwa Wenyeviti watatu wa Bunge hili. Nasi kama Kamati tunapenda kumpa uhakika Mheshimiwa Mwenyekiti tutampa ushirikiano wa kutosha ili aweze kutimiza heshima hii na jukumu hili kubwa alilopewa. Pia Mwenyekiti aliyepita alikuwa ni Mwenyekiti wa Bunge na sasa hivi yuko Serikalini, kwa hiyo tunamuombea kila la kheri Mheshimiwa Deo Mwanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuona umuhimu wa sekta ya kilimo. Kwa kipindi kifupi cha uongozi wake tumeshuhudia kasi kubwa ya uongezaji bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa lengo la kuongeza tija kwenye kilimo. Kwa haya mambo ambayo kwa kipindi chake cha takribani miaka mitatu ameyatenda kwenye sekta hii ya kilimo na kwa maono yake ya Tanzania kujitosheleza kwa chakula, lakini kuilisha Afrika na dunia nzima, hakika jina la Samia Suluhu Hassan

kwenye vitabu vya kumbukumbu za kilimo nchini kwetu, litaandikwa kwa wino wa dhahabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kipekee kabisa na kwa niaba ya Kamati napenda kutumia nafasi hii kumshukuru Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, ni Waziri makini, anaipenda kazi yake ya Uwaziri na kilimo kutoka moyoni, hachoki kushauriwa, ni mnyenyekevu na msikivu, kwa kweli anatoa ushirikiano wa kutosha kwa Kamati ili tuweze kufanya kazi na kuleta tija tuliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nisiwe mchoyo wa fadhila kumshukuru sana Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge na Naibu Waziri wa Kilimo, kwa ushirikiano mkubwa anaoipatia Kamati ambao kwa sehemu kubwa umechangia kuiwezesha Kamati kutekeleza shughuli zake kikamilifu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru pia watendaji wote wa Wizara ya Kilimo na taasisi zilizo chini ya Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu - Ndugu Gerald Geofrey Mweli, akisaidiwa na Naibu Katibu Mkuu - Ndugu Hussein Mohamed Omary. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee namshukuru Katibu wa Bunge - Ndugu Nenelwa Mwihambi, kwa kuwangoza vyema watumishi wa Ofisi ya Bunge katika uratibu na usimamizi wa shughuli za Kamati kwa ujumla hadi kukamilika kwa taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee Kamati yetu unavyoona inafanya kazi kwa weledi kwa sababu tumebahatika Makatibu wetu watatu wote ni wanawake na wanafanya kazi kwa juhudi kubwa sana, naomba kuwashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Fungu 43 - Wizara ya Kilimo, Fungu 24 – Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Fungu 05 – Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA KILIMO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 MAELEZO YA JUMLA**
**1.1 Utangulizi**

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote, napenda kutoa shukrani kwa niaba ya Kamati kwa kunipa nafasi ili niweze kutekeleza masharti ya Kanuni ya 118(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/ 2025.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii ina sehemu nne. Sehemu ya Kwanza ni utangulizi; Sehemu ya Pili inabainisha uchambuzi wa namna bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ilivyotekelezwa na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa Fedha 2024/2025; Sehemu ya Tatu inahusu maoni na mapendekezo ya Kamati; na sehemu ya nne inahusu Hitimisho.

**1.2 Msingi wa Uchambuzi**

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 6(1)(b) kikisomwa pamoja na kifungu cha 7(1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu

za Bunge, Toleo la Februari, 2023, kimeipa Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo jukumu la kushughulikia Bajeti ya Wizara ya Kilimo. Katika kutekeleza jukumu hili tarehe 25 Machi, 2024 Kamati ilichambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 43 – Wizara ya Kilimo, Fungu 24 - Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Fungu 05 – Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Aidha, Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti yanayotaka Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Wizara hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba Bunge lijadili hoja ya Waziri wa Kilimo kwa pamoja na Taarifa hii.

### 1.3 Mawanda ya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Katika kusimamia masuala ya kibajeti, Kamati imechambua **Fungu 43 -** Wizara ya Kilimo, **Fungu 24** - Tume ya Maendeleo ya Ushirika na **Fungu 05** - Tume ya Taifa ya Umwagiliaji. Uchambuzi huu ulifanyika baada ya Kamati kufanya ziara ya kujiridhisha kuhusu hali halisi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika mafungu yaliyotajwa hapo juu.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI

### 2.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu hoja ya Waziri wa Kilimo. Uchambuzi ulijielekeza katika maeneo mawili ambayo ni Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

## 2.2 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (2), baada ya ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, Kamati ilifanya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ili kuliwezesha Bunge kushauri ipasavyo kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo inajumuisha mafungu matatu, Wizara ya Kilimo - **Fungu 43**, Tume ya Maendeleo ya Ushirika – **Fungu 24** na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji - **Fungu 05**. Mambo yaliyochambuliwa ni pamoja na Ukusanyaji wa Maduhuli, Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya kugharamia Miradi ya Maendeleo na Upatikanaji wa Fedha kwa ajili ya kugharamia Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

### 2.2.1 Makusanyo ya Maduhuli kwa Wizara ya Kilimo – Fungu 43

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa Fedha 2023/2024 Wizara ya Kilimo ilijiwekea lengo la kukusanya jumla ya **Shilingi 6,77,254,000.00**. Hadi kufikia mwezi Februari, 2024 Wizara ilikuwa imekusanya **Shilingi 4,558,250,017** sawa na **asilimia 68** ya lengo lililokusudiwa. Mchanganuo wa makusanyo hayo unaonekana katika **Jedwali Na.01.**

***Jedwali Na. 1 Fungu 43 - Makadirio na Makusanyo Halisi katika mwaka wa fedha 2023/2024***

| UKUSANYAJI WA MADUHULI HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2024 | | |
|---|---|---|
| **MAKADIRIO (Tsh.)** | **MAKUSANYO (TSh.)** | **ASILIMIA** |
| **6,77,254,000.00** | **4,558,250,017** | 68 |

**Chanzo:** Randama ya bajeti ya 2023/2024 Fungu 43

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa makusanyo ya maduhuli unaonesha kwamba:-

**(a)** Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ukusanyaji wa maduhuli ulikuwa wa kuridhisha kwani hadi kufikia mwezi Februari, 2024, Wizara na Taasisi zake zilifikisha wastani wa **asilimia 68** ya lengo;

**(b)** Ukusanyaji huu pia unaweza kumaanisha kuwa makadirio ya maduhuli yalifanyika chini ya kiwango; na

**(c)** Mwenendo huu wa makusanyo unaonesha kuwa lengo linaweza kufikiwa ifikapo mwisho wa mwaka wa fedha.

### 2.2.2 Makusanyo ya Maduhuli kwa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji – Fungu 05

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa Fedha 2023/2024, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ilijiwekea lengo la kukusanya jumla ya **Shilingi 10,000,000,000**. Hadi kufikia mwezi Februari, 2024 Wizara ilikuwa imekusanya **Shilingi 1, 706,847,658** sawa na **asilimia 17** ya lengo lililokusudiwa. Mchanganuo wa makusanyo hayo unaonekana katika **J**

***Jedwali Na. 2 Fungu 05 - Makadirio na Makusanyo Halisi katika Mwaka wa Fedha 2023/ 2024***

| UKUSANYAJI WA MADUHULI HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2024 | | |
|---|---|---|
| **MAKADIRIO (Tsh.)** | **MAKUSANYO (TSh.)** | **ASILIMIA** |
| 10,000,000,000 | 1,706,847,658 | 17 |

**Chanzo: Randama ya bajeti ya 2023/2024 Fungu 05**

**Mheshimiwa Spika**, makusanyo ya maduhuli kwa fungu 05 yanaonesha kwamba: -

(a) Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imefika **asilimia 17** tu ya lengo kwa kukusanya jumla ya **Shilingi 1,706,847,658** kati ya **Shilingi**

**10,000,000,000** zilizokusudiwa. Makusanyo haya hayaendani na matarajio na lengo la Wizara.

(b) Kwa kipindi kilichobaki cha utekelezaji, ni vigumu kufikia lengo kwa kuwa asilimia 75 ya muda wa utekelezaji umeshapita;

(c) Mwenendo huu wa makusanyo unaleta shaka kwenye makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli iwapo ulikuwa na uhalisia. Aidha, mwenendo huu wa makusanyo unaweza pia kuashiria ukosefu wa mifumo madhubuti ya ukusanyaji wa maduhuli na usimamizi wake.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla, mwenendo wa makusanyo ya maduhuli ya Wizara unatoa mwelekeo wa kufikia lengo. Changamoto kubwa ipo kwenye ukusanyaji wa maduhuli ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ambayo makusanyo yake hayaoneshi kufikia lengo.

**2.2.3 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, kwa madhumuni ya kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua miradi ifuatayo: -

**i. Mradi Namba 4486** – **Mradi wa Ukarabati wa Maabara ya Udongo – TARI Mlingano.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea na kukagua Mradi wa Ukarabati wa Maabara ya Udongo ya TARI iliyopo Mlingano mkoani Tanga. Kituo hiki kina majukumu ya kuratibu na kufanya utafiti wa zao la mkonge na udongo. Kituo hiki pia kinawajibika kusambaza teknolojia zilizozalishwa, kuelimisha wakulima na wadau wengine kutumia teknolojia hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu ulitengewa **Shilingi 500,000,000** kwa ajili ya ukarabati. Hadi Kamati inautembelea, jumla ya **shilingi 350,000,000** sawa na asilimia 70 zilikuwa zimepokelewa ambapo ukarabati wa maabara ulikuwa umefikia **asilimia 65.**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu ukikamilika utaongeza tija kwa kuimarisha maabara ya udongo ili iweze kupima na kutoa takwimu zenye ubora wa kutambulika kimataifa. Kamati inaona kwamba, ili mradi huu ulete tija iliyokusudiwa, Serikali iweke vipaumbele katika ukarabati wa maabara hizi za TARI kwa kukamilisha maabara moja baada ya nyingine. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa Serikali inaendelea kukamilisha Ithibati ili maabara itambulike kimataifa. Kamati inaona pia kuwa ni vyema Serikali ikaongeza kasi ya kukamilisha ithibati hiyo ili maabara ilete tija iliyokusudiwa.

**ii. Mradi Na. 4486 - Ukarabati wa Ghala la Kipawa**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea na kukagua Mradi wa Ukarabati wa Ghala uliopo eneo la Kipawa, Dar Es Salaam. Ghala hili ni moja ya vyanzo vya mapato vya Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai (TSHTDA). Kamati ilielezwa kuwa mradi huu una lengo la kuongeza na kuimarisha uwezo wa taasisi katika kutekeleza majukumu yake ambapo inatarajiwa kuchangia **Shilingi 325,500,000** kama pato la ndani pamoja na kutoa ajira kwa Washitiri watakaotumia ghala hili.

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu ulitengewa jumla ya **Shilingi 790,000,000** ambazo ni fedha za ndani kwa ajili ya shughuli ya ukarabati wa Ghala. Hadi Kamati inatembelea mradi huu, shughuli ya ukarabati ilikuwa imekamilika. Kwa ujumla Kamati iliridhika na kazi iliyofanyika na kuitaka Serikali kuhakikisha inatumia ghala hilo kama ilivyokusudiwa ili kupunguza utegemezi wa Taasisi kwa Serikali.

**2.2.4 Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, **Fungu 43 -** Wizara ya Kilimo, iliidhinishiwa na Bunge Bajeti ya **Shilingi 112,019,631,000** sawa na **asilimia 13.9** ya bajeti yote kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Februari, 2024 Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi 74,573,773,949** kwa ajili ya Matumizi ya kawaida sawa na **asilimia 66.6** ya bajeti iliyotengwa. Jedwali lifuatalo linaonesha mwenendo wa upatikanaji wa fedha wa Fungu 43 kwa Mwaka 2023/2024.

**Jedwali Na. 3, Fungu 43, Hali ya upatikanaji wa fedha hadi kufikia Februari,** 2024

| UPATIKANAJI WA FEDHA FUNGU 43 MWAKA 2023/2024 | | | |
|---|---|---|---|
| **MATUMIZI** | **KILICHOIDHINISHWA PAMOJA NA NYONGEZA** | **KILICHOPOKELEWA** | **ONGEZEKO/PUNGUFU ASILIMIA** |
| MISHAHARA | 56,554,950,000 | 32,748,651.000 | 58 |
| OC | 55,464,681,000 | 41,825,122,949 | 75 |
| **JUMLA** | **112,019,631,000** | **74,573,773,949** | **66.6** |

**Chanzo**: Randama ya Wizara Fungu 43

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi unaonesha kuwa: -

(a) Upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida ni **asilimia 66.6** ya fedha iliyotengwa; na

(b) Hali ya upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida inaridhisha na hivyo kuleta matumaini ya kukamilisha lengo lililokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Fungu – 05 iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 73,547,775,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia mwezi Februari, 2024, fedha iliyopokelewa ni **Shilingi 11,364,521,943** sawa na **asilimia 15** ya fedha iliyoidhinishwa. Mchanganuo wa upokeaji wa fedha unaonekana katika **Jedwali Na. 4**.

**Jedwali Na. 4 Fungu 05 Hali ya upatikanaji wa Fedha kwa matumizi** ya Kawaida

| UPATIKANAJI WA FEDHA FUNGU 05 MWAKA 2023/2024 | | | |
|---|---|---|---|
| **MATUMIZI** | **KILICHOIDHINISHWA PAMOJA NA NYONGEZA.** | **KILICHOPOKELEWA** | **ONGEZEKO/PUNGUFU ASILIMIA** |
| MISHAHARA | 7,215,116,000 | 3,891,760,940 | 54 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| OC | 66,332,659,000 | 7,472,761,003 | 11 |
| **JUMLA** | **73,547,775,000** | **11,364,521,943** | **15** |

**Chanzo**: Randama ya Wizara Fungu - 05

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi unaonesha kuwa: -

(a) Upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida kwa ujumla ni **asilimia 15** ya fedha iliyotengwa; na

(b) Mwenendo huu wa upatikaji wa fedha hauridhishi na hautoi mwelekeo wa ukamilishaji wa lengo lililokusudiwa. Miradi mingi ya umwagiliaji imeathirika kutokana na upatikanaji wa fedha usioridhisha.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Fungu 24 - Tume ya Maendeleo ya Ushirika iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 17,383,074,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na **asilimia 88.8** ya bajeti ya Tume**.** Hadi kufikia Februari, 2024, Tume ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi 9,121,350,751** sawa na **asilimia 46** ya bajeti ya matumizi ya kawaida iliyoidhinishwa**.**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, mwenendo wa jumla wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida hauridhishi na hivyo unaonesha kwamba utekelezaji wa lengo unaweza usifikiwe kikamilifu.

### 2.2.5 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 43 Wizara ya Kilimo, Fungu 24 - Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Fungu 05 - Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Kamati ilishauri masuala mbalimbali ambayo Serikali iliyazingatia.

**Mheshimiwa Spika,** baadhi ya ushauri wa Kamati uliozingatiwa ni kama ifuatavyo: -

(a) Serikali imeanza kuzingatia ushauri wa Kamati wa kuhakikisha kuwa Programu ya BBT inaanzishwa kikanda na katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo

Halmashauri. Serikali imeendelea kuainisha na kutambua mashamba kwa ajili ya BBT katika mikoa mbalimbali nchini ambapo hadi kufikia Februari, 2024 jumla ya ekari 340,245.3 zilikuwa zimebainishwa kwa ajili ya BBT katika mikoa mbalimbali ikiwemo Dodoma, Kigoma, Mbeya, Singida, Pwani, Tanga, Njombe na Kagera. Aidha, Serikali imeahidi kuziwezesha Halmashauri ambazo zitatenga mashamba ya pamoja na kudahili vijana na wanawake kujenga miundombinu ya umwagiliaji.

(b) Serikali imeendelea kutoa elimu ya mpango wa ruzuku kupitia vikao vya Wakuu wa Mikoa, Wilaya, Maafisa Kilimo vipindi vya redio na runinga. Aidha, kutokana na mpango huo, hadi kufikia mwezi Machi, 2024, jumla ya wakulima 3,784,394 wamesajiliwa kati ya lengo la kusajili wakulima 7,000,000 ifikapo mwaka 2025/2026.

(c) Ili kukabiliana na upotevu wa mazao baada ya mavuno, Serikali imeendelea na ujenzi wa miundombinu ya kuhifadhi mazao ya kilimo baada ya kuvunwa ambapo hadi kufikia Februari, 2024, ujenzi wa ghala 28 umefikia wastani wa asilimia 75. Maghala hayo yamejengwa maeneo mbalimbali ikiwemo Ruvuma katika Halmashauri ya Songea (11), Madaba (9), Namtumbo (7) pamoja na ujenzi wa maghala 12 kupitia Mradi wa TANIPAC ambao umekamilika na kukabidhiwa NFRA.

**Mheshimiwa Spika**, Katika hatua mbalimbali, Kamati imeridhika kwamba ushauri wake unaendelea kuzingatiwa na Wizara pamoja na Tume katika utekelezaji wa majukumu yake. Aidha, upatikanaji wa fedha usioridhisha umeendelea kuwa kikwazo kwa Wizara na hivyo kushindwa kuzingatia ushauri wa Kamati. Hivyo Kamati inaisisitiza Serikali kutoa fedha kwa wakati.

### 2.3 Makadirio ya Maduhuli na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha, 2024/2025

#### 2.3.1 Makadirio ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ya Kilimo - Fungu 43 inategemea kukusanya jumla ya **Shilingi**

**7,000,254,000**. Kiasi kinachotarajiwa kukusanywa ni ongezeko la **asilimia 5** ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Mchanganuo wa lengo la makusanyo kwa fungu unaonekana katika **Jedwali Na.5.**

***Jedwali Na. 5Fungu 43 Ulinganisho katika Makusanyo ya Maduhuli***

| **ULINGANISHO WA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA 2023/2024 NA 2024/2025** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **CHANZO** | **2023/2024** | **2024/2025** | **Nyongeza/ Pungufu** | **Asilimia** |
| | 6,677,254,000 | 7,000,254,000 | 323,000,000 | 5 |

**Chanzo: Randama ya Wizara Fungu -43**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi unaonesha kuwa: -

(a) Kwa ujumla makadirio ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2024/2025 yameongezeka kwa **asilimia 5** ikilinganishwa na lengo la makusanyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024; na

(b) Kutokana na mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kufikia **asilimia 68** ndani ya robo tatu ya muda wa lengo, kuna uwezekano wa kufikia lengo la makusanyo lililowekwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kwa kuzingatia uzoefu wa makusanyo ya mwaka uliotangulia.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa **Fungu 05 -** Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inakadiriwa kukusanya jumla ya **Shilingi 3,600,000,000** ambayo ni pungufu kwa **asilimia 64** ya lengo la maduhuli kwa mwaka wa fedha 2023/2024. **Jedwali Na. 6** linaonesha mchanganuo wa makadirio hayo.

**Jedwali Na. 6Fungu 05 Ulinganisho katika Makusanyo ya Maduhuli**

| ULINGANISHO WA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA 2022/2023 NA 2023/2024 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **CHANZO** | **2023/2024** | **2024/2025** | **Nyongeza/ Pungufu** | **Nyongeza/ Pungufu%** |
| Mfuko (NIDF) | 10,000,000,000 | 3,600,000,000 | (6,400,000,000) | 64 |

***Chanzo: Randama Fungu 05***

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi unaonesha kwamba kwa ujumla makadirio ya maduhuli kwa mwaka 2024/2025 yameshuka kwa **asilimia 64** ikilinganishwa na lengo la maduhuli ya mwaka wa fedha 2023/2024. Kamati inaona bado ni muhimu Tume ikajiwekea mikakati itakayoiwezesha kuongeza makusanyo ya maduhuli kwa mwaka huu wa fedha ili kuleta tija iliyokusudiwa.

**2.3.2 Uchambuzi wa Matumizi ya Kawaida**

**Mheshimiwa Spika**, Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ya Kilimo, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na Tume ya Maendeleo ya Ushirika wanakadiria kutumia **Shilingi 215,915,362,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Fedha hizi ni ongezeko la matumizi ya kawaida kwa **asilimia 6** ikilinganishwa na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Mchanganuo wa Makadirio hayo unaonekana katika **Jedwali Na. 7.**

**Jedwali Na. 7 Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2023/2024**

| **Na.** | **FUNGU** | **TAASISI** | **MAKADIRIO KWA MWAKA 2023/2024** | **MAKADIRIO KWA MWAKA 2024/2025** | **ASILIMIA** |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 43 | WIZARA YA KILIMO | 112,019,631,000 | 123,750,689,000 | 9 |
| 2. | 05 | TUME YA UMWAGILIAJI | 73,547,775,000 | 71,884,610,000 | -2 |
| 3. | 24 | TUME YA USHIRIKA | 17,383,074,000 | 20,280,063,000 | 14 |
| | | **JUMLA** | **202,50,480,000** | **215,915,362,000** | **6** |

**Chanzo:** ***Randama za Fungu 43, Fungu 05 na Fungu 24***

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia ongezeko la **asilimia 6** kwenye bajeti ya Matumizi ya Kawaida, linatoa mwelekeo mzuri kwani fedha hizi zitaongeza msukumo wa kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa bajeti ya miradi ya maendeleo. Ongezeko hili la bajeti linategemewa kwenda sambamba na upatikanaji wake kwa wakati ili kutekeleza majukumu yaliyokusudiwa.
Utekelezaji wa Programu za Umwagiliaji, usambazaji wa mbolea pamoja na pembejeo za kilimo kwa wanachi kwa wakati, ufanisi wake unategemea upatikanaji wa fedha kwa kiwango stahiki na kwa wakati. Kama inavyoelekezwa katika Ibara ya 37 ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM). Ibara hii imeahidi kusimamia kikamilifu hifadhi na matumizi endelevu ya maji, ardhi ya kilimo na mazingira sambamba na kuongeza miundombinu ya umwagiliaji itakayoendeshwa kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na ongezeko hilo la bajeti ya Matumizi ya Kawaida, Kamati inaona kuwa, bado fedha iliyoongezwa haikidhi mahitaji kulingana na uzito wa majukumu makubwa yaliyopo katika kuhakikisha tija inaongezeka kwenye kilimo kwa kuboresha miundombinu ya umwagiliaji, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya hifadhi ya mazao, kuimarisha vituo vya utafiti, upatikanaji wa pembejeo, kuimarisha huduma za ugani pamoja na kuimarisha Usimamizi na Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika.

### 2.3.3 Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua makadirio ya jumla ya **Shilingi 1,016,013,881,000** kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo inayopangwa kutekelezwa na Wizara ya Kilimo, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Makadirio hayo ni ongezeko la **asilimia 24** ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 8**

**Jedwali Na. 8Makadirio ya Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2023/2024**

| NA. | FUNGU | TAASISI | MAKADIRIO KWA MWAKA 2023/2024 | MAKADIRIO KWA MWAKA 2024/2025 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 43 | WIZARA YA KILIMO | 465,698,366,000 | 683,286,032,000 | 31.8 |
| 2. | 05 | TUME YA UMWAGILIAJI | 299,964,223,000 | 331,899,223,000 | 10 |
| 3. | 24 | TUME YA USHIRIKA | 2,172,550,000 | 828,626,000 | -62 |
| | | **JUMLA** | **767,835,139,000** | **1,016,013,881,000** | **24** |

***Chanzo: Randama za Fungu 43, Fungu 05 na Fungu 24***

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa jumla unaonesha kwamba:-

(a) Bajeti ya Maendeleo kwa Wizara ya Kilimo, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na Tume ya Maendeleo ya Ushirika imeongezeka kwa **asilimia 24** ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2023/2024;

(b) Nyongeza ya bajeti ya **asilimia 24** inaweza kuashiria muelekeo wa kufikia malengo yaliyowekwa kwenye mpango wa kuendelea kuongeza tija na uzalishaji katika sekta ya kilimo;

(c) Nyongeza ya bajeti ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo inaweza kuleta tija kama Serikali itazingatia utoaji wa fedha hizo kwa mtiririko na kwa wakati;

**Mheshimiwa Spika**, kulingana na uchambuzi huu, Wizara na Taasisi zilizo chini yake zitaongeza uwezo wa utekelezaji wa miradi ikilinganishwa na utekelezaji ulivyokuwa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa Bajeti pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi

ya Wizara ya Kilimo, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji pamoja na Tume ya Maendeleo ya Ushirika, ninaomba kuwasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati kama ifuatavyo: -

**3.1 Wizara ya Kilimo – Fungu 43**

(a) Pamoja na Serikali kuendelea kuongeza bajeti ya kilimo, bado haikidhi mahitaji halisi ya sekta hii kwa kuzingatia matakwa ya utekelezaji wa Azimio la Maputo (2003) na Malabo (2014) linalozitaka nchi wanachama kutenga **asilimia 10** ya bajeti ya Taifa kwa ajili ya sekta ya kilimo. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kutenga bajeti na fedha hizo kutolewa kwa wakati ili kuwezesha utekelezaji wa malengo na mikakati iliyokusudiwa;

(b) Uzalishaji duni na usio na tija wa mazao ya kilimo unatokana na kukosekana kwa mbolea ya kutosha na kwa wakati; Kamati inaishauri Serikali kuweka nguvu na kuchukua hatua za makusudi za kuzalisha pembejeo hapa nchini ikiwemo mbolea, mbegu na viuatilifu;

(c) Pamoja na Serikali kuweka mfumo mzuri wa utoaji wa mbolea ya ruzuku nchini, bado mfumo huo haujafahamika ipasavyo kwa wakulima wengi na hivyo kutoleta tija iliyokusudiwa. Kamati inaishauri Serikali: -

i. Elimu iendelee kutolewa kuhusu uwepo wa mbolea ya ruzuku na namna ya kuipata ili kudhibiti mianya inayotumiwa na watu wachache ya kuuza mbolea kwa bei ya juu; na

ii. Wizara iendelee kuongeza kasi ya kutoa elimu kwa wakulima kuhusu matumizi bora na sahihi ya mbolea pamoja na viuatilifu.

(d) Hakuna tija katika kilimo bila uwepo wa wataalam wa kutosha (maafisa ugani) ambapo mahitaji ni takribani wagani 20,000, lakini waliopo ni asilimia 35 tu ya mahitaji. Upungufu huu hauwezi kuleta matokeo yanayotarajiwa. Kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu wa kutenga bajeti na kuajiri

Maafisa Ugani wa kutosha ili kutoa huduma za ugani na kuleta tija iliyokusudiwa.

(e) Hali ya upotevu wa mazao baada ya kuvunwa imeendelea kuwa kwenye tarakimu mbili (**asilimia 35**) ukilinganisha na shabaha ya kupunguza upotevu huo hadi **asilimia 5** ifikapo mwaka 2030. Hali hii inaathiri usalama na upatikanaji wa chakula cha uhakika wakati wote nchini. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuimarisha miundombinu na kukamilisha ujenzi wa maghala ya kutosha katika ngazi za vijiji, Kata na Wilaya hasa kwenye maeneo yenye uzalishaji mkubwa wa mazao ya chakula.

(f) Mahitaji ya mbegu bora na za kutosha ni suala ambalo haliepukiki iwapo tunataka kuzalisha kwa tija na kuwanufaisha wakulima na wananchi kwa ujumla. Kamati inaishauri Serikali yafuatayo: -

i. Kuendelea kuziwezesha taasisi zinazohusika na utafiti na uzalishaji wa mbegu kifedha, pamoja na kuimarisha miundombinu ya uzalishaji ili ziweze kuzalisha mbegu bora na za kutosheleza mahitaji yaliyopo nchini;

ii. Kuweka mazingira ya kushirikisha sekta binafsi katika uzalishaji wa mbegu ili kupunguza matumizi ya fedha za kigeni zinazotumika kuagiza mbegu;

iii. Iweke mikakati ya kudhibiti mfumuko wa bei za mbegu kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo kuweka bei elekezi. Aidha, wananchi wapate taarifa sahihi kuhusu bei hizo; na

iv. Mbegu ziwafikie wakulima kwa wakati

(g) Ukosefu wa masoko ya uhakika ya mazao ya kilimo katika maeneo mengi ya wakulima nchini na nje ya nchi, kumepelekea sekta ya kilimo kutochangia ipasavyo lakini pia kuwakatisha wakulima tamaa ya kulima kwa wingi. Ili kukabiliana na changamoto hii, Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za makusudi kuhakikisha upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo hapa nchini na nje ya nchi

unakuwa wa uhakika. Aidha, Serikali iweke mikakati mahsusi ya kuhakikisha kuwa mazao yanawekewa mnyororo wa thamani hapa nchini ili kuwanufaisha wakulima;

(h) Maendeleo ya sekta yoyote yanatokana na tafiti za kutosha kuhusu sekta husika. Sekta ya kilimo inahitaji kuziwezesha taasisi zake za utafiti ili kuongeza tija katika kilimo. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali: -

i. Kuendelea kuimarisha miundombinu ya utafiti kwa kujenga miundombinu mipya na kukarabati iliyopo. Aidha, ukarabati uzingatie vipaumbele ili kukamilisha eneo moja baada ya lingine kuliko ilivyo sasa ambapo ukarabati unafanyika kwa sehemu katika vituo vingi na hivyo kukosa tija;

ii. Kuendelea kuwekeza na kuimarisha taasisi za utafiti wa kilimo nchini ikiwa ni pamoja na kuwaongezea rasilimali watu na rasilimali fedha kwa ajili ya utafiti na kuendelea kuwajengea uwezo watafiti wa kilimo ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi na kukuza sekta ya kilimo nchini; na

iii. Kuongeza kasi katika kufufua uzalishaji wa mbegu za asili (mbegu za Wakulima). Kuendeleza na kutunza mbegu hizi kutasaidia kulinda chanzo cha nasaba za mimea ambacho ni msingi wa tafiti zote, lakini pia uzalishaji wa mazao ya asili utasaidia upatikanaji wa lishe bora katika chakula na kuchangia kujitosheleza kwa virutubisho na kupunguza ulazima wa virutubisho vya viwandani. Aidha, Serikali iweke mfumo wa kisheria utakaoruhusu uzalishaji na usambazaji wa mbegu za asili nchini.

Programu ya Jenga Kesho Bora (BBT) imeanza kuonesha mwelekeo mzuri katika maeneo machache yaliyoanza kutekelezwa. Ili programu hii inufaishe vijana wengi zaidi, Kamati inaishauri Serikali yafuatayo:-

i. Iboreshe mfumo wa upatikanaji wa vijana ili vijana wengi wapate fursa ya kushiriki;

ii. Ihakikishe fursa hii inawafikia vijana katika Halmashauri zao kwa kuanzisha mpango huu katika mikoa yote na Halmashauri zote nchini;

iii. Mikakati ya kuwawekea masoko ya uhakika iendelee ili kuwanaufaisha vijana hao ili tija iliyokusudia iweze kufikiwa;

iv. Iendelee kutekeleza mipango yake kwa kadiri ilivyojiwekea ili kutowakatisha tamaa vijana; na

v. Vijana waliopo katika mashamba hayo, waendelee kuhamasishwa kulinda ajira hizo ili kuwa mfano kwa vijana wengine wenye mahitaji hayo na kujenga uwezo endelevu kwa vijana.

### 3.2 Tume ya Taifa ya Umwagiliaji – Fungu 05

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu Utekelezaji wa Mipango ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kamati inashauri yafuatayo: -

(a) Ukusanyaji hafifu wa maduhuli ya Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji unaipotezea Serikali mapato. Kamati inaishauri Tume ihakikishe inaweka utaratibu utakaohakikisha kuwa watumiaji wa maji wanalipa tozo za maji na kuiwezesha Tume kufikia malengo iliyojiwekea;

(b) Mchango mdogo wa kilimo cha umwagiliaji katika sekta ya Kilimo unatokana na ufinyu wa bajeti na ucheleweshaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji pamoja na idadi ndogo ya wataalamu wa umwagiliaji. Kamati inashauri kuwa, Serikali iendelee kuongeza bajeti ya kutosha kwa ajili ya umwagiliaji. Fedha hizo pia zitolewe kwa wakati ili kufikia malengo ya kufikisha eneo la umwagiliaji hekta milioni nane (8) ambayo ni sawa na hekta milioni moja (1) kwa mwaka ifikapo mwaka 2030. Hatua hizi zitawezesha kufikia lengo la kukuza sekta ya kilimo kwa asilimia 10 (*Ajenda 10/30*);

(c) Kutokuwepo kwa mfumo madhubuti wa Miradi ya Umwagiliaji inayolingana na mahitaji ya wakulima hasa

kwenye maeneo ya vijijini, kumeendelea kuwa kikwazo cha kufikia malengo ya kuinua kilimo kwa njia ya umwagiliaji. Kamati inaishauri Serikali kuongeza juhudi katika kuweka mifumo imara na madhubuti katika Miradi ya Umwagiliaji katika maeneo yote nchini ikiwa ni pamoja na kuchimba mabwawa, kuvuna maji na kujenga miundombinu ya umwagiliaji ili kufikia lengo lililokusudiwa;

(d) Serikali iweke mazingira mazuri ili kuvutia sekta binafsi katika uwekezaji kwenye sekta ya umwagiliaji ili ardhi inayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji itumike kikamilifu na kuongeza tija.

**3.3 Tume ya Maendeleo ya Ushirika – Fungu 24**

(a) Mgawanyo wa majukumu na uwajibikaji katika Tume umepunguza ufanisi na kusababisha changamoto hasa za kiusimamizi na uwajibikaji wa Maafisa Ushirika. Kamati inaendelea kuitaka Serikali kukamilisha mapitio ya Sheria ya Ushirika ili kutatua changamoto zinazotokana na usimamizi na uwajibikaji;

(b) Kuhusu Wakala wa Ukaguzi wa Ushirika, Kamati inaishauri Serikali yafuatayo: -

i. Lijengee uwezo COASCO ili iweze kufanya kazi kwa kujitegemea badala ya kufadhiliwa na Ushirika inayoikagua;

ii. Iajiri watumishi wa kutosha na wenye uwezo katika sekta ya ushirika;

iii. Ihakikishe COASCO wanafanya ukaguzi ili kuvifikia vyama vya Ushirika katika mikoa yote.

(c) Pamoja na nia njema ya Serikali kuanzisha Benki ya Ushirika kwa lengo la kuwawezesha wakulima kupata huduma za kifedha kwa karibu zaidi, bado Kamati inaushauri ufuatao: -

i. Kuendelea kuimarisha benki hii kwa kuhakikisha inapata mtaji toshelevu;

ii. Iweke mfumo mzuri utakaoviwezesha vyama Vikuu vya Ushirika pamoja na Vyama vingine vya Ushirika nchini kununua Hisa za Benki hii kama njia ya kuimarisha na kukuza mtaji;

iii. Serikali iimarishe utendaji wa benki kwa kuwafanyia watumishi upekuzi (vetting) wa kutosha ili kuepuka kurudi kwenye anguko la awali la Benki hii. Aidha, Watumishi waliopelekea benki hii kufilisika wachukuliwe hatua za kisheria; na iv. Benki hii iendeshwe kibiashara ili iweze kushindana kwenye soko na benki nyingine za biashara ikizingatia kuwapa kipaumbele wakulima.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Maelezo ya Kuhitimisha

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo ni mwezeshaji na mratibu muhimu wa kufanikisha utekelezaji wa Mipango mbalimbali ikiwemo Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo awamu ya Pili na utekelezaji wa Malengo Endelevu ya Milenia (SGDs) hususani lengo namba 1 linalohusu kupunguza umaskini uliokithiri na lengo namba 2 linalohusu kutokomeza tatizo la utapiamlo kwa kuimarisha lishe bora.

### 4.2 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, kwa ushirikiano waliouonesha katika kipindi chote cha uchambuzi wa bajeti ya Wizara ya Kilimo. Kutokana na ufinyu wa muda sitaweza kuwataja kwa majina lakini naomba majina yao yaingizwe katika Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*). Majina ya Wajumbe hao ni haya yafuatayo:-

(1) Mhe. Deodatus Philip Mwanyika, Mb - Mwenyekiti
(2) Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri, Mb - M/Mwenyekiti
(3) Mhe. Job Yustino Ndugai, Mb - Mjumbe
(4) Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb - Mjumbe

(5) Mhe. Prof. Sospeter M. Muhongo, Mb - Mjumbe
(6) Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mb- Mjumbe
(7) Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb, - Mjumbe
(8) Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb - Mjumbe
(9) Mhe. Tauhida Cassian Galos, Mb - Mjumbe
(10) Mhe. Dkt. Medard Matogolo Kalemani, Mb - Mjumbe
(11) Mhe. Antipas Zeno Mgungusi, Mb - Mjumbe
(12) Mhe. Daud Silanga Njalu, Mb - Mjumbe
(13) Mhe. Eng. Ezra John Chiwelesa, Mb - Mjumbe
(14) Mhe. Francis Isack Mtinga, Mb - Mjumbe
(15) Mhe. Lucy John Sabu, Mb - Mjumbe
(16) Mhe. Ng'wasi Damas Kamani, Mb - Mjumbe
(17) Mhe. Prof. Patrick Aloysi Ndakimeki,Mb - Mjumbe
(18) Mhe. Janejelly James Ntate Mb - Mjumbe
(19) Mhe. Yustina Arcadius Rahhi, Mb - Mjumbe
(20) Mhe. Pauline Philip Gekul, Mb - Mjumbe
(21) Mhe. Abdulaziz Mohamed Abood. Mb - Mjumbe
(22) Mhe. Atupele Fred Mwakibete, Mb - Mjumbe
(23) Mhe. Salim Turky Toufiq, Mb - Mjumbe
(24) Mhe. Mohammed Said Issa, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuona umuhimu wa sekta ya kilimo. Kwa kipindi kifupi cha uongozi wake tumeshuhudia kasi kubwa ya uongezaji bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa lengo la kuongeza tija kwenye kilimo.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho lakini siyo kwa umuhimu napenda kutumia nafasi hii kumshukuru Mhe. Hussein Mohamed Bashe (Mb) - Waziri wa Kilimo na Mhe. David Ernest Silinde(Mb) – Naibu Waziri wa Kilimo, kwa ushirikiano mkubwa wanaoipatia Kamati ambao kwa sehemu kubwa umechangia kuiwezesha Kamati kutekeleza shughuli zake kikamilifu.
Nawashukuru pia watendaji wote wa Wizara ya Kilimo na Taasisi zilizo chini ya Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu Bwana Gerald Geofrey Mweli, akisaidiwa na Naibu Katibu Mkuu Bwana Hussein Mohamed Omary.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee namshukuru Katibu wa Bunge - Ndg. Nenelwa Mwihambi, *ndc,* kwa kuwangoza vyema

watumishi wa Ofisi ya Bunge katika uratibu na usimamizi wa shughuli za Kamati kwa ujumla hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo (Fungu 43, 24 na 05), kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Deodatus Philip Mwanyika (Mb)
**MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO**
Mei, 2024

**SPIKA:** Ahsante sana Makamu Mwenyekiti kwa wasilisho hilo.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kabla hajaanza kusoma taarifa ya Kamati alisema kwa kuzingatia muda taarifa ya Kamati anaomba iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge, kwa hivyo ukipitia ile taarifa kuna maneno hapo ameyaongeza ambayo ni ya muhimu kabisa, lakini kwa sababu hayamo kwenye hii taarifa mtu akienda kusoma Taarifa Rasmi za Bunge atakutana na Taarifa ya Kamati kama ilivyoletwa kama Makamu Mwenyekiti alivyokuwa amesema.

Waheshimiwa Wabunge, uchangiaji tutaanza tutakaporejea baadae, tutaanza na Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, atafuatiwa na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Charles John Mwijage atafuatia na Wabunge wengine wataendelea kutajwa kadiri muda utakavyokuwa unakwenda.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wengine ambao wameingia Bungeni baada ya tangazo letu la kwanza la wageni na hawa ni wageni wa Mheshimiwa Hussein Bashe, Waziri wa Kilimo ambao ni...

Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane, yupo Ndugu Angelina Ngalula ambaye ni Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi *(TPSF),*

karibu sana Bungeni. Huyu anavyo vyeo vingi, tungepata muda tungevitaja vyote, lakini kimojawapo nadhani kati ya wale juzi tuliwatambua wawekezaji wazawa kwenye madini huyu ni mwekezaji mzawa kwenye usafirishaji na nadhani anaendelea kupanua biashara yake, kwa hiyo, tunamtakia kila la kheri katika kuhakikisha anapanua huo uwekezaji na anazidi kuzalisha ajira nyingi zaidi kwa Watanzania. Tunakushukru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia Profesa Maulid Mwatawala ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi ya Udhibiti Ubora wa Mbegu, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Salum Awadhi Agani, Mwenyekiti wa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko, karibu sana. *(Makofi)*

Wengine ni Ndugu Vian Lweyendela, Mwakilishi *AGRA*-Tanzania; Ndugu Adam Grest Meya, *Chief of Part AGRA Tanzania;* Ndugu Omary Bakari - Mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko wa Pembejeo; na Ndugu Mohamed Nassoro Hamdan - Mjumbe wa *NEC* Mkoa wa Tabora. *(Makofi)*

Mgeni mwingine ni Ndugu Mwanne Mchemba - Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Mkoa wa Tabora, ahsante sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Wapo pia Ndugu Elias Mpanda, Katibu wa CCM Mkoa wa Tabora na Ndugu Javati Kayanda, Mjumbe wa Kamati ya Siasa Mkoa wa Tabora, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri ambao ni Mwenyekiti Mwenza wa *Agricultural Working Group* kutoka *FAO*, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye pia Mtendaji Mkuu wa *Agricultural Marketing and Development Trus*t, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wengine tena wa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, hawa ni Wenyeviti wa Bodi, Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa na Wakuu wa Idara Vitengo

na Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo, wote wasimame kwa pamoja, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wawakilishi wa sekta binafsi, wawakilishi wa sekta binafsi ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia vijana *wa Building Better Tomorrow (BBT),* karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia wapo Wajumbe wa Jukwaa la Wahariri Tanzania, karibuni sana, karibuni sana Bungeni na tunawatakia kila la kheri katika siku yenu muhimu kabisa ambayo mnatarajia kuisherehekea hapa Dodoma ya Uhuru wa Vyombo vya Habari, tunawatakia kila la kheri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo sasa nasitisha Shughuli Bunge mpaka saa 11.00 jioni ya leo.

*(Saa 7.19 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Joseph K. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Tayari tuna orodha ya wachangiaji wetu wa mchana

huu na walishasomwa asubuhi, lakini nitawasoma wale watatu wa mwanzo.

Tutaanza na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, atafuatiwa na Mheshimiwa Charles John Mwijage na Mheshimiwa Kiswaga Boniventura Destery ajiandae.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai na afya. Naomba nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri Bashe unafanya kazi vizuri sana, anafanya kazi ya Serikali kuliko anavyofanya kazi yake mwenyewe. Nikwambie ukweli, sisi Wabunge tunashirikiana na Waziri vizuri kwa sababu anatupokea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo naomba bajeti yangu niigawe katika mafungu matatu, kwanza nitaongelea bajeti ya kilimo, nitaongelea kilimo cha Tanzania, nitaongelea umwagiliaji Tanzania, nitaongelea umwagiliaji Jimboni kwangu Same Mashariki na kama nitapata muda nitaleta ombi langu kwa Serikali kama muda utakuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha Tanzania nakwenda kuangalia kwenye sensa ya kilimo, mifugo na uvuvi ya mwaka 2019/2020. Sensa ilituletea matokeo ambayo yanaonesha mambo yafuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sensa ya mwaka 2019/2020 ilisema kwamba kati ya kaya 12,007,405 zilizopo Tanzania, kaya 7,837,405 sawa na 65.3% zinajihusisha na kilimo, hilo ni la kwanza. Pili, sekta ya kilimo iliambiwa inachangia kiasi cha zaidi ya 20% ya bidhaa zinazosafirishwa nje ya nchi. Tukaambiwa tena sekta ya kilimo inachangia zaidi ya 40% ya pato la Taifa *(GDP)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sensa hii ikasema kilimo kinasaidia riziki ya zaidi ya theluthi mbili ya wananchi wa Tanzania. Hii ina maana gani? Ina maana kwamba sekta ya kilimo inachangia sana katika kukuza uchumi na kupunguza umasikini wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niendelee na umwagiliaji Tanzania na naomba nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na niipongeze Serikali ya Chama Cha Mapinduzi Awamu ya Sita, kwa nini? Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameleta mageuzi makubwa sana katika sekta ya kilimo upande wa umwagiliaji. Kwanza, bajeti ya kilimo yenyewe amehakikisha takribani 30% inakwenda kwenye umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sisi ambao tunatoka majimbo ya vijijini na majimbo ya wakulima tunachukulia kwamba umwagiliaji ndiyo kilimo cha uhakika. Sasa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan aliingia madarakani tarehe 19 Machi, 2021 na mwaka 2021/2022 bajeti yake ya kwanza ilikuwa shilingi bilioni 45 kwa umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2022/2023 Serikali ya Chama Cha Mapinduzi hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuona umuhimu wa umwagiliaji akapandisha kutoka shilingi bilioni 45 mpaka shilingi bilioni 366. Mwaka 2023/2024 akasogeza tena pesa za umwagiliaji mpaka shilingi bilioni 403 na mwaka 2024/2025 bajeti tuliyonayo hapa umwagiliaji wamepewa shilingi bilioni 410. Hii ina maana ongezeko hili ni la 900%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mageuzi makubwa sana na mimi namtafsiri Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na naitafsiri Serikali ya Chama Cha Mapinduzi ya Awamu ya Sita kwamba inawajali sana wakulima; 65.3% zaidi ya hao wako vijijini wanalima. Ukishawaonesha kwamba unawathamini kiasi hiki basi wewe umeshinda. Tayari umeshachaguliwa kwa sababu umejali chakula na biashara kwa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende upande wa umwagiliaji kwa upande wa Same Mashariki. Mimi Jimbo la Same Mashariki 100% ni jimbo la wakulima na wanalima kwa ajili ya chakula chao binafsi pia kwa ajili ya biashara. Wewe utakapojitahidi kuboresha kilimo ina maana umeboresha maisha yao. Mimi naipongeza tena hii Serikali. Unajua wenzetu huko nje wanatuambia "Ooh hao machawa, kila wakisimama Samia, Samia, Samia." Nitakuwa mtu

wa ajabu sana nisipomshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tena nitakuwa mwendawazimu nisiposimama nikasema Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anafanya makuu. Ngoja nikupe mfano, 100% ya wananchi wangu ni wakulima, wanachohitaji ni kuwezeshwa upande wa umwagiliaji, lakini tarehe 02 Julai, 2023 nilipewa pesa za umwagiliaji kule juu milimani na kata yangu moja ya Myamba ikapewa shilingi 1,735,126,280. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo niiambie Serikali kidogo kabla sijamaliza, hawa wanaolima tangawizi wanalima 72% ya tangawizi ya nchi nzima. Nimeishukuru Serikali imeniletea mradi wa skimu kwenye kata moja, lakini Mheshimiwa Bashe hii kata uliyokuja ukaiona Kata ya Myamba ndiyo uliyoiletea pesa shilingi 1,735,126,280. Ziko kata tisa ambazo ndizo zinazolima tangawizi ya nchi hii. Nakuomba kwa unyenyekevu hizi kata tisa za Mpinji, Bwambo, Kirangare na kadhalika nazo zinaomba msaada huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali katika ile mikataba ya skimu za umwagiliaji ambazo Serikali ilisaini, naiomba niishukuru tena Serikali ya Chama Cha Mapinduzi. Naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu hapa tambarare wananchi wangu wanalima mpunga, mahindi, maharage na matunda pamoja na mboga mboga. Nilipata miradi miwili Waheshimiwa Wabunge wenzangu, alinipa mradi wa Kata ya Ndungu, akanipa mradi wa Kata ya Kihurio ambayo hiyo kata inasogea kuhudumia na Kata ya Bendera na alinipa shilingi bilioni saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, shilingi bilioni saba zile kata mbili zitalima mpunga ambao zitashughulikia wananchi 16,000 wa kata mbili. Kwa hiyo, kwangu mimi nasema ni mageuzi makubwa na ninaiomba Serikali, Mheshimiwa Waziri endelea kuongeza pesa za umwagiliaji. Sisi tulioko vijijini hakuna kitu tunacholilia zaidi ya wananchi wetu waweze kulima kwa uhakika. Tunakupongeza sana unavyotusikiliza na kutujali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake unavyomwona Waziri, Mheshimiwa Bashe amekuja kwangu mara mbili, amekuja mara ya kwanza akiwa Naibu Waziri nikampeleka kwenye shida zangu, akaja mara ya pili akiwa Waziri nikampeleka kila mahali ninakolima; akaja Naibu Waziri Mheshimiwa Mavunde, yeye alifanya safari ya kuja Ndungu, Myamba na Kihurio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme ukweli aliyeleta ile mikataba miwili iliyosainiwa siku ya Jumanne naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Mavunde ambaye sasa ni Waziri wa Madini, lakini ndiye aliyekuja akawasikiliza wananchi wa Kihurio, akaleta pesa hizi za kuboresha Mto Saseni na skimu ya umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina dakika moja imebaki, naomba nikwambie kitu kimoja, Mheshimiwa Waziri nchi nzima inalima tangawizi takribani kilo 20,000 kwa mwaka. Wananchi wa Same Mashariki wenyewe wanalima tangawizi kilo 14,500 kwa mwaka. Naiomba sana Serikali hebu angalieni na kafanyeni utafiti mpeleke bei elekezi kwa sababu wananchi wangu wanateseka sana na bei ya tangawizi. Kama wameweza kulima 72% ya tangawizi ya nchi, tena wanailima ile bora inayolimwa kwenye miinuko na milima, naomba mkaangalie vizuri na fanyeni utafiti muwape bei elekezi ya tangawizi, wanateseka sana na bei ambayo iko chini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo naomba niseme naunga mkono hoja na nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, kuna marekebisho kidogo kabla ya Mheshimiwa Charles John Mwijage atachangia Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Charles Mwijage ajiandae na baada ya hapo atafuata Mheshimiwa Kiswaga Boniventura Destery.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia bajeti ya Serikali Wizara ya Kilimo ya mwaka huu 2024/2025 bajeti ambayo imesheheni mambo mbalimbali katika kukuza na kuimarisha sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii inaombwa pesa shilingi trilioni 1.2, kwa hiyo, leo tarehe 02 Mei, 2024 nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunipa fursa hii na afya njema namna hii ili niweze kuchangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa dhamira yake njema ya kukuza sekta hii na kuimarisha sekta ya kilimo, ama kwa hakika mama ni mama na anaupiga mwingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sifa namba moja ya mama ni kuhakikisha kwanza watoto wake wanapata chakula cha kutosha na hatimaye waweze kwenda kuwajibika kwa nafasi mbalimbali. Kwa hiyo, kwenye eneo hili Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia anafanya vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza sana Waziri mwenye dhamana, kwa kweli upele umepata mkunaji na ama kwa hakika Mheshimiwa Bashe unaitendea haki Wizara hii ya Kilimo. Nimuombe tu Mama yetu Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan impendeze kwamba kwa haya maono aliyonayo Waziri wake pamoja na yeye mwenyewe basi aendelee kumuacha katika Wizara hii ili aweze kutimiza ndoto zake katika kuwatumikia wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo Mheshimiwa Bashe hawezi kufanya haya yote peke yake bali ni kutokana na Katibu mahiri, Katibu Mkuu ambaye anafanya kazi pamoja na *delegation* yake, taasisi mbalimbali pamoja na wakurugenzi mbalimbali wa kahawa, korosho, tumbaku, *TOSCI*, *ASA, CPB, NFRA* na *TFC*. Kipekee zaidi nampongeza sana Meneja wa *TFC Tanzania* kwa kazi nzuri ambayo ameifanya ya kusambaza pembejeo za mbolea kwa maana ya mbolea ya ruzuku nchi nzima, kwa kweli mwaka huu hakuna malalamiko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata sisi Wana-Ruvuma ambao tunashika nafasi ya kwanza katika uzalishaji wa mazao ya nafaka hatumdai. Hatumdai Waziri na wala hatumdai Mheshimiwa Dkt.

Samia Suluhu Hassan. Kwa hiyo, tunaomba sasa kwenye hilo ongezeni jitihada za kuhakikisha kwamba mbolea hii inaendelea kufika kwa walengwa ambako ni chini kabisa kwa mkulima ambaye ndiye mlaji wa mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine naomba bila kupepesa macho niwapongeze sana Kiwanda cha *ITRACOM*. *ITRACOM* wanafanya kazi nzuri, lakini mbolea hii ya *ITRACOM* naomba niwaambie Watanzania wote wakulima kwamba ni mbolea nzuri, ni mbolea inayofanya vizuri na ni mbolea ambayo inachanganywa na samadi. Kwa hiyo, bado pia inatunza uoto wa asili na haiharibu ardhi, ikiwezekana basi wananchi wa Tanzania tumieni hii mbolea. Mimi mwenyewe ni mkulima na nimeitumia shambani kwangu, imefanya vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo naomba sasa niende kwenye suala la masoko ya mazao yetu. Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wizara ya Kilimo, wakulima wameendelea kuwekeza kwenye sekta hii ya kilimo, lakini changamoto kubwa ni masoko ya mazao ya wakulima ambayo baada ya kulima wanapata shida kwenye masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee niishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na nimshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, safari hii ametoa pesa nyingi sana kupeleka katika taasisi ya *NFRA* wamewekeza kwenye kununua mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo yote iko changamoto kwenye suala la bei ya mahindi, naomba Mheshimiwa Waziri unisikilize.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto hii inawavunja mioyo wakulima, bei ya mahindi ambayo yanalimwa, nichukulie labda yanalimwa Sumbawanga, Songwe, Njombe, Ruvuma na maeneo mengine, lakini inakuwaje kwenye suala la bei ya mahindi inakuwa tofauti tofauti? Mkulima aliyelima mahindi Songwe anapewa bei ya shilingi 1,000 kwa kilo, lakini mkulima huyo huyo ambaye amelima mazao yake labda tuseme Njombe na Mkoa wa Ruvuma

unakuta Ruvuma mkulima anaambiwa apeleke mahindi yake kwa shilingi 700 au 750.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu niambie Mheshimiwa Waziri vigezo vinavyotumika ni vigezo gani kwamba maeneo mengine mahindi yale yapangiwe bei nzuri ya kununuliwa na *NFRA* na maeneo mengine yapangiwe bei ndogo? Kwa sababu unapokwenda kuanza kulima ni lazima utapata gharama zinazofanana na maeneo mengine ya uandaaji wa shamba. Pia utapata gharama za kununua mbolea na bei ni elekezi nchi nzima wananunua mbegu kwa bei elekezi halafu atakwenda kulima mkulima wa Songwe na mkulima wa wapi watakwenda kulima wote watatumia mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hii mbolea wote wanapewa kwa mtindo wa ruzuku, lakini unakuta kwamba mkulima huyo huyo kwenye hiyo eka moja lazima atatumia viuatilifu. Sasa inakuwaje baada ya kuvuna Songwe wana bei juu, Dodoma wana bei juu na maeneo mengine wanakuwa na bei ndogo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sasa wakulima ni hawa hawa wa Tanzania, wakulima wake Mheshimiwa Waziri na kwa sababu ana nia njema ya kuwakuza wakulima na amesema kwamba kilimo sasa hivi ni kilimo biashara basi aweke uwiano wa ununuzi. Hata kama wanapishana wasipishane kwa kiwango kikubwa, shilingi 250 kwa 750 au shilingi 700 kwa shilingi 300. Hata ukiangalia kwenye usafirishaji *within the country* huwezi kukuta kwamba kuna eneo, kutoa mahindi labda Songwe kwenda Dar es Salaam yanazidi shilingi 150 kwa kilo, hapana. Kwa hiyo, kuwe na uwiano kwenye suala la masoko, kwa maana ya ununuzi wa mazao hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaamini kwamba ili kukamilisha ununuzi wa mazao yote haya na ili *NFRA* waweze kununua vizuri mazao haya ni vizuri sasa bajeti hii ya Wizara ya Kilimo yote kama ilivyo Wizara ya Fedha wawajibike kuipeleka fedha yote kama ilivyo. Wakipelekewa fedha yote kama ilivyo yale yote tuliyosomewa na Mheshimiwa Waziri na yaliyowasilishwa hapa leo kwenye bajeti yake yatatekelezeka na baadhi ya changamoto zitapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uhifadhi wa chakula kwenye sekta ya kilimo kunaendelea vizuri lakini kwenye masuala ya maghala bado yametajwa maghala hapa ambayo yanaendelea kujengwa katika nchi yetu. Bado maghala ni machache, changamoto ni kubwa kwenye kupakua hiyo mizigo inapopelekwa kwenye vitengo hivyo, gari zinachelewa kushusha ni kwa sababu maghala ni machache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nataka kuzungumzia suala la lishe; nataka kumjulisha Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kwamba mimi ni Balozi wa Lishe katika Mkoa wa Ruvuma. Huu ni mkoa ambao unashika namba moja kwa miongo zaidi ya mitano katika uzalishaji wa nafaka, lakini ni ngumu sana kuamini unapopata taarifa kwamba kuna udumavu. Naomba sasa sekta ya kilimo muweke kitengo mahsusi, muweke fungu maalumu kwa ajili ya kwenda kutoa elimu kwa wakulima. Wakulima hao wanaoshika nafasi ya kwanza katika uzalishaji wapate elimu kwa ajili ya kuboresha afya zao. Chakula ni kingi na cha kutosha, lakini hawana elimu ya matumizi. Naona jirani yangu hapa ananiangalia, anaona kama na mimi ni mdumavu, hapana, mimi nimejitahidi kidogo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana kwenye eneo hilo, walau kwenye kitengo hicho cha lishe nimeona amesema kwamba anaboresha mbegu ili ziwe na virutubisho vya kwenda kuboresha lishe, haitoshi kama hawatapata elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kwa namna ambavyo amepambana kuhakikisha kwamba changamoto ya sukari inaondoka. Changamoto ilikuwa kubwa sana, hiyo ndiyo namna nzuri ya uongozi, ukishabaini tatizo unakaa nalo chini na kupitia kwa Mheshimiwa Waziri pamoja na Mheshimiwa Rais wetu wakatafuta changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba matibabu ya changamoto ambayo yamefanyika kwenye sukari basi yawe ni matibabu endelevu, watafute namna nzuri ya kuweza kutibu changamoto hii. Ule ukiritimba wa namna ya uagizaji wa sukari kwamba badala ya kuwa wanaagiza watu tofauti tofauti wanakuwa wanaagiza tu

wale ambao wanazalisha sukari. Basi tafuta namna nzuri na kama kuna sheria inatakiwa ije irekebishwe hapa lete tuichakate ili tuone namna nzuri ambayo itapelekea changamoto hii isijirudie tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa nakupongeza wewe kwa kuchaguliwa kwako kuwa Mwenyekiti wa Bunge na mwisho kabisa naomba sana pamoja na uwekezaji kwenye sekta ya kilimo ni kwamba…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sekunde moja tu.

**MWENYEKITI:** Tafadhali hitimisha.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naomba sana hauwezi kuboresha kilimo endapo miundombinu inayopelekea kilimo hiki kuweza kuwa na utaratibu mzuri, kwa maana ya usafirishaji na nini, kama katika Mkoa wa Ruvuma kule Kigonsera – Matiri kilometa 30 hazijawekewa kiwango cha lami…*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naomba kuwasilisha, lakini pia naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Charles John Mwijage, atafuata Mheshimiwa Kiswaga Boniventura Destery na Mheshimiwa Munde Abdallah Tambwe ajiandae.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia bajeti ya kilimo, bajeti ya sekta ya kiuzalishaji *(production sector)*. Uzuri wa sekta za kiuzalishaji ni namba na namba huwa hazidanganyi. Serikali

imewekeza fedha nyingi kwenye sekta ya kilimo, takribani shilingi trilioni moja na mara moja mauzo ya nje ya nchi yamefika 2.3 *billion shillings*. Mtumishi hatusubiri kufika 2030 kupata shilingi bilioni tano lazima tukae chini tupange magoli upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasahau naunga mkono bajeti hii na napongeza msimamo wa Serikali kwenye sekta hii ya kiuzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia bajeti ya kilimo katika makundi mawili; mchango na fursa ya wakulima wa Tanzania katika kulisha Taifa hili, mchango wa wakulima na wakulima wa Tanzania wana jina lao wanaitwa wakulima wadogo na suala la pili nitakalochangia ni mchango na fursa ya kilimo *(crops)* katika kuleta fedha za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wakulima ambao tunawaita wakulima wadogo wameweza kutulisha. Kwa takwimu nilizopitia ni kwamba kwa muda wa miaka saba hatujawahi kupata tatizo la chakula. Nachukua fursa hii kuwapongeza wakulima wa Tanzania ambao kimsingi ni wakulima wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunazungumza tukiwa watu milioni 62 au 63. Miaka 23 ijayo au mwaka 2050 na ninashukuru Waziri mwenye dhamana ya Mipango amekalia kiti cha msimamizi wa Shughuli za Serikali Bungeni, uandike vizuri, miaka 23 ijayo nchi hii itakuwa na watu takribani milioni 120 mpaka milioni 140 kama tukienda kwa kasi ya chini. Ni wakulima hawa hawa ambao tunategemea kuwa wataweza kutulisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nawapongeza hawa wakulima, mimi napenda kujua mpango na mkakati wa Serikali ambao watafanya kwa ajili ya wakulima hawa ambao wanazalisha chakula. *A hundred plus percent* tunakula, tunashiba na kingine tunauza. Ni mbinu na mikakati gani itafanyika ili mwaka 2050 tuweze kufika tukiwa tuna chakula na tukiwa tunatumia watu hawa hawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoa ushauri na ninyi mtaongezea na wataalamu wenu. Moja, huyu mkulima mdogo ambaye tumekuwa tukimpongeza tusije tukadanganyika kuachana naye. Usije ukasema huyu mdogo umwache sijui ulete mkubwa, unamwacha aende wapi? Ushauri wangu ni kwamba ni lazima tuje na mpango na mkakati wa kuweza kuwalea hawa wakulima wadogo wadogo, kuwatoa kwenye nusu hekta kwa mtu na tuwapeleke kwenye hekta tano au hekta nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo ndipo ninapokwenda kwa Mheshimiwa Waziri, tuje na *BBT* ya kisasa, inaitwa *BBT* ya 2050. Unamfuata mtu pale kwake alipo, unapanua kipande chake cha shamba, unamweka kwenye ushirika bila kumwondoa mahali pake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ni hulka, kilimo ni tabia na kilimo ni utamaduni. Mtu aliyezoea kulima kwenye ubaridi ukimleta kwenye joto anaweza akaota mchana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni kubaini maeneo ya kilimo. Leo kuna tatizo linatokea, kwa mfano mvinyo unalimwa Dodoma na ni wa kipekee duniani. Dar es Salaam inahamia Dodoma, tutakuja kujenga kiholela au kujenga kisasa, eneo lote la kulima zabibu litakwisha. Sasa ile *Lusinde Wine* mtailima wapi? Hapo ndipo inapokuja mapema haja ya tujenge ghorofa ama tupeleke majengo kwenye miamba kusudi tuhifadhi ardhi kwa ajili ya mazao maalumu na mazao yajayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba tatu, kuongeza nguvu katika tija, ninaungana na Mheshimiwa Waziri na nimwambie Mheshimiwa Waziri, hakuna kificho, anasema ataongeza tija katika kilimo. Tija katika kilimo ni ardhi, *land classification*, mbolea na maji. Ninamwalika aje kwenye shamba langu la migomba achimbe kisima, aniwekee *pipes* za *irrigation*, niongeze *tonnage* nipate *tonnage* 64 kwa hekta. Asione aibu kuja kwa mtumishi mwenzake, lakini utaratibu huo huo uwafuate watu wote kule walipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba nne ni ushirikishwaji wa wakulima katika mashamba makubwa. Nakubaliana na mashamba makubwa, hizi *irrigation* zinazofanyika na ambazo

hazihusishi umwagiliaji. Nimeshamwelewa mtumishi, mfano wa *Gabiro Agri-business*, huu ni mfumo wa *irrigation* ambapo eneo linatengwa na amenihakikishia kwamba anakwenda kuanzia nao Kagera sehemu za *Burigi Farm* kwenye *irrigation* na kwenye ule mto mkubwa wa Ngono kwamba watu wanapewa eka tano halafu wanapewa pembejeo na mbegu, halafu yeye anachukua mazao na kwenda kuyauza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba tano ni kuhusiana na shughuli ya masoko; nimemsikia Mwenyekiti anasema masoko. Dawa ya masoko ni moja; moja ya fursa ni kwenda kwenye *niche market*. Nimemsikia Mheshimiwa Spika anamtangaza mjasiriamali mmoja au mwekezaji mmoja mwanamama ambaye ni chipukizi. Mheshimiwa Waziri aige mfano wangu, huyo waliyemtangaza leo mimi nilimpeleka kwenye mazoezi Vietnam na India na ameshakuwa mwekezaji mkubwa. Wawapeleke Watanzania yaani wanaposhuka *airport* waseme hawa ni Watanzania, waweze kuwekeza katika shughuli hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni mchango wa fursa ya sekta ya kilimo katika kutuingizia fedha za kigeni. Nampongeza Mheshimiwa Waziri amefikisha *2.3 billion shillings* kwenye mauzo. Napenda kukiri kwamba siridhiki na kiwango hiki, nchi ya Ukraine kabla haijapigwa na Urusi ilikuwa inapata *USD 27 billion*. Walifanya nini? Nitampa mfano wa pili, Uganda wanapata *USD* bilioni moja kwenye kahawa. Wanalima tani laki nne za kahawa, yeye za kwake anaona aibu kuzitaja, wanatuzidi nini? Eneo la kulima kahawa la Uganda nchi nzima linazidiwa na eneo la Mkoa wa Kagera na ndipo tunasema turudi kwenye kubaini maeneo, tupanue mashamba ya wananchi, tuwasaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la mbolea, kwa mfano Kagera mbolea ya chumvi chumvi hawaipendi. Akae na Mheshimiwa Waziri wa Mifugo, wale wanapenda kahawa iwekwe samadi. Wataalamu wa kahawa, amuulize Bwana Kanjagaile, wanakwambia *aroma* ya kahawa iliyowekwa samadi inapendeza sana. Sasa aanzishe utaratibu, awape ng'ombe halafu watalipa maziwa na samadi waweke kwenye kahawa. Hiyo ndiyo njia rahisi ya kuwapeleka watu kwenye ushirika, unaitwa ushirika wa Bashe,

yaani mtu atalazimika kwenda kwenye ushirika kusudi aweze kupewa ng'ombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia suala lingine la mpunga au mchele. Afrika inaagiza nje mchele uliokobolewa wenye thamani ya shilingi bilioni tano. Tanzania tunayo matabaka yote ya eneo la umwagiliaji, takribani hekta 27. Naipongeza Serikali kwa kumaliza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwenye Mto Ngono na kule Burigi, lakini bado hatujaweka nguvu ya kutosha. Tanzania tunayo fursa ya kuweza kulima mchele mwingi, Afrika mwaka kesho itahitaji tani milioni 40, *potential* ya Tanzania tunaweza kupata kirahisi…*(Makofi)*

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kingu, Taarifa tafadhali.

**TAARIFA**

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa Taarifa mchangiaji, kaka yangu Mheshimiwa Mwijage kwanza anachangia mchango wa kizalendo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa kwamba katika takwimu anazozitoa za uzalishaji wa mpunga, ninaungana naye, lakini katika kipengele anachokisema ni kwamba hatujaweka juhudi fulani. Hapa ninapozungumza wananchi wa Jimbo la Singida Magharibi, Kata ya Mgungira, 70% ya uzalishaji wao wa mchele unashambuliwa na ndege. Kwa hiyo, ni miongoni mwa mikakati ambayo Mheshimiwa Bashe na Wizara yake wanaweza wakaiweka ili ku-*compliment* kile ambacho wananchi wanakizalisha kwa ajili ya *export* ya nchi.

Kwa hiyo, nilikuwa nafikiria kumpa mchangiaji Taarifa hii muhimu sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Kingu. Mheshimiwa Charles John Mwijage unaipokea Taarifa?

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea, unajua ukiwa maarufu mtu anataka akupige Taarifa kusudi apandie hapo sasa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nazungumza nimesema nazungumzia mwaka 2050.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwijage muda wako umeisha, tafadhali naomba hitimisha.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika yangu iliyopotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia mwaka 2050 kwamba Tanzania tunaweza kuzalisha tani milioni 12 kutoka kwenye tani milioni mbili ya sasa. Tunaweza kuchukua *part of that 60 billion* ambayo Afrika ina-*import* tukaongeza kwenye mapato yatokanayo na kilimo na tukapata kwenye dola bilioni kumi kutoka kwenye sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na namuunga mkono Mheshimiwa Waziri na msaidizi wake na Wizara yake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Charles John Mwijage, sasa ni Mheshimiwa Kiswaga Boniventura Destery, ajiandae Mheshimiwa Munde Abdallah Tambwe na baadaye atafuata Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia Wizara ya Kilimo. Kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuiona Wizara ya Kilimo kwamba ndiyo *engine* ya uchumi na hivyo akatenga fedha nyingi ambazo kwa kweli ni historia. Tunapozungumza shilingi trilioni 1.2 nimehesabu, wale ambao tumezoea kuweka fedha kwenye begi, shilingi milioni mia mia ambayo ni sawa na mabegi 12,000. Maana yake hata wabebaji ni watu 12,000 wanabeba mabegi ya mia mia, sawa na

shilingi trilioni 1.2. Hongera sana kwa Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo ameionesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza pia Mheshimiwa Waziri na hapa ndipo ninapomshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutupa huyu kijana na msaidizi wake na Katibu Mkuu. Ni kwamba yale ambayo alikuwa anayaishi akiwa kule nyuma kabla hajapata Uwaziri ndiyo anayoyafanyia kazi sasa hivi na yale ambayo tumemshauri miaka yote ndiyo ambayo anayafanyia kazi sasa hivi. Hongera sana Mheshimiwa Waziri kwa kuendelea kutusikiliza na haya mambo yatatupeleka kwenye uchumi wa wananchi unaotarajiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapoipongeza Wizara, nazipongeza na benki kama vile *TADB* ambao ni wadau wakubwa wa kilimo, *CRDB* na *NMB*. Hao wote wanawezesha kilimo kwenda mbele, kwa maana ya wakulima, lakini pia na wale wafanyabiashara ambao wako kwenye sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwangu kule Wizara imebaini mabonde 13 ya umwagiliaji ambapo matatu yameanza kufanyiwa usanifu; Bonde la Sawenge na Bonde la Simiyu, yote haya yanafanyiwa usanifu. Pia kuna mabonde kumi ambayo sasa hivi yanahitaji fedha ili yaweze kufanyiwa usanifu, yakisanifiwa hayo upungufu wa chakula, upungufu wa mchele kule Magu utakuwa umekatika kabisa. Namwomba Mheshimiwa Waziri atupatie fedha ili tuweze kufanya usanifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, mwaka huu tumepata neema, neema ambayo Mwenyezi Mungu ametupa na neema hizi huwa hazijirudii mara mbili. Naomba sana, nimetembea kutoka Kigoma, Katavi, Morogoro mpaka Magu, mpunga umeiva sana. Ninamshauri Mheshimiwa Waziri wa Kilimo aendelee kuachia mipaka kwa utaratibu wa vibali ili wananchi wetu waweze kuuza mazao hayo nje. Tusipofanya hivyo mchele unakwenda kushuka mpaka shilingi 600. Kwa hiyo, tuachie mipaka ili wananchi waweze kuuza nje na wakiuza nje tutapata fedha za kigeni na ndipo tutapokuza uchumi wa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba utafiti ufanyike, kwenye zao la pamba sasa hivi ukipitia mashamba baadhi yake yamebadilika na kuwa *brown*. Kwa hiyo, sijui sayansi imegota? Watu wetu wa Bodi ya Pamba wanajitahidi sana kila mwaka, lakini sijui wamekosa usaidizi wa wataalamu wa kilimo hasa kwenye halmashauri zetu, ambao wangegundua ni tatizo gani linasababisha pamba kubadilika rangi na kuwa *brown*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamba inapobadilika rangi tu na kuwa *brown* inaangusha vitumba vyote na ndipo sasa tija inapokwenda kupotea. Kwa hiyo, tija inapopotea tunapata mazao kidogo mno. Nimwombe kabisa Mheshimiwa Waziri, hili jambo alichukulie *very serious* ili tuweze kumaliza matatizo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili pia hata kwenye mpunga wanasema wakulima mpunga unabadilika unakuwa njano unapotaka kuchanua, kwa hiyo, hauendelei tena kuchanua. Hebu utafiti ufanyike ili kuwasaidia wakulima wetu kwa sababu tunahitaji wakulima wapate tija iliyo kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mbolea ya ruzuku hii kule kwetu Magu inauzwa kwenye makao makuu ya Wilaya. Tunashauri mawakala hawa wauzaji wa mbolea kama inawezekana washuke kwenye makao makuu ya kata kwa sababu wananchi wetu wanapiga hesabu ya kufuata mfuko wa ruzuku makao makuu ya wilaya, anapata gharama kubwa. Kwa hiyo, wengine wanashindwa hata sasa kuitumia hiyo mbolea ya ruzuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushauri sana ama watu wa mbolea ya ruzuku wenyewe washuke kwenye halmashauri zetu wahamasishe wafanyabiashara wadogo wadogo kule chini ili waweze kuwa mawakala wa usambazaji mbegu ya ruzuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni fidia ya bei, Mfuko wa Fidia ya Bei ni muhimu sana kwa sababu duniani kote hilo jambo huwa lipo. Niombe wakati Mheshimiwa Mashimba hapa anajibiwa swali, mlitamka kwamba mfuko umekwishakuanzishwa kwa Tangazo la Serikali, lakini haujabainisha vyanzo vyake vya mapato. Naomba sana kwamba kuna wakati duniani mazao huwa

yanapanda, yakipanda tuangalie kama vyanzo vinaweza kuwa mazao yenyewe kwa sababu mazoea huwa ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano wakulima wetu wa pamba, walizoea bei ya shilingi 2,000 na mwaka jana ikashuka mpaka shilingi 1,060, mwaka huu tena inatarajiwa kushuka. Kwa hali ilivyo sokoni, ukiangalia na uki-*google* ni senti 70 maana yake tunampeleka tena kwenda…

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mazoea hayo ni kuwatengenezea Mfuko wa Fidia ambao unaweza kuchangiwa na sekta zote za mazao na sehemu nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilimradi tusiwakatishe tamaa wakulima wetu kwa sababu bila mfuko huo, kwa sababu duniani kule hasa nchi za Ulaya na nchi za Asia, kuna utaratibu huo wa kufidia wakulima hasa wanapoona kabisa kwamba bei iliyokuwepo mwaka jana na hii haimlipi mkulima kwa sababu wewe mwenyewe wakati wote Mheshimiwa Waziri unazungumza kilimo ni gharama na ni gharama kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wakipiga hesabu wanaweza kukata tamaa ya kulima na tusipotafuta utaratibu wa kuwasaidia hao wakulima tutawakatisha tamaa na wakulima wetu sasa ndiyo uchumi halisi ambao wanautegemea watu wote, sisi ambao tunatoka kwa wakulima.

Kwa hiyo, nakuomba sana tuletee, tunao ushauri wa kuweza kukusaidia utoke wapi, fedha hizi zitoke wapi, kwanza zinaweza kuchangiwa na mifugo, zinaweza kuchangiwa na madini, zinaweza kuchangiwa na kilimo chenyewe kwa sababu ndicho ambacho tunakitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hiyo wakulima wetu wanapopata fedha nyingi ndipo wanapokwenda sasa kununua bidhaa dukani, bidhaa zinazochangia kodi kwa nchi, kwa mfano wakienda kununua bati, kuna *VAT* na kuna kodi kwa nchi, wanapokwenda kununua *cement*, kuna *VAT* na kuna kodi kwa nchi, wanapokwenda kununua hata soda, hata majora, hata

nguo, kote huko kuna fedha, kodi za Serikali. Kwa hiyo, niombe kwenye mfuko huu, hata kama siyo leo…

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kama siyo leo, Serikali ione namna ya kutuletea mpango mzuri wa…

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiswaga kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Maganga.

**TAARIFA**

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa Taarifa mzungumzaji, anaongea vizuri sana. Mheshimiwa Waziri naomba ashike mchango wake vizuri kwa sababu wakulima sasa hivi wameanza kuvuna mpunga, lakini wanapata shida sana wanapotoa mizigo shambani, wanatozwa ushuru. Kwa hiyo, kwenye kuhitimisha hoja hii Mheshimiwa Waziri, utoe ufafanuzi kwa sababu bila wewe kuwalinda wakulima, ina maana watapata tabu sana kwenye nchi hii. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Nicodemas Maganga, Mheshimiwa Kiswaga kabla haujasema, naomba Waheshimiwa Wabunge tufahamu kwamba muda ambao tunatumia kutoa Taarifa ni muda wa mzungumzaji. Kwa hiyo, tuangalie pia *flow* ya mzungumzaji, halafu tuone kama tunamsaidia mzungumzaji ili kuweza kuhitimisha hotuba yake vizuri.

Mheshimiwa Kiswaga, tafadhali.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naenda la mwisho, naipongeza Serikali, Mheshimiwa Waziri hapa amezungumza, wafanyabiashara na Bodi ya Pamba wamenunua trekta 200 kwa ajili ya ku-*support* kilimo cha pamba. Tulikubaliana kwamba ziende kabla ya kilimo, lakini bahati mbaya zikawa zimechelewa hizi trekta. Sasa mpango wa zile kata 40, wafanyabiashara tumekubaliana kwamba zianze mwaka kesho wa kilimo ili tuweze kupeleka matrekta mapema mwezi wa tisa na maandalizi ya kupeleka wagani yaendelee, kwa sasa mwaka huu iwe *free trade* kwa sababu hatujawekeza chochote kwa wakulima, lakini mpango ni mzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuwaambia tu kwamba imekuwa ni mara ya kwanza kwa Mheshimiwa Waziri kubuni kitu kama hiki ambacho kinakwenda kuwasaidia wakulima hasa tutakapokwenda kukubaliana vizuri. Sisi tunashauri badala ya kupelekwa kampuni moja kule, tupeleke kampuni mbili au tatu ili ziweze kushindana, hata ule uwekezaji wenyewe unaweza kuwa na tija kamili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Munde Abdallah Tambwe, atafuata Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga ajiandae.

**MHE. MUNDE A. TAMBWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii na mimi kuweza kuchangia Wizara nyeti, Wizara ya Kilimo. Niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote waliotangulia kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo ameweza kuifanya ndani ya sekta yetu ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika, haijawahi kutokea toka nchi hii imepata uhuru, kupeleka shilingi trilioni 1.2 kwenye kilimo. Hii inaonesha ni jinsi gani Mheshimiwa Rais anathamini kilimo cha Watanzania, ni jinsi gani Mheshimiwa Rais anathamini watu wanyonge, ni jinsi gani Mheshimiwa Rais

alivyolibeba kundi kubwa la Watanzania la upande wa kilimo. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kutuongezea pesa kwenye kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini na mimi naungana na wajumbe waliopita kuiomba Wizara ya Fedha – Hazina kuhakikisha fedha hizi zinakwenda kufanya kazi kama ilivyoongelewa kwenye bajeti ya Serikali wakijua kabisa kilimo ni uti wa mgongo wa Watanzania, kilimo kinashika Watanzania wengi. Kwa hiyo, kutokupeleka fedha hizi kwa wakati, nina hakika watakuwa wamewakwamisha wakulima. Tunamuamini sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na tunaamini anajua nini maana ya kilimo na atapeleka fedha kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa waliyoifanya kwenye kilimo, wamefanya kazi kubwa sana. Watanzania wa nchi hii hasa wakulima, hawatasahau walivyopewa mbolea ya ruzuku nchi nzima. Hakika wana imani kubwa na Mheshimiwa Rais na hawana cha kumlipa Mheshimiwa Rais, hakika mwaka 2025 watampa mama huyu kura nyingi za heshima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena kurudia kuipongeza Serikali hasa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kwa kazi kubwa anayoifanya, lakini Katibu Mkuu wake wa Kilimo, Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na Menejimenti nzima ya Wizara ya Kilimo, wanafanya kazi kubwa, inaonekana, hakuna Mtanzania ambaye hajui. Hakika wametimiza *slogan* yao ya 'Kilimo Ni Biashara.' Leo hii kilimo ni biashara, ulime mpunga, utauza, ulime mahindi, utauza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani biashara ilikuwa inajulikana, tumbaku, kahawa, pamba ndiyo yalikuwa mazao ya biashara, lakini leo hii, chochote utakachokilima, ukilima mbaazi, ukilima ufuta, vyote ni biashara. Kwa hiyo, tunawapongeza sana kwa ubunifu wao mkubwa na *slogan* yao imeenda kutimia ya Kilimo Ni Biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana Wizara ya Kilimo kwa mpango wao na ubunifu wao wa *BBT*. Wakati wanabuni

kitu hiki, watu wengi walikuwa na mashaka nacho, mimi nawaambia, jambo hili ni geni, jambo hili ni jipya, ndiyo wameanza nalo na wanakwenda nalo vizuri sana. Leo Mheshimiwa Waziri ametuambia hapa, *BBT* imeajiri watu 475,000 na mimi nina imani kubwa, kule mbele tunapoendelea na *BBT*, tunaenda kuajiri mamilioni ya vijana Watanzania pamoja na kinamama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *BBT* imejikita sana kwa akinamama na kwenye vijana, kwa hiyo, tunaamini kabisa Mheshimiwa Waziri na Menejimenti yako, Mheshimiwa Naibu Waziri kazeni buti, songeni mbele, msisikilize maneno ya watu. Hakika ukitaka kufanya kitu, ukisikiliza miruzi mingi watakupoteza, *BBT* ni jambo jema na nimeona kwenye bajeti yenu, mmetenga halmashauri 100 kwa ajili ya kuweka *BBT* kwenye kila halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie Mheshimiwa Waziri, Mkoa wa Tabora ambako yeye anatoka, hakuna kilimo cha *BBT,* tunakuomba sana, katika hizi halmashauri 100, usisahau Halmashauri za Tabora hususan Tabora Manispaa. Tabora Manispaa tumetenga hekta 62 katika Kata ya Kalunde, tunakuomba sana Mheshimiwa Waziri, uje na mpango wa *BBT*, pale ni mjini, vijana wengi wamesoma, hawana ajira, wanakutegemea sana Mheshimiwa Waziri, utahakikisha *BBT* inaingia kwenye Mkoa wa Tabora, Mheshimiwa Mama Sitta anasema usimsahau na Urambo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Menejimenti yake nzima, wanafanya kazi kubwa, wanaleta heshima kwa wakulima. Wakulima sasa hivi wana pesa sana hasa wakulima wetu wa tumbaku wa Mkoa wa Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie uzalishaji wa tumbaku; mwaka 2019 katika Mkoa wetu wa Tabora ulishuka sana kiasi kwamba tulipata kilo 45,000 tu wakati *TLTC* wanaondoka, lakini alivyoingia Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu pamoja na Waziri wake Mheshimiwa Bashe na viongozi wenzake wote wa Wizara, waliamua maamuzi magumu ya kuweka wanunuzi wazawa, wanunuzi wazawa wamekuja kulikomboa zao hili kutoka kilo 45,000 mpaka leo tunanunua kilo 175,000,000, hii haijawahi kutokea toka tupate uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2011 ndiyo tulinunua sana tumbaku, zilikuwa kilo 120 lakini sasa hivi tumeenda kununua kilo 175. Limeongelewa kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwamba ifikapo mwaka 2025 tutanunua tumbaku kilo 195 karibu kilo 200. Lakini ingekuwa siyo changamoto ya mvua, tulikuwa tunakwenda kuvuka Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, nawapongeza sana Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tumeweza kutoka kwenye dola 1.6 mpaka dola *two-point* kwa kilo, kwa kawaida tumbaku ikiwa nyingi inashuka bei, lakini si kwa Awamu ya Sita, tumbaku nyingi lakini imepanda bei, tumeenda kuvuka wastani. Sasa hivi tumbaku ni dola mbili hadi tatu ambapo wastani wetu ni dola mbili, hiyo yote ni juhudi kubwa ya Mheshimiwa Waziri na maamuzi magumu ya kutafuta wanunuzi wazawa, wanunuzi wa nje walikuwa wanaturingia, wanatuwekea masharti mpaka tukapata kitu kinaitwa makinikia, tumbaku mbaya wanaichagua, wanaitupa, sasa hivi hamna tumbaku inayotupwa, tumbaku yote inanunuliwa. *(Makofi)*

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. MUNDE A. TAMBWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni pongezi kubwa na tutakaa…

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa

**MHE. MUNDE A. TAMBWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sitaki Taarifa. *(Kicheko)*

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Munde, kuna Taarifa tafadhali. Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa Taarifa tu mchangiaji anachangia vizuri sana, si kwamba tu bei imeongezeka, lakini pia madaraja ya tumbaku yameongezeka. Zamani yalikuwa madaraja 45 sasa ni madaraja 65 iliwemo *L1L, LM10* na *L1R* ambazo zote zina dola tatu, tatu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Munde, tafadhali, unapokea Taarifa?

**MHE. MUNDE A. TAMBWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naikubali hiyo Taarifa maana naona imetolewa na mtu wa maana kabisa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni changamoto za tumbaku, tunamwomba Mheshimiwa Waziri na Menejimenti yake nzima, tunaomba ruzuku sasa kwa wakulima wa tumbaku ambao kipindi kilichopita hatujawahi kupata ruzuku, lakini tunaomba ruzuku ya mabani, mabani yetu yamekwenda na maji sana, tunaomba tupate mabani ya kisasa. Tunaomba tuongezewe maghala ndani ya vyama vyetu vya msingi ili kusaidia ukusanyaji wa tumbaku kwa ukaribu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba sana Serikali ituboreshee zao letu la tumbaku kwa kuhakikisha tunapata mbolea kwa wakati pamoja na pembejeo zake. Baada ya kupata mbolea ya ruzuku, tunaiomba sasa Serikali pamoja na Wizara, Afisa Ushirika wetu wa Mkoa wa Tabora hana gari Mheshimiwa Waziri. Anafanya kazi kubwa sana, tunaingiza pesa za nje *USD* 420,000,000 mwaka huu na zote hizo anazisimamia Mrajisi wetu wa Mkoa na hana gari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakuomba sana kama Wizara mkae muone mtamsaidiaje huyu mtu wetu wa ushirika ambaye anasimamia mambo yote haya, anasimamia fedha zenu zote mnazozileta, mbolea na dawa, tunaomba sana mumuangalie kwa jicho la karibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naenda sasa kwenye suala la mabwawa, pale Tabora Manispaa Inala, tulijengewa bwawa zuri mwaka 2017 lakini bwawa lile halina tija kwa sababu halifanyi kazi vizuri, haliko vizuri. Tunaiomba Serikali itutengee bajeti ya kukarabati Bwawa la Inala. Bwawa hili la Inala pia lina mgogoro mkubwa wa ardhi, lilijengwa kwenye maeneo mengine ya watu, tunaiomba Wizara ya Kilimo na Wizara ya TAMISEMI ikae na hawa watu ili pesa za Serikali ziende zikafanye kazi ya kilimo kama zilivyopelekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata pesa kwenye Kata yetu ya Iyombo shilingi 4,000,000,000, kazi inaendelea, tumepata visima 120 Tabora Manispaa, kazi nzuri inaendelea na tunaishukuru sana Wizara, lakini Kakola, Magoweko tumewekewa mpango kwenye bajeti ya Serikali kwamba tutajengewa bwawa. Nimuombe sana Mheshimiwa Waziri bwawa hilo la Magoweko ni muhimu, kuna wakulima kule wazuri, tunaliomba liwepo ili tuendelee na kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sisi kama Tabora Manispaa tumeomba mabwawa katika Kata ya Itetemia, Isukamahela, Kata ya Misha – Nyakato, Kata ya Kalumwa – Uyui, Kata ya Kalunde na Kata ya Manolewito – Njanda. Tunakuomba sana Mheshimiwa Waziri lakini kaka yangu Mndoro unanisikia, tunajua uwezo wako wa kufanya kazi ni mkubwa sana na tunajua unajua kwamba kilimo cha uhakika ni kilimo cha umwagiliaji. Tunaomba sana mtuangalie katika suala zima la umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Tabora tuna Chuo cha Kilimo cha Tumbi, kile chuo kimefanya kazi kubwa. Tunaipongeza Serikali, mmewapa pesa kwa ajili ya utafiti, wametafiti mbegu za mahindi, mbegu zile zimetokea kupendwa sana kanda nzima ya Magharibi na zile mbegu zinafanya kazi vizuri mno, lakini wamepata mbegu ya mihogo, mbegu hii ni nzuri sana ya mihogo na ni mihogo lishe hasa kwa akina baba, mihogo hii kina baba wakila, inawasaidia sana, kwa hiyo, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri…*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hitimisha tafadhali, muda wako umeisha Mheshimiwa, tafadhali hitimisha. *(Makofi)*

**MHE. MUNDE A. TAMBWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, sana. Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, atafuata Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga, Mheshimiwa Cecil David Mwambe ajiandae.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi naanza kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri ambayo anaifanya katika Wizara hii, Mheshimiwa Waziri hongera sana, lakini pili, nampongeza msaidizi wake Naibu Waziri Mheshimiwa Silinde kwa kazi nzuri, ni msikivu, ni mpokea ushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile nawapongeza watendaji wa Wizara hii wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu Gerald, ni wasikivu, ni wachapakazi na ndiyo maana Wizara inafanya kazi vizuri na inasonga mbele. Hongereni sana watendaji wa Wizara ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nampongeza Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa *passion* yake kwenye kilimo. Tumeona sasa bajeti ya Wizara imetoka shilingi 900,000,000,000 mpaka shilingi 1,248,000,000,000. Hii ni maono yake kwamba yeye anathamini sekta ya kilimo lakini ana nia ya dhati ya kuwakomboa wakulima, lakini si hivyo tu, Mheshimiwa Rais anatoa fedha hizi kwa sababu ya ubunifu wa hawa Waheshimiwa Mawaziri na watendaji waliopo katika Wizara ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunampongeza Mheshimiwa Rais, lakini tunawapongeza watendaji na viongozi wa Wizara hii, Mheshimiwa Waziri pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa ubunifu wao, kila kukicha wanakuja na programu mbalimbali ambazo zinasaidia kuinua sekta hii ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia maeneo mawili; eneo la umwagiliaji na eneo la tasnia ya korosho na nianze na eneo la tasnia ya korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa usikivu wa Wizara hii, wakati mwaka jana tunafanya mkutano wa tathmini ya msimu wa korosho, tulipendekeza kwamba iundwe timu ya wataalamu ili kuangalia mnyororo wa thamani wa zao la korosho kuanzia uzalishaji hadi sokoni, zibainike changamoto, yatolewe mapendekezo ili Wizara ilifanyie kazi kulingana na tasnia ya korosho ilivyo na changamoto nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri kwa usikivu wake, aliunda tume ya watu makini, tume ya kizalendo, tume ambayo imekuja na ripoti ambayo Wizara imeshaanza kuifanyia kazi. Naipongeza ile tume kwa kazi nzuri kwa sababu imekuwa ina zaidi ya *volume* tatu ambayo inachambua tasnia ya korosho kuanzia uzalishaji, uuzaji mpaka uongezaji thamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda huu nitachangia baadhi ya maeneo na kwanza, tume imeangalia mfumo wa mauzo ya korosho ikasema kwamba kuna changamoto na malalamiko, ikapendekeza kwamba msimu huu ije na mfumo wa *TMX*. Mfumo huu ambao Waziri ameuwasilisha hapa ni kwamba miongoni mwa mabadiliko yaliyopo katika tasnia ya korosho ni kuwa msimu huu tutauza korosho kwa *TMX*. Mheshimiwa Waziri nakupongeza sana kwa maamuzi yako ya busara, umesema hapa kuna malalamiko na misukosuko mingi, lakini nakuhakikishia hao wanaolalamika siyo wakulima wa korosho, wakulima wa korosho wamepokea wazo hili na wanachotaka ni bei nzuri sokoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanachotaka wakulima wa korosho ni kwamba korosho yao iwe na tija, wanachotaka wakulima wa korosho ni wanufaike na zao lao la korosho, wale wanaolalamika siyo wakulima ni watu wengine, wakulima wamepokea wazo hili na wanasubiri kwa hamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni wakati *TMX* inaingia iangalie changamoto zilizojitokeza wakati tunatumia *TMX*

kwenye mazao ya ufuta ili tukienda kwenye msimu wa korosho, basi kusiwe na changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya kwanza wakati ule ilikuwa ni wahusika kutokuwa karibu na maeneo ya wakulima wa korosho kitu ambacho natarajia kwamba tukiingia kwenye msimu huu basi *TMX* itakuwa na utaratibu wa kuweka ofisi jirani na wakulima ili waweze kutatua changamoto za malipo pindi inapojitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo Kamati hii imependekeza ni kuhusu tozo zilizopo kwenye tasnia ya korosho. Tume imeeleza kinagaubaga kwamba kwenye tasnia ya korosho kuna tozo nyingi ambazo zinamuumiza mkulima sokoni. Bei ya mkulima inaathiriwa na tozo ambazo zinatozwa pale baada ya mauzo ya korosho, ninaishauri tume na pia ninakuomba Mheshimiwa Waziri kuwa sasa ni muda mwafaka wa kuzipitia zile tozo nyingine na kuziondoa ili mkulima apate bei nzuri sokoni na hii pia ni kwa sababu kwenye taarifa yako umesema kwamba Serikali itarudisha ile *export levy* ya 50% kwa hiyo, itatoa 100% kwenda kwenye tasnia ya korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mapendekezo yangu tozo ambazo tunaweza tukaanza nazo ni tozo ambazo tunazipeleka kwenye taasisi ambazo zinaweza zikapata fedha kwa utaratibu mwingine, kwa mfano, tozo ya *TARI,* hii tumeangalia kwenye mazao mengine wanachukua *lumpsum,* kama kwenye pamba wanachukua shilingi bilioni mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukafanya hivyo, tukatenga shilingi bilioni mbili tukawapa wao kama wanavyofanya kwenye pamba, badala ya kumkata mkulima wa korosho shilingi 25 kwa kila kilo. Uki-*compute* kwa hesabu ya uzalishaji wa korosho kwa mwaka ni zaidi ya shilingi bilioni sita au saba zinatolewa kwenda *TARI* wakati pamba na mazao mengine yanatoa mchango kama niliowaelezea hapo mwanzo, kiasi cha shilingi bilioni mbili au bilioni 1.5. Kwa hiyo, siyo lazima tumkate mkulima kila kilo shilingi 25 tunaweza tukachukua hiyo *lumpsum* tukawapa *TARI* ili waendelee na majumuku yao na huku mkulima hataumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tozo nyingine ni ile ambayo inaenda Bodi ya Korosho; Bodi ya Korosho ni taasisi ya umma, inaweza kuendeshwa kwa ruzuku ya kawaida kama wanavyopata taasisi nyingine. Hakuna sababu ya mkulima wa korosho kuchangia kila kilo shilingi 25 kwa ajili ya uendeshaji wa Bodi ya Korosho, kwa hiyo, naomba na hii nayo iondoke ili fedha hiyo iende kwa mkulima wa korosho kwa sababu Bodi ya Korosho ni kama ilivyo Bodi ya Chai, Bodi ya Kahawa na bodi nyingine na inaweza kuendeshwa kwa taratibu nyingine za uendeshaji wa shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo limeongelewa katika taarifa ile ni soko la awali. Mimi sipingi soko la awali, liliwekwa kwa ajili ya kuwawezesha wabanguaji wa ndani na wawekezaji wa ndani wapate korosho kwa urahisi, lakini soko hili limekuwa chanzo cha vurugu wakati wa msimu. Ni muda muafaka sasa kama tume ilivyopendekeza, utafutwe utaratibu mwingine wa kuwawezesha wabanguaji wetu wa ndani kupata korosho na kuna njia nyingi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza ukatafuta baadhi ya maghala na baadhi ya *AMCOS* wakawa wanaweza kununua kwa soko la awali au tukafuta kabisa waende mnadani na Serikali itoe motisha nyingine kwa wawekezaji wa ndani, kwa mfano, Ivory Coast wao wanatoa motisha ya kwa kila kilo inayobanguliwa na mbanguaji wa ndani anapewa ruzuku na Serikali na hii fedha utakuta kweli inakwenda kwa mbanguaji, siyo kama ilivyo sasa hivi, soko la awali kwa msimu uliopita hata kangomba wameingia, wameingia hata wale ambao walitaka kwenda mnadani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kwenda mnadani wao wakaenda kwenye soko la awali na ndiyo maana vurugu zingine zikaanza, ule mwongozo wa zamani ukafutwa, korosho zikasafirishwa usiku zikapelekwa bandarini. Kwa hiyo, naomba soko la awali nalo vilevile utolewe mwongozo mpya ili kuhakikisha kwamba halivurugi minada yetu wakati wa msimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tume ilipewa jukumu la kuangalia mpango wa Serikali wa kuongeza thamani kwa ile kongani ya ubanguaji korosho ya pale Maranje. Taarifa ya Kamati inasema ni wazo zuri kwa sababu lazima sasa hivi Serikali ijikite kuuza korosho-

karanga na siyo kupeleka korosho ghafi nje. Hii itatusaidia kupata bei nzuri kwa mkulima wetu wa korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninaomba kushauri, kwanza naipongeza Wizara, imeshapeleka Bodi ya Korosho zaidi ya shilingi bilioni tano kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Naiomba Bodi ya Korosho iongeze kasi ya utekelezaji maana Wizara imeshakamilisha jukumu lake la kutoa fedha hivyo basi, bodi iongeze kasi ya utekelezaji ili kongani hii ianze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna yale maeneo ambayo wamiliki wa awali wanatakiwa kulipwa thamani ya maeneo yao kwa sababu uthamini umeshakamilika sasa Bodi ya Korosho iwalipe kwa wakati ili shughuli ya ujenzi ianze. Taarifa ya Tume inasema mradi huu haukushirikisha taasisi nyingine kama vile Kituo cha Uwekezaji kwa hiyo, ni muda muafaka sasa kituo hicho kushirikiana na Bodi ya Korosho ili kuhakikisha kwamba wazo la Serikali la kuongeza thamani kwa kutumia Kituo cha Uwekezaji Maranje sasa kinapata wawekezaji ambao tayari Serikali imetuambia kuna wawekezaji wameonesha nia ya kuwekeza pale, basi Kituo cha Uwekezaji kishirikiane na bodi ili kuhakikisha wawekezaji hao wanapata ile nafuu ambayo inastahili kuwawezesha kuanza kuwekeza katika kituo hicho cha ubanguaji wa korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo limezungumziwa katika ripoti ile ni suala la upatikanaji wa pembejeo, naipongeza Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia, kwa miaka mitatu sasa hivi inatoa pembejeo za korosho bure kwa wakulima na hapa kwenye taarifa yako Mheshimiwa Waziri umesema na mwaka huu mnaendelea. Hongera sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, unachokifanya kwenye korosho kinaonekana, kwa hiyo, naomba Wizara iimarishe usajili wa wakulima kwa sababu ili zoezi hili lifanyike kwa urahisi, basi wakulima ni lazima wasajiliwe na wapate pembejeo inavyostahili na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga, atafuatia Mheshimiwa Cecil David Mwambe na Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka ajiandae.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hotuba ya Wizara ya Kilimo, hotuba inayoonesha matumaini makubwa kwa Watanzania na kubwa zaidi nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuiamini Wizara ya Kilimo na kutenga fedha kiasi cha shilingi trilioni 1.2, siyo jambo dogo. Ninaimani kabisa inaenda kupunguza makali kwa wakulima wa korosho, tumbaku, pamba na mazao mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kusema kwamba Mheshimiwa Waziri pamoja na msaidizi wake na timu yake mmeaminika kwa sababu ni vijana mlio na maono, ndiyo matarajio mliyonayo mkidhamiria kuja kubadilisha mfumo mzima wa kilimo, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hizi pongezi nasema kwamba Mheshimiwa Waziri katika hotuba yako kuna mambo mengi ya msingi umeyaeleza na mimi nitazungumzia suala ulilozungumza la *exchange rate* kuhusiana na korosho, tumbaku na pamba, lakini wewe umezungumzia kwenye tumbaku peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba Mheshimiwa Waziri na timu ya wataalamu wake, muangalie vizuri zaidi bila kuathiri mifumo ya kitaasisi ya kifedha kuona namna ipi ni bora tutakapoingia kwenye misimu hii ya mazao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo kubwa msimu wowote wa kupata fedha za kigeni unapoanza dola huporomoka bei, maana yake ni kama ilikuwa ni shilingi 2,600 basi inashuka mpaka shilingi 2,300 na inapoporomoka inaenda kuathiri bei halisi ya mkulima kwa sababu masoko tunayotegemea ni ya nje, kwa hiyo, hapo ni tatizo. Naomba sana Mheshimiwa Waziri pamoja na timu ya watalamu muangalie kwa mapana zaidi, msizungumze tu suala la tumbaku peke yake, bali tuzungumze kwa mapana zaidi kwa maana ya korosho, pamba, kahawa na mazao mengine ambayo yako kwenye *chain* ya mnyororo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya hivyo tutakuwa tumepunguza adha pamoja na yale malalamiko madogo madogo ya bei kwa sababu ndivyo ilivyo. Tulikaririshwa kuwa bei kubwa ndivyo inavyotakiwa kuwepo, lakini kuna mambo ya kitaalamu ambayo yanaendelea hatuwezi kuyapinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa maono mazuri aliyoyaanzisha ya *BBT*. Ni jambo zito na linahitaji uvumilivu wa hali ya juu, lakini nasema jambo lolote linapoanzishwa tulichukue liwe la timu ya nchi nzima kwa sababu ni suala la kiukombozi na ni suala linaloenda kutoa ajira kwa Watanzania, lakini tunapoliacha linabaki kwenye eneo la Wizara ya Kilimo peke yake tunakuwa hatuisadii nchi wala Waziri mwenye dhamana. Tuchukue *chain* nzima, awe Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa, Mtendaji wa Kata, Mwenyekiti wa Kitongoji na viongozi wote wasimamie jambo hili tutafika mahala ambapo tutapata tija na matumaini makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwijage ametoa mfano hapa kwamba tuangalie na maeneo. Ni eneo lipi linalohitaji uzalishaji wa zao fulani kisha tunaelekeza nguvu huko. Mwalimu alipoanzisha nchi hii na ndiyo maana hadi leo huwa tunamkumbuka kwa mazuri aliyoyafanya, aliangalia kila eneo, *zone* ya Ziwa Victoria aliangalia pamba na kahawa, Tabora akaangalia tumbaku, huko Kusini akaangalia mbao na korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila eneo alitumia utaalamu wa utafiti wa hali ya juu ndiyo maana tumefika hapa. Hii *BBT,* tunajua tuna tatizo kubwa la ajira kwa vijana, hawa uliowakusanya Mheshimiwa Bashe najua walikuwa ni wengi na wengine wataondoka, hakuna namna, hata vyuo walipoanza hawakumaliza wote, wengine waliondoka, wale wanaobaki wachache watakuwa ni sehemu ya darasa kwa vijana wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna namna, jambo hili lilianzishwa pale Igunga mwaka 2013 kama sikosei, walianzisha vijana, ni vizuri sana, lakini kwa sababu ya sijui ni mambo ya siasa au ni mambo ambayo yanarudhisha nyuma au sijui ni kwa sababu sasa kiongozi umepewa Wizara unabaki wewe kukalia *V8* na

makochi badala ya kufanya kazi na matokeo yake ndiyo tunashindwa kufika kwenye mafanikio mazuri ya nchi kwa kuwa unaona ukifanya hivi utaharibikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi amezungumza kwenye hotuba yake kuwa ni mwanafunzi wa Mheshimiwa Lowassa, basi toa maamuzi uyasimamie na sisi tutasimamia pale ambapo tunaweza kukuunga mkono na kukusaidia. Tunaamini mambo hayo utayafanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni huu Mradi wa *BBT,* mimi nadhani tuna wakulima wakubwa kwenye maeneo yetu wenye ekari 10, 20, 30 mpaka 50 na kama tuna mpango mzuri, changamoto kubwa ambayo ipo ni maeneo machache na siyo makubwa sana. Mwenyezi Mungu anatupa mvua na mipango mingine ya Serikali inaendelea kama kuchimba mabwawa. Tunapitisha hizi bajeti, lakini hela nazo haziendi, namuomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha naye atoe fedha kwenye kilimo ili tupate fedha za kigeni nyingi na mambo yaende, tusikwame. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nataka kusema nini? Ni kuhusiana na suala la *BBT*. Tuangalie ukienda ukanda wa kule kwa Mheshimiwa Silinde, ukitokea Mkoa wa Songwe unaenda mpaka Rukwa utaona mashamba makubwa yameandikwa mbegu za uzalishaji. Sasa unaanza kujiuliza haya ni ya watu binafsi au ni watu gani? Kumbe hawa wazalishaji wa mbegu wamechukua watu wachache wakawasaidia, wakawapa elimu na matokeo yake tunaendelea kuyapata. Kwa hiyo, ndivyo ilivyo kwa *BBT,* iende katika mfumo huo kwenye mikoa, wilaya na tarafa zetu, tutafika mahali ambapo ni pazuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kukupongeza Mheshimiwa Waziri kwa mipango mizuri, lakini lazima ioane na gharama tunayotumia kuzalisha na kupatikana kwa malighafi tunayoipata, kama ulivyoeleza kwenye mbegu za pamba, mimi naamini kuwa mbegu zilishapitwa na wakati, tufike sehemu tusiwe watu wa kuzungumza, ukiangalia takwimu hapa umesema umegawa *acre-packs* milioni 16.5, umepeleka milioni saba. Ukienda kwenye mbegu ulizogawa

unazungumzia ekari milioni mbili na kitu, ukienda kwenye uzalishaji hata kama ni yule kipofu hajaenda darasani hawezi kukuelewa. Kwa hiyo, hapa ni lazima tuwekeze kwenye utaalamu, tuwekeze kwenye utafiti na taasisi zinazosimamia zichukue mawazo ya wataalamu ili tufike tunakotarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni pacha wangu hapa amezungumza jambo la msingi sana. Mheshimiwa Waziri yamekuja mawazo mapya mazuri ni kwa sababu watu wana imani na wewe. Imani kubwa ya kwanza ni kuthubutu na kusimamia, hilo halina mashaka na jambo la pili ni ile mipango tusiipeleke kwa haraka, tuwe na mipango michache, lakini yenye tija na mafanikio ambayo itaacha alama kubwa ya kutosha na ndivyo itakavyoonekana kwamba vijana mmesimamia Wizara ya Kilimo na kuibadilisha kutoka uzalishaji wa chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumeondokana na malalamiko yasiyokuwa na sababu na kwenda kwenye usimamizi uliohalisi. Nakuomba Mheshimiwa Waziri, kwa yale aliyoyazungumza Mheshimiwa Kiswaga kwamba tuna kata 40 za majaribio na haijawahi kutokea kupata matrekta 200. Sasa kutoa malalamiko kwa wananchi, kutoa malalamiko kwa wakulima, hebu twende na utaratibu mzuri mliouweka katika Wizara yako, mshauriane vizuri ili kusudi huduma hii ifanye vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna vijana 230 wamefanya kazi nzuri na ya matumani makubwa. Naamini tukisimama nao tutavuka kutoka kwenye kilo laki tano na tutakwenda mpaka kilo milioni moja. Mimi naamini katika mikoa 17 na wilaya 56 za uzalishaji wa pamba tutafanya makubwa zaidi, tutapata fedha nyingi za kigeni na tutapunguza malalamiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna namna yoyote ya kukwepa madini, kukwepa kilimo cha pamba au kukwepa kilimo cha kahawa kwa sababu ndiyo sehemu inayotuletea fedha za kigeni. Tukisimama na haya tutakuwa sehemu nzuri na tutakuwa na *stock* ya fedha za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya haya machache naunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, nashukuru. Mheshimiwa Cecil David Mwambe, atafuatia Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka na Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga ajiandae.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia jioni ya leo. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake na watendaji wote walioko kwenye Ofisi ya Wizara ya Kilimo kwa namna ambavyo wanaisimamia hii sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kukupongeza wewe mwenyewe kwa kuchaguliwa kuliongoza Bunge letu. Ninaamini unastahili, ni wakati tu ulikuwa haujafika na sasa wakati wako umefika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hatua zote anazozichukua hasa kwenye kuboresha mambo mbalimbali yanayofanyika, ikiwa ni pamoja na ugawaji wa pembejeo kwa wakulima. Mimi nitajikita zaidi kwenye jambo moja tu la kilimo cha korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ameunda tume hivi karibuni ya kwenda kufanya uchunguzi kuhusiana na mambo mbalimbali yaliyoko kwenye sekta ya korosho. Tayari ameanza kuchukua hatua ikiwa ni pamoja na kuondoa mfumo kandamizi kwa wakulima uliokuwepo zamani wa kuuza korosho kwa kutumia minada kwa njia ya boksi. Hivi sasa amesema korosho zitakwenda kuuzwa kwa kutumia Mfumo wa *TMX* ambao tunaamini utafanya maboresho makubwa ikiwa ni pamoja na kuondoa ukiritimba kwa wanunuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza pia kwa hatua alizochukua kuboresha hizi skimu sambamba na kujenga upya Skimu ya Ndanda, Maparagwe pamoja na Skimu ya Nanganga. Huu utakuwa ni ukombozi mkubwa kwa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hatua zote alizozichukua Mheshimiwa Waziri bado yapo maoni na mambo mengi sana aliyoyapata kutoka kwa tume ambayo tunaamini atakwenda kuyafanyia kazi kwa 100% kama alivyoanza na suala la kuondoa

*box*. Mambo mengine tulikuwa tunashauri kwa uwazi na mengine kwa siri tunapopata nafasi ya kushauriana na Mheshimiwa Waziri, lakini pia tulijadili wakati wa kikao cha wadau wa korosho kilichofanyika hapa Dodoma mwaka jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza kabisa lilikuwa ni suala la kufuta ule mfumo wa ununuaji wa pembejeo kwa pamoja, tukatengeneza shirika fulani au chombo fulani pale kinaitwa *KCJE,* tunaomba uendelee kwa kadiri ilivyo na mapendekezo ya tume uliyoiunda wewe mwenyewe kwamba chombo hiki sasa kiondolewe na jukumu hili la kununua pembejeo pamoja na vifungashio likabidhiwe kwa bodi ili kuongeza uwazi pamoja na kufanya mfuko huo uweze kukaguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kushauri na kupendekeza ni wakati watu wa hiyo tume wametueleza uzalishaji wa korosho unashuka, lakini kwenye utafiti wao wamegundua kwamba kuna viuatilifu vingi vinavyotumika kwenye zao la korosho. Viuatilifu vingine siyo bora na ndiyo vinasababisha maua ama majani ya mikorosho kufa wakati wa uzalishaji. Nakuomba sana, kwa nafasi uliyonayo, kabla hatujaenda kwenye msimu mpya wa kilimo cha korosho ambao sasa hivi wananchi wameanza kutayarisha mashamba na hivi karibuni wataanza kupulizia dawa, pafanyike tena utafiti au marudio ya kupima ubora wa viuatilifu vyote vinavyotumika kwenye zao la korosho kwa sababu vingine na vimetajwa kabisa na wale watu uliowaagiza kwenye ile tume kwamba siyo viuatilifu bora na vinasababisha kuua korosho na hivyo kupunguza uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la tozo; kwenye zao la korosho kama ilivyo kwa mazao mengine kuna tozo mbalimbali, lakini nitazitaja hapa chache ambazo tunaomba sasa urudie kwenda kufanya tena utafiti upya. Hata hivyo, tume yako imeshauri kuwa tozo nyingine zipunguzwe na nyingine ziondolewe moja kwa moja ili kumwezesha mkulima kwa kuzingatia matumizi ya *TMX* sasa aweze kupata pesa ya kutosha itakayobaki mikononi mwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vyovyote vile wanunuzi wa korosho wanaponunua korosho zao, wanapotaka kuondoka na zile korosho tozo mbalimbali wanazokatwa wao zitakwenda ku-*reflect* kwenye bei wanayompatia mkulima wakati wananunua korosho, kwa hiyo, hawezi kulipa yeye gharama pasipo kupunguza sehemu nyingine, ndiyo maana mkulima anakuwa anabaki na pesa nyingi tu. Tozo mojawapo ambayo sisi kama Wabunge kwa pamoja, lakini pia tunaishauri na Kamati yako ilishauri, wao walisema ipunguzwe tozo ya *TARI,* kwa maana pesa inayokwenda kwenye hivi vyuo vya utafiti pamoja na Naliendele**.**

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulijaribu sisi kufanya utafiti, Tanzania hivi vyuo au *TARI* zipo nyingi siyo Naliendele peke yake. *TARI* zingine za kwenye tumbaku, pamba, karanga huko, mahindi na kwingine kwingi wanapewa pesa ya pamoja siyo kiasi kikubwa kama ambavyo kwetu sisi ipo. Wakulima wa korosho wanakatwa shilingi 25 kwa kilo ili kuchangia *TARI*. Ukienda kwenye tumbaku au sukari wanatoa kama shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya kuchangia maendeleo, kwa ajili ya kuchangia *TARI.* Sisi tunaomba hili jambo lifanyiwe marekebisho na utafiti ufanyijke upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo tozo nyingine ya Bodi ya Korosho na wenyewe wanapata shilingi 25. Kimsingi Mheshimiwa Waziri na wewe unaweza ukawa shuhuda kwamba hata utendaji wa Bodi yetu ya Korosho ambayo tuna taarifa kwamba muda wake unakaribia kuisha. Hii pesa wanayoipata matumizi yake hayapo wazi sana na hatuoni kwa nini mkulima akatwe kwa sababu hii kwanza ni taasisi ya Kiserikali, hata kama mkulima anakatwa lakini basi achangie kwa kiasi fulani tofauti na ilivyo sasa shilingi 25 yote inakwenda na ukiangalia hiyo pesa ni nyingi sana, pamoja na majukumu mengi walionayo bodi, lakini tunaomba kidogo ipunguzwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tozo nyingine ambayo ni shilingi mbili, inatozwa kwenye *task force.* Kuna kitu kinaitwa *task force* kwenye mazao haya ya korosho. Wakulima wanakatwa pale shilingi mbili wanaenda kuchangia kwenye hiyo *task force* ambazo kazi zake kimsingi hazieleweki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo tozo nyingine ya elimu; elimu kwenye *level* ya mkoa wanakata shilingi 30 na kwenye *level* ya wilaya nafikiri wanakata shilingi 20. Hata hivyo kwenye *level* ya vijiji sasa hivi wamezidi kushusha hivi vitu, wanakatwa shilingi 20 tena ya elimu. Makato yanayokatwa kwenye shilingi 20 ya *level* ya kijiji yanaonekana wazi matumizi yake, lakini makato yanayokatwa kwa ajili ya *level* ya mkoa pamoja na *level* ya wilaya kwa kiasi fulani, hai-*reflect* moja kwa moja kwenye *level* ya kijiji na wakulima hawaoni faida yake ya moja kwa moja. Kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri utakapokuja ku-*wind up* basi utusaidie na hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine ambalo linaleta *conflict* kubwa sana. Mwaka juzi Mheshimiwa Waziri Mkuu, miaka mitatu iliyopita nafikiri ama minne alitoa tamko kwamba zao la korosho liondolewe kitu kilikuwa kinaitwa unyaufu. Kimsingi Mheshimiwa Waziri hata ukifanya utafiti, ukienda kuongea hata na watu wa *TBS* wanasema ni kweli na ni wazi kabisa kwamba mazao haya yananyauka yanapokuwa maghalani, linapotoka kwa mkulima kufika kwenye chama cha msingi, mpaka kufika ghala kuu kwa vyovyote vile yananyauka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi mmeanzisha utaratibu wa *insurance*. Ninafahamu kuna *conflict* kubwa kati ya *WRB* ambao wako Wizara ya Kilimo, ukiwaweka wao pamoja na watu wa Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na ninyi watu wa Wizara ya Kilimo. Pesa iliyolipwa na wakulima waliokatwa wanunuzi shilingi saba kwa ajili ya *insurance* mpaka sasa *National Insurance Corporation* hawajaweza kuirudisha ile pesa yote kwa wale wanunuzi wetu wa korosho. Kitu hiki kitakuja kuwa-*cost* tena baadaye kwetu sisi (kitakuja kuwa-*cost* kwa wakulima) kwa sababu hawawezi kuacha wakapata hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimwombe sana Mheshimiwa Waziri aangalie namna ya kufanya, unyaufu wanunuzi wa korosho waliupokea na bado upo, pamoja na lile tamko la Waziri Mkuu. Kama ulivyounda Tume sasa hivi ya kwenda kuangalia matatizo yaliyopo kwenye zao la korosho na kwamba unataka kufanya maboresho. Hebu watume watu wachache wakufanyie utafiti, wakueleze vizuri kuhusu hili suala la unyaufu ili muachane na hizi habari za *insurance* kuachana na madeni haya ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu peke yake unyaufu umekuwa kama 0.73% ukilinganisha na miaka mingine ambapo gharama hizi tofauti na hata pesa iliyolipwa na *insurance,* ambao wale watu wakulima wanunuzi wamekatwa *almost 1.7 billion* lakini *premium* nzima ni kama *2.8 billion. Insurance* hawataki kuwalipa wakulima wanunuzi na mwisho wa siku wanunuzi hili jambo watalihamishia kule na itakuwa hivyo baada yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kumekuwa na ukatishaji wa tamaa kwa wabanguaji wadogo wadogo. Mimi ninaweza nikatoa mfano ambao pia mwaka jana niliutoa. Kuna mbanguaji mdogo wa korosho ana kiwanda yuko pale Mtwara na wewe unamfahamu Mheshimiwa Waziri amekuja kwako mara nyingi anaitwa Mkemi. Huyu ndugu yetu alipata hasara kwa sababu ya Bandari ya Mtwara sasa hivi inasafirisha sana makaa ya mawe, inatumika kama *dirt port.* Vumbi lililotoka kwenye makaa ya mawe likaenda kuingia kwenye korosho. Vumbi lile linaathiri sana hata watu wa Mtwara, lakini huyu ndugu yetu anatakiwa alipwe na Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi nafikiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ni mwaka wa tatu, mwaka wa nne hajawahi kuwa *refunded*, lakini yeye ni mnununzi. Kwa hiyo, kwa vyovyote hasara hii anayoipata atakwenda kuirudisha hasara hii kwa wakulima. Kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri jambo hili mlimalize…

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. CECIL D. MWAMBE**: …kabla msimu wa korosho haujaingia. *(Makofi)*

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mfanyabiashara huyu anayetajwa ambaye amefanya biashara ya korosho ambaye Waziri mwenye dhamana ndiye anawasilisha

bajeti yake hapa, amepata madhara makubwa ikiwemo kuuziwa nyumba zake, mali zake na jambo hili liko wazi sana. Jambo hili lipo wazi kwa sababu makaa ya mawe yanapita bandarini pale, lakini mpaka leo Serikali haijachukua hatua yoyote na huyu mtu anaendelea kuathirika kisaikolojia. Kama utaniruhusu kesho tumlete hapa uangalie na afya yake. Huyu mtu anahitaji *compensation* kubwa ya Serikali…

**MWENYEKITI:** Hitimisha Taarifa Mheshimiwa tafadhali.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, …

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwambe tafadhali karibu.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea Taarifa ya Mheshimiwa Katani kwa sababu na yeye anamfahamu na sisi tunatoka eneo moja namna anavyoathirika mfanyabishara huyu. Jambo hili lipo kwa wafanyabiashara wengi siyo yeye peke yake wamekuwa wanalalamika, kuhusiana na pesa zao za *bond* lakini pia sasa hivi jambo jipya lililoanza hili suala la *insurance*.

Kwa hiyo, kwa kusisitiza kwa sekunde chache nimwombe Mheshimiwa Waziri aondoe hiki chombo cha pamoja kinachonunua pembejeo. Pembejeo zote zinazotumika kwenye korosho sisi kama Wabunge tuna taarifa, zipo ambazo hazifai na ndiyo zilizosababisha kushuka kwa zao la korosho. Wazifanyie tena utafiti kabla hatujaanza msimu mpya wa korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Cecil Mwambe. Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mheshimiwa Yahya Ally Mhata ajiandae.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashukuru kwa nafasi na awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha na kunipa uhai kusimama mbele ya

Bunge lako Tukufu jioni hii ya leo tukichangia kwenye hii bajeti ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mama yetu, Mama Samia Suluhu Hassan. Sisi Wana-Liwale hatuna deni naye kwenye sekta ya kilimo, hatuna deni naye, hatumdai ila yeye ndiyo anatudai na ahadi yetu ni mwaka 2025 tutamlipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye pembejeo za korosho tumefanya vizuri sana, tunapata pembejeo za korosho bure kabisa. Sasa kabla sijaanza kuishauri Serikali naomba nianze na kile ambacho wananchi wa Liwale wamenituma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, baadhi ya wananchi wa Liwale bado wanadai fedha zao zilizotumika kusafirisha pembejeo kutoka RUNALI, Chama cha Mkoa kwenda kwenye Vyama vya Msingi, bado wale wasafirishaji wanadai fedha zao mpaka leo. Kwa mfano, yupo msafirishaji mmoja anaitwa Hamidu Wamu, huyu mmoja peke yake anadai zaidi ya shilingi milioni 122.7 kutoka RUNALI. RUNALI wanasema hizo fedha bado hawajapata kutoka Wizarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, niendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutupatia mahindi ya msaada na hapa naomba ieleweke, mahindi hayo ya msaada tumeyapata kwa sababu mazao yetu mengi yameliwa na wanyama (tembo) ndiyo maana tukahitaji mahindi ya msaada. Sasa yale mahindi ya msaada yamekuja na bei ya shilingi 900 kwa kilo. Mahindi ya wafanyabiashara kutoka Songea wanaleta pale Liwale yanauzwa shilingi 700. Sasa muone kwamba huu ni msaada au ni vinginevyo. Kwa hiyo, yale mahindi yamekuja hayajanunuliwa mpaka leo kwa sababu yanashindana na bei ya soko. Kwa hiyo, tunaomba muendelee kuangalia bei ya soko ikoje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ninaunga mkono pale Mheshimiwa Cecil Mwambe aliposema kwamba kwenye korosho viuatilifu ni vingi mno na vinachangia kushusha uzalishaji, siyo viuatilifu tu, ni viuatilifu sambamba na Maafisa Ugani.

Mimi namshauri Mheshimiwa Waziri naomba kuwe na ubobezi kwenye ugani, kuna watu wabobee mahindi, wengine wabobee mpunga, wengine korosho, lakini unamleta Afisa Ugani, korosho yenyewe ndiyo anakuja kuiona Liwale, sidhani kama anakuwa ni msaada. Kwa hiyo, mimi ushauri wangu hapa tupate maafisa ugani ambao wamebobea kwenye haya mazao na wawe washauri wetu kwenye hivi viuatilifu. Wenzetu hawa wanaofanya utafiti wa viuatilifu, basi watuletee viuatilifu ambavyo wanaona kweli vinaweza kuzalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye ushauri, kwanza niishukuru Serikali kwenye taarifa yao wamesema Sheria ya Vyama vya Ushirika inaletwa kwa ajili ya kufanyia mapitio. Mimi hili jambo mwaka jana nilichangia na nikaomba hilo kwamba Sheria ya Vyama vya Ushirika ifanyiwe mapitio. Hii kwa mfano unaonekana kuna hiki chombo kinaitwa Tume ya Kuendeleza Ushirika na jukumu la kwanza la Tume ya Ushirika wameandika pale wenyewe kwamba ni kuandikisha na kufuta Vyama vya Ushirika na jukumu la pili ni kufanya ukaguzi. Hapa kwenye ukaguzi napo kuna kizungumkuti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu kinaitwa *COASCO,* huyu *COASCO* hapo anaingiaje? Mimi sijaona uhusiano wa *COASCO* na hii Tume ya Ushirika. *COASCO* inafanya ukaguzi. Sasa kama inafanya kazi kwa niaba ya Tume, *findings* zake inazipeleka wapi? Mfano mzuri mwaka juzi walikuja Liwale wakafanya ukaguzi kwenye vyama kadhaa na wakakuta kwenye chama kimoja kina uharibifu mkubwa sana. Zile ripoti, alipokuja Afisa Ushirika (mtu wa Mrajisi Mkoa) alikuja akaisoma mbele ya wanachama, haikujadiliwa akasema hii haina mjadala, inapelekwa TAKUKURU. Leo ni mwaka wa tatu ipo TAKUKURU, hatujui nini kinaendelea. Mali za wanachama zimepotea, hatujui kesi ipo TAKUKURU au ipo wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hawa *COASCO* wajibu wao ni kuishia pale TAKUKURU? Je, TAKUKURU wasipofanya kazi wao wajibu wao ni upi? Huyo huyo Mrajisi wa Mkoa mwaka huu amekuja na ripoti nyingine, akamwambia *DC* achukue hatua. *DC* akasema kabla sijafanyia uchunguzi hii ripoti mpya nataka ripoti ya

mwaka juzi, kwa sababu kuna watu walituhumiwa mpaka leo wapo mtaani, leo mnaleta watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukirejea kwenye jukumu la Tume la Usimamizi na Ukaguzi, hili jukumu la usimamizi bado hawajalifanyia kazi vizuri. Mimi kwangu wao ndiyo wamekuwa chanzo cha migogoro, wanatengeneza mgogoro, halafu wanakuja kama vile wanataka kuja kutatua mgogoro, kumbe lengo lao ni kuingiza watu wao. Mwaka huu wametuvurugia sana uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna chama kimoja cha umoja, wamechukua fomu vizuri na uchaguzi umeenda vizuri, lakini *from nowhere* wakaja wakasema tunafuta uchaguzi kuna malalamiko. Hawajaja kuwaambia malalamiko hayo ameleta nani, ni mwanachama nani amekuja kulalamika? Ndiyo kwanza fomu zimechukuliwa, sasa shida ipo wapi? Wakatengeneza huo mgogoro mpaka leo kile chama hakijafanya uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiingia kwa undani shida yao siyo kwamba kile chama kina mgogoro, mgao wa fedha hawajaletewa, kwa sababu bodi ya kwanza ambayo tuliiondoa waliingiza mkono pale, lakini hii bodi mpya iliyoingia sasa hivi wameshindwa kuingiza mkono, kwa sababu bodi ile ya kwanza kile chama kilikuwa kinaenda kufa. Mkuu wa Wilaya anajua, *GSO* anajua, mpaka Mkuu wa Mkoa anajua. Sasa wanang'ang'ania kuirudisha ile bodi ambayo wao walikuwa wanapata hela. Hii bodi ambayo sasa imesimamia vizuri chama kinakwenda hawaitaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wametangaza uchaguzi unafanyika tarehe 6 Mei (kesho kutwa), lakini Mkuu wa Wilaya, *GSO* hawajui ni watu gani wanaingia kwenye hiki chama. Tunakwenda kuingiza watu wale wale waliotupeleka mbali. Hii dhana ya kusema hao ni wasimamizi wa Vyama vya Ushirika, mimi nasema siyo sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi kwenye *COASCO; COASCO* mmesema wao kazi yao ni kufanya ukaguzi. Sasa kama *COASCO* wanafanya kazi ya ukaguzi na Tume jukumu lao la msingi ni

ukaguzi, kwa hiyo hii *COASCO* inaonekana kama ndiyo chombo cha Tume, *COASCO* ni chombo cha Tume. Sasa swali langu ni *COASCO* tangu wameanza ukaguzi mbona kwenye ripoti hii hawatuambii kesi ni ngapi wamepeleka mahakamani, wangapi wamefungwa, vyama vingapi. Hapa wametoa taarifa kuna chama sijui kimepata hati safi, kuna vyama vingine vinapata hati ya kuridhisha, vingine vina hati mbaya. Sasa hivyo vyenye hati mbaya ni vipi? Hatua gani zimechukuliwa? Wao kwenye ripoti yao wanatuambia nini juu ya hivi vyama ambavyo vimekwenda na ripoti mbaya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikikwambia kwamba hawa jamaa wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika hawako sawasawa ninamaanisha, kwa sababu mimi kwangu kuna vyama zaidi ya viwili au vitatu vimepoteza fedha za wakulima, lakini vile viko peponi kwa sababu tu mikono yao imeingia, kwa sababu Tume inajua hizo fedha zimepoteaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye chama ambacho Tume hawajui pesa zake zimeendaje ndiyo wanakiandama. Mheshimiwa Waziri, tuma watu waende wakakague Vyama vya Ushirika Liwale, vipo vyama vinadaiwa mpaka leo na wakulima lakini hawa *COASCO* hawajavigusa, wala Mrajisi wa Mkoa hajavigusa. Jambo hili haliwezi kuwa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimwombe sana Mheshimiwa Waziri kama alivyosema kwamba kuna hii Sheria ya Marekebisho ya Vyama vya Ushirika inakuja, mimi naomba ije. Hapa kwenye ripoti amesema ipo kwenye ngazi ya Mawaziri. Tunaomba ikiwezekana kwenye Bunge lijalo hii sheria ije tuifanyie maboresho. Kama *COASCO* tunawaamini kwamba kweli ni wakaguzi basi wapewe meno, haiwezekani kesi zao zikaishia TAKUKURU halafu zinaishia hivyo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi alikuja Mrajisi wa Mkoa tukamhoji, tukamwambia bwana zile *findings* ulizofanya mwaka juzi ziko wapi? Akasema zipo TAKUKURU, kwa hiyo, ndiyo zimeisha. Kwa hiyo, TAKUKURU ni hiyari yao wapeleke au wasipeleke na wasipopeleka nani anahoji, Tume au *COASCO*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na hayo tu na ninaomba Sheria ya Ushirika ije mapema tuifanyie maboresho na iendane na *slogan* ya mama. Mama anataka kuinua wakulima, kuinua wakulima ni pamoja na kuinua Vyama vya Ushirika. Vyama vya Ushirika vinakuwa ni mkombozi wa wakulima, kwa sababu ni wakulima wenyewe wamekaa mahali, wameungana, wanataka kufanya mambo yao ili yaende. Sasa wakitokea watu hawa wanaotaka mgao, wanatuharibia na siyo kwamba wanatuharibia tu, wanaharibu na kura za mama za mwaka 2025. Mimi nimeshawaambia kwamba mama sisi hatumdai, ila yeye anatudai sisi na mwaka 2025 tunakwenda kumlipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na uchangiaji, niwatangaze wageni ambao tunao hapa Bungeni.

Kwanza, tunao wageni wa Wahehsimiwa Wabunge, wapo wageni 18 wa Mheshimiwa Constantine Kanyasu ambao ni Viongozi wa Madhehebu mbalimbali ya Kikristo kutoka Wilaya ya Geita na Viongozi wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Wilaya ya Geita, Mkoa wa Geita. Kama wapo wasimame, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; ni wanafunzi 70 na watumishi wawili kutoka Chuo cha Uhasibu Dar es Salaam. Wasimame kama wapo, ahsante sana na karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na uchangiaji, Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga atafuatiwa na Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, ajiandae.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Kilimo. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa maono yake

makubwa sana juu ya sekta hii ya kilimo, kwa kuwatambua wakulima wa Tanzania na kuongeza bajeti hadi kufikia shilingi trilioni 1.2. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na timu yake yote, kwa maandalizi mazuri ya bajeti. Kimsingi bajeti yenu ina mvuto, kwa hiyo naomba mwende muisimamie vizuri, ili iweze kuleta matokeo yale ambayo tunayakusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nipende kumfikishia ujumbe Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe kutoka kwa wananchi wa Ludewa kwamba wao zaidi ya 90% ni wakulima. Wanaomba sana Waziri wao wa Kilimo wamuone, wamekuandalia mashamba ya chai. Kuna *block farms* pale Madope ziko 18, Kata ya Madope, wanatamani sana ufike. Kuna mashamba ya Kawawa Ligumbilo wana changamoto ya zile *CPU machine* ya kukobolea kahawa, wanatamani sana na wako tayari kama utabanwa sana basi Naibu wako watampokea aweze kuwatembelea, hawajapata bahati ya kumwona Waziri wa Kilimo muda mrefu kidogo, ulipanga kuja bahati mbaya uliishia Njombe. Kwa hiyo, wamesisitiza sana wanakuomba sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba uniruhusu nitoe pole nyingi sana kwa wazazi, walimu na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Manda kwa kuunguliwa na bweni wiki hii, wanafunzi zaidi ya 240 sasa hawana makazi. Kwa hiyo, ninatoa pole sana kwa wananchi wale na nina imani Serikali ipo na inashughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo naomba sasa niendelee kutoa mchango wangu. Kama ambavyo Wabunge wengine wameeleza na taarifa ya Mheshimiwa Waziri kwamba 75% ya Watanzania ni wakulima na wako vijijini na hiyo ndiyo ajira yao na kilimo kinachangia siyo chini ya 26% kwenye Pato la Taifa. Kwa hiyo, ni sekta nyeti na nimesoma bajeti ya Mheshimiwa Waziri, kwa kweli inajitahidi kutoa majawabu kwenye maeneo muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na baadhi ya mazao, kwa mfano zao la kahawa, kule kwangu Ludewa kuna wakulima wapatao 1,094 ambao kwa mwaka jana waliweza kuvuna tani 150

za kahawa, nimeona taarifa yako Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 28 umezungumzia vizuri eneo hilo. Kwa hiyo, ninaomba sana zao hili la kahawa linawapa wananchi wa eneo la Kimata kipato kizuri sana, wananchi wa eneo la Liunji, Ligumbilo, Mawengi, Lusala, wanapata fedha nyingi za kuweza kusomesha watoto wao kupitia zao hili la kahawa. Kwa hiyo, naomba sana maeneo haya kwenye mipango hii wananchi wale wa Kimata na maeneo mengine waweze kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nikija kwenye zao la chai, kule kwetu kuna hekta 16,300 zikiwemo hizo *block farms* 18 ambazo tayari Wizara imeweza kuzipima na kuandaa hati miliki kwa wananchi wale ambao wameunganisha mashamba yao na wameweza kuwasaidia sana hasa kupitia taasisi inaitwa *NOSCI*, wamekuwa wakitoa sana miche bora na kuwasaidia wale wananchi kupata masoko.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ninaomba eneo hili tuendelee kuwasaidia wananchi hasa eneo la kuwagawia miche kwani miche ni changamoto kule ili waweze kupata mavuno mengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika Wizara hii ni Wizara nyeti sana na kuna uhusianao wa karibu sana kati ya miundombinu ya barabara na kupata mafanikio kwenye sekta ya kilimo cha zao la chai. Kwa hiyo, naomba sana sekta mtambuka hasa watu wa *TARURA*, waweze kusaidia sana kuangalia barabara zinazoenda kwenye maeneo haya na kuyatengea fedha za kutosha na kuweza kukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika, kidogo naomba hamasa iweze kutolewa kwa vijana kwenye zao la chai, kwa sababu zao hili linaonekana kama zao la watu wenye umri mkubwa (wazee), kwa vijana kidogo hawana mvuto sana na zao la chai. Kwa hiyo, Wizara iendelee kutoa hamasa kwa vijana kwenye zao hili la chai ili waweze kuzalisha kwa wingi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona pia kwenye huu ukurasa wa 152 umezungumzia mpango wa Wizara katika kuandaa mabwawa kwa ajili ya umwagiliaji wa mazao haya, naomba hili liweze kufanyika na kutengewa fedha za kutosha ili kilimo kikiwa

rahisi zaidi hata vijana wanaweza wakavutiwa kuingia kwenye zao hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni zao la korosho. Ludewa kuna hekari 5,789 ambazo zimelimwa zao la korosho ila bahati mbaya sana mikorosho ile ilipandwa miaka mingi iliyopita, mingine kabla ya uhuru. Kwa hiyo, changamoto kama soko la korosho kuwa mbali imechangia sana kuwavunja moyo wakulima wa zao hili, kwa sababu kule tuko kandokando ya Ziwa Nyasa, Tarafa yote ya Masasi zao hili la korosho linakubali, lakini inapofika kwenye soko wakulima wale wanalazimika kwenda Ruvuma, wakati mwingine kwenda Lindi na hivi viuatilifu, ile *sulphur* huwa inachelewa sana, unaweza kukuta wao wanatakiwa waitumie mwezi wa tano inakuja inapatikana kwa kuchelewa kidogo.

Kwa hiyo, ninaomba Serikali iweze kuweka mkazo kwenye viuatilifu kwa sababu kule kuna wakulima wengi na ardhi ambayo inakubali ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliona watu wa Magereza nao wanataka waanze kulima korosho, halmashauri nao walitaka wachukue eneo kubwa. Kwa hiyo, naomba yale ambayo umeyasema ya kuongeza uzalishaji wa miche, pia kule yaweze kufikiria kwa sababu bahati mbaya sana Ludewa ina hali ya hewa yote, chai inalimwa, kahawa inalimwa lakini kando ya Ziwa Nyasa korosho inastawi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Tarafa ya Mwambao wameomba sana waweze kupewa mbegu ya kisasa ya muhogo. Tuliwahi kuchukua mbegu kidogo Butiama, Ofisi ya Mbunge iligharamia. Tuliwagawia ile mbegu inastawi ndani ya miezi tisa tofauti na mbegu yao ya asili ambayo inatumia miaka miwili na nusu mpaka mitatu, kwa sababu kile ni chakula muhimu na ndicho ambacho wanakitegemea kule. Ninaomba hilo liangaliwe sana kwa wananchi wa Kilondo, Lumbila, Makonde, Lupingu na maeneo mengine kama Iwela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niende pia kwenye zao la ngano. Awali ya yote namshukuru sana Mheshimiwa

Rais, kupitia Waziri wa Kilimo kwa kugawa mbegu ya ngano tani 20. Mbegu hii imeweza kuwasaidia wananchi kupanda hekta 1,514 kwenye kata kumi za Ludewa na wanatarajia kupata mavuno ya tani 4,465. Kwa hiyo, wananchi wale wamenituma niishukuru sana Serikali kwa kuwagawia mbegu bora na mbegu ile imeota vizuri, imestawi na mavuno yatakuwa mazuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika nikienda kwenye eneo la umwagiliaji...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa, tuna changamoto ya muda, tafadhali hitimisha.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa muda, lakini vilevile lile eneo la umwagiliaji Bonde la Luhuhu, Masimavalafu na mengine nimeyaona humu, eneo lile la Luhuhu lina mafuriko ya mara kwa mara, hivyo, mradi huu sasa utakwenda kutatua changamoto hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, atafuatia Mheshimiwa Khadija Hassan Abood, Mheshimiwa Venant Daud Protas ajiandae.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nichukue nafasi hii jioni ya leo kwanza kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ameniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako hili Tukufu kutoa mchango wangu katika bajeti hii ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo ada, nami ninamshukuru sana Rais wetu, mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi

kubwa anayoifanya ya kuhakikisha kwamba wananchi wa nchi hii wanastawi kimaendeleo na kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba niwashukuru viongozi wa Wizara wakiongozwa na ndugu yangu Mheshimiwa Bashe na Katibu Mkuu kwa kazi kubwa anayofanya katika kuhakikisha kwamba kilimo chetu kinasonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa shukrani zangu za pekee kwa Waziri wa Kilimo, Waziri wa Kilimo amekuwa msikivu sana. Sisi watu wa Kusini, watu ambao uchumi wetu unategemea zao la korosho, kwa takribani miaka mitatu tulikuwa tunatoa malalamiko jinsi gani zao hili la korosho lisivyomsaidia mwananchi wa Kusini. Ndugu yangu Mheshimiwa Bashe mwaka huu amekuwa msikivu na kuunda tume ambayo imekuja na majawabu ya yale ambayo tulikuwa tunayaeleza. Kwa hiyo, ndugu yangu Mheshimiwa Bashe mimi kwa hili, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu tunakuunga mkono na tunakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya changamoto ambayo inalikabili zao la korosho ni bei. Bei ya korosho imekuwa siyo rafiki kwa wakulima. Bei ya korosho hailipi gharama za mkulima, lakini tume imekuja na majawabu ambayo nina hakika kabisa kwa usikivu wa Waziri ndipo hapa tutakapohakikisha kwamba mkulima wetu wa korosho anajiondoa katika umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tume imekuja na mapendekezo kwamba badala ya utaratibu wa kulaza boksi kama vile Mheshimiwa alivyosema kwamba sasa hivi twende na *TMX,* ni mauzo ya kimtandao kwamba sasa hivi mtu yeyote aliyepo duniani anapotaka kununua korosho, pale alipo anaweza akafanya *transaction* huko alipo na akanunua korosho zetu za Tanzania tofauti na utaratibu wa awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kushangaza sana, jambo la kushangaza kweli kweli. Bodi ya Korosho au utaratibu wa ununuzi wa korosho unazungumza bayana kwamba stakabadhi ghalani zitatumia mnada katika kuuza korosho zake, lakini Bodi ya Korosho badala ya kutumia mnada walikuwa wanatumia *tender*,

walikuwa wanatumia zabuni. Sasa zabuni na mnada ni vitu viwili tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zabuni unaangalia bei ndogo ndiye unayempa, mnada watu wanashindana, mwenye bei kubwa ndiye anapewa ule mzigo. Kwa hiyo, utaratibu ambao tume yako Mheshimiwa Bashe umekuja nao kwamba sasa *TMX* ije kama mbadala wa lile sanduku, naomba utaratibu huu uanze kwenye zao la ufuta, karanga, mbaazi na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nini maana yake, tume imekuja na mapendekezo Mheshimiwa Bashe kwamba lazima tuwe na bei elekezi. Bei elekezi ndiyo bei ambayo itam-*guide* yule anayeingia kwenye mnada aanzie pale. Bei elekezi haitoki hewani, utaangalia gharama halisi za uzalishaji, utaangalia *profit margin* kwamba mkulima anataka apate kiasi gani, utaangalia *future investment* zake na utaangalia *risk* mbalimbali ambazo mkulima huyu ameziepuka katika uwekezaji wake wa zao la korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunategemea kabisa siku ya mnada basi Bodi ya Korosho au yule ambaye atapewa majukumu ya kuangalia bei elekezi, ataangalia vigezo vyote hivi vinne ambavyo mtu atakayekuja pale atahakikisha kwamba anakuja kununua korosho zenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa zamani ulikuwa unachekesha, unashangaa bodi inapokea maombi 70 ya wanunuzi wa korosho, wanaotokea kwenye mnada hawafiki kumi, hawa wengine wote walikuwa *cautioning,* jambo hili kwa kweli lilikuwa linaumiza sana wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaamini kabisa kwa utaratibu huu na ninaomba niwahakikishie wananchi wangu wa Jimbo la Nanyumbu, kwa utaratibu huu tumeshapata mwarobaini wa bei nzuri ya korosho ambao watu wa Mangaka, watu wa Likokona, watu wa Michiga na sehemu mbalimbali za Jimbo letu tulikuwa tunalalamika kwamba korosho zetu za Nanyumbu zinakuwa na bei ndogo ukilinganisha na maeneo mengine wakati ni wilaya moja na mkoa mmoja. Kwa hiyo, Mheshimiwa Bashe hili mimi ninakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, tume imekuja na mapendekezo mbalimbali, tume yako Mheshimiwa Bashe ni tume imara sana, wamekuja na mapendekezo ya kupunguza tozo ambazo kwa kweli zilikuwa zinamnyonya mkulima. Mkulima alikuwa anakatwa zaidi ya shilingi 120 tozo mbalimbali, tozo ambazo ukiziangalia hazina mantiki, kwa mfano, kule kwenye mkoa mkulima alikuwa anakatwa shilingi 30 ya elimu na shilingi 20 ya afya. Ukija ngazi ya wilaya mkulima alikuwa anakatwa shilingi 20 za elimu, ukija ngazi ya kijiji mkulima anakatwa shilingi 20 tena, sasa unaanza kujiuliza makato yote haya ya mtu mmoja yana kazi gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tume imependekeza kwamba yale makato ya ngazi ya mkoa yaondolewe na mimi naunga mkono mia kwa mia, hakuna sababu, kwanza hata matumizi yake sisi kama Waheshimiwa Wabunge hatuyajui. Kwa hiyo, afadhali tumpunguzie mkulima hizi shilingi 50 ambazo zilikuwa zinaenda mkoani sasa ziende kwa mkulima na mkulima atapata bei nzuri ya mazao yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine Mheshimiwa Bashe, tume imekuja na mapendekezo kwamba shilingi 25 ambayo walikuwa wanapeleka kwenye *TARI* - Naliendele, sote tunakubali Naliendele inafanya kazi kubwa sana ya utafiti, lakini kiwango cha pesa ambacho mkulima alikuwa anachangia ni kikubwa. Shilingi 25 kwa kilo kwa mkoa ambao unazalisha tani 300,000, maana yake ni shilingi 7,500,000,000. Mkulima anachangia shilingi 7,500,000,000, ni hela nyingi sana. Hakuna zao ambalo linachangia kwenye utafiti kuliko korosho, kwa nini tusitoe *lumpsum?* Kwa hiyo, nafikiri tume imependekeza na sisi Wabunge tunaona kwa kweli wakati umefika *at least* tuamue kwamba zao la korosho litachangia shilingi bilioni 2.5, hizi zingine ziende kwa wakulima zikaongeze bei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika kwenye Bodi ya Korosho, shilingi 25 kwa kilo, Bodi ya Korosho haina sababu ya kupewa hizi fedha. Bodi ya Korosho ni taasisi ya umma, bajeti yake inapita hapa, tunaipitisha kwa shughuli mbalimbali na zinakuwa *audited*, hizi fedha ziondolewe kwenye Bodi ya Korosho apelekewe mkulima ili mkulima apate bei nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tume pia ilikuja na mapendekezo ambayo hata mimi nakubaliana nayo. Ile taasisi iliyoundwa pale ndani ya bodi, *KCJE* kwa kushughulika na manunuzi ya *sulphur* na gunia, ile iko pale kwa kweli ni kinyume na utaratibu. Kwanza taasisi ile haina wataalamu wa ununuzi, haina wataalamu wa kufanya shughuli hizi, badala yake tume imependekeza kwamba shughuli hii iende ikasimamiwe na *Tanzania Fertilizer Company* ambayo ni Wakala wa Ununuzi wa Pembejeo, bora ikafanye shughuli ile ambayo wao ni wataalamu zaidi wa shughuli hii kuliko hawa jamaa.

Kwa hiyo, hawa jamaa ambao mmewaleta hapa waondoke wakafanye shughuli zingine na hivi itapunguza mlolongo mkubwa sana wa fedha za Serikali kutumika visivyo sahihi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemaliza dakika kumi?

**MWENYEKITI:** Ni kengele ya pili hiyo tafadhali.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tutumie kengele ya kwanza kujielekeza kuhitimisha kwa sababu hatutakuwa na hata sekunde moja ya nyongeza ili tuweze kuendana na muda ambao tumebakiwa nao.

Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, Mheshimiwa Venant Daud Protas ajiandae na Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nasafi. Kwanza kabisa nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Naibu wake, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu na watumishi na watendaji wote wa

Wizara hii. Pia naipongeza Serikali kwa kutuletea bajeti nzuri iliyojitosheleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuongeza bajeti kwenye sekta hii ya kilimo, sekta ambayo itainua uchumi wa nchi pamoja na kutengeneza ajira kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka nijielekeze kwenye umwagiliaji. Serikali ina mpango wa kununua mitambo 30 ya kuchimba visima pamoja na mitambo mitatu ya kuchimba mabwawa, ninaendelea kuishauri na kuiomba Serikali bajeti hii itoke kwa wakati, pia kuna haja ya kuongeza zaidi kwenye eneo hili la umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayaona mabadiliko ya tabianchi na mambo mengine yanajitokeza hapa duniani, mafuriko, ukame na vitu vingine, ni lazima sasa kilimo chetu tujielekeze kwenye sekta hii ya umwagiliaji kwa kujenga mabwawa ya kutosha yatakayohifadhi maji ya kuchimba, lakini maji mengine haya ambayo hayataleta mafuriko katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri mabwawa hayo yatakapojengwa yajengwe na mabwawa mengine ya *reserve* kwa ajili ya kuhifadhi maji, mengine yawe tu maji tunayatumia lakini mengine tunahifadhi maji, kwa hiyo, kuwe na *reserve* ya mabwawa ya aina mbili. Tukitengeneza mabwawa hayo ya aina mbili tutakwenda kuendelea na kilimo na kazi za uzalishaji kwa kipindi kirefu, kama hayatatokea majanga mengine ya ukame na maafa mengine badala ya kuyaachia haya maji yakatuharibia badala ya kututengenezea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ujenzi wa mabwawa, ninaendelea kuishauri Serikali kuongeza wataalamu wa kuendesha miradi ya umwagiliaji, kwa sababu tunapokuwa na mabwawa na maji, lakini hatuna wataalamu, kazi yetu itakuwa haijafikia tunapohitajika, lazima tuwe na wataalamu wa kutosha, sasa hivi tuna changamoto ya wataalamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali tuendelee kuongeza fedha kwenye utafiti, utafiti wa mambo yote, kwenye mbegu, viuatilifu, mbolea na kwenye mambo mengine ya udongo na vitu vingine, hapo kilimo chetu kitakuwa kimetimia kwa sababu tumejipanga vizuri kwenye sekta zote zinazohusiana na mambo ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upotevu wa mazao na masoko; kilimo chetu na mazao yetu tunayolima lazima sasa tufanye pia na utafiti wa kujua soko linahitaji nini, ni mazao gani wananchi walime kwa maana ya mazao ya biashara. Tukiachilia mbali yale mazao yetu ya chakula ambayo yatatufaa sisi wenyewe ndani ya nchi, lakini kwenye mazao ya biashara lazima kuwe na utafiti wa kutosha, soko linahitaji nini badala ya kulima tu baadaye mazao yetu yakapotea au tukapeleka nchi za nje baadaye tukaambiwa yana kemikali hii, yana kemikali hii hayafai. Hiyo ni hasara kwa mkulima na kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upotevu wa mazao, tuwe na mbadala. Mazao yale yanayobaki namna ya kuyahifadhi, elimu ya namna ya kuyahifadhi na vifaa vya kuhifadhia ikiwemo kusindika, mfano parachichi. Parachichi ikiwa haijauzika imebaki kuna namna ya kutengeneza mafuta ambayo mafuta hayo bei yake yanakaribiana na mafuta ya *olive oil*. Kwa hiyo, hapa tutakuwa tumenusuru upotevu wa mazao kama yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie na mazao mengine vipi tutaweza kuyasindika ili yafae kwa matumizi mengine. Kuna baadhi ya mazao baada ya kuyasindika pia tunaweza tukapata mbolea kupitia mazao hayo badala ya kuyatupa tukatengeneza mbolea. Hapo nilikuwa naishauri Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu, nataka nijikite sasa kwenye mbegu za asili. Kilimo hifadhi kinasaidia sana kuhifadhi ardhi yetu, lakini tunapata mazao yaliyo bora. Kilimo hiki kinasaidia kuweka mazingira yetu ya kilimo kwenye ikolojia tunayoihitaji bila kupoteza hali ya uoto wa asili. Watafiti wetu wadogo wadogo na watafiti wetu wakubwa ndani ya nchi wamejaribu kufanya tafiti mbalimbali kuhusiana na mbegu hizi za

asili ambazo nyingi katika hizo zina virutubisho vya kutosha bila ya kuongezewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri zile mbegu zilizofanyiwa utafiti zipewe ithibati na *TOSCI* ili mbegu hizi zisambae kwa wakulima wadogo wadogo tuweze kupata mazao yaliyo bora. Madaktari wetu wanajitahidi sana kutupangia namna ya afya bora, lakini tunachokula kitu gani? Tunajipangia mlo lakini je, yale mazao yapoje? Kwa sababu kumekuwa na maradhi mengi sasa hivi ambayo yanasababishwa na vyakula ambavyo tayari vina kemikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tayari kuna watafiti wetu wamechukua mbegu zetu tayari wameshazifanyia utafiti. Hizi mbegu zinatakiwa Serikali iongeze nguvu pale zipewe ithibati, wananchi tuuziwe na nyingine zizalishwe kwa wingi. Mtu mwenyewe ataamua chakula gani cha kula, atakula hiki cha mbegu za asili au atakula hiki chakula ambacho cha mbegu za biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara yetu ya mazao ya kuzalisha kwa wingi iendelee na iendelee kwa sababu tunapata na tutalima kwa wingi, lakini hizi mbegu zetu za asili tuzihifadhi na tuendelee kuzitumia kwa sababu nyingine zinajitosheleza zenyewe bila kuongezewa virutubisho ikiwemo na viuatilifu vya asili, Maafisa Ugani wamekuwa wachache na elimu ya ugani ni ndogo. Mwananchi analima, anatumia viuatilifu, lakini baadaye badala ya kutengeneza anaharibu, anajaza dawa matokeo yake vyakula vinaleta athari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hawa Maafisa Ugani wanahitajika ili kutoa elimu kwa mkulima mkubwa na mkulima mdogo. Mkulima ana eka zake mbili, lakini baadaye analima hapati faida kwa sababu mazao ameyaharibu, ametia dawa nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali, hili nilikuwa nalisemea kila bajeti ya Wizara ya Kilimo kuhusu viwanda vya mbolea. Naipongeza sana Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Morocco kuanzisha hicho kiwanda kikubwa cha mbolea. Pia

nashauri tuendelee na kutengeneza au kuanzisha viwanda vingine hata vidogo vidogo vya mbolea za asili ambazo tutatumia malighafi ya ndani ya nchi bila ya kutumia dawa na kemikali ili tuitumie hata kama mtu mwenye bustani yake ya eka mbili au eka tatu tuweze kutumia hizi mbolea zetu za asili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo hifadhi nakipigia debe kwa sababu ya kuhifadhi udongo na kuhifadhi kupata mazao yaliyo bora yasiyoathiriwa na kemikali yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea, mazao ambayo Tanzania tupo juu katika kuyauza ambayo tunafika nafasi ya kwanza au ya pili, Serikali tuwekeze, tusije tukashuka tukawa wa tano na wa sita. Tuwekeze pale pale tuendelee kukamata hili soko la dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tusisahau kuongeza uzalishaji wa zao la pareto. Zao la pareto linahitajika duniani na lina soko...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hitimisha muda umepita.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia napongeza taasisi zote zisizo za Kiserikali zinazoshirikiana na Wizara katika kunyanyua sekta ya kilimo na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante, ahsante sana. Mheshimiwa Venant Daud Protas atafuatiwa na Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mheshimiwa Tunza Issa Malapo ajiandae.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi kuwa mmoja wa wachangiaji katika bajeti yetu ya mwaka 2024/2025 ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuona kilimo ni uti wa mgongo kwa kuwasikia wakulima wa Tanzania na kuongeza bajeti kila mwaka. Mwaka jana tulipitisha hapa bajeti ya shilingi bilioni 900 lakini mwaka huu

tumepitisha bajeti ya shilingi trilioni 1.2. Hiyo ni hatua kubwa ambayo Mheshimiwa Rais anakwenda kuwakomboa wakulima katika maeneo yetu mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuendelea kupigania sekta ya kilimo kutoka moyoni kwa sababu yeye mwenyewe ametoka mazingira ya wakulima na wafugaji, kwa hiyo, anajua kitu gani wakulima wanahitaji. Kwa hiyo, bado wakulima wana imani naye na Mheshimiwa Rais bado ana imani naye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninahoja chache sana na hoja ya kwanza Mheshimiwa Waziri narudi tena kwenye Bunge hili; mwaka jana nilikwambia Mkoa wa Tabora tulitenga eneo ambalo wewe katika ndoto zako unahitaji eneo utengeneze mashamba makubwa *(block farm),* lakini sisi Jimbo la Igalula tulitengeneza *block farm* na wewe unaifahamu, ulikuja kuitembelea ukiwa Naibu Waziri. Sasa umepata Uwaziri nadhani umeisahau *block farm* yangu ya Kalangasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikuombe mwaka huu nakukumbusha ya mwisho tunaenda kwenye uchaguzi, nataka unapokuja kuhitimisha unipe majibu sahihi ile *block farm* ya Kalangasi inakwenda kufanya kazi au umeifuta? Kama umeifuta twende ukawajibu wananchi kuwa *block farm* hakuna ili tumalize mzozo kwa sababu tumekuwa na siasa nyingi, hatuelewi wapi na wapi; na tunaenda wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, tunamshukuru Mheshimiwa Rais ameweka ruzuku kwenye mbolea, ametusaidia sana kwa sababu wakulima wasingeweza kumudu kununua mbolea kwa bei iliyokuwepo, lakini bado kuna changamoto katika upatikanaji wa mbolea. Mwaka jana hapa Mheshimiwa Waziri ulisema utajitahidi mbolea zifike kwa wakulima maana kwamba wakulima waliopo kwenye vijiji na kata zao, lakini saa hizi mbolea zinafika kwenye maeneo ya miji yaani Tabora Mjini, lakini mwananchi wa Loya, Igalula, Kigwa, Goweko anakwenda kuifuata mbolea zaidi ya kilometa 100 sasa unakuwa badala ya kumsaidia unamwongezea gharama na adha ambayo anaipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kwenye majibu ambapo unapokuja hapa, wananchi wangu wa Igalula, Kigwa, Loya, Miswaki mbolea wataifuata Tabora Mjini tena mwaka huu au utawapelekea kule? Naomba majibu haya unapokuja kujibu haya, utakapokuja kuhitimisha bajeti yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, tunafahamu mlituhimiza sisi wawakilishi wa wananchi twende tukawahimize wananchi wetu kulima kilimo cha kisasa. Tukaenda kuwapa elimu juu ya kulima kwa kutumia mbegu zilizo bora. Mimi niipongeze *ASA* wamekuwa watu muhimu sana kwenye suala hili na nimpongeze Mkurugenzi Mkuu ambaye ni Ndugu Sophia amekuwa anatupa ushirikiano sana na mbegu zake zimekuwa ni bora. Tumekuwa na changamoto *ASA* wanauza mbegu kwa bei nafuu sana, lakini mbegu zake zinawahi kuisha. Wanaingia madalali na wafanyabiashara wanakwenda kumuuzia mkulima mbegu mpaka shilingi 20,000 kwa kilo mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huyu mwananchi ambaye tulimwambia alime kwa kutumia mbegu za kisasa, unakwenda kumwongezea mbegu mpaka kwa shilingi 20,000. Naomba sasa kama tumeshindwa sisi wenyewe kuzalisha, kwenye bajeti hii tunaomba muiongezee fedha Taasisi ya *ASA* iweze kuzalisha mbegu nyingi za bei nafuu ili ziweze kwenda kuwasaidia wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne, Mheshimiwa Waziri mwaka jana hapa tulipitisha shilingi bilioni 900 lakini lazima sasa twende kwenye usimamizi. Tunaweza kupitisha hizi shilingi trilioni 1.2 zikawa hewa kama Mheshimiwa Waziri wa Fedha asipokupa fedha, wewe utakuwa pale umekaa hauwezi kufanya kitu chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kuna mradi wa Bwawa la Goweko tuliupitisha hapa mwaka juzi ambao unagharimu shilingi bilioni sita ambayo wewe mwenyewe tulikwenda tukazindua. Nilikushukuru Bwawa likaanza na tukaweka vifijo, mbwembwe tukazindua pale, lakini nikwambie mpaka leo katika shilingi bilioni sita umenipelekea shilingi milioni 900.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bwawa wamechimba chimba matuta pale, mvua imekuja imesambaza matuta. Sasa umekwenda kuweka fedha ambayo imekwenda kupotea. Kama tunahitaji kweli kusaidia kilimo cha umwagiliaji, tukianzisha jambo tulimalize kwa sababu tunakwenda kujenga miundombinu ambapo siyo rafiki. Kama tunakwenda kujenga mabwawa ya umwagiliaji lazima yakakae kwenye kutega maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapokwenda kujenga nusu kwa kutengeneza matuta halafu baadaye unasubiri fedha, mvua ikija haina *guarantee* kuwa lile tuta litazuia yale maji, inaharibu miundombinu na ile fedha inakuwa imepotea.

Mimi nikuombe Bwawa langu la Goweko ulinipa shilingi bilioni sita, umepeleka shilingi milioni 900 sasa watakwenda kuanza upya. Nikuombe kama tunakwenda kuwasaidia wananchi wangu na wakulima wa Goweko lile bwawa tunahitaji ili liweze kuwasaidia kulima kilimo cha kisasa. Peleka fedha zote ili ziweze kusaidia na kama hamuwezi kupeleka fedha zote, tafuteni mkandarasi mwenye nguvu ambaye anaweza kuacha kusimama pindi Serikali inatafuta fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri mimi nikuombe hizi trilioni, mabilioni kama utakuwa huna fedha itakuwa ndoto hatuwezi kuwasaidia wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine uliniletea wataalamu kufanya skimu za umwagiliaji katika Kata ya Loya maeneo ya Mwamabondo, nataka nijue, mwaka jana uliniambia unanijengea skimu, tunamaliza bajeti, mwaka huu kwenye bajeti hii umefuta kabisa hiyo skimu sijaisikia. Sasa nataka nijue *imehagia* katika mti gani ambayo tuweze kuitungua ili wale wananchi wa Mwamabondo Kata ya Loya ile skimu yao tulienda kuwaambia watajengewa mwaka jana, nikawaambia na bajeti Mheshimiwa Waziri ameshanipa, kumbe ikawa hewa na leo sasa nataka nikwambiaje... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, atafuatiwa na Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma ajiandae.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi jioni hii na mimi nitoe mchango wangu juu ya hoja iliyopo mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutuletea mradi mkubwa wa umwagiliaji ambao unaenda kufanyika katika ukanda wa Mto Ruvuma ambapo kata tano zinaenda kufaidika; Kata ya Mchoteka, Nalasi Magharibi, Nalasi Mashariki, Mchesi, Lukumbule pamoja na Misechela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukrani hizo na naomba tu nimpe taarifa Mheshimiwa Waziri na Mkurugenzi wa Umwagiliaji kuwa wakati tunaenda kufanya upembuzi yakinifu wa eneo lile kwa ajili ya shughuli ya umwagiliaji na tujiandae kufanya upembuzi yakinifu wa namna ya kuzuia tembo kutoka Msumbiji ambao ndiyo njia yao kuu ya kupita katika maeneo hayo na sasa hivi ndiyo wanacheza katika maeneo yale kwa ajili ya kufuata chakula wanacholima Watanzania.

Kwa hiyo, naomba upembuzi yakinifu huu uendane sambamba na namna ambavyo madhara ya tembo yatakavyoweza kuzuiliwa ili shughuli ile iende vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nitapenda sana niishukuru Wizara yetu kupitia Bodi ya Korosho kwa namna ambavyo wameendesha zoezi la kusajili mashamba ya wakulima. Mimi mwenyewe ni mkulima, nimesajili lakini kuna changamoto ambazo naomba wakazifanyie kazi kutokana na zoezi zima hili ambalo linaendelea, limekosa kuwapa fursa wakulima wengi kutokana na mradi wenyewe unavyoendeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza shamba maana yake maeneo yale ni nje ya mji au ni nje ya makazi ya watu kwa maana ya vijiji. Kwa hiyo, malipo yanayotolewa kwa wale makarani wanaopita kufanya zoezi lile kidogo imeleta changamoto na imeleta mwanya wa kusababisha kudai rushwa kwa sababu mashamba mengine yapo zaidi ya kilometa nne, tano mpaka 25. Unampa shilingi 1,500 kwa mteja, analazimika atembee kilometa kumi mpaka 15 bila ya kupewa gharama zozote anaendaje? Kwa hiyo, kwenye jambo hili kidogo limetia doa kwenye mfumo huu kwa sababu wakulima wetu uwezo wao ni mdogo sana wa kuweza kumiliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, naomba Serikali kupitia Bodi ya Korosho itangaze gharama ya kumchukua huyu karani kwenda shambani ni ya mkulima ili kila mtu aelewe kwamba inabidi amuhudumie yule karani anayeenda kupima yale mashamba ili waweze kumlipa. Kitendo hicho kimeleta changamoto kubwa sana na malalamiko kwa wakulima wetu wengi wameshindwa kuwatumia watu kwa sababu nao wanaofanya kazi ile wametumia mwanya kuona kama sehemu ya kudai mapato, lakini ni uhalisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kumpeleka mtu zaidi ya kilometa 15 bila kumpa usafiri na shamba hilo maana yake halitakuwa limehakikiwa. Kwa hiyo, hili zoezi linaweza likachukua muda mrefu kulingana na uwezo wa wakulima wetu. Kwa hiyo, naomba mkafanye marekebisho ili wakulima waweze kupima mashamba yao yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupima basi zoezi la kutoa hati kwenye haya mashamba lifanywe haraka sana ili wakulima hawa wapate uwezo wa kuweza kukopa kwenye vyombo vyetu vya fedha ili kuhudumia hayo mashamba kwa kutumia hati ya hayo mashamba yao ambayo tayari yatakuwa yameshapimwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine niishukuru Serikali, mwaka jana wakati wa bajeti kama hii Mheshimiwa Waziri wa Kilimo alitoa ahadi kwamba mbolea itapelekwa kwenye vituo huko huko walipo wakulima kupitia vyama vyetu vya ushirika, lakini bahati mbaya safari hii kwa Wilaya ya Tunduru hili zoezi limeshindikana, wakulima bado wameendelea kutembea

mwendo mrefu kuja Tunduru Mjini kufuata mbolea kutokana na Vyama vya Ushirika kushindwa kufanya lile zoezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa pamoja na Vyama vya Ushirika kushindwa kufanya, hata mawakala waliokuwepo kulingana na bei ambazo zilitolewa (bei dira) kutokana na maeneo yanayopelekwa pembejeo, kwa mfano, Tunduru Mjini kilo 25 ya *SA* ilikuwa inauzwa shilingi 23,800 na kilo 50 ni shilingi 45,700.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Lukumbula ambako ni kilometa 80 kutoka mjini, kilo 25 ilikuwa inauzwa shilingi 24,000 yaani ni tofauti ya shilingi 200. Kwa kweli hii siyo uhalisia, gharama ya kupeleka kilo 25 ya unga kutoka Tunduru Mjini mpaka Lukumbula ni shilingi 2,000 lakini analazimika yule *agent* kwamba apeleke kwa shilingi 200 kitu ambacho si sawa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya tuliyokuwa nayo ile mbolea inatoka Dar es Salaam kwa kutumia magari makubwa ya tani 30 ambayo hayawezi kwenda moja kwa moja mpaka kwenye kata au makao makuu ya tarafa. Hii ni kwa sababu barabara zetu uwezo wake si zaidi ya kubeba magari yenye tani 15 mpaka 20. Kwa hiyo gari la tani 30 maana yake litashindwa kubeba kupitisha hiyo mizigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya nyingine hata *calculations* walizozifanya hawakuangalia kwamba kuna kushusha na kupakia, kwa hiyo, mbolea ambayo ni gharama inamuendea huyu mfanyabiashara. Kwa hiyo, naomba sana waka-*review* bei dira kwa upande wa Tunduru na maeneo mengine ili mbolea iweze kufika kwenye makao makuu ya kata na wananchi waweze kufaidika na huu mradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine niliomba sana, tuna maghala ya muda mrefu ya Bodi ya Korosho kwenye wilaya yetu yana zaidi ya miaka mitano hayajajengwa. Tunaomba fedha wakajenge ghala lile la Bodi ya Korosho lililopo pale Mjini Tunduru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyama vya msingi vingi vinapima korosho kwenye majumba ya watu. Tuweke mpango wa kujenga maghala kwenye vijiji ili waweze kupima korosho kwenye maghala

ambayo ni ya kisasa kwa sababu inahatarisha. Unapopima kwenye majumba ya watu usalama unakuwa ni mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nitaungana na wenzangu kuhusu suala la *export levy*. Nimefurahi kusikia kwamba kuna utaratibu wa kuendelea kuomba *export levy* ili iweze kurudi kwa 100% kwa mkulima. Jambo la *export levy* lilianzishwa na wananchi wenyewe na wadau wa zao la korosho miaka ya nyuma na tuliwapa *TRA* ili waweze kukusanya kwa urahisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kulikuwa na malengo mahususi ya kuhakikisha kwamba *export levy* inakusanywa na mojawapo ilikuwa inaenda kuendeleza zao la korosho, kuendeleza ubanguaji na kuendeleza miche ya korosho. Vilevile ilikuwa ni kwa ajili ya *research* pamoja na huduma mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba turejee sheria ya nyuma ili iweze kuhakikisha kwamba yale tuliyopangiwa na tuliyokubaliana mwanzo yaendelee kufanyika badala ya kuendelea kuwakandamiza wakulima kwa kuwatoza tozo mbalimbali. Hiyo ya 110 haina faida kwa mkulima, shilingi 25 ya Bodi ya Korosho nayo haina faida kwa mkulima na shilingi 25 ile ya Naliendele inapunguza bei ya mkulima. Kwa hiyo, ninaomba sana Serikali iangalie tozo hizi ziondolewe ili kuongeza bei ya mkulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hilo la *export levy* kwa taarifa ya Mwenyekiti inachajiwa *(charged)* dola 150 kwa tani ambayo siyo chini ya shilingi 416,000 kwa tani moja. Hii yote inatakiwa irudi kwa mkulima ili kuendeleza zao la korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, ambalo ningependa kuzungumza… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa kuzingatia muda. Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, atafuata Mheshimiwa Dkt.

Christine Gabriel Ishengoma, Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi kilimo ni biashara, hilo si jambo ambalo linabishaniwa, lakini biashara yoyote ile ni lazima upate faida. Hakuna mtu ambaye anafanya biashara ili aifurahishe tu nafsi pasipo kupata faida. Nini msingi wa kuyasema hayo? Pamoja na majukumu mengi sana ya Wizara yetu hii ya Kilimo kuna jukumu moja linasema, kuratibu masoko na kuongeza thamani ya mazao ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi mchango wangu mkubwa leo utaegemea hapo, Wizara ina kazi ya kuratibu masoko na kuongeza thamani ya mazao ya kilimo ili sasa ile kauli inayosema kilimo ni biashara kweli mkulima afaidike na kilimo anacholima, hatutaki kuona kwamba tunalima kwa mazoea. Kama sisi watu wa kule Mtwara unakuta babu alikuwa na shamba la mikorosho basi na mimi Mheshimiwa Tunza ninalirithi ninafanyaje, ninakwenda. Tunatakiwa tuhame huko twende kwenye kuzalisha kwa tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila siku nikisimama kuchangia Wizara hii ya Kilimo ninasema mimi naona mgogoro mkubwa unaotokea kati ya wakulima, Serikali na wanunuzi ni kwa sababu tija yetu katika uzalishaji wa mazao ni ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapohudhuria mawasilisho mbalimbali, kwa mfano mimi nitaongelea zao moja la korosho, tunapohudhuria kuna nchi zinalima korosho, siyo Tanzania peke yake. Wenzetu sasa hivi ekari moja wanapanda mikorosho mpaka miche 70, lakini sisi tunaambiwa ekari moja tupande miche 25, matokeo yake ni nini? Hata ukija kuvuna unavuna kiasi kidogo, ukienda kukutana na tatizo la soko kwamba sokoni bei imeshuka, bei ni ndogo maana yake unazidi kupigwa na unazidi kulalamika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kuhudumia shamba hasa shamba la mikorosho kwa sababu nina uzoefu nalo, mpaka upate hiyo korosho unayokwenda kuiuza ghalani ni kazi kubwa sana. Kwa hiyo, wito wangu kwa Serikali ni kwamba Serikali itafute namna ya kuongeza tija ya uvunaji wa mazao yetu mengi ya kilimo na hasa yale mazao ya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma taarifa ya Kamati inaeleza kabisa kwamba kuna upungufu wa Maafisa Ugani, waliopo ni 35% tu. Sasa kama kuna Maafisa Ugani 35% na hao Maafisa Ugani wenyewe ambao ni 35% sitaki kutumia neno baya, lakini lazima tuambiane ukweli kwa ajili ya kujenga nchi yetu, hao Maafisa Ugani 35% wamechoka. Wamechoka kwa maana ya kwamba mtu tangu aliposoma huko shuleni hakuna mafunzo kazini. Wameletewa baadhi ya vitendea kazi, lakini unaambiwa pikipiki haina mafuta hawezi kwenda shambani. Tunategemea huyu mkulima ambaye anahitaji asaidiwe anasaidiwa na nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimefurahi, wakati Mheshimiwa Waziri anawasilisha amesema vile vyuo ambavyo vimeunganisha na zile taasisi zetu, kwa mfano pale *TARI* Naliendele wanakwenda kuvifanya viwe vituo vya mafunzo. Mimi hilo ninaliunga mkono kwa sababu lilikuwa ni kilio changu kikubwa. Sasa tusiishie kwenye maandishi, twendeni tukatekeleze ili tija ambayo imekusudiwa ipatikane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkulima akivuna sana, hata kama akiuza kwa bei ndogo kuna unafuu ataupata kuliko analima sana, anavuna kidogo, anakwenda sokoni anakutana na bei ndogo na ndiyo maana wakulima wengi unakuta wanalalamika wanalima kwa mazoea kwa sababu kilimo ndiyo wameshakizoea tena, lakini ukilinganisha na gharama wanazoingia kwenye kilimo na faida wanayokuja kuipata kwa kweli faida ni ndogo sana au haipo kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inakuja kuuza korosho kwa njia ya mtandao *(TMX),* sisi Waheshimiwa Wabunge na wananchi wa mikoa inayolima korosho hili kwetu ni jambo zuri, lakini tatizo linalokuja kwenye uwekezaji. Tunaomba wafanyie majaribio

mfumo huu ili tunapokwenda kuuza ile tija iliyokusudiwa iweze kupatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitoe angalizo, hata kama mfumo ni wa mtandao bado wanaoshughulika ni binadamu. Tunaomba binadamu wanaokwenda kuwaweka hapa wawe binadamu wema, sisi tunataka wakulima wetu wafaidike. Suala siyo mtandao, suala ni kwamba kwenye mtandao huo ni lazima kuna mtu atawasha kompyuta, atafanya jambo, ataingiza *data,* yule uaminifu wake tunaomba uwe wa kueleweka ili tija iliyokusudiwa ipatikane. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali wamesema wanakwenda kujenga Kongani ya Viwanda pale Nanyamba, tunaomba ikajengwe. Mimi Tunza ukiniuliza ninatamani kama korosho zote tunazolima Tanzania zibanguliwe, tupeleke korosho na karanga. Sasa haya yote vile viwanda vilivyofungwa wamefanya tafakari? Vile vimefungwa hivi tunavyokwenda kuvijenga vitakwenda kufanya kazi iliyokusudiwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, Mheshimiwa Waziri mimi ninamtakia utekelezaji mwema, lakini watuangalie kule kwetu, zile tozo kama vile za *TARI* na Bodi ya Korosho sisi Waheshimiwa Wabunge tumezichoka. Tumemwambia Mheshimiwa Waziri, sasa ufike wakati na sisi atusikilize. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tunza. Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, atafuatia Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Bashe, Naibu wake, Katibu Mkuu wake na Wizara nzima kwa kazi nzuri wanayoifanya, kwa kweli wanafanya kazi nzuri kwa kuisimamia Wizara ya Kilimo. Ninawapa hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo ninaomba niongee haraka haraka kuhusu bajeti. Tunamshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi anayoifanya kwa kupandisha bajeti kila mwaka ambapo bajeti ya sasa hivi mwaka 2024/2025 ni shilingi trilioni 1.2 ambayo inatolewa. Hii ni kubwa sana na haijawahi kutolewa tangu miaka yote hiyo ya nyuma. Kwa hiyo, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo tunaloomba kwa Wizara ya Kilimo na kwa Mheshimiwa Waziri ni kuzisimamia hizi fedha ziweze kutumika vizuri. Kwa upande wa Wizara ya Fedha, hizi fedha ziweze kutoka kwa wakati kusudi mipango yote ya kilimo iweze kutimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, unajua kuwa 65.6% ya wananchi wanaishi vijijini na wanategemea kilimo, wanafanya shughuli za kilimo na wanazalisha mazao ya chakula kwa 100%. Vivyo hivyo tunamshukuru Mheshimiwa Rais na kumpa pongezi kwa kuona kuwa kilimo anakipa kipaumbele na anajua kuwa wakulima wadogo wadogo ndio wazalishaji wakubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na mpango wa *BBT,* ninawapongeza sana Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Bashe kwa kusimamia mpango huu wa *BBT*. Mpango huu wa *BBT* unatoa ajira kwa vijana na kwa wanawake. Kwa hiyo, ninashauri kuwa hii mikoa ambayo kama Mheshimiwa Waziri alivyosema na sisi Kamati tulivyosema kuwa ni jambo zuri ikienda kwenye mikoa na kwenye halmashauri kwa sababu huko kwenye halmashauri na kwenye mikoa kwa mfano Mkoa wangu wa Morogoro unakuta vijana au wanawake au wakulima wengine wanalima mpunga, wanalima mazao ya bustani, wamezoea mazao hayo. Kwa hiyo, akipeleka *BBT* huko watakwenda vizuri, kwa sababu hatawasumbua wala hawatasumbuka, *BBT* yao wataifanyia hapo.

Kwa hiyo, ninaomba ile mikoa ambayo bado haijatenga maeneo iweze kutenga maeneo kwa sababu Serikali imesema itakuwa pamoja nao kwa mambo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ninaloomba ni ushauri na kuwa karibu na hawa vijana walio kwenye *BBT* na kufanya ufuatiliaji

pamoja na tathmini ili kuona kama mpango huu wa *BBT* unakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninaloongelea ni kuhusu kilimo cha umwagiliaji. Tukitaka kilimo kibadilike, kiwe cha biashara, kiwe chenye tija na kiwe cha kijani ni lazima tufanye kilimo cha umwagiliaji. Kilimo cha umwagiliaji ni kweli kinatoa ajira, usalama wa chakula, kinaleta uchumi na mambo mengine ya mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha umwagiliaji kinaambatana na vitu vingi na hapa nitasema kuwa kilimo cha umwagiliaji kinaambatana pamoja na mbegu. Kwa hiyo, lazima tuwe na kilimo cha umwagiliaji kwanza na vilevile tuwe na mbegu bora. *ASA* wanazalisha mbegu, *TARI* wanatafiti na *TOSCI* wanaangalia ubora. Kwa hiyo, hawa watu wote wakienda kwa pamoja ninaamini kuwa kilimo pamoja na mbegu vitakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba, licha ya kuzalisha na kuongeza mbegu mpaka kwenye 60% lakini tukazane katika kuwahusisha wakulima pamoja na sekta binafsi kusudi tuweze kuzalisha mbegu za kutosha na bei iweze kuwa nzuri na hasa iwe elekezi, wananchi waweze kutumia mbegu bora na kufanya kilimo chenye tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Morogoro tumepata mafuriko, mafuriko haya yanaenda vizuri pamoja na kujenga mabwawa. Ninaishukuru sana Serikali yetu juzi juzi tarehe 30 imesaini miradi ya umwagiliaji na Mkoa wa Morogoro tumeweza kupata mabwawa mawili ambayo yatafanyiwa usanifu na mabwawa haya yatajengwa Mlimba pamoja na Ifakara. Ninaamini hiyo itasaidia kupunguza mafuriko ambayo yanakuja mara kwa mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri, Mkoa wa Morogoro ulipata mafuriko wilaya zote, lakini tathmini haijafanyika huko kwa kiwango cha kutosha. Unakuta Mvomero tuna mafuriko ya kutosha, Malinyi wamepata mafuriko ya kutosha na Ulanga wamepata mafuriko. Naomba miongoni mwa

mabonde hayo 22, Bonde la Kilombero nalo liangaliwe ili tupate mabwawa mengine na tuweze kupunguza mafuriko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kilimo cha umwagiliaji pamoja na mbolea, mbolea hapa nchini inazalishwa kwenye viwanda vichache, kama sikosei ni kama viwanda viwili. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali iwavutie wawekezaji ili waweze kuwekeza kwenye uzalishaji wa mbolea kusudi tuweze kupata mbolea na iweze kuwa ya kutosha ili kumfanya mkulima anapotumia mbolea alime kilimo cha kisasa na kilimo chenye tija. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais, kwa kutoa ruzuku kwenye upande wa mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na kilimo cha umwangiliaji na utafiti, tuna utafiti wa udongo, magonjwa na kila kitu. Kwa hiyo, tukazane kwenye utafiti kwamba licha ya kuongeze fedha, tuongeze zaidi fedha kwenye utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na kilimo cha umwangiliaji siwezi kuachia bila kumshukuru Mkurugenzi wa Tume ya Umwagiliaji, anafanya vizuri sana mahali popote alipo. Tumetembelea na ni kweli tumeona miradi inakwenda vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na kilimo cha umwagiliaji pamoja viuatilifu; zao la pareto ni zao bora lakini mpaka sasa hivi linazalishwa huko Makete na kwingine, hivyo nilikuwa ninashauri kuwa lizalishwe hata kwenye mikoa mingine kusudi tuweze kupata viuatilifu kwa bei rahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaona unawasha taa sijui tayari? Kengele sijaisikia. Tayari au bado? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na maafisa ugani; hawa ndio wanaofanya kazi ya kilimo. Tunataka elimu lakini bila ya mkulima kupata elimu kilimo hakiwezi kwenda vizuri. Kwa hiyo ninawaomba sana. Hongera sana Serikali kwa kuwapa vitendea kazi. Vitendea kazi wamevipata, lakini awafuatilie, fuatilieni kusudi waweze kuwa karibu na mkulima. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na Mwenyezi Mungu akubariki kwa hayo machache niliyoyaongea, ninakushukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, ninapowasha taa ninakuashiria uhitimishe kwa sababu nina *management* ya muda hapa. Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma. Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao, atafuatia Mheshimiwa Lucy John Sabu. Mheshimiwa Lucy John Sabu.

**MHE. LUCY J. SABU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia katika hotuba ya bajeti ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara inayoongozwa na Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe pamoja na Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara na ninawapongeza kwa kazi nzuri wanayoifanya, ninawapongeze kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati. Tunampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuendelea kuwa msikivu na wakati wote ambapo tumekuwa tukimshauri mambo mbalimbali amekuwa msikivu kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiupekee kabisa nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuleta maendeleo kwa ajili ya wananchi wake. Nimpongeze pia kwa kuendelea kuongeza bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa sababu imekuwa ikiongezeka kwa miaka mitatu mfululizo kutoka shilingi bilioni 294 na hivi sasa Wizara ikiwa inaomba shilingi trilioni 1.2. Ama kweli mama ana mapenzi ya dhati katika Wizara hii ya Kilimo na kwa sababu kilimo kinawagusa wananchi wetu kwa kweli tuna kila sababu ya kumpongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisisitize zaidi kwamba ongezeko hili la bajeti lazima liende sawa sawa na tafsiri pana kwa kutoa matokeo chanya kwa vijana. Kama tunavyofahamu katika sensa vijana wameoneka ni kundi ambalo lina idadi kubwa ya watu kwa zaidi ya 70%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiupekee kabisa niipongeze Wizara kwa kuisimamia vyema Programu ya Mradi ya *BBT* ambao ni mahsusi kwa ajili ya vijana na wanawake. Ningependa kushauri mambo machache hususan katika eneo hili na nisisitize kama ambavyo kwenye Kamati tumesisitiza kwamba ishuke haraka zaidi kwenye halmashauri zetu ili kuweza kuongeza wigo mpana na kutoa fursa nyingi kwa vijana kuweza kujiajiri katika eneo hili la kilimo. Pia ilenge katika kuzalisha mbegu ambazo zitaweza kusaidia kupunguza changamoto ya uhaba wa mbegu katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia *BBT* iongeze wigo wa kuzalisha mazao ya mboga mboga ama kilimo cha mboga mboga kwa sababu sekta hii imeendelea kukua kwa kasi sana kwa zaidi ya 11% na itatusaidia kuweza kupata mapato na ajira kwa ajili ya Taifa letu. Nisisitize zaidi eneo la ruzuku ya pembejeo ziweze kuwalenga zaidi vijana na wanawake ili waweze kujikwamua katika eneo hili la kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Simiyu ni mkoa kinara katika uzalishaji wa zao la pamba na tunaipongeza Serikali kwa kuendelea kuhakikisha kwamba wanalisimamia zao hili ili kuwawezesha wakulima katika Mkoa wa Simiyu kunufaika na zao hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee tunaipongeza Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambapo uzalishaji umeongezeka kutoka tani 88,000 hadi kufikia tani 140,000 katika msimu wa mwaka 2023/2024. Juhudi hizi zimekuwa kubwa kweli kweli na ni kutokana na uongozi wa mkoa. Mkuu wa Mkoa Mheshimiwa Dkt. Yahya Nawanda anafanya kazi nzuri sana ya kusimamia zao hili, pamoja na Wakuu wa Wilaya wote wamekuwa wakizunguka katika mkoa mzima kutoa hamasa kwa ajili ya zao hili la pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakumbuka miaka mitatu iliyopita wadau wa zao la pamba pamoja na Bodi ya Pamba tulikubaliana kwamba watatenga kiasi cha shilingi 27 kwa ajili ya kutoa hamasa katika zao hili. Nipende tu kusisitiza kwamba waendelee kutoa, watoe hicho kiwango cha fedha ili kuweza kuwasaidia na hivyo zao hili liweze kuwanufaisha wananchi wa Mkoa wa Simiyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru Serikali kwa ajili ya Mradi wa Umwagiliaji wa Kasori katika Wilaya ya Bariadi. Kiupekee kabisa nimpongeze Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya Mheshimiwa Simalenga kwa usimamizi mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali kwa kutuletea fedha kiasi cha shilingi bilioni tisa ambazo zimetumika katika awamu ya kwanza na sasa tumepokea kiasi cha shilingi bilioni tatu ambazo zinaenda kukamilisha mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niisisitize Wizara kwamba wajiandae kutoa elimu kwa ajili ya wananchi ambao wanazungukwa na mradi huu ili uweze kuwanufaisha katika kilimo cha umwagiliaji, lakini pia uweze kuwasidia vijana wote ambao wanazungukwa na mradi huu, hii itawasaidia wananchi wote ambao wanajishughulisha na shughuli mbalimbali hasa za kilimo cha pamba, mboga mboga na kuhakikisha kwamba wanaweza kunufaika na kilimo na kulima kwa mwaka mzima mfululizo pasipokuwa na changamoto yoyote ya uhaba wa mvua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia kuikumbusha Wizara kwamba Mkoa wa Simiyu katika Wilaya ya Bariadi tuna eneo ambalo lilikuwa likitumika kwa ajili ya Maadhimisho ya Nane Nane, Nyakabindi. Mheshimiwa Waziri analifahamu na nimwombe aangalie namna bora ambayo itaweza kusaidia eneo hili ili liweze kuendelea na atakapokuwa anahitimisha hoja yake atueleze ama kama itampendeza alete Mradi wa *BBT* katika eneo hili la Nyakabindi ili vijana waweze kunufaika na fursa ambazo zinaweza kupatikana katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alikuja mwaka jana katika Maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani Kitaifa

yalifanyika Simiyu na alitoa maelekezo kwamba wanatakiwa wajenge kisima kikubwa katika eneo hilo. Cha kusikitisha ni kwamba hadi hivi sasa hamna chochote kilichofanyika. Nimwombe tu Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha hoja yake tupate pia majibu ya jambo hili kwamba ni lini kisima hiki kitajengwa ili kiweze kuwanufaisha vijana wa Mkoa wa Simiyu ambao wanajishughulisha na kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiupekee kabisa nitoe shukrani za dhati kwa fursa hii na niwaombe Wizara waendelee kufanya kazi kwa juhudi ili kuendelea kuisadia Wizara hii ya Kilimo kwa sababu ina manufaa na wananchi wote na Watanzania. Niwatakie kila la heri katika utekelezaji wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa fursa hii na ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwisha na tunayo orodha ndefu ya wachangiaji, ninaomba wale wachangiaji wote ambao walitarajia kuchangia leo na wamekosa fursa wawasiliane na *caucus* zetu za vyama vya siasa ambavyo vimo humu Bungeni kwa ajili ya kuratibiwa upya.

Baada ya tangazo hili ninaahirisha Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.42 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 3 Mei, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*